Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 15 Julai, 2009**

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MSEMAJI WA MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambiya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZARA WIZARA YA KAZI, AJIARA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Randama ya Makadirio ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 215

### Mwekezaji wa Kiwanda cha Mafuta ya Alizeti

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kupitisha Bajeti ya mwaka 2008/2009, Serikali iliahidi kutafuta mwekezaji wa kujenga kiwanda cha mafuta ya Alizeti ili yaweze kuwa na kiwango cha soko la kimataifa kwa lengo la kuinua uchumi wa wananchi wa Singida wakiwemo Wanawake na vijana.

Je, Serikali imefikia hatua gani katika mpango huo wa kupata mwekezaji?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa wakati wa kupitisha Bajeti ya mwaka 2008/2009, Serikali iliahidi kuhamasisha kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta ya alizeti ili yaweze kuwa na kiwango cha soko la kimataifa kwa lengo la kuinua uchumi wa wananchi wa Singida wakiwemo Wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa juhudi za kutekeleza ahadi hiyo zimeanza ambapo Wizara yangu imefanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kampuni ya *Mount Meru Millers* ya Arusha ambayo tayari ina kiwanda cha kutengeneza mafuta ghafi Singida na *Habib Investment Ltd.* kutoka Uganda kwa ajili ya kuwekeza katika eneo la kuongeza thamani za mazao ya kilimo ikiwemo Alizeti. *Mount Meru Millers* wana mipango ya kuwekeza kiwanda kikubwa zaidi cha kusindika aina nyingi za mbegu kama mbegu za Karanga, Ufuta, Pamba na kadhalika kuliko kilichopo sasa hivi kinachosindika mbegu za Alizeti tu.

Vile vile, wapo wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza katika mradi wa kusindika na kusafisha mafuta ya kupikia (*edible oil*) nchini na tayari wengine wamejiandikisha katika kituo cha Uwekezaji nchini.

Baadhi ya kampuni zilizojiandikisha ni *Simon Group Ltd*. ya Mwanza; *Natural Aromatics Ltd.* ya Dar es Salaam; *Isukanjia Trading Co. Ltd.* ya Dodoma; *Kisumwa Machinery Co*. ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kushawishi wawekezaji zaidi ili wawekeze katika maeneo mbalimbali nchini na hasa ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na hivyo kuchangia na kuinua uchumi. Suala la kujenga Viwanda na kuendesha biashara limebakia kuwa jukumu la Sekta Binafsi wakati Serikali imebaki najukumu la kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji ili sekta binafsi iweze kuwekeza ipasavyo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya mtani wangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na nia yake thabiti ya kuwasaidia wakulima wa zao la Alizeti mkoa wa Singida napenda kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametamka wazi kwamba ameshapata wawekezaji kama wawili hivi akiwepo *Mount Meru Millers* ambaye tayari ana kiwanda Singida. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja naye huyu mwekezaji ili kumwunganisha na uongozi wa Mkoa wa Singida ili aweze kupata msukumo wa karibu kuweza kuona umuhimu wa haraka kuweka kiwanda hicho kwa kuwasaidia wakulima wa zao la Alizeti Singida mapema iwezekanavyo?

La pili, kwa kuwa, kuna mwekezaji aliyeko hapo hapo Mkoani Singida Namzawa ambaye tayari amefunga mashine ndogo ya kusafisha mafuta haya ya Alizeti katika Mji mdogo wa Shelui anayejulikana kwa jina la Alfan Shams. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kumwezesha huyu Mwekezaji mzawa ambaye tayari ameonyesha nia ya kutaka kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Singida wa zao la Alizeti ili apate nguvu kubwa ya kuweka kiwanda Kikubwa kwa ajili ya kusaidia wakulima wa zao hili la Alizeti na mafuta haya yaweze kupata soko la kimataifa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo.

Kwanza kabla ya kutoa majibu haya napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kuona umuhimu wa kuendeleza Mkoa wa Singida na amekuwa akifanya hivyo toka alivyoanza kuwa Mbunge, nampongeza sana.

Vilevile nampongeza siyo tu kuwa anataka kuendeleza Singida, bali vilevile ameitikia ule mwito wa kilimo kwanza kwa kuweza kuongezea thamani mazao ya kilimo. Vilevile anaisaidia Wizara yangu ya Viwanda kupigia debe maendeleo ya viwanda na kwa hiyo namshukuru sana.

Sasa swali la kwanza alilouliza ni kwamba nakubali kabisa kwamba nitamshawishi mwekezaji huyo twende naye Singida ili tuweze kukutana na Viongozi wa Singida akiwemo Mheshimiwa Diana Chilolo, ili kuona kama kuna jambo ambalo tunaweza kulifanya ili kuongeza msukumo na kuharakisha uwekezaji ambao tayari ameshaupanga. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa kuona umuhimu wa Viongozi wa Singida nao kushiriki ipasavyo.

Kuhusu swali la pili ningependa sana kumpongeza Mwekezaji huyu Alfan Shams kwa kuwekeza katika kinu cha kusindika na kusafisha mafuta ya Alizeti.

Sasa maombi yake ya kumwezesha nitajitahidi kuona ni namna gani tutamwezesha kupitia *exporter guarantee scheme au export credit scheme* na vilevile

*SME credit scheme na scheme* nyingine zitakazokuwepo ili kuweza kumwinua huyu mwekezaji mdogo aweze siku moja kuwa mwekezaji mkubwa kama yule wa *Mount Meru Millers*.

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, wakulima wakulima wa Rukwa ni sawa na wale wa Singida kwani nao pia wanalima sana Alizeti na kutengeneza mafuta kwa kutumia mashine ndogo ndogo. Ni lini basi Serikali itawaona wakulima wa Rukwa na kuwasaidia kuleta wawekezaji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eliatta N. Switi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kuona Wanawake wanachangamkia suala hili la viwanda na kwa sababu ni Wanawake wengi ndiyo wanaolima ni dhahiri kwamba ni wao ndiyo ambao wataendelea kilimo kwa kuweza kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Kama nilivyosema suala la kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ni muhimu siyo tu kwa Singida na siyo tu kwa Rukwa bali ni kwa nchi nzima pale pote ambapo kuna mazao ambayo yanaweza kusindikwa ili kuongeza thamani.

Kwa hiyo, na mimi nimepokea wito wa Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Rukwa kwamba na Rukwa nayo iwe katika mipango ya kuweza kumtafuta au kuhamasisha wawekezaji wa kubwa ili washirikiane na wale wadogo katika kuendeleza zao la Alizeti na mazao mengine ambayo yanaweza yakatumika kutengeneza mafuta ya kupikia kwa sababu mafuta ya kupikia huwa yanayoagizwa nje yanatumia fedha nyingi sana za kigeni pengine ni mahali ambapo fedha zinatumika zaidi ukiacha mafuta ya petroli.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako mazuri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na swali linalofuata kwa sababu wote mnaosimama sasa hivi mmesimama baada ya swali la nyongeza.

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na swali lake analielekeza katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 216

**Huduma za Matibabu – Hospitali ya Bumbuli**

**MHE. WILIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Bumbuli ni kubwa kieneo na watu takribani 150,000; na kwa kuwa, hospitali ya Wilaya ya Lushoto ipo umbali wa zaidi ya kilomita hamsini (50) kutoka waliko watu wengi; na kwa kuwa ipo hospitali kubwa ya Bumbuli ya dhehebu la Kikristo la Kilutheri.

Je, Serikali haiwezi kufanya makubaliano na wamiliki wa hospitail hiyo ili ifanywe kuwa teule ya *Designated Hospital* na kuwawezesha wananchi wa Bumbuli wanufaike na maendeleo ya huduma za afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo Mbunge wa Bumbuli kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo kwa sasa ni kwamba Hospitali ya Wilaya inatakiwa kuhudumia watu 250,000. Kwa mujibu wa taarifa ya sensa ya mwaka 2002, Wilaya ya Lushoto ina jumla ya watu 419,970. Kwa idadi hii ni dhahiri kwamba hospitali ya Wilaya iliyopo inakabiliwa na mzigo mkubwa wa kuwahudumia wananchi wa Wilaya hiyo wakiwemo wananchi wa Bumbuli. Kwa kulitambua hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imeingia makubaliano (*Service Agreement*) na hospitali ya Bumbuli inayomilikiwa na Kanisa la Kilutheri ili hospitali hiyo iweze kutoa huduma kwa wananchi wa Bumbuli kwa niaba ya Hospitali ya Wilaya. Mkataba uliopo sasa ni wa kutoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto. Huduma zitaendelea kupanuliwa ili hatimaye hospitali hiyo itoe huduma zote zilizomo katika Kitita cha Huduma za Afya (*National Essential Health Package*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote napenda kuliarifu Bunge Tukufu kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na TAMISEMI na wadau mbalimbali iliandaa utaratibu wa Halmashauri kuingia makubaliano (*Service Agreement*) ya utoaji wa huduma za afya katika maeneo yao na Mashirika ya Dini au sekta binafsi zenye vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo hayo. Katika makubaliano hayo ni kwamba vituo hivyo vitatoa huduma kwa wananchi kwa niaba ya Halmashauri. Makubaliano hayo yanaweza kuhusisha kitita chote cha huduma za afya (*National Essential Health Package*) au sehemu tu ya huduma, kama vile huduma za afya ya uzazi na mtoto.

Halmashauri inapoingia makubaliano hayo kupitia utaratibu wa *Service Agreements* inawasaidia wananchi kupata huduma za afya kwa gharama nafuu. Aidha, utaratibu huu unategemewa kuzisaidia Halmashauri katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Huduma ya Afya ya Msingi (MMAM), kwani vijiji ambavyo tayari vina Zahanati au vituo vya afya, Halmashauri hazitakuwa na haja tena ya kujenga vituo vingine bali kuingiza makubaliano na wamiliki wa vituo hivyo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Awali kabisa napenda kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto pamoja na Wizara yake na TAMISEMI kwa hatua hii nzuri iliyojulikana.

Kwa kuwa, utaratibu huu sasa utaongeza kazi kwa madaktari waliopo pale Bumbuli. Je, Waziri haoni kwamba sasa kuna haja ya kuongeza madaktari pale Bumbuli maana wananchi sasa watakwenda kwa wingi na vilevile tukizingatia kwamba hospitali ile vilevile na kituo cha mafunzo cha *Clinical Officers*?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William H. Shellukindo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hospitali ya Bumbuli imepanua huduma zake na kwamba kuna chuo pale, ninachotaka kusema ni kwamba kwa vile sisi tumeingia ubia na hospitali hii na kwa sababu kwa kawaida Serikali huwa inatoa ruzuku ya vitanda yaani *bad grant* na mishahara ya wafanyakazi yaani *salary grant* kwa hospitali ambazo zimeingia ubia ningeishauri Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto waweze kuangalia mahitaji yao ili waombee nafasi ya ajira kupitia utumishi na baadaye TAMISEMI ili watumishi tukiwatuma kule ambao wanakwenda katika Halmashauri ya Wilaya hii wengine waweze kupelekwa kule katika hospitali ya Bumbuli.

**MHE. RAMADHANI ATHUMANI MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja la nyongeza.

Pamoja na matatizo makubwa ya suala la afya katika maeneo yetu hususani katika kituo cha afya cha Chalinze ambacho ni kituo kinachohudumia vijiji 11 vya Kata ya Chalinze pamoja na vijiji jirani vya Mkoa wa Tanga na Morogoro. Lakini pia kituo hicho cha afya cha Chalinze kinahudumia majeruhi wa ajali za barabarani ambao wakifika pale wanapata huduma ya kwanza hatimaye kupelekwa Tumbi, lakini huduma inayotolewa pale ni hafifu kwa maana ya vitendea kazi ni vichache kufuatana na matukio yanayojitokeza pale. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kujenga hospitali kubwa eneo la Chalinze ili iweze kuhudumia wananchi wa maeneo mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Morogoro, Tanga na hususan wale wanaopata ajali za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno Mbunge wa Chalinze swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa kwamba kituo cha afya cha Chalinze hakikidhi mahitaji kulingana na huduma ambayo inatoa na hususani kwa majeruhi na kuhudumia Mikoa jirani.

Mheshimiwe Mwenyekiti, lakini kwa sasa hivi Serikali imetenga pesa nyingi kuweza kukiboresha kile kituo cha Tumbi, nitakachoweza kusema ni kwamba bado katika mpango wetu wa Maendeleo ya Afya ya Msingi yaani MMAM, tunao uwezo wa kuweza kukipanua kile kituo cha Afya cha Chalinze ili kiweze kuwa na vitendea kazi vya kutosha na kuongeza Wataalamu. Lakini kwa sasa hivi hatuwezi tukawa na hospitali kubwa pale na hospitali nyingine ya Tumbi ambayo tunaioboresha.

Kwa hiyo, namshauri tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tushirikiana Halmashauri kupitia TAMISEMI kupitia Wizara ya Afya ili tuone kwamba tunaweza kuwapatia vitendea kazi vya kutosha na watumishi wa kutosha ili waweze kupata hiyo huduma na wakati huo wengine wale ambao wamepata majeraha makubwa wawepe kupelekwa katika hospitali ya Tumbi na wengine watapelekwa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Na. 217

**Kujenga Hospitali katika Kambi ya Jeshi Kaboya**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, zahanati ndogo ya Jeshi iliyoko Kambi ya Jeshi Kaboya inahudumia Askari na wananchi wote wanaofika hapo kupata huduma hasa wananchi wa vijiji vya Katoke, Kimbugu, Izigo, Bushumba, Mauongwe, Bugasha, Bisole na Nyakashenye na kwa kuwa nimekuwa nikiomba mara nyingi Serikali ijenge hospitali katika eneo hilo:-

Je, ni lini hospitali hiyo itajengwa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la KUjenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Jeshi ya Kaboya haina zahanati nzuri kutokana na majengo yake kutokamilika kujengwa. Ni kweli kuwa Mheshimiwa Ruth Msafiri amekuwa akiomba mara kwa mara kujengwa kwa hospitali katika Kambi ya Kaboya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara imeelekeza raslimali katika kuimarisha na kujenga hospitali za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Zahanati ya Kambi ya Kaboya mwaka huu wa fedha Wizara itakamilisha ukarabati wa majengo yanayotumika sasa, na mwaka 2010/2011 Wizara itaomba fedha kwa ajili ya kuikamilisha ujenzi wa majengo yaliyoanza.

**MHE. GOSBERT B. BLANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo kusema kweli hayakuridhisha hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi limeuliza ni lini Zahanati ndogo ya Jeshi la Kaboya itajengwa na hapa Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kujenga hospitali za Kanda. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kulihakikishia Jimbo la Muleta Kaskazini, kwamba Zahanati hiyo haitakaa ijengwe hata kidogo?

Swali la pili, kwa kuwa Zahanati hiyo ina upungufu mkubwa sana wa watumishi pamoja na madawa na vifaa mbalimbali vya Zahanati. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na upungufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Blandes yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alizungumza na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kuhusu kuona uwezekano wa kuingiza ujenzi huo katika mwaka huu wa fedha na Mkuu wa Majeshi Gen. Devis Mwamnyange alikwenda yeye mwenyewe kwenye eneo la Kaboya na asubuhi hii Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa amenielekeza kwamba nimjulishe Mheshimiwa Ruth Msafiri kwamba Mkuu wa Majeshi amekubali kuingiza ujenzi wa hospitali hiyo katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa maana hiyo katika ujenzi huo kwa vyovyote vile habari ya watumishi, zana na nyenzo nyingine pia itazingatiwa.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Kaboya ni sawasawa na matatizo ya Rwamishenyi, Biharamulo Twiga kwenye Jeshi yaani Makao Makuu ya Jeshi hawana hata *dispensary* yoyote ya kuwasaidia.

Je, katika orodha hiyo na Rwamishenyi pamoja na Biharamulo ipo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Blandes pia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage kwamba sijapata maelekezo yoyote kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba hiyo pia ipo. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaedelea maana yake Mheshimiwa Naibu Waziri anategemea maelekezo, huo ndiyo utaratibu wa kijeshi. Sasa baada ya maswali hayo tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi.

Na. 218

## Miradi Iliyofadhiliwa na World Bank – Kiomboi

**MHE. JUMA HASSAN KILIMBAH:** Kwa kuwa, miradi ya maji inayofadhiliwa na *World bank* kwenye awamu ya 2006/2007 ni ile ya Komboi; na kwa kuwa, mradi huo ulitakiwa kuikamilisha mwishoni mwa mwaka wa fedha 2007 lakini hadi sasa haujakamilika:-

(a) Je, ni sababu gani zilizochelewesha mradi huo usikamilike hadi sasa?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuhakikisha kuwa, miradi hiyo inakamiliska na kuwachukulia hatua wahusika na baadhi ya Watendaji ambao kwa namna moja au nyingine wameshiriki kuchelewesha mradi huo?

(c) Je, ni lini miradi ya awamu ya pili itaanza ile ya Nguvumali (Ndago), Ngungia, Mlandala, Nganguli ambayo yote ilitakiwa itekelezwe katika mwaka huu wa fedha 2008/2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Katika mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilikuwa moja kati ya wilaya 14 zilizotekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira kama *Pilot Project* na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi huo ndiyo unaotumika kutekeleza Programu nzima ya Kuendeleza Sekta ya Maji katika Halmashauri zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi haukukamilika kutokana na kukosekana kwa maji ya kutosha katika visima sita vilivyochimbwa Salasala, Mjini Kiomboi. Kazi ya kutafuta visima vipya ilikamilika mwezi Agosti, 2007 baada ya kuchimba visima vingine vinne katika eneo la Pyululu Mjini Kiomboi. Mabadiliko hayo ya kazi ndiyo yaliyosababisha gharama za mradi na muda wa utekelezaji kuongezeka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali za kukamilisha mradi huu ni pamoja na kufanya usanifu mpya wa bomba kuu la kuchukua maji kutoka kwenye visima vipya, makadirio ya gharama zilizoongezeka na utafutaji wa fedha za ziada ikiwa ni pamoja na kuomba kibali cha kujenga mradi huu kwa gharama mpya ambacho kilipatikana kutoka Benki ya Duania mwezi Juni, 2008 wakati ambao mradi ulikuwa unamaliza muda wake.

Hadi sasa miundombinu yote ya mradi huo imekamilika ambayo ni matanki manne (4), vituo vya kuchotea maji 18, mabomba yenye urefu wa kilomita 26 na ufungaji

wa mitambo ya maji. Kazi ya kuvuta umeme hadi kwenye mitambo imekamilika. Kazi inaendelea na mkandarasi ni kukabidhi mradi kwa Halmashauri ya Wilaya mwishoni mwa mwezi Julai, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi huu kumetokana na matatizo ya upatikanaji wa vyanzo vya maji. Hakuna taarifa yoyote kuwa ucheleweshaji wa mradi umetokana na kutowajibika kwa Watendaji. Hata hivyo, kama kuna uthibitisho kuwa mtumishi yeyote alihusika na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi huu kwa makusudi Serikali haitasita kumchukulia hatua za kinidhamu kufuatana na Kanuni za Utendaji kazi Serikalini.

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zote ambazo hazikutelekezwa chini ya mradi wa maji na usafi wa mazingira sasa zitatekelezwa na Program ya Kuendeleza Sekta ya Maji. Vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya Vijiji 13 ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imevipa kipaumbele katika utekelezaji.

Vijiji hivyo ni Iguguno, Kihonda, Kidarafa, Mkalama, Mtamba, Gumanga, Nyahaa, Mlandala, Nguvumali, Mugungia, Ng'anguli, Ujugu na Mingela.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kwamba tarehe 25.6.2009, Benki ya Dunia ilitoa kibali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kusaini mkataba kati yake na Mtaalam mshauri ili kazi ianze. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba inatarajiwa kusaini mkataba huo leo tarehe 15 Julai, 2009 na kwa maana hiyo utekelezaji utaanza katika mwaka 2009/2010.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza haya maswali ninaomba tu kwanza, ili kuweka kumbukumbu vizuri kwenye kijiji. Wakati anajibu Naibu Waziri, ametamka Ujugu, hatuna kijiji kinachoitwa Ujugu ila kinaitwa Ujungu. Baada ya sahihisho hilo sasa maswali ni haya yafuatayo:-

(i)Katika majibu yake, Naibu Waziri ameelezea mradi wa Kiomboi kwamba tayari shughuli zote zimekamilika ikiwa ni pamoja na kutandaza mabomba, kujenga matenki na shughuli zote, lakini kinachoshangaza ni kwamba, toka kazi hiyo ikamilike sasa yapata miezi minne, huduma ya utoaji maji kwa wananchi wa Kiomboi bado haijaanza.

Namwomba Naibu Waziri aniambie ni tatizo gani hasa ambalo sasa linazuia ile huduma isianze kutolewa ili wananchi waweze kupata maji.

(ii)Nashukuru Kipengele (c) kwamba, leo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Iramba inasaini mkataba kwa vijiji kumi na tatu (13) kwa ajili ya kuanza miradi ya uchimbaji wa maji. Nataka kujua Naibu Waziri kama mtalaam wa Maji, anipe *time frame* itakuwa ni

muda gani hii miradi itakamilika ili wananchi wa Iramba wapate matumaini kwamba, baada ya muda fulani maji yatatoka katika vijiji vyao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Killimbah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kuhusu miradi imeshakamilika lakini haitoi maji. Naomba nikubaliane naye kwamba, hata mradi unapokamilika kuna kipindi lazima kipite kwa sababu miradi hii inajengwa kwa taratibu za ukandarasi, ni lazima wakandarasi na mwajiri wajiridhishe ili mkandarasi aweze kukabidhi mradi huo na nimesema katika maelezo yangu kwamba, mkandarasi huyu anatarajiwa kukabidhi mradi huo kwa Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, kilichobaki ni kukabidhi tu halafu tutafanya *commisioning* ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Killimbah kwamba, nitafuatilia kama mradi umeshakamilika kama kuna vikwazo vyovyote basi tutaviondoa maana sasa ni ufuatiliaji tu. Hili nadhani niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Killimbah kwamba, sasa mradi huu utakuwa umefikia mwisho wake na utaanza kazi.

Mheshimi.wa Spika, kuhusu lini mradi utakamilika. Kwanza, nataka niwapongeze Halmashauri ya Iramba kwa kuweza kwenda na mchakato huu, mpaka mkahakikisha kwamba, tayari mmepata kibali. Hii ni hatua nzuri sana, mkikumbuka jinsi tulivyokwenda kwa kusuasua katika utekelezaji huu wa miradi wa vijiji kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu swali lake niseme hivi tutarajie kwamba, katika kipindi kama cha miezi sita hivi kazi yote ya usanifu itakuwa imekamilika halafu kazi ya ujenzi itaanza. Sasa mpaka hapo tutakapokuwa tumefanya mikataba ya ujenzi naomba nisitamke kwamba, mwezi fulani mkandarasi atakuwa amemaliza kazi lakini namhakikishia kwamba, katika mwaka huu kazi ya ujenzi ule wa mwishoni huko itakuwa imeanza.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, inaonekana licha ya vifaa vya kisasa tulivyo navyo vya kutafiti maji ya ardhini, visima virefu bado inatokea hali kama ilivyotokea huko Iramba kwamba, visima vinachimbwa na maji hayapatikani.

Je, Serikali inajua kwamba, kuna watu waliopewa vipaji na Mwenyezi Mungu vya kugundua maji hata bila vifaa, watu hawa wanaitwa *water dousers* na kwamba, Tanzania pia wapo, wageni na wenyeji. Serikali sasa itakubali ushauri wangu kwamba, pale ambapo wanatumia vifaa watumie pia na watu wa namna hiyo, kuthibitisha uwepo au kutokuwepo kwa maji ardhini ili kupunguza gharama za kuchimba kwa kubahatisha?

**MWENYEKITI**: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutumia sayansi hiyo nyingine ambatanishi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mramba, kufuatilia habari hiyo. Niseme kwamba, *water dousers,* watalaam hao Serikali tunawafahamu na wamo pia hata katika *literature* zote za *water resources* lakini, kwa kawaida kabla ya kuanza kuchimba tunatumia mbinu zote za kutafuta maji, ikiwemo hata mbinu ya *water dousing.* Lakini pia tunatumia mbinu zingine kutazama hali ya nchi kutuelekeza kwamba, mahali kama hapa maji yanaweza yakawepo nchini kuangalia milima ikoje na viashiria vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mramba kwamba, watalaamu hao sisi tunawakaribisha na tutashirikiana nao kwa sababu vipaji vyao ndivyo vilivyopelekea mpaka huu utalaam wa kisasa tunaoutumia wa kutumia vifaa vya kisayansi ukatokea. Kwa hivyo tunawatambua na ningependa tushirikiane nao hata kule Rombo kuwatumia watalaam hao.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa dhati ya moyo wangu nipende kupongeza Waziri wa Maji na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya na hata kutupa habari mara kwa mara na tunafahamu taratibu za miradi hii inavyokwenda, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika miradi hii ya *World Bank* ambayo tumeisubiri kwa muda mrefu sana na hata Jimbo la Kibakwe inayo vijiji vitano vya Kidenge, Chinyahuku, Makose, Wiyenzele na Kisima na kama ambavyo Naibu Waziri amejibu ni kweli kwamba, leo hii hata kule Mpwapwa mikataba inasainiwa, kwa hiyo inaonesha namna ambavyo Wizara hii iko makini na inavyofanya mambo yake kwa *standard* inayofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kujua tu kwamba, umakini na sasa uharaka wa uhitaji wa maji ambao wananchi hawa wamesubiri kwa miaka karibu minne unakwenda mwaka wa tano. Je, hali hii wataisukuma kwa kasi hii wanayokwenda nayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoweza kusukuma suala la maji pale kijijini kwake lililokuwa limekatisha tamaa wananchi na mpaka wamekuja kutushukuru hapa, tutafanya kasi hiyohiyo katika kusukuma suala hili la vijiji kumi (10).

Nirudie kusema kwamba, katika Halmashauri 99 Halmashauri 74 tayari kundi lile la kwanza zimeshapata ridhaa kilichobaki ni Halmashauri zenyewe kusaini mikataba hiyo, sisi kasi ni ileile tutajitahidi kusukuma kadri ya uwezo wetu.

Na. 219

**Ujenzi wa Kiwanja cha Kisasa – Dodoma**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Dodoma unakua kwa kasi na ongezeko la vyuo na kushamiri kwa biashara:-

Je, ni kwa kiasi gani suala la kujenga kiwanja cha ndege cha kisasa cha Dodoma linapewa kipaumbele ikizingatiwa suala hili limeongelewa kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mifenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Mji wa Dodoma Serikali inaona haja ya kuwepo kwa kiwanja cha ndege cha kisasa, kuweza kuhudumia ongezeko la watu wanaohitaji usafiri wa haraka wa kwenda na kutoka Dodoma. Katika utekelezaji wa azma hiyo Serikali kupitia mamlaka ya viwanja vya ndege kwa kushirikiana na mamlaka ya Ustawishaji Dodoma (*CDA*), imetenga hekta 5,000 eneo la Msalato, Nje kidogo ya Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya Ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege.

Lengo la Serikali ni kujenga kiwanja kikubwa cha Kimataifa chenye uwezo wa kuhudumia ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania, ilimteua Mhandisi Mshauri kampuni ya *Arabs Consulting Engineers (ACE*) kutoka Misri, ili kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali chini ya ufadhili wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi ya Afrika *(BADEA).* Kazi hii imekamilika kwa asilimia 95 na Mhandisi Mshauri amewasilisha rasimu ya taarifa ya mwisho Serikalini. Aidha, zoezi la kuwaondoa wananchi waliojenga kwenye eneo linalohitajika kwa ujenzi wa kiwanja limetekelezwa baada ya ya Serikali kutoa shilingi bilioni 1.6 katika mwaka wa fedha 2008/2009 ambazo zilitumika kuwafidia waliokuwa wamejenga katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, itasafisha eneo hilo na kujenga uzio ili kulinda uvamizi. Wakati huo huo Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na *BADEA* na taasisi mbalimbali za fedha ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho.

**MHE. MOSSY SULEIMANI MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tumechelewa sana kupata kiwanja cha kisasa katika Mji wa Dodoma, na kwa kuwa, Tanzania ina urafiki mkubwa sana na Serikali ya China, kwanini Serikali ya Tanzania isifanye maongezi ya moja kwa moja na Serikali ya China, ili iweze kupata uwanja huu wa kileo kabla ya mwaka 2012?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mossy kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo ambalo Mbunge amelitoa ni zuri na Wizara yangu italishughulikia hivi sasa kwa kujua umuhimu wa Jiji la Dodoma, tumeanza tayari maongezi na wenzetu wa China kwa ajili ya maboresho ya kiwanja kilichopo ili kiweze kutoa huduma nzuri zaidi wakati tunasubiri ujenzi huu wa kiwanja cha Msalato. Tunakamilisha mkopo na *BADEA* lakini katika kipindi hiki kabla kiwanja hakijajengwa tunatarajia kwamba, tutakuwa na maboresho makubwa sana katika kiwanja chetu cha Dodoma ambacho tunakitumia sasa.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge baada ya majibu hayo ya Waziri tutaendelea na swali linalofuata, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mwanza.

Na. 220

**Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kinapanuliwa katika kiwango kikubwa:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa majengo na ofisi katika kiwanja hicho ni magofu na hayana hadhi ya kiwanja?

(b) Je, Mkoa wa Mwanza ulipata mgao kiasi gani kati ya mgao wa shilingi bilioni moja zilizotengwa kwa ajili ya mikoa ya Mwanza na Kigoma.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Mwanza, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) inaendelea na utekelezaji wa mpango wa kuendeleza na kukiimarisha kiwanja cha Ndege cha Mwanza kwa kupanua miundombinu ya kiwanja pamoja na kujenga majengo ya kisasa ili kuondokana na majengo ya sasa ambayo hayakidhi mahitaji ya usafiri wa anga katika Kanda ya Ziwa. Upanuzi huu wa miundombinu pamoja na majengo utahusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria , jengo la mizigo, jengo la kuongozea Ndege, jengo la hali ya hewa, ujenzi wa sehemu ya kugeuzia ndege pamoja na kusimika mitambo mipya ya kuongozea ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ya mradi wa ukarabati viwanja vya ndege vya Mwanza na Kigoma, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenyewe, na hapa napenda nimpongeze sana kwa kufuatilia kwa karibu sana maendeleo ya mradi huu wa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Fedha zote hizi zilitumika kukifanyia ukarabati wa maegesho ya ndege '*apron*' kiwanja cha ndege cha Mwanza.

Aidha, mwaka huo Serikali ilipata msaada kutoka shirika la kimataifa linalohudumia wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*MONUC*) kwa ajili ya matengenezo ya *runway* ya Kigoma, na hivyo kutoa fursa ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya viwanja hivyo viwili kutumika katika kiwanja cha ndege cha Mwanza.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, niulize swali moja tu dogo la nyongeza. Kwanza labda na mimi nipende tu kuishukuru Wizara hii kupitia Waziri wa Miundombinu pamoja na Makamu wake kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kweli kwa Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Uwanja wa Ndege wa Mwanza unapendeza sana kwa hivi sasa. (*Makofi*)

Lakini ninachotaka kuuliza, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema chombo *TAA* kwa kifupi kinaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi wa Uwanja huu. Labda niulize, Je, huu mpango umefikia hatua ipi, ili walau Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza tuufahamu? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maria Hewa Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Mwanza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia kwa karibu ujenzi wa uwanja huu inaonyesha jinsi ambavyo Mheshimiwa Maria Hewa, alivyo na upenzi wa maendeleo katika Mkoa wake wa Mwanza. Kwa hiyo, nataka tu nimfahamishe Mheshimiwa Maria Hewa pamoja na Wabunge wengine kwamba, baada ya mwaka uliopita kutenga fedha hizo tulizozitumia mwaka jana lakini vilevile kwa mwaka huu Serikali imetenga fedha za ndani Shilingi Milioni 782,000, 532 ambazo zitatumika kwa ajili ya kuendelea kuufanyia matengezo uwanja huu.

Lakini isitoshe kuna fedha za nje ambazo tunategemea zitatoka baadaye kiasi cha Shilingi Bilioni 5.8 ambazo zikiishapatikana na kupata labda *co-finacing* ya wafadhili wengine, Uwanja huu wa Mwanza utaendelea kuboreshwa na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni ili uweze kuwa wa kisasa zaidi.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Benki ya *BADEA* iliishakubali kutoa pesa lakini kinachosubiriwa ni pesa kutoka Serikali ya Tanzania ili waweze kuanza shughuli hiyo. Je, Serikali ya Tanzania iko tayari kutoa mchango wake ili uwanja huo uanze kujengwa sasa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shibiliti kama ifuatavyo. Katika mwaka huu wa fedha tutatumia pesa za Serikali jumla ya Shilingi Milioni 582 kwa kazi maalum ya kukamilisha mikataba na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kazi ambayo inatarajiwa kuanza kule, kwa pesa za *BADEA*, lakini pia kwa mchango wa Serikali. Serikali inafahamu masharti ya pesa hizi tunazokopa hasa kwa benki ya BADEA na tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunayatekeleza. Tumefanya hivyo Songwe, na kutenga pesa Shilingi Bilioni 18 mwaka huu kwa ajili ya kulipa sehemu ile ya Serikali ili *BADEA* iweze kutupatia pesa. Kwa sasa hivi mchango wa Serikali ni huo na tumeutoa na tunahakikisha kwamba, pesa za *BADEA* zitaendelea kutoka kama ambavyo zimepangwa.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kuendeleza kiwanja cha Mwanza, ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze pale *Kilimanjaro International Airpot* kuna karakana ambayo inaweza kutumika kutengenezea ndege, hata kupiga rangi kwa ndege kubwa kabisa.

Lakini mwekezaji aliyeko pale hajaendeleza kabisa karakana ile. Ningependa kujua Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, karakana ile inafanya kazi ili kuweza kuliongezea taifa fedha zaidi?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kutoa majibu kwa swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Owenya, kama ifuatavyo.

Katika kiwanja cha *KIA,* tuna mwekezaji *KADCO* hivi sasa, na ndani ya majukumu ya *KADCO* ni pamoja na Hanga hiyo ambayo Mheshimiwa ameitaja. Kumekuwa na matatizo katika uwekezaji na kampuni hiyo na Serikali sasa hivi imefanya maamuzi ya kununua hisa za kampuni mbili ambazo zinahusika kwenye *KADCO* yaani *Mott Mac Donald* na *Saif* ili izirudishe Serikalini na tuanze kutafuta mwekezaji mwingine ambaye atakuwa na uwezo wa kuwekeza katika miundombinu ya *KIA.*

Na. 221

**Wanafunzi wanaosomeshwa na Serikali kukatishwa Masomo.**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Je, kwa nini baadhi ya walimu wakuu wa shule za Sekondari huwarudisha nyumbani wanafunzi wanaosomeshwa na Serikali pindi fedha zinapochelewa kufika?

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA -NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr.Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaogharamiwa elimu ya sekondari na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Halmashauri za Wilaya, hawapaswi kufukuzwa, kusimamishwa masomo au kurudishwa nyumbani pindi fedha zinapochelewa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 Serikali ilitoa mwongozo kwa Wakuu wote wa shule za Sekondari, Maafisa Elimu wa Mikoa, Maafisa Elimu wa Wilaya, wa Msingi na Sekondari, Wakurugenzi Watendaji wa Halmshauri na Manispaa, kuhusiana na utaratibu wa kuwahudumia wanafunzi wanaosomeshwa na Serikali.

Hivyo Wizara yangu inawaagiza tena Wakuu wa shule wote kutowarudisha nyumbani wanafunzi wanaogharamiwa na Serikali pindi Serikali inapochelewa kupeleka fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanashauriwa kutoa taarifa mara moja kwa Serikali au kwa Waheshimiwa Madiwani wao, pindi wanafunzi hao wanapoachishwa shule kwa sababu hizi. Aidha, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya Wakuu wa Shule watakaobainika kukiuka maagizo haya.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muongozo uliotolewa na Wizara mwaka 2005 inawezekana kabisa kwamba, umesahaulika kwa Wakuu wengi wa shule za Sekondari.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, kuna haja ya kutoa muongozo mwingine kuwakumbusha wanaohusika ili wasiendelee kuwasimamisha masomo wanafunzi wanaolipiwa na Serikali?

(b) Mheshimiwa Waziri, anasemaje kuhusu wanafunzi kurudishwa nyumbani wale wanaoshindwa kuchangia au kununua madawati? Kwanini wasiruhusiwe kukalia hata vigoda wakati wazazi wao wanajikusanya kuweza kupata fedha za kununua madawati?

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA -NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Dr. Festus Bulugu Limbu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeishatoa muongozo, imeishapeleka kumbushio kwenye mikutano ya pamoja, tumeishawaelekeza hivyo na kwa kuwa hivi

sasa shule hizi tumeishazikabidhi Serikali za Mitaa, naamini Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, analisikia hili atalikumbushia tena na kwa pamoja tutalihimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi kurudishwa nyumbani kwa ajili ya michango tulikataza. Tulisema kwamba, mwanafunzi aliyefaulu kwa vyovyote vile apokelewe shule, na hii ya kushauri kwamba, akakalie kigoda sidhani kama itakuwa ni hekima sana, maana kigoda ataandikaje? Akienda na kigoda aende na tofali? Sidhani kama hili ni jambo jema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe rai kwa Halmshauri zetu zote tukishirikiana na wananchi wote, tuwapatie zana zinazostahili watoto wetu ili elimu bora itolewe. Tukumbuke, urithi bora usiodhulumika ni elimu pekee. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Elimu bado hawajasoma Bajeti yao, tutakuwa na muda wa kushauri mambo mengi siku hiyo.

Kulingana na muda naomba tuendelee na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 222

**Uwiano wa Uwepo wa Nyenzo na Ufaulu wa Wanafunzi**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sekondari nyingi hapa nchini hasa zile za Kata hazina nyenzo muhimu kama vile maabara, hosteli, upungufu wa walimu na kadhalika, na kwa kuwa, shule zote nchini hufanya mtihani mmoja bila kujali kama shule inajitosheleza kwa nyenzo muhimu au haina nyenzo:-

Je, Serikali itatenda vipi haki kutokana na ufaulu mbaya au mzuri kwa wanafunzi waliosoma kwenye Sekondari zenye nyenzo duni?

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA -NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa changamoto mbalimbali kwa shule za sekondari nchini, hususani shule zilizojengwa hivi karibuni katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa shule zote za Serikali nchini hufanya mtihani mmoja wa Taifa japokuwa zinakabiliwa na changamoto tofauti. Kwa kutambua hilo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuboresha na kuinua viwango vya ufaulu nchini. Jitihada hizo ni pamoja na:-

Katika mwaka wa 2008 Serikali imepeleka jumla ya vitabu 15,000 vya masomo ya Hisabati, Baiolojia, Kemia, na Fizikia kwa shule za sekondari kwa msaada wa shirika la Marekani (*USAID*) Aidha, katika mwaka 2009/2010 msaada huu utaongezwa mara tano.

Pili, Serikali imeandaa mradi mkubwa wa kujenga na kuweka vifaa vya maabara katika shule zote za sekondari nchini wenye gharama ya dola za Kimarekani 592 milioni. Mradi huu utatekelezwa kwa awamu katika awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MES*). Kukamilishwa kwa mradi huo kutatoa fursa kwa wanafunzi wa sekondari kufaulu masomo ya Sayansi.

Tatu, katika kuhakikisha shule zinakuwa na vifaa vya kufundisha na kujifunzia, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MES*), kila mwaka hutoa ruzuku kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule zote za Sekondari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kutoa elimu bora kwa usawa kwa shule zote za sekondari nchini na kuhakikisha haki inatendeka kwa shule zote za sekondari. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kwa majibu yake mazuri yenye kuonyesha juhudi kubwa ya Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa suala la uhaba wa hosteli haliathiri tu ufaulu wa wanafunzi katika shule za sekondari bali pia linahamasisha suala la kupata mimba kwa watoto wa kike na vilevile kuongeza mdondoko mkubwa shuleni.

Je, Serikali katika kulipa kipaumbele suala hili hapa nchini na kwa Bajeti ya mwaka 2009/2010 imetenga fedha kiasi gani ili kukabiliana na changamoto hii ambayo imekuwa ni tatizo kubwa hapa nchini?

(b) Kwa kuwa, Mkoa wa Manyara ambao una wafugaji wengi, Sekondari nyingi za Kata zimejitahidi kujenga hosteli lakini juhudi za wananchi zimeishia kwenye *lenter*. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuunga mkono juhudi hizi za wananchi, ili kukamilisha ujenzi wa hosteli hizo hasa katika wilaya ya Mbulu ambako kuna Sekondari 24 lakini kuna hosteli moja tu iliyoko katika sekondari ya Haidom?

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA -NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niwataarifu Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai, 2009 shule zote za sekondari na kiasi kikubwa cha fedha kimehamishiwa Serikali za Mitaa kwa Mheshimiwa Mama Celina Kombani. Kwa hiyo, baadhi ya hoja nyingi kama zilichelewa kutolewa wakati ule, basi huku kwetu zikija tutazihamishia huko.

Hata hivyo, naomba nishukuru tu kwamba, Mheshimiwa Martha amekumbushia suala la ujenzi wa hosteli. Ni kweli lakini namuomba yeye mwenyewe kama Mbunge na Mjumbe katika Halmashauri yake, pamoja na Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, tushirikiane kuona namna gani tutawasaidia wananchi hawa kumalizia hiyo kazi waliyoianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amechanganya mambo mengi, mimba na mdondoko. Mimba ni hoja tofauti, na kamwe hosteli haiwezi ikawa dawa ya kuzuia mimba.

Lakini inaweza ikawa kisaidizi kimoja tu nadhani ni vyema sisi kama Waheshimiwa Wabunge humu ndani tukashirikiana kwa pamoja kutafuta suluhu ya kudhibiti hizi mimba. Tutajenga hosteli wanaweza wakafanya mambo mengine, mdondoko ni ukweli kwa sababu kuna umbali kutoka shule zilipojengwa na wanapoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, natambua kwamba wafugaji wengi uhamahama na hivyo uhitaji kubakiza watoto wao wasome na kwamba juhudi kubwa walizoonyesha wananchi kujenga hayo maboma hadi kufikia Mtambapanya.

Bado naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kupitia Halmashauri yake pamoja na Serikali za Mitaa waone namna bora ya kuzimalizia ili watoto wetu waweze kupata elimu ambayo ni haki yao kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata hatuna muda tumalize maswali mawili yaliyobakia. Swali lililobakia la pili kutoka mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Archt. Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, na linaulizwa Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 223

**Kuzalisha Nishati Kwa kutumia Jua Na Upepo**

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na jua la kutosha na upepo mwingi katika baadhi ya maeneo:-

(a) Je, kuna mkakati gani endelevu wa kulitumia jua hilo na upepo huo katika uzalishaji wa nishati?

(b) Kwa nini vifaa vyote vya *solar* visiondolewe kodi kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upepo unaweza kuwa chanzo cha nishati rahisi na isiyoharibu mazingira katika kusukuma maji na pia uzalishaji wa umeme. Kwa muda mrefu, nishati itokanayo na upepo imekuwa ikitumika kwa ajili ya kusukuma pampu za maji katika baadhi ya mikoa hapa nchini. Kitaalamu upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme unahitaji kufanyiwa utafiti wa kina kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja ili kuweza kujua kasi ya upepo na jinsi unavyobadilika kwa kutumia teknolojia za kisasa, kwa lengo la kubaini kasi muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark imewezesha utafiti kwa kupima kasi ya upepo katika maeneo manne nchini. Maeneo hayo ni Gomvu, Mkoani Dar es Salaam, Mkumbara Mkoani Tanga, Litembe Mkoani Mtwara na Karatu Mkoani Arusha. Katika utafiti huu, vituo vya Mkumbara na Karatu vilionyesha kuwa wastani wa kasi ni takribani mita 5 kwa sekunde kwa kutumia mitambo maalum, kasi hii inaweza kuzalisha umeme ingawaje kwa bei ya juu kuliko maeneo yenye kasi ya zaidi ya mita 7 kwa sekunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *TANESCO* inaendelea kusimamia ukusanyaji takwimu za kasi ya upepo hapa nchini. Vituo vya Makambako Mkoani Iringa na Kititimo Mkoani Singida vimeonyesha wastani wa kasi ya upepo wa zaidi ya mita 8 kwa sekunde. Kutokana na matokeo hayo, wawekezaji kadhaa wameonyesha nia ya kufanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kuzalisha umeme wa zaidi ya megawati 50 kutokana na upepo katika maeneo hayo. Uwezekano wa uzalishaji huo umezingatiwa katika mpango kamambe wa uendelezaji umeme 2007-2031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na zoezi la kubaini maeneo yenye kasi ya upepo muafaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Nia ni kufanikisha utengenezaji wa ramani ya upepo kwa nchi nzima, utakaoongeza hamasa ya uwekezaji kwenye nishati ya rasilimali hii.

Mionzi ya jua inaweza kutumika kuzalisha umeme kwa matumizi ya majumbani na katika maeneo ya mbalimbali kama vile vituo vya afya, zahanati, mashule na hata katika vituo vya mawasiliano kwa ajili ya kuendeshea mitambo mbalimbali. Kutokana

na udogo wa soko la nishati ya mionzi ya jua, Serikali inaendesha miradi miwili ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati ya jua hapa nchini. Kuna mradi wa mfano Mwanza na Serikali pia inasimamia mwingine wa umeme wa jua unaofadhiliwa na SIDA (Sweden) ambao umeendeleza kutekelezwa katika Mikoa ya Tanga, Iringa, Morogoro, Kigoma, Pwani, Mtwara na Mbeya.

Aidha, pamoja na juhudi za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali (ASIZE), zinatekeleza baadhi ya miradi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati ya jua nchini. Kwa upande mwingine, Makampuni binafsi kama Umeme Jua, *Rex Investments, Ensol*, RESCO, *Chloride Exide*, Zara, *Aglex*, *GESCO, Swift holdings* na kadhalika tayari wanafanya biashara ya vifaa vya umeme wa jua hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia haya yote tangu mwaka 2005 Serikali iliondoa ushuru wa kuagiza vifaa vya mfumo wa nishati ya jua pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na *Import duty* kwa lengo la kuwezesha wananchi wengi kutumia nishati hiyo.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa anakiri kabisa kwamba huu umeme wa jua unasaidia sana katika kuboresha mazingira na tukizingatia kwamba mazingira yanaharibiwa sana na haya mambo ya kuharibu *horzone layer*. Lakini mpango kabambe wa TANESCO wa mwaka 2007 mpaka 2031 ni muda mrefu, kwa nini Serikali isifanye jitihada za makusudi kabisa katika kuharakisha uzalishaji wa hii nishati ya umeme kupitia hii njia ya upepo?

Swali la pili, pia nimshukuru kwa kukiri kwamba Serikali imeshaondoa ushuru wa aina zote katika vifaa vya umeme nuru *(solar*) na sasa ningeomba kwamba Serikali basi itakuwa tayari kushirikiana na Wizara zinazohusika kwa mfano Wizara ya Afya, Elimu katika kuweka umeme huo wa nuru (*solar*) katika vituo vyetu vya afya ambako umeme haujafika pamoja na kwenye mashule yetu ili watoto wetu waweze kusoma vizuri haya masomo ya Kisayansi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana niombe tu *technical team* mtusaidie naona vipaza sauti vina usumbufu fulani havileti usikivu mzuri. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie kuzingatia hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema utafiti wa upepo kwa kawaida unachukua kama mwaka mmoja hivi kubaini kama upepo ule utakaozalishwa hapo kwa sababu lengo mwisho wa siku ni kuweza kuwapatia wananchi umeme kwa gharama nafuu.

Sasa upepo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba unazalisha umeme nafuu lakini pia ni umeme ambao hauathiri mazingira. Lakini tatizo lake ni kwamba uwekezaji unaupelekea pale kwenye kupata nishati ya umeme wa upepo ni

mkubwa kidogo kwa sababu yale ma-*turbine* na kadhalika. Kwa hiyo kwa kiasi hicho utafiti unaofanywa lazima ubaini kama umeme utakaotokana na uwekezaji huo utaweza kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Fuya Kimbita kwamba utafiti unaendelea na kwa sasa hivi maeneo hayo mawili yameonekana kwamba yana uwezo huo, lakini pia katika namna hiyo Serikali inaendelea kubaini maeneo ambayo upepo unaweza kuzalishwa kwa kiasi kidogo cha upepo kama maeneo ya Mafia na Kilwa ili kubaini kwa maeneo hayo upepo japo wa megawati moja au mbili unaweza kusaidia kwa maeneo hayo kwa kutumia nguvu ya nishati ya upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, la umeme nuru nakubaliana naye kabisa kwa maeneo yaliyo mbali kwa kuwa umeme nuru sio ambao unatoa umeme mwingi mkubwa lakini unafaa katika kuendesha labda zahanati au shule, vi-kompyuta viwili au vitatu na kadhalika ni umeme ambao kusema kweli Serikali tunaufanyia kazi ya kuhamasisha matumizi haya. Isipokuwa lazima tukubali tu kwamba hata katika mazingira ya dunia kwa wenzetu waliotutangulia kidogo katika matumizi haya umeme nuru umefanyiwa utafiti mkubwa lakini bado gharama ya matumizi yake ni mkubwa kidogo kwa sababu lile suala la *panel* na nini kwa kawaida gharama zake ni kubwa.

Lakini kwa kadri utafiti unavyofanya kwa suala hili na sisi tutakwenda nalo sambamba ili kubaini matumizi bora ya umeme nuru katika vituo vya afya na mashule.

Na. 224

**Nishati ya Uranium**

**MHE. MARGARET A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, bei za mafuta zinapanda mara kwa mara duniani hali inayosababisha Mataifa mengine kuona haja ya kutumia nishati mbadala kama “*uranium*”, na kwa kuwa, tafiti zinaonyesha kuwa, kuna sehemu nchini zilizo na madini hayo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalinda wananchi na wafanyakazi katika maeneo yaliyothibitika kuwepo nishati hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2007, kumekuwa na ongezeko kubwa la shughuli za utafutaji wa madini ya *uranium* hapa nchini ambapo Kampuni kubwa za kigeni zinaendelea na shughuli za utafutaji wa madini hayo katika mikoa ya Kusini

*(Ruhuhu Basin, Selous Basin,* Namtumbo na *Mbamba Bay* Mkoa wa Ruvuma) na Kanda ya Kati (Bahi Mkoa wa Dodoma na Manyoni Mkoa wa Singida), ambapo tafiti hizo zinaashiria uwepo wa madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi Mataifa makubwa yamekuwa yanatumia uranium kama chanzo cha nishati ya kuzalisha umeme.

Aidha, kuna baadhi ya nchi zilizo kwenye hatua za juu miongoni mwa nchi zinazoendelea pia zinatumia uranium kuzalisha umeme au ziko kwenye hatua za kukamilisha miradi hiyo husika. Kwa maana hii suala la usalama wa matumizi ya uranium yamefanyiwa kazi ya kina na hatua muhimu zikazingatiwa katika hatua zote za matumizi ya madini haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu kwa sasa haijaanza uchimbaji wala matumizi ya madini hayo kwa uzalishaji wa umeme na matumizi mengine ya viwandani na maabara, Serikali kwa kuzingatia uzoefu wa Mataifa mengine duniani uliopatikana katika usimamizi wa masuala ya uranium kama madini na kama nishati, na kwa wakati muafaka, itaweka mikakati ya kuwalinda wananchi katika maeneo yaliyothibitika kuwepo viashiria vya madini hayo. Hata hivyo, madini hayo hata kama yapo, yapo chini ya ardhi na hayajathibitika kuwa na madhara kwa binadamu katika hali yake hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali imeweka utaratibu wa kuwalinda wananchi wake dhidi ya madhara ya madini hayo kupitia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004; Sheria ya Nguvu ya Atomiki *(Atomic Energy Act, 2004*); Sheria za Afya na Usalama Mahali pa Kazi na Sheria ya Madini ambayo inatarajiwa kuwasilishwa hapa Bungeni baada ya mchakato wake kukamilika.

Kwa maana hiyo basi napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwa ujumla kwamba itakapofika hatua ya kuchimba na kuyatumia madini haya, Serikali itakuwa imechukua hatua zote zinazohitajika kuwalinda wananchi na wafanyakazi wote watakaohusika.

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nashukuru pia Serikali imekiri kwamba kuna maeneo utafiti unaendelea na kwamba wakati muafaka itaweka taratibu zinazohusika. Sasa nataka kufahamu je katika hatua hiyo ya kutafuta utafiti ambao najua kwamba wanachimba vishimo vidogo vidogo ili wapate sampuli ya kuthibitisha kwamba madini hayo yapo au hayapo, je, hawa watu sasa hivi wanalindwalindwaje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya urani hupatikana kwenye mazingira ya kawaida kwenye miamba kama *uranite* ambapo metalia urani inakuwa imeungana na *oxygen*, katika hali hiyo metalia urani haitoi mionzi inayoweza kudhuru binadamu. Ndiyo maana wananchi wa maeneo ya katikati

Dodoma na Kusini Songea, Namtumbo na Lindi mwa Tanzania wanaishi bila ya matatizo yoyote licha ya kuwepo kwa madini ya urani katika ardhi yao siku zote hizo.

Urani inakuwa hatarishi wakati wa matumizi pale ambapo metali ya urani imetenganishwa na *oxygen* wakati huo metalia urani hutoa mionzi ambayo ndiyo yenye madhara kwa binadamu. Sasa hatua hiyo inafikiwa baada ya kufanyiwa *processing* fulani ya hayo madini. Ndiyo maana nikasema kwa kuwa hatua hiyo hawa wawekezaji wa sasa wanatarajia kuifikia, kufikia mwaka 2012/2013 sisi kwa wakati huo tutakuwa tumeshaanza kuweka mikakati ya makusudi kabisa na taratibu za kuwalinda wananchi wanaoishi kwenye mazingira hayo na wale wanaofanyia kazi madini ya urani kuwalinda na madhara ya mionzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nilikuwa napenda kutumia nafasi hii kuongezea majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Mkanga kama ifuatavyo. Sheria ya Madini kwa sasa kama ilivyo na kanuni zake za mwaka 1999 zinamruhusu na kumpa uwezo Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Kamishna wa Madini kuwezesha watafutaji wa madini ya urani kusafirisha sampuli nje ya nchi kwa zile ambazo wanazifanyia uchunguzi kujua kama kuna kiwango gani cha urani katika maeneo ambayo wameona wanayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hivyo tunachofanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba sampuli ambazo sasa hivi wanaendelea kuzifanyia kazi tunawapa kibali kuzipeleka nje kwa ajili ya kujiridhisha kitaalam kwenye maabara ili tuone kama kuna mashapo ya kutosha kwa ajili ya kibiashara, kwa hivi sasa usimamizi unaendelea chini ya mamlaka ambayo yamekabidhiwa kisheria.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya nyongeza na suala zito na la msingi ni usalama pia wa hawa wachimbaji ambao wanasaidia kupatikana kwa hizo sampuli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge naomba mkubali kwamba muda kwa kweli wa maswali umepita sana na tunayo hoja ambayo imewasilishwa leo mezani itatupasa kwa kweli tupate muda wa kuanza hoja hiyo kwa kuwa tutaihitimisha leo, sasa kabla sijaingia kwenye hiyo hoja ninaomba nitoe matangazo ambayo yamenifikia hapa mezani.

Kwanza nimepokea tangazo kwa Wabunge wanaotoka Zanzibar lakini wanasema tangazo lao hili linamlenga sana Mheshimiwa Nsanzugwanko. Wanasema nimpe pole kwa kipigo cha timu ya Kigoma kutokana na ushindi mkubwa sana tena wa kiufundi waliouonyesha wale vijana wa huko Visiwani kwa kuwapiga watoto wa Kigoma. Sasa sijui kama Nsanzugwanko ndio mmiliki wa hiyo timu ya Kigoma, lakini nimeambiwa nikupe pole lakini nadhani pole hiyo imekufikia. (*Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kumpa pole Mheshimwa Nsanzugwanko lakini nadhani na Wabunge wote wa mkoa wa Kigoma tusimwache Mheshimiwa Nsanzugwanko peke yake sasa niwatangazie wageni ambao wamejumuika nasi leo.

Wageni wa Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ni wageni wafuatao. Kwanza kabisa ni mke wake Mama Anna Mkuchika, Mama Anna Mkuchika tunaomba usimame. Karibu sana mama Anna Mkuchika na tunakupongeza kwa kweli Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri tunaamini ni kwa sababu yako wewe ndiyo maana kazi nzuri za Mheshimiwa Mkuchika zinaonekana. Tunakushuru sana. (*Makofi)*

Lakini yuko Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dr. Florence Turuka, tungeomba na yeye asimame. Halafu wako Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa wa Wizara naomba Wakurugenzi na Maafisa wote wasimame. Wako kwenye *Speaker's Gallery* pale mbele. Watu wa *TV* tunaomba mtusaidie kuonyesha wageni wetu kwenye *screen* za Bunge. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea wakati *technical team* inafanya hiyo kazi ni wale waliosimama pale mbele. *(Makofi)*

Halafu kuna Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi zifuatazo *TBC, TICRA, TSN* na *TASUBA,* tungeomba wasimame tafadhali. Tunawashukuru sana kazi zenu ni nzuri na tunaona mnavyotusaidia kujenga nchi yetu.

Halafu Waheshimiwa Wabunge wako Wenyeviti na Makatibu Watendaji Bodi na Mabaraza ya Taasisi hizo chini ya Wizara. Wako hao viongozi kutoka BMT, BASATA, BAKITA na Mfuko wa Utamaduni wa Taifa na TASUBA, naomba na wao wasimame tafadhali. *(Makofi)*

Tunawashukuru sana karibuni sana, karibuni sana na tunawapongeza kwa kazi yenu. Halafu tunao Wajumbe wa Kamati ya Maudhui, tunaomba na wao wasimame. Wako upande wetu wa kulia pale karibuni sana. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, Waziri ametuletea pia Makocha kutoka nchini Cuba wanaofundisha Michezo yetu hapa nchini na hao ni kama ifuatavyo. Yuko Josse Silver, Kocha wa Judo, yuko Andrea Scatis, Kocha wa *athletics*, yuko George Bravo, Kocha wa *athletics* na yeye, yuko Jovan Utador, Kocha wa *boxing*. Tunawashukuru sana karibuni sana na tunawashukuru kwa mafunzo kwa timu zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge vile vile tunaye Rais wa *TFF* Ndugu Leodgar Tenga. Nawashukuru sana kuna watu hapa wanachombeza Yanga sasa sijui maana yake nini. Lakini nadhani tutambue tu huyo ni Rais wa *TFF,* hii habari ya Yanga wanaijua wenyewe. Yuko pia Makamu wa Rais wa *TFF* Ndugu Athumani Nyamlani. Naomba Mheshimiwa Makamu wa Rais wa *TFF* usimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu wako wageni tisa (9) wa Mheshimiwa Balozi Seif Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hawa wageni ni viongozi wa *SACCOS* za Kinduni na Mkadini Jimbo la Kitope. Naomba hawa viongozi wa *SACCOS* wasimame. Wako huku karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru viongozi hawa wa

*SACCOS* kwa kweli wametekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mheshimiwa Lucas Selelii ana wageni wake kama ifuatavyo. Bwana Abdallah Ibazu Diwani wa Kata ya Itobo Nzega, na wewe sasa sijui ni Mtera, Alhaj Mussa, Imam wa Msikiti wa Itobo Nzega na yeye hatujui yuko wapi. Halafu Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi anaye mgeni ambaye ni Kulwa Masasi, Mwenyekiti wa Vijana Kata ya Kamnyonge Musoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Halafu wako wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara kutoka Chama cha Ushirika cha Masasi Mtwara hao ni Bwana Fikiri Mohamed Makarani, Mwenyekiti wa Chama hicho na Bwana Mweli Omega, Katibu wa chama hicho. Ningeomba wasimame pale walipo. Hao wako upande wangu wa kulia. Karibuni sana tunawashukuru kwa kudumisha Ushirika.

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o Mwenyekiti wa *TAPAC* ambao ni hawa wafuatao. Bwana Milisenti Obasso ambaye ni *Country Director* wa *USAID Health Policy Initiatives.* (*Makofi)*

Halafu yuko Sheikh Hassan Kinyisa Omar *Deputy Director* wa *Religious Affair Supreme Council of Kenya Muslims*. Karibu sana. Yuko Rev. Kanon Gedion Gyamugisha yeye ni *Godwill Ambassador* wa *HIV* na *AIDS.*

Halafu Rev. Amina Sandewa yeye ni *National Coordinator for TENELELA*, tunakushukuru. Kuna Bishop James Okombo ambaye ni *National Coordinator for TENELELA.* Ahsante sana. *Bi. Pet Alleman Senior Technical Advisor* wa *USAID Global Health Fellows Programme.* Karibuni sana tunawashukuru.

Halafu tunao wafanyakazi 10 kutoka Asasi ya Kiraia inayotoa msaada wa Kisheria *NORA* ambao wako Dodoma kwa ajili ya Mkutano. *NORA GROUP* karibuni sana. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako Wabunge 32 kutoka Bunge la Wanafunzi *CBE* Dar es Salaamwa na Mwanza wakiongozwa na Spika wa Bunge hilo ambaye ni Julian Assenga, tungeomba kwanza Spika asimame halafu hao Wabunge nao wafuate.

Mheshimiwa Spika tafadhali asimame na sasa ningeomba Wabunge wote msimame kutoka katika hivyo vyuo nilivyovitaja. Karibuni sana Waheshimiwa Wabunge basi na nyie muone Wabunge wenzenu tunafanyaje mambo hapa ndani, karibuni sana na tunawatakia kila la kheri kwenye shughuli zenu za Ubunge, lakini muende tu taratibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu inaniambia kwamba kuna wanafunzi 15 kutoka *Mzumbe University*, tafadhali simameni. Nashukuru sana hii ndiyo orodha ya wageni niliyopewa leo lakini kuna vikao vya kazi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kamati ya Nishati na Madini kuwa leo tarehe 15 Kamati itakuwa na ziara ya kutembelea Ofisi za Wakala wa Jiolojia Tanzania kuanzia saa 8.00 mchana. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mna kazi hiyo leo maalum kupitia kwenye Kamati yenu saa 8.00 mchana.

Halafu Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Mifugo na Maji anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa tarehe 15 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Na. 231 jengo la Utawala saa 7.00 mchana.

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wa Wajumbe wa Kamati hiyo Na. 231 mhudhurie.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Huduma kwa Wabunge anaiomba Kamati ya Maandilizi ya tafrija ikutane saa 10.00 jioni Kantini kwa ajili ya shughuli ya maandalizi ya tarehe 18 Julai, 2009 itakayofanyika katika viwanja vya Bunge. Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo nadhani sasa nimruhusu Katibu aweze kuniongoza kwa shughuli zinazofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
### Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aweze kusoma Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2009/2010, Mheshimiwa Waziri Kapteni George Mkuchika tafadhali karibu uwasilishe hotuba yako.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Asasi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka hai na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu leo. Vile vile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi, kwa imani kubwa kwangu na kwa kuendelea kunisaidia kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, nikiwa Mbunge wa Jimbo la Newala na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Aidha, naendelea kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Newala, kwa kuendelea kunisaida katika utekelezaji wa majukumu yangu kama Mbunge wao. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais, Wananchi wa Newala na Watanzania wote kwamba, nitaendelea kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu kwa faida ya Taifa zima. Vile vile, ninaendelea kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu mpendwa, Anna Ernestina na watoto wangu, kwa uvumilivu wao wa kukosa kuwa nami wakati mwingi ninapokuwa safarini kutekeleza majukumu ya kitaifa. Nawashukuru kwa kunitia moyo na kwa mapenzi yao kwangu. Mungu azidi kuwabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti, ambapo ameeleza kwa ufasaha utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha 2008/2009. Aidha, ameainisha malengo ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Malengo ya Milenia 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na miongozo mingine ya Kitaifa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Napenda pia kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo (Mb), Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake, iliyotupa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Hotuba hiyo imetupatia mwelekeo wa hali ya uchumi na mapato ya Serikali na kuonesha maeneo yaliyopewa kipaumbele katika bajeti na hasa kwa jinsi alivyoshauri namna ya kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani, ambazo zimeathiri au zitaathiri baadhi ya sekta hapa nchini. Wizara yangu tayari imeanza mchakato wa awali wa kubainisha maeneo yanayoathirika na mtikisiko huu, ambapo bajeti ya mwaka huu, imejaribu kuzingatia namna ya kukabiliana na athari hizo. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hotuba za Mawaziri walionitangulia. Maoni ya Wabunge hao, yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali, ikiwemo Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takriban mwaka mmoja na nusu sasa, tangu Rais afanye mabadiliko makubwa ndani ya Serikali mwezi Februari, 2008, kwa kumteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia utendaji makini, uadilifu, unyenyekevu kwa watu wote na ushupavu wa Waziri Mkuu wetu. Katika kipindi hiki, sote tumeona jinsi Mheshimiwa Pinda alivyoshughulikia suala la kubana matumizi ya Serikali kwa kupunguza kwa kiasi kikubwa, idadi ya semina, warsha na makongamano, ambayo hayakuwa na ulazima mkubwa. Sambamba na hili, Serikali kupitia Agizo la Waziri Mkuu, imeratibu ununuaji wa magari kwa lengo la kuhakikisha kuwa, ununuzi wa magari unafanywa pale inapobidi na kwa kibali maalumu.

Aidha, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, natumia fursa hii, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Pinda, kwa kuagiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kutenga fedha katika bajeti ya mwaka wa 2009/2010, kwa ajili ya shughuli za utamaduni, michezo, kuhimiza kilimo cha kisasa cha kutumia matrekta madogo ya kusukuma kwa mikono *(power tiller)* na kuwaagiza viongozi kuwa mfano

bora kwa wananchi kwa kuwataka kila mmoja wao kuwa na shamba la mfano. Vile vile tunapongeza sana juhudi zake za kuendeleza mapambano dhidi ya mauaji ya walemavu wa ngozi (Maalbino).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia niwapongeze Wabunge wapya waliojiunga nasi hivi karibuni katika Bunge hili Tukufu, ambao ni Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Taifa lilipata misiba mikubwa ya Marehemu Chacha Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime; Marehemu Richard Said Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini; Marehemu Vuai Abdallah Khamis, aliyekuwa Mbunge wa Magogoni; Marehemu Faustine Kabuzi Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda na Marehemu Phares Kabuye, aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Natumia fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu hao na vyama walivyokuwa wanaviwakilisha katika Bunge hili. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutumia nafasi hii vilevile, kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa kujadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu, tarehe 02 Juni, 2009. Kadhalika, ninaishukuru Kamati hii kwa kutembelea Taasisi na Miradi mbalimbali inayosimamiwa na Wizara yangu, ikiwa ni pamoja na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hii, yamezingatiwa katika bajeti hii kadiri ilivyowezekana na tutaendelea kuyafanyia kazi maelekezo mengine yaliyobakia na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ina majukumu yafuatayo: Kuandaa Sera za Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo; Kusimamia utekelezaji wa Sera za Habari, Utamaduni na Michezo; Kuandaa Mipango ya ukuaji wa Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo; Kuhamasisha uanzishwaji wa vyombo vya Habari katika maeneo ambayo hayavutii sekta binafsi; Kukuza na kuimarisha fani mbalimbali za utamaduni nchini, hususan sanaa za maonesho, filamu, muziki na sanaa za ufundi wa mikono kama kielelezo cha utaifa na chanzo cha ajira; Kuenzi kazi zilizotia fora katika Sekta ya Utamaduni; Kuimarisha na kukuza Kiswahili na matumizi ya lugha za asili ambazo ni vijenzi vya lugha hiyo na kutoa mafunzo ya lugha za kigeni kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa; Kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo nchini; Kukuza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika fani za habari, utamaduni na michezo; Kuandaa na kusimamia viwango na ubora wa kazi za Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo; Kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo; na Kusimamia Maendeleo ya Watumishi katika Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara yangu ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 313,451,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2009, jumla ya shilingi 607,581,059 zilikuwa zimekusanywa, ambazo ni sawa na asilimia 194 ya lengo la makusanyo ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi 12,428,716,200 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo zilijumuisha mishahara ya Wizara shilingi 1,505,474,300; Mishahara ya Taasisi shilingi 2,824,747,000; Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara shilingi 3,618,494,900; na Matumizi Mengineyo (OC) ya Taasisi shilingi 4,480,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Juni, 2009, jumla ya shilingi 12,223,779,200 zilikuwa zimetolewa na kutumika, ambazo ni sawa na asilimia 98 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara yangu ilitengewa jumla ya shilingi 9,929,221,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi 10 ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 9,279,221,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 650,000,000 ni fedha za nje. Hadi mwezi Juni, 2009 jumla ya shilingi 6,233,565,000 zilikuwa zimetolewa na kutumika, ikiwa shilingi 5,700,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 533,565,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara imeendelea kutekeleza Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025, pamoja na Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, ambayo ni kuwa na Taifa lenye raia wenye ufahamu, linalothamini utamaduni wake na lenye wananchi mahiri katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viashiria vya mafanikio haya ni pamoja na:-

- Kuanza kutumika kwa Uwanja wa Taifa, ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Hu Jintao, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, mwezi Februari, 2009.

- Kuendelea kupanda kwa kiwango cha mpira wa miguu nchini na kuiwezesha Timu ya Taifa kucheza katika robo fainali ya mashindano ya CHAN huko Ivory Coast mwezi Februari, 2009, baada ya kutoshiriki katika fainali hizo kwa kipindi kirefu cha miaka ishirini na tisa.

- Kuongezeka, kuimarika na kukamilika kwa miundombinu ya Sekta za Habari, Utamaduni na Michezo hususan Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa).

- Kuongezeka kwa watumiaji wa Tovuti ya Wananchi na kuanza kutumika kwa Maktaba ya Kisasa ya Picha.

- Kuendelea kusimamia maadili katika vyombo vya habari kupitia Sera na Sheria za Sekta ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ndiye Msemaji Mkuu wa Serikali kupitia Idara ya Habari (MAELEZO). Wizara kama Msemaji Mkuu wa Serikali, hufanya kazi zifuatazo: Kukusanya na kusambaza taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu shughuli za Serikali kote nchini; Kusimamia Tovuti ya Wananchi ambayo pamoja na mambo mengine, inawawezesha wananchi kuwasiliana moja kwa moja na serikali yao; Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji; Kusimamia shughuli za vyombo vya habari; Kuratibu maombi ya wanahabari wa nje wanaotaka kuja kufanya kazi Tanzania kwa vipindi mbalimbali; na kusajili magazeti na majarida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mchango mkubwa unaotolewa na Sekta ya Habari, hususan na vyombo vya habari katika maendeleo ya jamii, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 - 2010, Wizara yangu imepewa jukumu la kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari kwa mujibu wa sheria. Katika kutekeleza jukumu hilo, mchakato wa kupitia upya Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003, umeanza tangu mwaka 2008. Mkutano wa kwanza wa wadau wa Sekta ya Habari, ulifanyika tarehe 28 Mei, 2009 ili kupata maoni kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sera hiyo. Mchakato wa marekebisho ya Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003 unaendelea ili Sera hiyo iweze kuendana na mazingira ya sasa ya kisiasa, mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa vyombo vya habari katika maendeleo ya nchi yetu, mchakato wa kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari umeanza. Mchakato huo upo katika hatua ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Tunaamini kuwa, Baraza litaridhia pendekezo hili ili Muswada wa Sheria hiyo uweze kuletwa katika Bunge lako Tukufu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Habari na Utangazaji, pamoja na mambo mengine, ina lengo la kuhakikisha kuwa, wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kutoa maoni kwa uhuru katika masuala yanayowahusu. Ni kwa msingi huu, Serikali imeanzisha Tovuti ya Wananchi ili kuleta mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Wananchi na Serikali yao. Tovuti hiyo ilianzishwa na Serikali kwa madhumuni ya kuwa chombo kitakachowawezesha wananchi na serikali kuwasiliana moja kwa moja; kuwawezesha Raia wa Tanzania popote walipo duniani, kuwasilisha hoja zao, maoni na malalamiko yao serikalini kwa kutumia mtandao wa intaneti na simu za mkononi; na kuiwezesha serikali kurudisha majibu na kutoa maelezo ya kina, kuhusu hoja zilizowasilishwa kutoka kwa wananchi kwa kupitia njia hizo hizo (intaneti, ujumbe mfupi “SMS”).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tovuti hii inaiwezesha Serikali kupata maoni ya wananchi kuhusu huduma wanazopatiwa na Watumishi wa Umma na kutafuta njia muafaka za kuboresha huduma hizo. Tangu Tovuti ya Wananchi ianze kutumika mwaka

2008, Serikali imepokea hoja za wananchi zipatazo 51,471. Hoja zilizokwisha shughulikiwa ni 27,584. Hoja ambazo hazihusiani na kazi za serikali zilikuwa 23,887. Uanzishwaji wa Tovuti hiyo pia umeanzisha mtandao wa mawasiliano kati ya Idara ya Habari (MAELEZO) na Vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano vya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali katika jitihada za kuimarisha utendaji, uwajibikaji na uwazi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukabiliana na changamoto ya kujibu hoja za wananchi haraka na kwa ufasaha na hivyo kutatua matatizo yanayowakabili wananchi. Hii ni pamoja na kuzihamasisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na wadau wengine, kujibu hoja za wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa habari ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine. Ili mtu aingie katika taaluma yoyote ile, pamoja na sifa nyingine, lazima awe na kiwango cha elimu kinachokubalika kuingia katika taaluma hiyo. Waandishi wa habari ni vivyo hivyo. Mwandishi wa Habari ni yule ambaye amepata mafunzo ya kitaaluma na maadili ya namna ya kukusanya na kutayarisha habari na taarifa kwa matumizi ya vyombo vya habari na anayetegemea kazi hiyo ili kuweza kumudu maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma hiyo hutolewa kwa waandishi wa habari wanaofanya kazi za kukusanya habari kwa kuandika, kurekodi, kupiga picha au kutangaza matukio hai *(Live Broadcasts),* kuhariri habari, kusanifu habari, kuandika makala, kutayarisha vipindi na kuchora katuni. Mafunzo kwa waandishi wa habari ni muhimu sana ili kuwawezesha kuzingatia maadili ya taaluma yao, ambayo ni Ukweli na Usahihi wa habari, kutenda haki, kuwa waadilifu na kuwa huru wakati wa shughuli za kutafuta na kuandika habari. Hivyo, mafunzo ya uandishi wa habari ni muhimu ili habari zitolewe na watu waliobobea katika taaluma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika maendeleo ya nchi, Serikali mwaka 2006, iliahidi kuanzisha Programu Maalum ya Mafunzo kwa Waandishi wa Habari ndani na nje ya nchi ili kuwainua kitaaluma na kuwawezesha kubobea kwenye nyanja mbalimbali kama vile Uchumi, Sheria, Uhasibu, Kilimo, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu hiyo haijaanza kwa sababu imependekezwa iwekwe katika Muswada wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari. Mapendekezo ya Muswada huo hivi sasa yako tayari kujadiliwa na Baraza la Mawaziri (BLM). Hata hivyo, kwa kutambua mabadiliko na umuhimu wa kujenga uwezo wa kitaaluma katika Sekta ya Habari, vyombo vya habari vimeendelea kutoa fursa za mafunzo kwa wanahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwaka jana wakati nawasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Wizara yangu imehifadhi hazina kubwa ya picha za viongozi mbalimbali wa serikali waliopo na waliostaafu au kufariki dunia na matukio mengine muhimu tokea enzi za Ukoloni wa Waingereza. Picha hizo zilianza kuhifadhiwa tokea mwaka 1948, katika hali ya karatasi na *negatives*. Kutokana

na mabadiliko ya teknolojia na umuhimu wa kuhifadhi picha kama kumbukumbu ya historia na utamaduni wetu, Wizara yangu ilianzisha Mradi wa Kubadilisha Mfumo wa Uhifadhi wa Picha hizo ili kuwa katika mfumo wa dijitali. Mradi huo ulianza mwaka 2006/2007 na hadi mwezi Juni, 2009 picha zipatazo 2,000,000 zimewekwa katika mfumo wa dijitali. Mradi huu unaifanya Serikali kuwa na maktaba mpya na ya kisasa ya picha na mfumo mzuri wa kuhifadhi nyaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), limetimiza mwaka mmoja na robo tangu lilipobadilishwa na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, mwezi Machi, 2008. Mabadiliko hayo yalilifanya liwe Shirika la Utangazaji wa Umma likiwa na jukumu la kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha Umma wa Tanzania kwa njia ya redio na televisheni. Aidha, Shirika limefanya mabadiliko makubwa katika utendaji wake, ikiwa ni pamoja na kuboresha vipindi vyake, kuongeza usikivu wa matangazo yake sehemu kubwa zaidi ya nchi na kutafuta vyanzo zaidi vya mapato ili kukidhi mahitaji yake katika kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa na TBC katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/09, imeanza kutekelezwa. Kutokana na fedha za bajeti ya maendeleo, TBC imeanza na inatarajia kukamilisha ufungaji wa mitambo ya Televisheni Mkoani Singida na Redio ya FM Mikoa ya Singida, Lindi na Rukwa. Mradi wa Singida unatarajia kukamilika ifikapo mwezi Oktoba, 2009. Vituo vya Redio vya FM vya Mjini Lindi na Sumbawanga, vinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Mradi wa Kukarabati Studio za Televisheni za TBC1 umekwishaanza kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2009. Ukarabati huu mkubwa wa studio hizi ni wa kwanza tangu mitambo katika studio hiyo ifungwe mwaka 1999 na unatarajiwa kuboresha matangazo ya televisheni kwa kiwango kikubwa na kuifanya iwe ya kisasa. Pia ukarabati wa mtambo wa urushaji matangazo kwa OB-VAN unafanywa na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2009. Kukamilika kwa ukarabati huo kutaboresha matangazo ya moja kwa moja kutoka nje ya studio kila inapotakiwa kufanya matangazo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utendaji wa siku hadi siku, TBC imeboresha na kuimarisha matangazo yake ya redio idhaa za TBC Taifa, TBC FM na TBC International. TBC Taifa imeongeza muda wa matangazo na hivi sasa idhaa hiyo inatangaza kwa muda wa saa 24 kila siku. Vipindi vya elimu kwa umma, habari na matukio vimeboreshwa sana hadi kuzifanya idhaa za TBC kwenye redio na televisheni kushika namba moja kwa usikivu na ubora kwa nchi nzima kwa mwaka huu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa juhudi inazozifanya ili kuwezesha TBC kupata udhamini wa Serikali katika kukamilisha ujenzi, ukarabati katika majengo yaliyoko Makao Makuu, Barabara ya Nyerere, Dar es Salaam na ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya TBC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya Mwaka 2003, sehemu ya IV, inaruhusu kuanzishwa kwa Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ambayo Wajumbe wake wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Utangazaji, baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008, kwa mamlaka niliyopewa na Sheria hiyo, niliwateua Wajumbe wanne kuunda Kamati ya Maudhui. Wajumbe hao Mama Maria Kashonda, Bwana Walter Bgoya, Dkt. Wilbard Lorri na Dkt. Amos Mwakilasa, watakaokuwa chini ya Uenyekiti wa Dkt. Suleiman Juma Omar, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Kamati hii itafanya kazi kwa muda wa miaka minne. Majukumu ya Kamati hii ni Kumshauri Waziri kuhusu Sera ya Utangazaji; Kufuatilia na kudhibiti maudhui potofu ya utangazaji; Kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya utangazaji; na kushughulikia malalamiko yatokanayo na utangazaji na maudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Kamati hii mpya ianze kazi mwezi Novemba, 2008, jumla ya mashauri matatu yanayohusu upotoshaji wa maadili ya utangazaji yamewasilishwa na kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Sekta ya Utangazaji imeendelea kukua. Katika kipindi hiki, wawekezaji wengi zaidi walijitokeza kuomba leseni za utangazaji kwa vituo vya redio na televisheni, hasa wale walioko katika maeneo ya nje ya Miji Mikuu ya Mikoa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka imepokea maombi mapya 26 kwa ajili ya leseni za redio na televisheni, ambayo yanafanyiwa kazi pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vingine 31. Hadi mwezi Juni, 2009, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetoa leseni kwa vituo 53 vya redio na vituo 28 vya televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza utangazaji nchini, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

- Imefanya Mkutano Mkuu wa Watangazaji nchini na watayarishaji wa vipindi wa kujitegemea kuhamasisha ukuzaji na uboreshaji wa maudhui ya ndani;

- Imefanya mikutano mitano ya wadau katika mchakato wa kuhama kutoka teknolojia ya Utangazaji kwa mfumo wa analojia kwenda mfumo wa dijitali. Mikutano hiyo ilihudhuriwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kamati ya Kiufundi ya Utangazaji kwa mfumo wa dijitali, Shirika la Utangazaji Zanzibar na Kamati za kushughulikia masuala ya uhamaji wa mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda dijitali za nchi za Afrika Mashariki;

- Mamlaka kupitia Kamati yake ya Maudhui imesikiliza malalamiko ya wananchi na wadau mbalimbali kuhusiana na ukiukwaji wa maudhui uliofanywa na vituo mbalimbali vya utangazaji; na

- Mamlaka imesajili vituo vya redio 128, vituo vya TV 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utangazaji nchini Tanzania, bado inakabiliwa na changamoto nyingi; moja ya changamoto hizo ni ile ya kutakiwa kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa sasa wa kutumia teknolojia ya analojia kwenda dijitali. Kwa mujibu wa makubaliano ya Nchi Wanachama wa Shirika la Mawasiliano Duniani, uhamaji kutoka teknolojia ya analojia kwenda dijitali unatakiwa uwe umekamilika ifikapo mwaka 2015. Mchakato wa kubadili mfumo unaendelea vizuri na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) sasa inachambua maombi ya makampuni yatakayojihusisha na usambazaji na urushaji wa matangazo. Makampuni haya yanajulikana kwa jina la kitaalamu kama *Multiplex Operator*. Jumla ya Makampuni sita yalijitokeza kuomba leseni ya urushaji matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendana na mabadiliko haya, Shirika la Utangazaji linakamilisha taratibu chache zilizobaki ili liweze kuanza utumiaji wa teknolojia ya dijitali katika utangazaji wa vipindi vyake sambamba na ile ya analojia. Kuanza utangazaji kwa kutumia mfumo wa dijitali na analojia kwa pamoja kwa wakati huu wa mpito, kutatoa mwanya wa kupanuka kwa mtandao wa dijitali na kuhakikisha kuwa, wananchi wanaotumia vifaa visivyo na uwezo wa kunasa mawimbi ya dijitali, wanaendelea kupata huduma ya vyombo vya habari hadi hapo watakapoweza kubadili vyombo vinavyoweza kunasa matangazo kwa mfumo wa dijitali au hadi pale matangazo katika mfumo wa analojia yatakapokoma mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), ilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni (Cap. 212) ya mwaka 1961. Wamiliki wa Kampuni hii ni Serikali ya Tanzania, yenye asilimia 99 na asilimia moja inamilikiwa na Mhariri Mtendaji. Kampuni inaendeshwa kwa kuzingatia malengo yaliyoainishwa katika mpango mkakati wa miaka mitano. Mpango wa kwanza ulijumuisha kipindi cha kuanzia 2004 - 2008 na Kampuni imeanza kutekeleza mpango mwingine unaoanzia mwaka 2009 hadi 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kampuni imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendelea kuchapisha Gazeti la HabariLeo lililozinduliwa mwezi Desemba, 2006 na linapendwa na wasomaji na wenye matangazo mbalimbali.

- Kujenga uwezo wa watumishi na hivyo kuwa na watalaamu wenye ujuzi na uzoefu katika Sekta ya Habari, mazingira bora zaidi ya kufanyia kazi, mtandao mpana wa usambazaji magazeti hadi katika ngazi ya wilaya.

- Kufungua Ofisi Zanzibar, Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Mashariki (Morogoro) na Kanda ya Pwani (Tanga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina wajibu wa kukuza, kuendeleza na kueneza utamaduni. Aidha, sanaa hutoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuunganisha wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

- Kudurusu Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 ambapo vikao mbalimbali vya wadau wa ndani vimefanyika na rasimu ya Sera iliyodurusiwa imekwishapatikana. Hatua inayofuata ni kuitisha kikao cha wadau wa nje ili kujadili rasimu kabla ya kuandaa na kuwasilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri.

- Kuratibu na kuwezesha maonesho ya kazi za mikono kwa wasanii na wajasiriamali yaliyofanyika katika vituo viwili vya Same Mkoani Kilimanjaro na Lushoto katika Mkoa wa Tanga. Jumla ya Wasanii 60 walishiriki katika maonesho, ambapo kila kituo kilikuwa na wasanii 30.

- Wasanii 13 na walimu wawili walishiriki katika Tamasha la Muziki wa Asili na Ngoma za Asili nchini Namibia mwezi Agosti, 2008, ikiwa ni mwendelezo wa shughuli za utamaduni zilizofanyika nchini Afrika Kusini.

- Tamasha la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania lilifanyika mwezi Oktoba, 2008 ambapo vikundi vya ndani kutoka Dar es Salaam, Manyara, Dodoma, Singida, Mwanza na Pwani vilishiriki. Vikundi vya nje ya nchi vilivyoshiriki ni kutoka Kenya, Uganda, Ethiopia, Afrika Kusini, Zimbabwe, Zambia, Rwanda, Norway, Sweden, Italia na Japan.

- Imeandaa mikutano mbalimbali ya wadau ili kuanza kutekeleza Programu ya Kuhifadhi Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kufuatia kuridhiwa kwa Programu hiyo na Baraza la Mawaziri na Baraza la Mawaziri wa Utamaduni Afrika.

- Wiki ya Mfuko wa Utamaduni Tanzania ilifanyika mwezi Juni, 2009 Mjini Bagamoyo. Wiki hii ilijumuisha maonesho ya kazi za mikono, jukwaani na utoaji wa Tuzo ya Zeze. Aidha, Mfuko wa Utamaduni Tanzania, ulitambua kazi bora na kuwaenzi wadau sita waliotia fora kwa kazi zao katika Sekta ya Utamaduni.

- Mkutano Mkuu wa sita wa Sekta ya Utamaduni ulifanyika Mjini Morogoro mwezi Desemba, 2008 ambapo jumla ya wadau 250 walishiriki, wengi wao wakiwa Maafisa Utamaduni katika Halmashauri mbalimbali.

- Maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Duniani yalifanyika Kitaifa Mkoani Ruvuma mwezi Mei, 2009.
- Vipindi 52 vya Lugha ya Taifa, vipindi 52 vya Kumepambazuka, katika redio na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili katika Televisheni viliandaliwa na kurushwa. Vipindi hivyo vimekuwa msaada mkubwa kwa wananchi katika kuelewa

maana, matumizi na maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla. Aidha, vipindi hivi vimesaidia kurekebisha upotoshaji wa Lugha ya Kiswahili.

- Jumla ya istilahi 200 na orodha ya makosa ya matumizi ya maneno 104, pamoja na usahihi wake, vilisambazwa kwenye Idhaa za Kiswahili 89 za ndani na nje ya nchi katika kutekeleza maazimio ya Kongamano la Kimataifa la Idhaa za Kiswahili Duniani lililofanyika mwezi Novemba, 2007 Jijini Dar es Salaam.

- Mafunzo ya maadili ya filamu kwa wadau wa filamu yalitolewa kwa njia ya mikutano, semina, warsha, vipeperushi na magazeti. Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza imetoa semina kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Mafunzo kwa Maafisa Utamaduni. Aidha, imetoa nakala za Sheria Na. 4 ya Mwaka 1976, vipeperushi zaidi ya 300 kwa Wadau mbalimbali katika Wiki ya Utumishi wa Umma na katika Mkutano wa Wadau wa Filamu.

- Wizara iliteua shule tano za msingi, Walimu 10 na Wanafunzi 75 katika Mkoa wa Morogoro na kuendesha mafunzo ili kuibua vipaji na ubunifu wa mbinu za uigizaji na mbinu za kutumia sanaa katika kufundishia masomo.

- Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), liliendeleza na kukuza vipaji kwa wasanii 560. Mafunzo yalifanyika katika Mikoa ya Ruvuma (Wilaya ya Tunduru), Tanga (Manispaa), Tabora (Manispaa), Dar es Salaam (Ilala na Kinondoni) na Dodoma (Chamwino).

- Wasanii 124 na wajasiriamali 19 wanawake kutoka Mikoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam wa sanaa za ufundi walitambuliwa na kushiriki katika mafunzo ya sanaa za ufundi yaliyoratibiwa na BASATA na kuendeshwa na *The Great Lake Consortium for International Training and Development [GLC] na The Arts Council Lake Erie West [ACLEW]* kutoka Marekani.

- Wasanii na wadau wa muziki 128 walipewa mafunzo ya muziki katika Ofisi za BASATA, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho hicho, Wizara pia ilitekeleza yafuatayo:-

- Kufanya utafiti wa lugha za asili ili kubaini maneno yanayoweza kutumika katika Kiswahili badala ya yale yanayotatanisha ulifanyika katika Mikoa ya Mwanza, Ruvuma na Singida.

- Maonesho ya Vitabu vya Kiswahili yalifanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Machi, 2009 ambapo wanafunzi kutoka katika Shule za Msingi 11 na za Sekondari 13 za Jijini Dar es Salaam walishiriki katika usomaji wa vitabu. Aidha, Wachapishaji tisa wa Vitabu walishiriki katika maonesho hayo.

- Ilishiriki Mkutano wa Kwanza wa Umoja wa Afrika unaohusu Mitaala, Usomaji na Maendeleo ya Sekta ya Vitabu uliofanyika mwezi Machi, 2009 Jijini Dar es Salaam.

- Ilifanya Marekebisho ya Waraka wa Kuanzishwa kwa Itifaki ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili hatimaye kuweza kuridhiwa na Baraza la Mawaziri.

- Ilishiriki kwenye Baraza la Sekta ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, Utamaduni na Michezo ya Afrika Mashariki mwezi Aprili, 2009 Jijini Dar es Salaam.

- Iliandaa na kufanya Warsha ya Utafiti kwa ajili ya kujenga uwezo wa Maafisa Utamaduni mbinu za kufanya utafiti katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha Mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa.

- Ilifanya Utafiti wa Mila na Desturi katika Mikoa ya Shinyanga, Kilimanjaro na Kigoma.

- Imeboresha kituo cha kuhifadhi kumbukumbu kwa kutumia Wataalamu kutoka Nyaraka za Taifa kwa kuweka zana za kisasa za kuhifadhia kumbukumbu.

- Imeandaa michoro ya awali ya Jumba la Utamaduni ambayo imejadiliwa na kupata maoni kutoka kwa wadau. Kazi ya uthamini wa ardhi, mazao na mali zilizoko katika eneo la barabara kutoka barabara kuu ya Bagamoyo kwenda eneo la Mradi wa Jumba la Utamaduni (Kiromo) ili kukamilisha mchakato wa malipo ya fidia kwa wahusika wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, lilipanga na kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kusoma na kutoa ithibati kwa Miswada ya vitabu 60 vya taaluma mbalimbali.

- Kutafsiri hati mbalimbali za bidhaa zinazopitishwa katika bandari zetu pamoja na vyeti vya shule, ndoa, kuzaliwa na hati za talaka. Aidha, makala ndefu kama vile Kanuni za Utumishi, Katiba za Vyama na Sera za Serikali, vimefasiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

- Kutoa na kuratibu upatikanaji wa wakalimani wa Kireno na wafasiri wa Kiingereza na pia kuratibu upatikanaji wa wataalamu hao kwa ushirikiano wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ajili ya mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya Umoja wa Afrika, iliyofanyika Sharm El-Sheikh, Misri; Addis Ababa; Ethiopia na Mikutano ya Bunge la Afrika iliyofanyika Afrika Kusini.

- Kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho. Jumla ya makosa 220 yalibainishwa na kuorodheshwa pamoja na usahihi wake. Makosa hayo yameorodheshwa katika mfululizo wa makala za “Zingatia Matumizi Sahihi ya Kiswahili” ambayo yatachapishwa katika Kitabu cha “Makosa ya Kawaida Katika Kiswahili” kwa ajili ya matumizi ya umma.

- Kuhariri na kuweka urari wa matumizi ya lugha katika matini za programu za kompyuta kwa ajili ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Ushirikiano na Kampuni ya *Microsoft*. Jumla ya istilahi 1,958 zilipokelewa na visawe vyake vilisanifiwa. Kazi hiyo ilikamilika na ripoti kuwasilishwa kwenye Kampuni ya *Microsoft*.

- Kufanya uhariri wa kitabu cha Kiswahili kwa wageni: ‘’Furahia Kiswahili Hatua ya Kwanza”. Jumla ya masomo 20 yalihakikiwa. Hatua inayofuata itahusu uchoraji wa picha na vielelezo vingine takriban 30, pamoja na uandaaji wa sherehe (*Glossary*) ya Kiswahili/Kiingereza na Kiingereza/Kiswahili.

- Kukamilisha Kitabu cha Mwongozo wa Waandishi wa Kiswahili Sanifu na kupeleka Muswada Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili uthibitishwe na Kamati ya Elimu ya Kutathmini Vitabu kabla ya kuchapishwa kwa matumizi ya shule.

- Muswada wa Kamusi wenye istilahi 1,400 katika uwanja wa diplomasia na ushirikiano wa kimataifa umeandaliwa. Lengo la Kamusi hii ni kuwasaidia wafasiri na wakalimani wanaotoa huduma katika Vikao vya Umoja wa Afrika na pia kurahisisha kazi za wanadiplomasia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, lilitekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuhuisha Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 ya kuundwa Baraza.

- Kuendeleza ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonesho na Mafunzo ya Sanaa.

- Kuanzisha majadiliano na Shirika linaloshughulika na Hakimiliki na Hakishiriki Duniani (*World Intellectual Property Organisation* (WIPO)) ili kushirikiana katika utafiti wa sanaa za jadi hapa nchini.

- Kuanzisha mchakato wa kutafiti mchango wa sanaa katika Pato la Taifa, kuandaa rasimu ya kuunda vyama vya sanaa vyenye sura ya Kitaifa kwa lengo la kuimarisha utawala bora katika maendeleo ya sanaa nchini, uhakiki wa usajili wa wasanii na wote wanaojishughulisha na kazi za sanaa na kuzitambua kumbi za maonesho ya sanaa na burudani.

- Kushirikisha Watumishi katika mafunzo ya Elimu ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ilitekeleza yafuatayo:-

- Imekamilisha rasimu ya awali ya marekebisho ya Sheria Na.4 ya mwaka 1976 baada ya kupitiwa na wadau wa ndani na nje.

- Ilikagua filamu na kanda za video 385 katika Mkoa wa Dar es Salaam.
- Ilifanya utafiti kuhusu vibanda vya filamu vilivyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo imebainika kuwa kuna zaidi ya vibanda 750 vinavyotumika.

- Ilikusanya takwimu za kumbi za maonesho ya filamu, maktaba na maduka ya filamu katika mikoa minane.

- Ilisimamia mchakato wa kuundwa kwa umoja wa wadau wa Filamu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009 , ilitekeleza yafuatayo:-

- Ilidahili wanafunzi 121 kwa ajili ya kujiunga na mafunzo ya stashahada.

- Ilidahili washiriki 100 kwa ajili ya kujiunga na mafunzo ya muda mfupi.

- Imehifadhi ngoma na miziki 30 ya jamii 15 za Kitanzania katika Kituo cha Utafiti na Uhifadhi.

- Imeratibu Tamasha la 27 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania.

- Imekamilisha Ujenzi wa Ukumbi wa Maonesho na ukumbi huo umefunguliwa rasmi mwezi Oktoba, 2008. Aidha, imekamilisha ujenzi wa mabweni matatu na nyumba moja ya Mtendaji Mkuu.

- Imekamilisha michoro ya jengo la utawala, mabweni mawili na majengo mengine mawili yanayokusudiwa kuwa vitega uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni Tanzania (MFUKO) katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, ulitekeleza yafuatayo:-

- Umefadhili miradi 21 iliyolenga kuboresha shughuli za vikundi na kuleta ufanisi katika shughuli za utamaduni.

- Umepitia na kurekebisha Hati ya Udhamini ambayo inatarajiwa kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2009/2010. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha MFUKO ili kupunguza athari za utegemezi wa ufadhili wa nje.

- Uliratibu Wiki ya MFUKO iliyofanyika mwezi Juni, 2009 ambayo ilitoa ufahamu wa umuhimu wa utamaduni. Pia, MFUKO ulisambaza sera, kalenda na vipeperushi katika Wilaya zote nchini, Balozi za Tanzania nje ya nchi, Wizara, Viongozi wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge.

- Tuzo ya Zeze ambayo hutambua kazi na huduma za wadau waliotoa mchango mkubwa kwenye shughuli za utamaduni ilitolewa kwa watunukiwa sita wakati wa Wiki ya MFUKO.

- Ulifanya ziara katika nchi mbalimbali zikiwemo Afrika Kusini, Ghana, Uholanzi na Ethiopia kwa nia ya kujenga ushirikiano na kujifunza mbinu za kuendeleza shughuli za MFUKO.

- Ulikamilisha mchakato wa kuanzisha Chuo cha Muziki wa Taarab Asilia. Kazi inayoendelea ni kuongeza vifaa na kuboresha studio.

- Kufanya Utafiti wa awali na mawasiliano kati ya MFUKO na Asasi inayokuza vipaji vya asili vya wanawake wa vijijini iliyoko Swaziland ili kuanzisha mpango huo hapa Tanzania.

- Katika kukuza taaluma ya useketaji wa nguo, mawasiliano na wataalamu kati ya Ghana na Tanzania yamefanyika ili kuweza kuijengea taaluma hii mazingira ya tasnia za utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo katika Sekta ya Michezo:-

- Iliratibu ukamilishaji wa ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo ambapo awamu ya kwanza iliyohusu ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wenye uwezo wa kuchukua watu 60,000 umekamilika kwa asilimia 100. Uwanja huo ulizinduliwa mwezi Februari, 2009 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Mheshimiwa Hu Jintao, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China.

- Imekamilisha taarifa za ujenzi wa uzio wa Eneo Changamani la Michezo ambapo ujenzi huo unatarajia kuanza katika mwaka wa fedha 2009/2010.
- Imeanzisha mchakato wa awamu ya pili ya ujenzi wa Eneo Changamani ili kupata mjenzi kwa utaratibu wa Jenga, Miliki, Hamisha *(Build Operate and Transfer (BOT))* na kuendelea kutunza na kukarabati Uwanja wa Uhuru ili kukidhi mahitaji ya wadau.

- Imeendesha mafunzo ya utunzaji wa viwanja vya michezo kwa mameneja na kufanya tathmini ya viwanja 13 katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Morogoro, Mtwara, Lindi, Tanga, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Dodoma na Singida.

- Iliratibu na kusimamia Sherehe za Siku ya Michezo Tanzania zilizofanyika Kitaifa tarehe 19 – 21 Septemba, 2008 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam. Jumla ya Vyama 20 vya Michezo vilishiriki katika maadhimisho hayo na kuonesha baadhi ya kazi zao na kuhudhuriwa na zaidi ya watu 3,000. Aidha, Mikoa ya Dodoma, Tanga, Mtwara na Kigoma, iliadhimisha Siku ya Michezo Tanzania katika mikoa yao.

- Iliratibu na kugharimia ushiriki wa Timu za Tanzania katika Michezo ya Olimpiki na Paralimpiki yaliyofanyika huko Beijing – China mwezi Agosti na Septemba, 2009. Jumla ya wachezaji 11 walishiriki katika michezo ya riadha, kuogelea na kunyanyua vitu vizito kwa watu wenye ulemavu wa viungo.

- Imewezesha kupatikana kwa wataalam/walimu wanne wa michezo kutoka Cuba katika fani za riadha, ngumi na mipango katika michezo. Tunaamini kuwa wataalamu hao watatumika vyema katika fani hizo na hatimaye kuleta maendeleo katika sekta ya michezo kwa ujumla wake.

- Mafunzo ya Tiba kwa Wanamichezo yalifanyika katika vituo vya michezo vya Songea, Arusha na Dar es Salaam. Jumla ya Madaktari wa Tiba ya Wanamichezo 160 walishiriki katika mafunzo.

- Imeendesha mafunzo ya ufundishaji michezo ngazi ya stashahada katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Jumla ya washiriki 34 wamehitimu mafunzo katika ufundishaji wa michezo ya mpira wa miguu, netiboli, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, mpira wa mikono na riadha na wengine 24 wanaendelea na mafunzo.

- Ilisajili Vyama vya Michezo 138 ikiwa ni pamoja na kudurusu Katiba za Vyama vya Michezo 173. Aidha, iliendesha mafunzo ya usajili na Utawala Bora kwa Wasajili Wasaidizi wa Wilaya 18 za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizofanywa au kuratibiwa na Wizara yangu katika kuendeleza Sekta ya Michezo ni pamoja na:-

- Kukamilisha ujenzi wa Jumba la Michezo ya ndani kwa asilimia 90 na kuanza mchakato wa ujenzi wa hosteli katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

- Mashindano ya Kombe la Taifa ya Mpira wa Miguu yalifanyika kwa ufanisi mkubwa kwa mwaka wa tatu mfululizo ambapo jumla ya mikoa 23 ilishiriki mashindano hayo na Mkoa wa Ilala (kimashindano) kuchukua ubingwa kwa mwaka 2009.

- Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (Taifa Stars) ilifuzu na kushiriki katika fainali za mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani (CHAN) na kupata nafasi ya tano kati ya nchi nane zilizoshiriki mashindano hayo. Kiwango cha soka cha Tanzania katika mpangilio wa FIFA kimepanda kutoka 105 mwezi Desemba, 2008 hadi nafasi ya 97.

- Timu ya Taifa ya Vijana wenye umri chini ya miaka 17 ilishiriki katika mashindano ya COPA COCA-COLA yaliyofanyika nchini Afrika Kusini na kupata ushindi wa tatu kati ya timu nane zilizoshiriki mashindano hayo.

- Mashindano ya Kombe la Taifa kwa mchezo wa Netiboli yalifanyika Wilayani Kibaha kwa ufanisi mkubwa ambapo jumla ya mikoa 17 ilishiriki katika mashindano hayo ambapo Mkoa wa Pwani ulikuwa bingwa mpya wa Kombe la Taifa kwa mwaka 2009.

- Vyama vya kriketi na tenisi viliandaa mashindano ya kimataifa hapa nchini katika jitihada za kuongeza uzoefu wa michezo mikubwa ya kimataifa kwa wachezaji wa Tanzania na kukuza utalii wa michezo nchini.

- Wizara imeandaa Muswada wa Kitabu cha Elimu Dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa wanamichezo katika kuimarisha dhana ya kutumia michezo kama nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya Mwaka 1967 na Marekebisho yake katika Sheria Na. 6 ya Mwaka 1971. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Baraza la Michezo la Taifa lilitekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya ufundishaji michezo kwa jamii kwa Walimu 620 katika Halmashauri za Wilaya 16 ambazo ni Meru, Arusha, Babati, Hanang, Karatu, Ngorongoro, Geita, Biharamulo, Liwale, Moshi, Iringa, Bukombe, Maswa, Bariadi, Njombe na Halmashauri ya Mji Njombe.

- Kuandaa na kuendesha mafunzo ya Kimataifa ya Ufundishaji na Uongozi wa Michezo kwa jamii kwa Washiriki 40 wa Tanzania na 8 wa Kimataifa kwa ushirikiano na Shirikisho la Michezo kwa Wote Ulimwenguni.

- Kukamilisha majadiliano ya ushirikiano na *UK Sports Charity na International Development through Sports (IDS)* kuhusu uanzishwaji wa Kituo cha Kimataifa cha Uongozi wa Vijana kupitia Michezo.

- Kutoa mipira 160 ya Soka, mipira 160 ya Netiboli na *Bips* 500 kwa ajili ya mafunzo kwa Wilaya 15 za Tanzania Bara.

- Kusimamia na kuendesha chaguzi za Vyama vya Michezo ya Gofu, Netiboli na Ngumi na hivyo kuimarisha uongozi na utawala bora katika michezo hiyo.

- Kukusanya mapendekezo kutoka kwa Wadau kuhusu marekebisho ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa.

- Kuandaa mpango wa utatuzi wa kero kati ya Vyama vya Michezo vya Taifa vya Tanzania Bara na Zanzibar.

- Kuendesha mafunzo ya Elimu ya Kinga dhidi ya Virusi vya UKIMWI, kupitia Michezo kwa Walimu 620 Tanzania Bara.

- Kuendesha mafunzo ya Elimu ya Kinga dhidi ya Virusi vya UKIMWI kwa Watumishi wa BMT na Vyama vya Michezo vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara imeendelea kushughulikia upatikanaji wa watumishi wenye sifa kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, kwa kuajiri watumishi wapya wenye sifa kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa Ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nafasi wazi zilizokuwepo ni 66. Kati ya hizo, nafasi 54 zimejazwa na nafasi 12 hazikupata waombaji wenye sifa. Vilevile, nafasi tatu za Wakurugenzi waliostaafu zimejazwa kwa uteuzi. Aidha, mchakato wa kujaza nafasi mbili za Wakurugenzi Wasaidizi waliostaafu hivi karibuni umekwishaanza. Watumishi watano walipandishwa vyeo na watumishi 12 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwajengea uwezo watumishi, Wizara imewagharimia watumishi 58 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi; mafunzo ya Shahada ya Uzamili watumishi 13, Stashahada ya Uzamili watumishi watatu, Stashahada ya juu watumishi watano, Stashahada ya kawaida watumishi watatu, Cheti cha Taaluma ya Uhasibu [CPA (T)] watumishi wawili na ngazi ya Cheti watumishi watano. Vilevile, Wizara imepeleka jumla ya watumishi 27 kwenye mafunzo mbalimbali ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi sita kuhusu Sheria Na. 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kupambana na janga la UKIMWI nchini, Wizara imeendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha watumishi kuhusu upimaji wa VVU/UKIMWI kwa hiari ambapo jumla ya watumishi 150 kati ya lengo la watumishi 172 wamepata fursa ya kupima afya zao ikiwa ni pamoja na kuchukua majibu. Aidha, Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi, walipata mafunzo na elimu ya mapambano dhidi ya UKIMWI na kushiriki zoezi la kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Ni matarajio ya Wizara kuwa wale wote waliopima afya zao, wataendelea kulinda hali waliyojikuta nayo baada ya kupokea majibu. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na TACAIDS, inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya hali halisi ya athari ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika wizara na taasisi inayozisimamia. Taarifa ya zoezi hili, itatumika kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na UKIMWI katika Wizara na taasisi inayozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuwawezesha watumishi kushauri Uongozi wa Wizara juu ya mambo mbalimbali yanayoihusu Wizara na maslahi yao, Wizara imeendelea kutumia tawi lake la TUGHE na Baraza la Wafanyakazi katika kutoa

ushauri juu ya utekelezaji wa malengo ya Wizara. Hii ni katika kutekeleza dhana ya ushirikishwaji wa watumishi katika sehemu za kazi ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha rasilimali za Wizara zinatumika vizuri na kwa madhumuni yaliyowekwa, Wizara imeendelea kutumia Kamati ya Kuratibu, Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali, pamoja na Kamati ya Ukaguzi ya Wizara na Bodi ya Zabuni ya Wizara, kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha zilizotengwa kutekeleza shughuli mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001, kama ilivyorekebishwa mwaka 2004, pamoja na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2001 ili kuhakikisha kuwa, huduma zenye viwango vinavyokubalika zinatolewa na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu. Ni kutokana na usimamizi huu, Wizara imeendelea kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu mfululizo tangu ilipoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ni miongoni mwa Wizara zinazotekeleza Programu ya Pili ya Maboresho katika Utumishi wa Umma. Kupitia Programu hiyo, Wizara imeweza kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja, ambao umeweka viwango vya utoaji huduma kwa wateja wetu. Pia, Wizara imeweza kuboresha utunzaji wa kumbukumbu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu utunzaji wa kumbukumbu na kununua kompyuta na samani za masjala ili kutunza kumbukumbu kwa njia ya elektroniki. Kwa kupitia programu hii, Wizara imeweza kuendesha mafunzo kwa watumishi wote kuhusu Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi na kuwezesha kuanza kutekelezwa mfumo huo ambao kwa sasa upo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM), kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari, unatarajiwa kuwasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri (BLM) wakati wowote kuanzia sasa. Mapendekezo ya Muswada huo wa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari, yanajumuisha pamoja na mambo mengine:-

- Uanzishwaji wa chombo huru kitakachosimamia viwango vya elimu na taaluma ya habari pamoja na maadili ya taaluma hiyo kitakachoitwa Bodi ya Usimamizi wa Taaluma ya Habari.
- Kufutwa kwa Sheria za Vyombo vya Habari zilizopitwa na wakati na ambazo zinalalamikiwa na wadau.

- Kuweka utaratibu bora zaidi na unaoendana na wakati wa usajili na umiliki wa vyombo vya habari.

- Uanzishwaji wa Mfuko wa kuendeleza waandishi wa habari kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwaka ujao wa fedha, itaendesha mafunzo ya Watendaji wa Wizara, Idara na Wakala mbalimbali, wanaohusika na Tovuti ya Wananchi. Aidha, itafanya mkutano wa Makatibu Wakuu wa Wizara zote,

kuzungumzia umuhimu wa Tovuti ya Wananchi ili kuondoa kasoro zinazohusiana na kucheleweshа majibu ya hoja za wananchi katika Tovuti. Aidha, Wizara yangu inaendelea kufanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuainisha majukumu ya pande hizo mbili kwa ofisi za habari za mikoa ambazo hivi sasa ni Sehemu za Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara yangu itaendeleza awamu ya pili ya mradi wa picha kwa kuanzisha mtandao wa kuuza picha popote duniani kupitia *E-commerce Project*. Mtandao huu utawawezesha wadau kupata picha hizi kwa gharama kidogo kutoka katika maktaba yetu. Aidha, katika awamu hii, picha za kumbukumbu za kitaifa na kimataifa zitahifadhiwa katika “CD” na kutunzwa katika sehemu nyingine ili kuondoa uwezekano wa kupoteza kumbukumbu hizo endapo kutatokea janga lolote kama moto katika maktaba ya picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, imejipanga kuelimisha watangazaji juu ya umuhimu wa kukuza na kuboresha maudhui na vipindi vya Tanzania ndani na nje ya nchi ili kuwezesha sekta ya utangazaji kushiriki katika kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. Mamlaka pia itaelimisha wananchi faida za mfumo wa utangazaji katika teknolojia ya dijitali. Njia mbalimbali zitatumika katika kutoa elimu hiyo, ikiwa ni pamoja na televisheni, redio, vipeperushi, warsha na njia nyingine zitakazowezesha wananchi kuelewa mabadiliko hayo. Kwa upande wa ving’amuzi vitakavyotumika kupokelea matangazo yatakayokuwa yakirushwa na mrusha matangazo ya dijitali, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, itaandaa utaratibu ili kuhakikisha kuwa, vifaa vyenye ubora vinapatikana kwa bei nafuu na kwa urahisi. Mamlaka pia itaendelea na uratibu na usimamizi wa vyombo vyote vya utangazaji nchini na kutathmini upatikanaji wa huduma hii kwa wananchi na mchango wake katika maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC): Kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 Serikali imetenga fedha za maendeleo shilingi bilioni mbili ili kukamilisha ufungaji wa mitambo ya Redio za FM kwenye mikoa yote 10 ambayo haina mitambo hiyo. Mitambo hiyo ya FM itafungwa Zanzibar na Mikoa ya Iringa, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani, Ruvuma na Mtwara. Hatua hii itapanua wigo wa usikivu wa redio kwa njia ya FM kuenea mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Televisheni ya Taifa yaliyoko Mikocheni, unatarajiwa kuanza mwaka 2009/2010, kwa mkopo wa shilingi bilioni 12.3 kutoka Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa udhamini wa Serikali mara baada ya kukamilisha taratibu stahiki. Mradi huu unakadiriwa kuchukua miaka mitatu kukamilika.

Pia ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya TBC na Studio za Redio lililoko Barabara ya Nyerere, unatarajiwa kufanywa kutokana na mkopo huo na utakamilika katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo ya televisheni yanatakiwa kuhama toka mfumo wa *analojia* kwenda *dijitali* ifikapo Juni 2015, kwa mujibu wa Shirikisho la Mawasiliano ya Kimataifa (ITU). TBC imeanza kujizatiti ili kuendana na mabadiliko hayo kwa kufuata mwongozo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Katika awamu ya kwanza, TBC itajielekeza kufanya mabadiliko hayo kwa kuanza kurusha matangazo kwa mtindo wa dijitali katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza kabla ya Desemba 2009 na kukamilisha urushaji wa matangazo katika mikoa yote kabla ya mwisho wa mwaka 2012. Mfumo huu utawezesha TBC kuwa na mikondo ya televisheni (TV channels) zaidi ya moja kabla ya Desemba 2009. Pia, TBC itaweza kubeba mikondo mingine kwa ajili ya televisheni nyingine kama Msambazaji wa Umma (Public Multiplexor).

Mheshimiwa Mwenyekiti, TBC itaboresha vipindi na matangazo yake kufikia viwango vya kimataifa na kuhakikisha vituo vyake vinaendelea kuvutia watazamaji na wasikilizaji. Katika kutimiza azma hii, TBC imepata haki pekee ya kutangaza mashindano ya mpira wa miguu ya Kombe la Dunia kwa redio na televisheni nchini Tanzania, yatakayofanyika Afrika Kusini mwaka 2010. Haki hizi zinajumuisha mashindano mengine ya kimataifa yanayoambatana na mashindano ya Kombe hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Magazeti la Serikali (TSN) katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, limepanga kufanya yafuatayo :-

- Kunakili picha na makala kwenye kompyuta. Katika mradi huu, picha 328,098 na makala 617,726 zitanakiliwa na kuhifadhiwa kwenye kompyuta na hatimaye kurahisisha upatikanaji wake.

- Kuwasiliana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Teknolojia ya Mawasiliano (ITU) ili liipatie Kampuni utaalam wa kuendesha biashara ya picha na makala kupitia mtandao.

- Kutekeleza Mpango Mkakati wa kuimarisha Ofisi za Kanda, kuanzisha redio na televisheni yake. Kukamilisha Mpango wa Biashara wa Kampuni ikiwa ni pamoja na kubadilisha mtazamo wa Kampuni. Mpango huu utasaidia kuongeza faida ya Kampuni.

- Kufungua Ofisi katika Mikoa ya Mtwara na Iringa ikiwa ni nyongeza ya Ofisi zilizofunguliwa katika Kanda tisa hadi kufikia Juni, 2009.

- Kuendeleza mazungumzo na wabia ili kuweza kujenga jengo la kisasa mahali yalipo Makao Makuu ya Kampuni, Mtaa wa Samora Jijini Dar es Salaam na nyumba za kisasa za kuishi kwenye kiwanja cha Kampuni kilichoko eneo la Mbezi Beach.

- Kukamilisha utafiti juu ya usambazaji wa magazeti vijijini. Mradi huu utahusisha Serikali za Vijiji na taasisi zilizo kwenye kata, ikiwa ni pamoja na shule za

sekondari za kata. Kwa kuanzia, mradi huu utafanya majaribio katika Wilaya za Muheza Mkoani Tanga na Gairo Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara itatekeleza yafuatayo katika Sekta ya Utamaduni:-

- Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatenga bajeti kwa ajili ya shughuli za utamaduni.

- Kuendesha mafunzo ya kukuza vipaji na ubunifu katika sanaa kwa watoto wa shule tano za msingi.

- Kuendesha warsha na maonesho ya sanaa za ufundi wa asili na kuweka kumbukumbu katika mikoa mitatu.

- Kuadhimisha Siku ya Utamaduni Duniani tarehe 21 Mei, 2010.

- Kusimamia na kuendesha Tamasha la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania mwezi Oktoba, 2009.

- Kushiriki matamasha na maonesho matatu nje ya nchi katika utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano.

- Kupokea vikundi vitatu vya utamaduni kutoka nje ya nchi katika kutekeleza mikataba ya ushirikiano.

- Kuratibu na kusimamia Mkutano Mkuu wa Saba wa Sekta ya Utamaduni.

- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya Maadili na Utamaduni wa Mtanzania katika redio na televisheni.

- Kufanya utafiti wa lugha za asili katika Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Rukwa.

- Kuendesha mafunzo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu kwa waandishi/wahariri wa vyombo vya habari.

- Kuchapisha vijarida na kusambaza matokeo ya utafiti wa mila na desturi.

- Kuendesha mafunzo ya mbinu ya kufanya Utafiti na Uhifadhi wa Mila na Desturi kwa Kanda ya Kaskazini.

- Kuendelea kufanya utafiti wa Mila na Desturi za kudhibiti kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mwanza.

- Kufanya utafiti kuhusu chimbuko la vifo vya Maalbino katika Mikoa ya Kagera, Shinyanga na Tabora.

- Kuendelea kutekeleza Progamu ya Kuhifadhi Urithi wa Ukombozi Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, litatekeleza yafuatayo:-

- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni.

- Kusoma miswada ya vitabu vya taaluma na kuvipatia ithibati.

- Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kimataifa na shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi.

- Kuendelea kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho.

- Kuhariri Kamusi ya Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa.

- Kukamilisha uhariri wa kitabu cha kufundisha wageni Kiswahili: ''Furahia Kiswahili Hatua ya 1" na kukichapisha.

- Kuendesha mafunzo ya msasa kwa vyombo vya habari.

- Kukamilisha mchakato wa kupata jengo kwa ajili ya Ofisi za Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza itatekeleza yafuatayo:-

- Kukagua na kupanga katika madaraja filamu 500 (Video, DVD, VCD na VHS) na kutoa vibali.
- Kuandaa na kukamilisha mchakato wa kuandika kanuni za utekelezaji wa Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ili zitangazwe na kusambazwa.

- Kukusanya taarifa na takwimu za kumbi za sinema na michezo ya kuigiza ili kuzipanga katika madaraja.

- Kupitia na kuhakiki miswada ya utengenezaji wa filamu na kutoa vibali.

- Kuhamasisha jamii na kutoa elimu kwa wadau 250 kuhusu kulinda, kuendeleza utamaduni, maadili na ujumi wa Watanzania katika filamu na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Baraza la Sanaa la Taifa litatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendeleza na kukuza stadi za sanaa kwa wasanii 600.

- Kuendesha mafunzo ya stadi za uongozi na utawala katika vikundi na kuendesha kozi fupi tano kwa viongozi 50 wa vikundi vinavyoendesha shughuli za sanaa katika Mikoa ya Mara, Kagera, Dodoma, Mwanza na Manyara.

- Kuendeleza na kukuza vipaji vya sanaa kwa watoto 200 kwa kuwapatia stadi za uchoraji na utambuzi na hadithi simulizi kwa shule za msingi 10 kutoka katika Mikoa ya Pwani na Morogoro.

- Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa maonesho na mafunzo ya sanaa.

- Kufanya utafiti wa mchango wa sanaa katika kuleta ajira, kuongeza kipato na kuondoa umaskini.

- Kusaidia na kuratibu vyama vitano vya sanaa vya Taifa katika kuendesha shughuli za maendeleo ya sanaa kwa wanachama wake.

- Kuendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria Na. 23 ya mwaka 1984 iliyounda Baraza.
- Kuandaa na kuchapisha jarida maalumu la habari za sanaa na wasanii.

- Kuboresha Tovuti ya Baraza.

- Kuanzisha hifadhi ya taarifa (database) za wasanii, vyama vya sanaa na wote wanaojishughulisha na kazi ya sanaa.

- Kuandaa na kuendesha shughuli mbili za utunishaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 itatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 120 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini.

- Kuendelea kutayarisha mtaala wa mafunzo ya shahada ya kwanza.

- Kuendeleza ushirikiano na washirika wetu ambao ni Chuo Kikuu cha Stavanger na Chuo Kikuu cha Utrecht.

- Kuendesha Tamasha la 28 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania litakalofanyika Septemba 28 hadi Oktoba 3, 2009 ambapo kaulimbiu yake ni Sanaa na Utamaduni katika kukuza Utalii.

- Kuimarisha kituo cha utafiti na uhifadhi wa ngoma na muziki wa Kitanzania.

- Kutekeleza awamu ya pili ya mpango wa kuboresha utumishi wa umma.

- Kujenga jengo la utawala na bweni moja ikiwa ni sehemu ya mpango kabambe wa TaSUBa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni Tanzania (MFUKO), katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 unakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendesha mafunzo kwa Maafisa Tawala na Maafisa Biashara wa Mikoa ili kuongeza uelewa wa shughuli za utamaduni na mchango wake katika kuinua maisha ya Watanzania.

- Kuendesha mafunzo ya kuongeza uelewa kwa Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara zote kuhusu shughuli za utamaduni na mchango katika kuinua na kuboresha maisha ya Watanzania na kuchangia Pato la Taifa.

- Kuendeleza vituo vya utamaduni ambavyo vitakuwa sehemu za maonesho na masoko ya bidhaa za utamaduni.

- Kuwajengea uwezo na kuweka taarifa *(capacity building and mapping)* za watengeneza filamu wanaoinukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara yangu itatekeleza majukumu yafuatayo katika Sekta ya Michezo:-

- Kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Michezo.

- Kusimamia mchakato wa awamu ya pili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo.

- Kuratibu na kuhakikisha kwamba timu za Tanzania zitakazokidhi viwango vinavyotakiwa zitashiriki katika Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika huko Delhi, India mwezi Oktoba mwaka 2010.

- Kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatenga bajeti kwa ajili ya shughuli za Maendeleo ya Michezo.

- Kuandaa mkakati wa pamoja na mamlaka za Serikali za Mitaa kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya michezo.

- Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha viwanja vya michezo inavyomiliki na kujenga viwanja vipya

- Kutoa mafunzo ya stashahada ya elimu ya ufundishaji michezo na stashahada ya uongozi na Utawala wa Michezo kwa wanachuo 24 waliopo sasa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na wanachuo wapya watakaojiunga mwezi Oktoba 2009.

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu michezo katika vituo vya michezo Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea).

- Kudurusu Katiba za vyama na vilabu vya michezo na kuvisajili. Kutoa ushauri kwa Vyama na Vilabu vya Michezo kuhuisha Katiba zao ili kuimarisha utawala bora na uongozi katika michezo.

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya michezo na kuhamasisha Serikali za Mitaa kujenga miundombinu ya michezo ili kuinua viwango pamoja na kuchochea ari ya kukuza ushindani, ufundishaji, uamuzi na uchezaji wa michezo nchini. Kuendelea kuboresha miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ikiwa ni pamoja na kujenga hosteli ya wanachuo na kuongeza vitendea kazi.

- Kutoa huduma za kinga na tiba kwa kufanya upimaji wa afya na kuendesha kliniki za wazi kwa wanamichezo.

- Kuhamasisha wanawake kujihusisha zaidi katika michezo ili kuongeza ushiriki wao ikiwa ni kuwahamasisha pamoja kugombea nafasi za uongozi katika Vyama na Vilabu vya michezo.

- Kuendelea kushirikiana na Wizara za Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI katika kuimarisha somo la Elimu kwa Michezo shuleni na vyuoni.

- Kuendelea kutafuta walimu wenye ujuzi na uzoefu wa kimataifa katika kufundisha timu za taifa za michezo mbalimbali kupitia mikataba ya ushirikiano na nchi rafiki.

- Kuratibu shughuli za Siku ya Michezo Tanzania itayoadhimishwa nchi nzima na kilele chake kuwa tarehe 21, Septemba 2009 huko Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Baraza la Michezo la Taifa linakusudia kufanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha jamii kushiriki michezo na kutoa huduma bora kwa wadau wa michezo.

- Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundishaji michezo kwa walimu wa michezo wapatao 1,800 katika Wilaya 40 za Tanzania Bara.

- Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa Vyama vya Michezo vya Taifa kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Michezo.

- Kuandaa na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa BMT na Vyama vya Michezo kuhusu elimu ya maambukizi ya VVU.

- Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Baraza.

- Kuratibu programu za wabia na wadau wengine wa michezo wanaotumia michezo kama zana muhimu ya kutekeleza malengo ya taifa na kimataifa.

- Kukamilisha ukusanyaji wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa.

- Kushiriki katika mikutano, matamasha na mashindano yanayoandaliwa na wadau au wabia wa Baraza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala na Rasilimali Watu: Katika mwaka 2009/2010, Wizara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS).

- Kuainisha maeneo ya kuingia ubia na sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza shughuli zote ambazo si za msingi *(core functions)* kwa wizara.

- Kuendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi watakaostahili kulingana na miundo ya utumishi ya kada zao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.
- Kuhakikisha upatikanaji wa watumishi wenye sifa kujaza nafasi wazi zilizoidhinishwa katika Ikama na kwa kuzingatia mwongozo wa masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma.

- Kuwajengea uwezo watumishi kwa kugharamia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

- Kuimarisha Dawati la Malalamiko na kusimamia utendaji wa dawati hilo.

- Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha watumishi juu ya ugonjwa wa UKIMWI na upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari ili waweze kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara na kujilinda dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

- Kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara wa kupambana na VVU/UKIMWI na kuutekeleza.

- Kutoa huduma ya msaada kwa watumishi wanaoishi na VVU waliojitokeza, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali kupitia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa Mwaka 2006.

- Kuendesha mafunzo kuhusu Utawala Bora na kusimamia utendaji kazi wa watumishi kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na mapambano dhidi ya Rushwa.

- Kuendesha mikutano ya wafanyakazi wote na ile ya Baraza la Wafanyakazi.

- Kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo ili Sekta hizo ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Serikali inaamini kuwa Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo zina nafasi kubwa sana katika kuchangia maendeleo ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kuleta amani na furaha katika jamii.

Pamoja na kuwa katika kutumia fursa hizo bado kuna changamoto ambazo ni lazima zipatiwe ufumbuzi ili kutumia fursa hizo ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Serikali inafahamu jambo hili na ni kwa sababu hiyo, Serikali ya Awamu ya Nne, imeendelea kutilia mkazo maendeleo katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo, ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti ili kuendeleza sekta hizi. Ninaamini kuwa, changamoto zilizopo zitaendelea kupata ufumbuzi hatua kwa hatua na hasa kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo. Tukidhamiria tunaweza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009 katika kutimiza malengo yetu. Utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu, umewezekana kutokana na ushirikiano mzuri uliopo miongoni mwa Viongozi na Wafanyakazi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara. Shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mjini, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo; Dkt. Florens Martin Turuka, Katibu Mkuu na kwa Watendaji na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu, kwa juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba, wanatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo, ambao wametuunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Nawashukuru wahisani wote ambao wametusaidia na nina imani wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote, lakini nitaje wachache ambao ni Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Sweden, Norway, Denmark, Ujerumani, Japan na Finland; Mashirika ya Kimataifa ya UNICEF na UNESCO. Pia, ninapenda kuyashukuru Makampuni za Vodacom (T) Limited, Tanzania Breweries Limited (TBL), Serengeti Breweries Limited, NMB Bank, NBC Bank, Mohamed Enterprises (T) Limited, SBC Limited, Benki ya Posta, Coca Cola Afrika - Kanda ya Tanzania na IPP Ltd.

Navishukuru vyombo vyote vya habari nchini kwa kufanya kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu. Ninaamini vyombo vya habari vitaendelea na kazi ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha kwa kuzingatia maadili. Pia, ninamshukuru sana Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka 2009/2010, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 414,853,000 kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya Mapato, ukilinganisha na shilingi 313,451,000 zilizopangwa kukusanywa mwaka 2008/2009. Ongezeko hili linatokana na lengo la kukusanya shilingi 180,000,000 kutoka Uwanja wa Taifa, ukilinganisha na shilingi 120,000,000 mwaka 2008/2009. Kadhalika, shilingi 150,000,000 zitakusanywa kutoka vibali vya kupiga picha za video, ukilinganisha na shilingi 66,000,000 mwaka 2008/2009 na ada ya matangazo na uchapishaji shilingi 20,000,000, ukilinganisha na shilingi 6,000,000 kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara imetengewa shilingi 15,817,088,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha Mishahara ya Wizara – shilingi 1,639,876,000; Mishahara ya Taasisi – shilingi 4,695,821,000; Matumizi Mengineyo ya Wizara – shilingi 5,181,302,000; na Matumizi Mengineyo ya Taasisi – shilingi 4,300,089,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 6,597,264,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya

Maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 6,279,221,000 ni fedha za ndani na shilingi 318,043,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutetekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2009/2010, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 22,414,352,000, ambapo kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 15,817,088,000 na shilingi 6,597,264,000 ni fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabla sijaendelea na hotuba yangu au hotuba ya Kamati, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwq kunipa uwezo ili nisimame mbele yenu hapa nisome taarifa ya Kamati. La pili, ambalo ni kubwa zaidi na ni muhimu hasa kwangu mimi mwenyewe, namshukuru sana mke wangu mpendwa, Biubwa Said, aliyenirejesha ujana kwa namna anavyonitunza, kunienzi na kunivumilia kwa yote ninayoyafanya. Pia, naishukuru familia yangu yote. Mwenyezi Mungu, awazidishie mapenzi kwangu mimi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na kuliomba Bunge lako Tukufu, liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majukumu ya Kamati hii ni kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, pamoja na kusimamia na kuishauri wizara hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 02 Juni 2009, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam na kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na kuchambua Makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009, Kamati ilitoa ushauri kuhusu maeneo mbalimbali kwa Wizara hii na Taasisi zake, ikiwa ni pamoja na Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC) na utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa mteja ndani ya

Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imejitahidi kutekeleza ushauri wa Kamati. Maelezo ya Wizara yalionesha kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati utaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2009/2010, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati malengo ya Asasi zilizo chini ya Wizara hii kwa mwaka ujao wa fedha. Asasi hizo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Katika maelezo hayo, majukumu ya jumla ya kila Asasi na malengo yake kwa mwaka 2009/2010 yalielezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia na kuchambua kwa kina, Kamati imeridhishwa na malengo yaliyopangwa na kila Asasi kama yalivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri alipokutana na Kamati. Aidha, Kamati inasisitiza utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vyema majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 22,207,349,300. Kati ya fedha hizo, Shilingi 15,610,085,300 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 6,597,264,000 kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara kwa Mwaka 2009/2010. Baada ya kupitia mafungu yote, Kamati inaunga mkono hoja ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na kuliomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha maombi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia majukumu ya Wizara hii, pamoja na malengo yaliyowekwa kwa kila Asasi, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia malengo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 na majukumu ya msingi ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), pamoja na kuzingatia ukweli uliopo wa umuhimu wa kila Taifa/Serikali kuwa na chombo cha habari, Kamati inaishauri Serikali kuiongezea TBC ruzuku itakayolisaidia Shirika kuwa na uwezo wa kurusha matangazo yake kwa Watanzania wengi na hasa waishio maeneo ya vijijini ili waweze kupata habari za uhakika na kwa wakati. Katika kuzingatia ushindani uliopo wa vyombo vya habari ni vyema Serikali sasa ikaamua kwa dhati kuliwezesha kifedha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ili liweze kukidhi mahitaji yake na hasa katika kuboresha mitambo ya kurushia matangazo, pamoja kuongeza usikivu hasa maeneo ya pembezoni. TBC pia ihakikishe Television ya Taifa nayo inarusha matangazo yake katika nchi nzima badala ya kusikika mikoa michache tu.

Hata hivyo, Kamati inasikitishwa sana na hatua ya Wizara ya Fedha kutoona umuhimu wa kuidhinisha mkopo wa kuliwezesha Shirika la TBC kukarabati majengo yake yaliyopo Mikocheni. Kwa kuzingatia vikao vilivyoketi baina ya Kamati, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, mara kadhaa kuhusu umuhimu wa Serikali kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na Sheria ya Mikopo ya Udhamini ya Serikali, Kamati inashangaa ni kwa nini mpaka leo hakuna maamuzi yenye kuonesha udhati wa Serikali kupitia Hazina katika kulishughulikia suala hili nyeti na lenye maslahi ya Taifa. Inashangaza sana kuona Hazina bado kila siku wanaendelea kudai taarifa za kiufundi za kuonesha uwezekano wa mradi huo kutekelezwa chini ya Mpango wa Government Guarantee licha ya taarifa hizo kupelekwa kwao mara kadhaa kupitia Wizara ya Habari na Utangazaji na TBC. Kamati inaomba sana Serikali hasa kupitia Hazina (Wizara ya Fedha), wafikie muafaka na mradi huu muhimu uanze kutekelezwa. Ni aibu kwa Taifa letu kutokuthamini majengo ambayo jiwe la msingi liliwekwa na mpendwa wetu sana, Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi toka Aprili, 1995 mpaka sasa, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ili kuweza kumalizia matengenezo ya majengo yale yaliyotumia pesa nyingi za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Kiswahili Tanzania, Kamati inashauri Baraza hili lisaidie kukabiliana na tatizo la Kiswahili kutotumika vizuri, licha ya kuwa ni Lugha ya Taifa Nchini na ni mojawapo ya lugha rasmi inayotumika katika Umoja wa Nchi za Afrika. Serikali kupitia Wizara ihakikishe kuwa, Kiswahili kinatumika wakati wote kwenye shughuli za Serikali, ikiwa ni pamoja na mikutano ya Bodi za Wakurugenzi. Aidha, ili kukuza matumizi ya Lugha ya Kiswahili na kuwawezesha wananchi kutathmini thamani halisi ya fedha walizotengewa kwenye Wilaya na Mikoani, Kamati inashauri kuwa, BAKITA lisaidie Hazina kuandaa Vitabu vya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 kwa Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mfuko wa Utamaduni Tanzania, ulianzishwa ili kuchochea ubunifu na kuongeza kipato katika Kaya, sambamba na kuhimiza ajira za kujitegemea, Kamati inaishauri Wizara kuwatumia vizuri Maafisa Utamaduni katika ngazi zote za Wilaya na Mkoa ili waweze kuihamasisha jamii katika kubuni njia za kujiongezea kipato na kuendeleza utamaduni wetu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha katika kila bajeti ya mwaka kwa ajili ya Maafisa Utamaduni kutekeleza majukumu yao kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mila na lengo la kuanzisha Mfuko wa Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imedhamiria kuondoa Ushuru wa Forodha kwenye kamera maalum za kupigia picha za filamu zinazotumika chini ya HS Codes 8525.80.00 kwa lengo la kuhamasisha Sekta ya Filamu na kuongeza ajira na pato kwa vijana, Kamati inaishauri Wizara kujipanga kuitumia fursa hii vizuri kwa manufaa ya vijana na makundi mengine katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa filamu na michezo ya kuigiza imeongeza ajira kwa Vijana na Pato la Taifa, Wasanii wengi wamekuwa hawafaidiki na kazi zao

kutokana na ujanja unaofanywa na mapromota na wasambazaji, jambo ambalo huwakosesha Wasanii pato lao na kuikosesha Serikali mapato. Kamati inaomba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia, kuraharakisha na kukamilisha uhuishaji wa Sheria ya Hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, Uwanja wa Taifa ulijengwa kwa gharama kubwa ili pamoja na kutoa nafasi nzuri ya michezo kwa watazamaji wengi, pia kuingizia Serikali mapato. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko mengi na tuhuma juu ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na michezo inayofanyika katika uwanja huu, hasa Mpira wa Miguu. Kwa sababu hiyo, Kamati inaishauri Wizara kupitia Baraza la Michezo la Taifa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kuweka utaratibu na usimamizi mzuri na wa wazi wa kuhakikisha kuwa, mapato yote ya Uwanja wa Taifa yanakusanywa ipasavyo na hayavuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti matumizi holela ya maduhuli katika nyanja za michezo ni maoni ya Kamati kuwa, Mapato na Matumizi yanayotokana na Uwanja huo, yakaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ina maoni na ushauri wa jumla kwa Wizara hii kama ifuatvyo:-

Kwa kuzingatia maelezo ya Waziri kuwa mauzo ya picha ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mwaka 2008/2009, Wizara ilipanga kuuza picha 50,000 hadi Juni 2009 zilikuwa zimeuzwa Picha 400 tu, kwa kuwa Ofisi na Taasisi nyingi za Serikali ziliieleza Wizara kuwa hazikuwa na Bajeti ya Ununuzi wa Picha ya Mheshimiwa Rais, kwa mwaka huu unaomalizika. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, kila Ofisi, Wizara na Taasisi za Serikali, inanunua na kutundika Picha Mpya ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeruhusu uhuru wa Vyombo vya Habari, kumekuwa na tuhuma na tabia ya kutumia uhuru huu vibaya. Aidha, Kamati imeipongeza Wizara kwa kufuta Magazeti 29 na kutoa karipio kali kwa wamiliki binafsi wa vyombo vya habari na wahariri wanaotumia vyombo vyao vibaya, kwa kuingilia uhuru wa wahariri. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kupitia Wizara hii, kuharakisha kutungwa Sheria ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, Balozi zetu nje ya Nchi na wadau wengine, kufanya maandalizi ya kutosha ili uwanja wa kisasa wa Taifa uweze kutumika kikamilifu kwa mazoezi ya wachezaji wa Kombe la Dunia litakalofanyika mwakani nchini Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mechi za Kombe la Dunia zitachezwa Afrika Kusini, hii ni fursa kwa Uwanja wa Taifa kutumika katika kuongeza mapato na akiba yetu ya fedha za nje. Aidha, michezo ya mpira wa miguu itakayofanyika Uwanja

huu, itaongeza chachu kwa vijana wetu kujifunza mbinu za kisasa za kucheza mpira na kuitangaza nchi yetu nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu hairidhishwi hata kidogo na mwenendo wa sasa wa kutokuwa na mahusiano mazuri kati ya TFF na ZFA, juu ya uwajibikaji baina yao katika uendeshaji wa masuala ya soka hapa nchini, ambao unapelekea malumbano. Kamati inaishauri na kuiagiza Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kuitisha kikao cha pamoja kabla ya kuahirishwa kwa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge hili, baina ya Kamati yangu, TFF, ZFA, Uongozi wa Wizara na wadau wengine wa mchezo wa mpira wa miguu ili kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa George Mkuchika, (Mb) na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa kipindi kigumu alichopitia akiwa kama Waziri wa Habari; magazeti mengi yalipogoma kuandika habari zake, lakini kwa busara zake na uzalendo na moyo wa kujituma, aliendelea kuitumikia Serikali kwa moyo wake wote. Aidha, shukrani za dhati ziwaendee Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, (Mb), Katibu Mkuu, Dkt. Florens Turuka na Wataalam kutoka Wizara hiyo, waliotusaidia katika kuchambua Bajeti ya Wizara. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati.  Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Pia namshukuru Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati hii, kufanya kazi ya kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009 na Mapendekezo ya Wizara kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha taarifa yangu, napenda kuwashukuru na kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii, kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:  Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub S. Masoud - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Salim Abdullah Khalfan, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Dora H. Mushi, Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika na Mheshimiwa Joel Bendera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kuwashukuru Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu walioihudumia Kamati hii Ndugu Rachel Nyega, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Brown Mwangoka, kwa kuratibu vyema na kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa uwasilishaji wako mzuri. Nitumie nafasi hii kumshukuru mke wako kama ulivyosema, kwa kukufanya uendelee kuwa kijana badala ya kuzeeka.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamruhusu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nadhani busara ya Kiti inaniambia niwataje wale wachangiaji ambao watatangulia ili kama hawako ndani ya Ukumbi wa Bunge, waweze kujiandaa na kurudi Ukumbini.

Waheshimiwa Wabunge, msemaji wetu wa kwanza ilikuwa awe Mheshimiwa Martha Mlata, lakini kwa kuzingatia *appointment* yake na Daktari *General Hospital*, kwa hiyo ameniomba achangie jioni. Kwa hiyo, mchangiaji anayefuata atakuwa Mheshimiwa Elietta Switi, ndiye atakayeanza.

Waheshimiwa Wabunge, samahani hawa ninaowataja wako katika makundi yafuatayo; wako Wabunge ambao hawajawahi kuchangia hata mara moja, nadhani nimefanya makosa nimeruka jina la Mheshimiwa Janet Kahama; kwa hiyo, Mheshimiwa Janet Kahama ndiye atakayeanza, hawajawahi kuchangia hata mara moja.

Waheshimiwa Wabunge, kundi la pili ni la Wabunge waliochangia mara moja. Kundi hilo linaongozwa na Mheshimiwa Martha Mlata, ambaye ameomba udhuru amekwenda hospitali; atafuatiwa na Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Kingunge Ngombare-mwiru na yeye ameomba nimuingize kwenye orodha ya wachangiaji wa jioni na Mheshimiwa Faida Bakar.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio kundi la wale ambao wamechangia mara moja. Waliochangia mara mbili sasa watakaofuata wanaongozwa na Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Suzan Lyimo.

Wale ambao wamekwisha changia mara mbili na hii itakuwa ni mara ya tatu, yuko Mheshimiwa Halima Mdee. Kwa hiyo, ndio orodha yangu ya wachangiaji. Kwa

kuzingatia muda, kwa kuzingatia Kambi ya Upinzani na kwa kuzingatia jinsia, nitaendelea kufuata utaratibu wa hali ilivyo kwa majina haya ambayo nimeyasoma.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Mama Janet Kahama simwoni humu ndani, Mheshimiwa Elietta Switi ajiandae na kama atakuwa hajarudi, Mheshimiwa Mwadini ujiandae. Baada ya kusema hayo, naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, aweze kutoa Taarifa ya Kambi ya Upinzani.

Naomba nimwite Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, aweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Amani, kwa kutuwezesha sote kufika hapa tukiwa wazima wa afya, tukiwa tayari kuwajibika kama tulivyoagizwa na Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kambi ya Upinzani Bungeni, chini ya Uongozi thabiti wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, kwa kuendelea kuniunga mkono na kunisaidia pale ninapohitaji msaada wao katika utendaji wangu wa kazi ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wananchi wote wa Wilaya ya Kilwa, Chama changu cha Wananchi (CUF), chama kinachojikita katika kusimamia na kutetea Haki na Usawa kwa Watanzania bila kujali Itikadi, Dini wala Rangi. Pamoja na hao, napenda pia kuwashukuru Viongozi na Wanachama wote wa CUF, Wilaya ya Kilwa. Kwa pamoja, napenda kutambua ushirikiano wanaonipa ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa juhudi zao katika kuhakikisha mipango ya Wizara, inakwenda kama ilivyopangwa. Sambamba na hilo, nawapongeza wanamichezo na wanahabari wote katika kuhakikisha kuwa, wananchi wanapata kile wanachostahili katika tasnia nzima ya michezo na habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia ya habari; dhana ya uhuru wa habari inazitaka mamlaka husika, kuondoa vikwazo vya kisheria na kiutawala ili kumwezesha kila raia kuwa huru kudai na kupata taarifa kutoka kwenye asasi za umma na za binafsi. Uhalali wa dhana hii unatokana na maelekezo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwamba, kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi; anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inadhihirisha kuwa, kupata habari ni moja ya haki za msingi za raia. Serikali ina jukumu la kusimamia haki na kutetea haki za wananchi wake. Hivyo, kusambaza habari ni jukumu la Serikali, ingawa hata vyombo binafsi vinayo majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa na kupokea habari kunatambuliwa duniani kote kuwa ni moja ya haki za binadamu. Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, zina matamko rasmi ambayo serikali imeridhia kuhusu haki ya kupokea na kutoa habari. Haki hii, kama zilivyo haki nyingine zote, hutolewa kwa kuzingatia wajibu wa kila raia kwa jamii na uhuru binafsi wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhima ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na yombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majarida, televisheni, filamu, video, intaneti, picha, vipeperushi, katuni na mabango. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano yamerahisisha upataji na utoaji habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nii ina maana kwamba, Serikali inatakiwa kuzipitia na kuzihuisha sheria zote zinazokataza kutolewa kwa taarifa zenye manufaa kwa umma kwa kuwa kupata na kutoa taarifa ni haki ya msingi ya Mtanzania, kinyume chake ni Tanzania kuendelea kuvunja haki ya msingi ya kutotambua haki hiyo ya uhuru wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya Na. 116 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, inazitaka Serikali zake zote mbili, kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari kwa mujibu wa sheria; kuinua ubora wa taaluma ya habari kwa kushirikiana na wamiliki wa vyombo vya habari vya binafsi, kwa kushirikiana na vyombo vyao vya uwakilishi; kuweka mipango ya kuwaelimisha waandishi wenye vipaji katika taaluma maalum ili tuanze kuwapata waandishi wanaoweza kuyasanifu na kuyachambua masuala ya uchumi, siasa, ulinzi na kadhalika katika vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kwa takwimu; ni jinsi gani imeinua ubora wa taaluma ya habari kwa kushirikiana na vyombo vyao vya binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wa tasnia ya habari wamekuwa wakiilalamikia serikali kwa kuwa na wadau katika kile kinachoitwa mgongano wa maslahi, kwani Serikali ni mmiliki wa vyombo vya habari, msajili ya vyombo vya habari, mtunga sera, msimamizi na mwisho ni mshindani kwenye tasnia nzima ya habari. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri ategue kitendawili hiki ili kusawazisha pale penye mabonde miongoni mwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo tunamtaka Waziri alitolee ufafanuzi, pale habari zinazoandikwa kuwa za ukweli lakini ni za aibu, mhusika na mwandishi ndio wanaofahamu kuwa ni ukweli kabisa. Mwandishi analaumiwa na hata chombo chake kufungiwa; katika hili Serikali inasimama wapi?

Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa, taaluma ya habari ni moja ya nguzo muhimu sana katika jamii. Kwa nchi nyingine duniani, Sekta ya Habari nayo inachukuliwa kama nguzo ya nne katika utawala mzima wa nchi, kwa maana ya kuwa nguzo nyingine zikiwa ni Bunge, Serikali na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waandishi wa habari wawe ni wa sekta binafsi au sekta ya umma, wote kwa ujumla wao wanahitaji kupatiwa masilahi bora, pamoja na kufanya kazi katika mazingira bora vile vile. Imetubidi tuseme hili la maslahi ya waandishi kutokana na ukweli kuwa, ubora wa taaluma hiyo unaweza kufifia na kudharauliwa na jamii, kutokana na waandishi kutopatiwa kile wanachostahili kupata, tofauti na watumishi walio katika sekta nyingine kama vile wahandisi, askari, walimu, madaktari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba, waandishi wamekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi na mazingira bora ya utendaji kazi kwa taaluma nyingine. Swali linakuja je, wao ni nani anawasemea matatizo yao? Je, ni kweli wanapatiwa wanachostahili na waajiri wao? Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya au kuweka viwango vya stahili zao, pamoja na vitendea kazi vyao, iwe ni kwenye television, radio au magazeti. Kwa kufanya hivyo ni kurejesha heshima ya uandishi wa habari na kuufanya mhimili huu ambao sio rasmi kama ile mitatu, kufanya kazi inayotarajiwa na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu Sera ya Taifa ya Utamaduni ingawa Sekta ya Utamaduni imekuwa katika mfumo wa Serikali tangu mwaka 1962. Nafasi ya Sekta ya Utamaduni katika maendeleo ya Taifa letu, bado haijatambuliwa kikamilifu. Mipango ya maendeleo imekuwa ikibuniwa na kutekelezwa bila kujali utamaduni wa wananchi, mfano; matumizi ya uzoefu, stadi na elimu ya jadi, havitiliwi maanani. Utamaduni haupewi dhima katika maamuzi na mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nukuu hiyo ni dhahiri kuwa, Serikali siyo kama haielewi umuhimu wa tamaduni katika mipango ya sekta mbalimbali za uchumi katika nchi yetu, bali inafanya makusudi tu. Haya makusudi ni kwa manufaa ya nani? Je, tamaduni zetu zinahusishwa vipi katika mpango mzima wa maendeleo ya michezo mathalani kulenga shabaha, kuruka kwa upondo, bao na riadha hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kuwa, Tanzania tutakuwa miaka yote tunashindwa kwa sababu ya kutokuthamini na kuvienzi vile vya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu uliopo katika Sekta, Maafisa Utamaduni hufanya kazi za Maafisa Michezo na Maafisa Vijana, hii inawazidishia mzigo wa kazi na hawana marupurupu yoyote, wao wanabakia kufanya kazi tatu kwa pamoja. Kweli huku ndio kuwekeza ili kuibua vipaji? Pamoja na hilo, kutokana na ukubwa wa wilaya zetu, bado tumekuwa tukiona matatizo makubwa wanayoyapata katika kutimiza majukumu yao. Sote tunajua ukubwa wa wilaya zetu, matatizo ya miundombinu yetu tunayafahamu, lakini tunamsaidia vipi mtumishi huyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuitaka wizara husika, kutoa takwimu zinazoonesha nchi yetu ina Maafisa Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo na Vijana wangapi katika wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, filamu zina faida kubwa sana katika jamii, kwani ndiyo njia rahisi sana kufikisha ujumbe katika rika zote kwenye jamii. Aidha ni kivutio kikubwa zaidi kibiashara. Filamu ni njia nyepesi ya kuutangaza na kuufikisha ujumbe lengwa na mtayarishaji wa filamu. Sambamba na hilo, filamu inaweza kutumiwa kuharibu kabisa maadili na tamaduni za jamii husika kama hakutakuwa na chombo cha kudhibiti sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, filamu na video ni vielelezo vinavyoweza kuchochea vitendo vya uvujaji maadili katika jamii na pia vinaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kuielimisha jamii uzuri wa mila na tamaduni zetu. Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa, wahusika katika sekta hii ya filamu, wameshindwa kutumia uhalisia wa mila na tamaduni za makabila yetu katika filamu na badala yake wale wenye makabila hayo, wanaona kama wanadhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi kwa kuwa wengi wamekuwa wakijaribu kutengeneza filamu za makabila mbalimbali lakini je, waigizaji wako sawasawa na wanawiana na jamii husika au ni bora liende tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kasoro kwani ujumbe unaofika sio ule uliokusudiwa. Hivyo basi tunawaomba wahusika hili walifanyie kazi kwa makini kama kweli lengo ni kutangaza mila na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni kwa kipindi kirefu umekuwa ukifanya kazi zake kwa msaada mkubwa wa ufadhili kutoka mashirika ya nje. Mfuko huu umekuwa ni kitovu cha kuendeleza sanaa na utamaduni wa Mtanzania. Aidha, sambamba na hilo, Mfuko huu kwa upande mwingine umekuwa ni chanzo kimojawapo cha ajira kwa wajasiriamali wengi hapa nchini kupitia sanaa zao wanazozitengeneza na kuziuza au sanaa zinazooneshwa majukwaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mwaka uliopita ilitenga Shs.200 milioni kwa ajili ya kuundeleza Mfuko huu na kutoa mishahara kwa watumishi wa Mfuko. Tatizo lililopo kwa sasa katika Mfuko ni kwa jinsi gani gharama za uendeshaji zitaweza kulipwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia kwa makini suala hili la kuusaidia Mfuko huu kuweza kuongezewa fungu mbali na lile la kusaidia vikundi

mbalimbali vya sanaa katika kujiendesha la mfuko wenyewe kuzidi kuandaa maonesho ya sanaa kwa vikundi vinavyosaidiwa ili viweze kuuza kazi zao ndani ya nchi au nje ya nchi. Kwa kufanya hivyo tunaamini kabisa tutakuwa tumeongeza ajira na kuiongezea Serikali wigo wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia ya michezo haikuanza leo wala jana bali ni tasnia kongwe mno, kwa kuwa watu wote hasa Watanzania tunaamini kuwa mwanadamu wa kwanza aliishi Tanzania. Ushahidi huo upo na mabaki muhimu ya vifaa na mifupa vilivyoachwa na aina ya binadamu, vinakadiriwa kuwa na umri wa miaka milioni moja na sabini na tano elfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa binadamu huyo alikuwa anakimbia, hivyo mkimbiaji wa kwanza duniani alikuwa ni Mtanzania. Kwa mtiririko huo tunaweza kunyumbulisha mambo mengi ambayo ushahidi wake upo. Jambo la msingi ni kuuliza ni kwa vipi sasa Tanzania tumeshindwa kuyaenzi na kuyaendeleza yale yaliyokuwa yakifanywa na huyo babu yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya michezo katika dibaji inasema wazi kuwa ni muhimu kuendeleza michezo ya jadi ikiwa ni pamoja na kuifanyia utafiti na kuifundisha katika sehemu mbalimbali kama vile shuleni na vijijini. Michezo ya jadi ina nafasi kubwa katika utamaduni wetu na inaweza kuendelezwa kwa urahisi kuliko michezo ya kigeni. Hii ni kwa sababu wataalam wake wapo hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka majibu hadi sasa toka sera hii ya michezo isainiwe na Mheshimiwa Sarungi (Mb) mwaka 1995 wakati huo akiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni hadi sasa utafiti kuhusiana na michezo hiyo na kuendelezwa  mafanikio yake yako vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Ubadhirifu katika Vyama vya Michezo; Majukumu ya Wizara ni pamoja na kuimarisha utawala bora katika Michezo nchini, kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Na hapo ndipo vyama vya michezo vinapopata uangalizi. Hapa nchini kwetu vyama vya michezo ni vingi sana. Na mojawapo ya kero kubwa katika vyama hivi ni ubadhirifu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii ndio yenye jukumu la kufuatilia uwajibikaji na maadili katika vyama hivi kupitia kwa msajili wa vyama vya michezo. Pamoja na ukweli wa kuwepo kwa mikingamo mingi ya kikatiba inayolinda kuingiliwa kwa vyama hivi na taasisi au Wizara yoyote kutoka nje. Lakini wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Michezo inaweza kumwita mkaguzi wa kutoka nje ya chama na hivyo kutambua kama kuna ubadhirifu wowote, pia msajili ana uwezo wa kuhakikisha kuwa vyama hivi vyote vinakuwa na vikao vya mwaka na kutaarifiana juu ya mapato na matumizi kwa wanachama. Aidha kuweka wazi mikakati yao ya kuendeleza michezo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ambazo wizara inaweza kuzuia matatizo mengi ambayo yana malalamiko mengi katika vyama hivi ni kwa kupeana taarifa. Kambi

ya upinzani inapenda kujua toka tumetoa rai hii kwa wizara husika kumwezesha msajili wa vyama ili aweze kufanya kazi zake kwa umakini, vyama vya mikoa na wilaya ngapi tayari vimekaguliwa? Kwani hii ndiyo njia pekee ya kuondoa kero na kuwafanya wadau wa michezo kuchangia maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili Taifa **(**BAKITA**)**; liliundwa kwa Sheria Na.27 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1983. Sasa ni takribani miaka 25 yaani robo karne tangu kuundwa kwa Baraza hilo. Madhumuni ya kuanzishwa kwa baraza ni wazi yana manufaa sana kwa maendeleo ya jamii yetu yote kwa ujumla na kwa sasa umuhimu wake ndio unazidi kuwa mkubwa zaidi kutokana na Lugha ya Kiswahili kuwa mojawapo ya Lugha zinazotumiwa katika vikao vya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja kati ya kero kubwa katika Baraza hili ni ukosefu wa majengo kwa ajili ya Baraza hili. Pamoja na ukweli kuwa Baraza la Kiswahili ni moja kati ya mabaraza ambayo yameundwa kwa muda mrefu sana uliopita, lakini imeshindikana kuwa na majengo yake hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliyoko madarakani imechukua takribani miaka 41 kuweza kugundua tatizo hili. Lakini hiyo si hoja sana, suala tunalolihoji ni ukweli kuwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi millioni 400 na katika bajeti ya 2007/2008 tulipitisha jumla ya Shilingi millioni 100**.** Hiyo ni jumla ya shillingi millioni 500, jasho la walipa kodi wanaotaabika wakichangia nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa ni miaka takriban minne, mwaka jana tulihoji lakini Serikali haikujibu kabisa suala hili, Je kiwanja kwa ajili ya majengo ya BAKITA kimepatikana? Au hadi sasa mchakato bado unaendelea na utaendelea mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Serikali iwaeleze Watanzania nini kinaendelea hadi sasa wakati fedha za walipa kodi million 500 zilikwishatengwa. Kama kupatikana kwa kiwanja kunachukua muda mrefu kiasi hiki, je kujenga itachukua muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa kunisikiliza katika kueleza hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Kilwa, lakini wewe ndiye Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Habari Michezo na Utamaduni, tunakuombea kila la kheri sijui kivuli chako kitaisha lini lakini tunakushukuru sana kwa uwasilishaji wako mzuri na umeweza kufikisha azma yako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza wasemaji wote waliopita, Msemaji wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, sasa tunaingia kwenye mjadala wa pamoja, na kama nilivyosema, msemaji wetu wa kwanza ambaye hajawahi kuchangia

kabisa ni Mheshimiwa Janet Kahama na ninaona yupo ndani ya ukumbi kwa sasa.  Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Janet Kahama aanze kuchangia na Mheshimiwa Elietta Switi atafuatia.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Naanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, aliyenijalia kuweza kuwa hai siku ya leo ili nami niweze kuchangia katika eneo hili  muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Sir George II Capt. Naona mnacheka lakini yeye mwenyewe anajua ni Sir George wa pili baada ya Sir George wa kwanza, pamoja na Naibu Waziri Bendera, ambaye ni hodari kwa michezo akiwemo Katibu Mkuu wao na viongozi mbalimbali katika eneo hili.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sintazungumza mengi sana kwani najua kazi waliyoifanya ni kubwa sana, huko tulikotoka ni mbali sana kuhusu masuala yote ya habari, michezo na utamaduni na kadhalika, kwa kweli mpaka hivi sasa hawa vijana wawili wamefanya kazi nzuri sana; hongereni sana.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nitoe ushauri kidogo kuhusu habari, wazungumzaji waliokwishachangia wamezungumza vizuri sana na wametoa mawazo mazuri sana kuhusu habari, sheria na haki wamezigusa, lakini ninachokiomba kwa wanahabari mara nyingi wanahabari wanapendelea sana wakati mwingine kuandika zaidi habari za mtu mmoja mmoja na matukio ya vitu kama hivyo, naomba sana wajikite zaidi katika maeneo ambayo ni ya muhimu ya maendeleo ya Taifa letu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru sana pale nitakapoona magazeti yote kwa ujumla yanaandika zaidi mbali na michezo na shughuli nyingine lakini yakiandika zaidi maendeleo ya barabara zetu nchini, maendeleo ya maji ni visima vingapi vimechimbwa, maendeleo ya elimu, maendeleo ya ustawi wa jamii na afya na kadhalika, mimi nadhani tukifika hapo tutakuwa tumemtendea mwananchi na Watanzania wote haki, lakini pia tutamfanyia haki Mwenyezi Mungu zaidi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba kidogo nichangie katika eneo la michezo, kwa kweli michezo imeendelea sana katika nchi yetu ya Tanzania, tunashukuru sana Serikali imejitahidi sana katika eneo la Michezo. Siku hizi kwa sisi tuliosoma zamani tulikuwa tukicheza michezo ya kushika kijiko na mayai, magunia, kuvuta kamba, *Netball* na kadhalika, hapa katikati miaka ya nyuma, hayo yote yalikuwa yamesinzia, lakini siku hizi ni lazima nikubali kuwa yamefufuliwa yote hayo na tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine katika eneo hili, wafikirie na kujitahidi sana katika eneo la wazee. Wawapatie mazoezi mazuri ambayo yanamsaidia mzee. Mazoezi yasiyokuwa na nguvu kuharibu afya, yaliyo ya taratibu, bila shaka mmeona mazoezi ya Wachina ni yale ya taratibu ambayo ni muhimu sana kuwawezesha wazee hawa waweze kuwa imara na kuishi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigusie eneo la utamaduni. Ndugu zangu katika utamaduni kumekuwa na mmomonyoko mkubwa sana katika nchi yetu, maadili yamemomonyoka sana. Mimi ninapoona watoto wadogo wakiwemo wajukuu zangu mchana wanaangalia sinema kama ile ya *paradise* na nyingine kidogo ninafikiri upande mwingine ni nzuri lakini upande mwingine sinema nyingine kwa kweli siyo nzuri. Tunashukuru kuwa wamejitahidi sana bodi kuhakikisha kuwa wamechuja chuja maeneo mengine ambayo si mazuri lakini naomba wazidi kuwa wakali katika nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utamaduni naomba nizungumzie kuhusu vazi. Vazi la Kitanzania mpaka sasa hivi mimi sijalijua ni lipi, kulikuwa na wanamitindo walikuja hata hapa Mlimani Club vazi likachaguliwa, lakini kila nikiliangalia lile vazi ambalo hata mimi nalivaa mara kwa mara, bado nakumbuka kuwa vazi lile lilikuwa hasa ni la nchi ya Ghana. Ninachotaka kusema vazi letu hata siyo moja tuna mavazi mazuri sana, tuna vazi la kimasai ni vazi la mvuto wa ajabu duniani kote, tuna vazi la kibarbaigi ni vazi zuri sana, lakini pia tukumbuke tuna khanga ambayo ni kipande cha nguo peke yake kimeanzishwa Tanzania na hakuna mahali pengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Swaziland wamejaribu kuvaa nguo hizo na bado wanazivaa lakini wanategemea soko lao kutoka huku kwetu, Japan walikuwa wakitengeneza, India wametengeneza Khanga lakini asili ya khanga ni vazi la Kitanzania na ni nguo ambayo zamani walikuwa wakijitanda tu na kujifunga na wanasema kuna aina mia moja ya kutumia khanga ambayo najua sisi sote tunazijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vazi hili lisiishie kwa wanawake lakini pia kwa wanaume, tunachoomba ni kupata wanamitindo wazuri na hata kama inabidi tuwaalike wenzetu labda kutoka Afrika Kusini, Afrika Magharibi, ambao kwa kweli wao wameendelea sana katika mambo haya ya *designing* ili waje watusaidie wakiangalia sana vazi la kimasai, kibarbaigi, wakitumia na khanga yetu; tufanye nini ili tuweze kupata vazi moja kwa wanawake na vazi moja kwa wanaume ambalo asilia tutasema hili ni vazi la Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ningekuomba sana niweze kuendelea kipengele cha maadili ambacho kama nilivyogusia hapo mwanzo, kumekuwa na mmomonyoko mkubwa sana. Mimi huwa nashtuka sana kila ninapotembea nakutana na watoto wadogo wakienda shule na wengine wako tu vijiweni, lakini mara nyingi mimi ndiye ninayeanza kuwaamkia watoto hamjambo, wanasema hatujambo na wengine Shikamoo, lakini kwa kawaida inabidi kimaadili mtoto ndiye anayemuanza mkubwa na tulikuwa tukitumia neno shikamoo, mimi sijali shikamoo ina maana gani wala sijali marahaba ina maana gani, lakini limekuwa neno la kiutamaduni kwetu. Sasa leo mtoto hawezi kumwamkia mkubwa mpaka mkubwa amwombe mtoto amwamkie, mimi nadhani huu ni utovu kabisa wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi unaweza kukuta ndani ya daladala au kwenye hafla fulani, watoto wamekaa, wazee wamesimama badala ya watoto kuwapisha wazee hili jambo halipo kwetu hata huko Ulaya kwenye mabasi unapoingia mtoto anajua kabisa kuna eneo la mama mjamzito na picha unaiona, lakini watu wazima

kuna eneo lao la kukaa, lakini mtoto hapa utamkuta ameng'ang'ania kwenye gari au kama kwenye sehemu nyingine ya tafrija akae tu wewe mtu mzima umesimama, mimi sijaona kitu kama hicho naomba mkazanie kabisa kungalia eneo kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nasema tuachane na desturi ambazo si nzuri na tabia mbaya ambazo pia tunaziiga nyingi sana kutoka nchi za nje, hasa tabia za kuvaa mavazi ya ajabu ajabu ya kuonesha miili yetu hata ukiwa na miguu mizuri namna gani, ioneshe kwa kipimo chake inapofikia nguo yako kuvuka magoti, hata tumbo likiwa zuri na hata kama umeweka kipini kwenye tumbo haina haja kuwaonesha watu wengine; umeweka kipini kwenye tumbo na kadhalika. Kwa hiyo, tuangalie sana maadili yetu hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, kuna tabia ambayo mimi naweza kusema iko kwa wasukuma zaidi lakini nimeona kabila nyingine wanazo za kupiga magoti mpaka leo tabia ya kupiga magoti mimi sijaliona. Lazima nimpongeze pia Mama Anna Mkapa kwa kipindi chake kingi, nakumbuka sana anapomsalimu mtu yeyote akiwa mke wa Rais alikuwa akipiga magoti. Kwa hiyo yeye ametupa mfano wa kupiga magoti kwa sababu anakumbuka alipotoka na yeye ni Mchaga, Wasukuma wao ndiyo kabisaa, humu ndani ya Bunge mnaona tunapigiana magoti. Kwa hiyo tuendelee kuhakikisha kuwa watu wengine hasa vijana wote wanafundishwa na wazazi wao waweze kuwa na mila na desturi nzuri kama hizo tusiziache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amezungumzia kuhusu suala la kuhifadhi picha Maktaba. Mimi nilikuwa nikiona kuwa maktaba kama hizo za picha za watu mashuhuri, picha za kale ningetoa ushauri tu zisiishie katika mikoa michache ziishie katika Mikoa yote ili wananchi wote waweze kujua kabisa kuwa wajasiri wa zamani walikuwa ni akina nani na watu mashuhuri wa zamani wote walikuwa ni akina nani. Hiyo nilitaka kutoa tahadhari kwamba isambazwe katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utoaji wa habari katika hilo, mtakapokuwa mmeweka katika maktaba yenu basi habari ziwe za usahihi, wakati mwingine kunakuwa na makosa ambayo yanafanywa, naomba wafanye tathmini nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu Baraza la Kiswahili (BAKITA), baraza hili limejitahidi sana kufanya kazi yake kutafsiri na kuendelea huku na huku lakini kwa bahati mbaya wanahitaji jengo zuri ambalo lina heshima yake na kazi wanayoifanya mpaka sasa hivi ni kazi kubwa sana. Tunavyoelewa sisi sote ni kuwa Lugha ya Kiswahili sasa hivi ni Lugha ya Afrika nzima na mimi nimekwishaona watu wakitoka Ulaya au wakiwa huko Ulaya wakifundishwa Kiswahili wakija hapa wanajua Kiswahili. Kwa maana hiyo Kiswahili ni Lugha ya Afrika; kwa hiyo tutendee haki, na nimefurahi hawa wasemaji wengine wamezungumzia kuhusu Kiswahili kuwa kitapanuliwa zaidi katika maeneo mbalimbali, kitaingizwa hata katika vitabu vyetu tunavyotumia Bungeni na katika vitabu vya bajeti, kitu ambacho kitatusaidia wengi na hasa wengi ambao hatutakuwa tunaelewa kiingereza kiasi hicho. Nimezungumzia kuhusu eneo hilo kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mama Kahama, kwa kweli kumbe ulikuwa unasubiri uchangie bajeti hii ukiwa na nia yako ya dhati. Niseme tu nakupongeza; umesahau kutuambia hilo suala la kupiga magoti kwa Wasukuma sijui ni wote wanaume na wanawake wanapiga magoti? Lakini pia hujatuambia vizuri na wale wazee watu wazima wanaoamkiwa Shikamoo badala ya kusema marahaba wanasema ahsante; sasa sijui hiyo nayo ndiyo utamaduni? Lakini yote Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya mambo haya, nadhani atatusaidia na namwona Mheshimiwa Sanya amecheka sana, sasa sijui ni miongoni mwa wanaoitikia ahsante! *(Kicheko)*

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, ninapenda sana nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa siku ya leo, lakini pia niombe Mwenyezi Mungu awabariki sana Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Joel Bendera na wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Habari Utamaduni na Michezo, kwa kufanya kazi katika mazingira magumu, lakini kazi nzuri inayotambulika ulimwengu mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imetupatia heshima kubwa kwa kuwezesha uwepo wa TV na Radio Tanzania ambazo zinatupa huduma kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya habari ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Katika haya ninaamini kabisa kwamba, vyombo vyetu vinafanya vizuri japokuwa vipo vyombo ambavyo vinamilikiwa na watu binafsi, ambavyo kwa namna moja au nyingine japo vinapewa uhuru bado watu hawa wanaomiliki vyombo hivi wanakuwa na malumbano ya mara kwa mara, ingawa sasa hivi tabia hii wameiacha na sisi tunasema huo ndiyo ustaarabu. Vyombo hivyo vya habari wakati mwingine vimetumika isivyo kwa maana ule uhuru umevuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamiliki hawa japo wameacha malumbano, bado wanaandika masuala ya watu binafsi badala ya kuandika masuala ya kitaifa. Tanzania ni nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki na nchi ya tatu katika Bara la Afrika katika kutumia vyombo vyake vya habari, lakini tunahitaji kuboresha mambo kadhaa. Jambo la kwanza ambalo tunapaswa kuboresha ni ile tovuti ambayo Rais wetu alisema kwamba iwepo na itumike ili kila mwananchi aweze kutoa mawazo yake kwa Serikali na aweze kutoa mawazo yake kuhusu mambo ya rushwa na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kuboresha ni kuhakikisha kuwa mfumo wa utangazaji kama alivyoeleza Waziri katika hotuba yake, unakuwa wa dijitali badala ya analojia ambayo inatumika sasa hivi ili tuweze kuingia katika ushindani wa kisasa kwa teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tunapaswa kulirekebisha au kulifanya ni sera yetu ili iweze kuingiza tovuti yenyewe na *blogs* ziingie katika sera ile.

Sera ya Habari na Utamaduni ya mwaka 2003 inasema habari na michezo ni biashara, kwa hiyo wale wanaokuwa katika fani hii walipwe vizuri na waweze kuenziwa kwa kazi zao. Tunaomba Sheria ya Habari ifike mara moja katika Bunge letu ili iweze kupitishwa na hawa wanaokuwa katika fani hii waweze kulindwa na sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maktaba zijengwe ambazo zitakuwa na vitabu na majarida, mabango na hata filamu ambazo watu wanaweza kwenda kutazama na kununua. Sasa hivi maktaba hizo zipo katika mashule na Vyuo, wengi wa wananchi hawajafikiwa na huduma hii. Lakini kama Serikali itathibitisha kwamba maktaba hizi zinajengwa mahali pote nchini walau kila Mkoa, tutakuwa katika mazingira mazuri na tunaweza kuwa tunahabarishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TV na Radio ya Taifa ni mali yetu Watanzania, lakini inasikitisha kama Redio yetu na TV yetu ina jengo kama ilivyoelezwa katika hotuba iliyowekewa msingi tangu mwaka 1995 hadi leo halijaendelezwa tuulize kulikoni, ni lini hili jengo litamalizika? Je, Serikali yetu haioni kwamba ni sifa au ni heshima kuwa na majengo ya Serikali ambayo tunayatumia sisi wenyewe na yakatupa sifa, lakini pia hawaoni kwamba ni hasara kwa jengo kama lile kukaa miaka yote hii bila kutumika wakati kuna fedha nyingi zimewekwa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri na wewe Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na kuliomba Bunge lako Tukufu ili Wananchi wa Rukwa wajue kwamba Serikali imeandaa kuwapelekea mitambo ya dijitali ifikapo Oktoba badala ya sasa ambapo *TBC* haisikiki kabisa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza *TBC* kwa kuchaguliwa kuwa watangazaji pekee wa soka ya kimataifa itakayofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Switi kwa mchango wako na nafikiri kule Rukwa wamekusikia. Ningeomba hiyo *mic* yako uizime ili umruhusu sasa msemaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Meryce Emmanuel ajiandae.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Utukufu, kwa kunipa uhai siku ya leo na kuniwezesha kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu, kutekeleza wajibu wangu ambao nimekabidhiwa na Wananchi wa Jimbo la Wete na Wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi sana ya kuchangia lakini muda ni mchache, nitagusia mambo machache ambayo pengine wengine watakuwa hawajayagusa. Kwanza, nitaangalia ukurasa wa 16 ambapo Waziri anazungumzia suala la mafunzo kwa Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa Habari kupata mafunzo ni jambo la wajibu na kama Serikali inatekeleza wajibu huo, basi inapaswa kupongezwa kwa hatua yake hiyo. Umuhimu wa mafunzo haya ni kuwapelekea Waandishi wa Habari kuweza kujifunza na kufahamu maadili ya kazi yao ili hatimaye wananchi na wadau wa habari wafaidi utekelezaji ulio bora wa Waandishi wa Habari hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili yaliyozungumzwa katika kitabu cha Waziri ni ukweli. Usahihi wa habari, amezungumzia kutenda haki, kuwa waadilifu, kuwa huru na mambo mengine kama hayo; sasa kama hayo ndiyo maadili ya mwandishi wa Habari hebu tutazame malalamiko ambayo yanakuja kwamba Waandishi wa Habari wanakiuka maadili yao msingi wake ni upi, kwa sababu ukikiuka maadili ya Uandishi wa Habari athari yake kila mtu anaijua; ni mvurugano katika jamii, usalama wa nchi unakuwa mbovu, matatizo baina pengine hata mke na mume inakuwa balaa katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapomlaumu Mwandishi wa Habari nimesema angalieni mzizi wa tatizo hilo, kama hao wanapata mafunzo katika vyuo ambavyo Serikali inavitambua, mafunzo ambayo baadaye watendaji hao wanapata vyeti; kufuzu mafunzo hayo inakuwaje maadili yanvunjwa, tuangalie mambo matatu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tuangalie waandishi wenyewe hulka na tabia zao, tuangalie taaluma ambazo zinatolewa katika vyuo hivi ambavyo wanakwenda Waandishi wa Habari kujifunza, lakini pia tuangalie tabia na mienendo ya wadau wa habari. Tukichanganya yote hayo tutaweza kuujua mzizi wa fitina ambao mara nyingi unaelemezwa kwa Waandishi wa Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani si vema sasa, panapotokea matatizo katika mambo ya uandishi kukimbilia vyombo vya habari au kuwafungia waandishi wa habari. Tuzame ndani tuangalie tatizo liko wako wapi, hatimaye tutafute dawa hata kama ni chungu lakini itatuwezesha kufikia mahali tukawa na maadili mazuri katika uandishi wa habari. Kwa hiyo, nashauri Wizara kwamba panapotokea kutofahamu baina ya waandishi na mwenye kuandikwa basi tuangalie katika nyanja tatu hizi, mafunzo wanayopata, wadau wenyewe wa habari na mwandishi mwenyewe wa habari kuliko kumtupia lawama mtu mmoja peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapenda sana waandishi wa habari na hasa wale ambao wanafuata maadili ya kazi zao. Waandishi wamekuwa wanaisaidia sana jamii, wanaelimisha jamii, lakini waandishi wanasaidia kutanabaisha, kuondoa kero za wananchi wetu. Mimi nasikiliza sana hizi radio na *TV* naangalia vipindi ambavyo kidogo vinanigusa gusa, vile ambavyo vinakwenda kinyume na maadili na mambo yangu huwa siangalii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mdogo, kuna radio moja inaitwa *Clouds FM*, *Clouds FM* wana watangazaji mahiri kweli kweli. Nitakupa mfano mdogo, juzi moja walikuwa na kipindi cha asubuhi kile ambacho wana swahiba wao mmoja wanamwita Bonge, Bonge siku hiyo aliamka siku asubuhi kwenda Kariakoo akakuta uchafu umekithiri sana. Bonge akasema hali ile halimgusi Diwani, Halmashauri, Mkuu wa Wilaya, bali linamgusa Mkuu wa Mkoa mwenyewe moja kwa moja. Lakini nashukuru Bonge kukata simu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa William Lukuvi Mbunge akapiga simu *Clouds FM*, kutoa maelezo, kukata simu Mheshimiwa Lukuvi wadau wa kutoa taka pale Dar es Salaam nao wakapiga simu *Clouds FM*. Matokeo yake nini? Alfajiri siku ya pili takataka zikawa zimeondoka. Kwa hiyo, wanafanya kazi nzuri. Siyo *Clouds FM* peke yao, lakini kuna waandishi wengi na watangazaji wengi ambao wanaisaidia jamii na wanaisaidia Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo maendeleo ya viwanja vya michezo. Kumekuwa na hatua mbalimbali za kuimarisha viwanja vya michezo na ni hatua ya kupongezwa kwa sababu kuendelezwa kwa viwanja vya michezo maana yake ni kuendeleza wachezaji. Sasa tulikuwa tunalalamika hapa siku nyingi kwamba kuna sehemu za wazi ambazo vijana wanatumia kwa ajili ya michezo vimevamiwa na watu binafsi ama kujenga nyumba, kujenga maduka au kwa jambo lolote lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wengine walilalamika kwamba viwanja vingi vya michezo nchini vimehodhiwa na Chama ambacho Mheshimiwa Waziri, anakiongoza. Sasa lalamiko hili mara nyingi jibu lake huwa linatolewa hapa Bungeni, lakini kwa mujibu ukiangalia taswira za watu wengine huwa wengine hawalifurahii. Sasa nadhani tufike mahali kwamba ikiwa tunalaumu wengine kwamba wanahodhi viwanja wazi kwa ajili ya kuwanyima fursa watoto kucheza michezo lakini pia ifike wakati pia na viwanja vyote vya michezo ambavyo vinahodhiwa na taasisi kama hizo virudishwe Serikalini ili kila mtu apate fursa ya kuvitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *FIFA* wanasaidia sana kuimarisha viwanja vya michezo, wana mradi wanaita *Goal project*, miongoni mwa viwanja ambavyo vinafaidika ni kile pale ambacho wataalam wa mambo ya televisheni hapa Bunge wanavionyesha. Lakini nilipata taarifa kwamba kuna kiwanja kilichoko Gombani, Pemba kitasaidiwa na huu mradi wa *Goal Project* wa *FIFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata habari kwamba kuna mpango wa kuweka nyasi za bandia katika kiwanja hiki, ni hatua ya kupongezwa. Lakini tatizo ni kwamba, hatuambiwi lini mradi huu utaanza na kwa sababu kule Pemba wanamichezo wanasubiri kwa hamu sana huu uwanja uweze kuwekwa nyasi za bandia kwa ajili ya kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uwanja huu ulijengwa na Wakorea, walipojenga uwanja huu waliweka ile minara ya kuwekea taa. Nyie huku mnasema kusimika minara, lakini ile minara haijawekwa taa bado. Sasa nilitaka kujua iwapo katika *project* hii baada ya kuziweka hizi nyasi za bandia katika uwanja wa Gombani hivi na taa za uwanja ule zitawekwa? Kama haumo basi namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu

tunaposema kwamba *world cup* itachezwa *South Africa* na pengine uwanja wetu wa Taifa wa Dar es Salaam utafaidika, Uwanja wa Amani wa Unguja na Uwanja wa Gombani Pemba ni viwanja vizuri ambavyo vikiendelezwa vinaweza vikachukua mechi kubwa za Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nigusie hii balaa iliyotokea hivi karibuni ya mvutano baina ya *TFF* na *ZFA* ambaye swahibu wangu, mpenzi wangu, rafiki yangu sana Mheshimiwa Hafidh alikuwa anazungumzia sana katika Bunge hili. Hawa watu wanavutana muda mrefu na kwa kweli aliunda kamati ya kutatua matatizo yao. Kamati hii Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Hafidh Tahir, Mbunge, Katibu wake ni Mwakalebela ambaye nafikiri ni Katibu wa *TFF*. Lakini watu hawa tangu mwaka 2006 hawajakaa kikao hata kimoja. Sasa sijui wanatatua kitu gani, umekuwa ni mzozo ndani ya mzozo. Sasa nadhani hawa watu pamoja na kwamba imeundwa kamati ya kutatua matatizo ya soko nchini lakini nadhani hiyo kamati pia ina matatizo, *Sub-hanallah*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua huu uonevu ni mwendelezo, ukiuanzia chini unaibuka mpaka juu. Nina taarifa hapa kwamba hata timu ya Taifa ya Zanzibar achilia mbali wachezaji wa timu ya Taifa ya Zanzibar ni wachezaji wa timu ya Taifa ya Muungano lakini timu ya Taifa ya Zanzibar ile kubwa ya *above* 20 ina wachezaji wawili tu kutoka Pemba. Lakini nina habari kwamba *under* 20 timu ya Zanzibar haina mchezaji hata mmoja kutoka Pemba. Sasa huu ni mwendelezo wa mambo, nadhani kabla hatujakwenda kuangalia kilemba kimechafukaje, pia tuangalie na shuka nayo imechafuka vipi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi lakini kwa sasa niipongeze Wizara, niipongeze Serikali kwa kurudisha michezo mashuleni na kwa kweli na ile hali ya ku-*promote* michezo ya SHIMIWI imetupelekea kupata timu bora za Taifa, iwe ni za wanawake, wanaume za *above* 20 na *under* 20 na leo tumearifiwa kwamba wamekuja makocha wapya kutoka *Cuba* ambapo kuna walimu wa *boxing*, kuna walimu wa riadha na mwalimu pia wa judo. Nimesikia pia katika taarifa ya habari makocha hawa watakuwa wanalipwa na Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba na Zanzibar nao wanapaswa kufaidika na makocha hawa waliokuja kutoka Kibaha. Naiomba Wizara na Serikali, mipango iandaliwe mahsusi, tusifanye katika makosa ya Mheshimiwa Tahir na watu wake, tuhakikishe kwamba makocha hawa pia wanatumika kusaidia michezo kule Zanzibar. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo kuhusu utamaduni. Tanzania ni tajiri sana wa utamaduni na hii inatokana na uwingi wa makabila ambao Tanzania inayo. Lakini mama Janeth Kahama kasema hapa utamaduni unamomonyoka na wakati utamaduni unamomonyoka, utamaduni wetu, sisi wenyewe tunachekelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize, hivi hawa bibi zetu walipokuwa wanacheza ilikuwa ni lazima wakate viuno?

**MBUNGE FULANI:** Kunyonga kiuno.

Haya kunyonga kiuno. Nitatoa mfano mdogo, nakumbuka ngoma ya Msewe kule Pemba wanacheza wanaume na wanawake, wanaume wanafunga mang'anja miguuni, wanacheza miguu na mabega, lakini akina mama wanacheza shingo peke yake na kichwa. Sasa Msewe siku hizi ukiangalia hautazamiki kwa watu kama sisi, hatuwezi kuuangalia tena. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Wanacheza viuno vitupu. (*Kicheko*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Yaani badala ya kutoka kwenye shingo umehamia kwenye kiuno sasa huu si Msewe. Kwa hiyo, tunaharibu ngoma zetu kwa sababu tunadhani kwamba kunyonga kiuno ndiyo uzuri wa kucheza ngoma na hii tunaichekelea na tunaendelea kuichekelea na ni tatizo, tunaharibu tamaduni zetu kwa sababu tunadhani kwamba kwa kufuata wageni wanavyofanya tutakuza tamaduni kumbe tunaharibu utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba *TBC* wanafanyakazi kubwa sana, pamoja na vyombo vingine vya habari kama *channel Ten* na wengine. Tatizo ni moja kwamba, ndugu zetu jamani wa *TBC* wanafanyakazi katika mazingira magumu. Wanaishi katika nyumba ambazo siku za mvua wanaweka ndoo kukinga maji kujizuia wasilowe, kule maeneo ya Pugu kuna jengo wanakaa pale. Pia wana jengo liko Mikocheni ambalo hata Mheshimiwa Masoud amelizungumza kwamba limewekwa msingi na tangu Rais wa Awamu ya Pili, lakini hadi hii leo jengo bado ni gofu halijamalizwa na kwa maana hiyo tunawapata tabu hawa watendaji wa *TBC* kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Sasa nadhani tufikirie kumaliza jengo lao hilo ili wahamie kule, wafanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waandishi wanafanyakazi katika hali ngumu sana, mishahara yao ni midogo, marupuru madogo na inatokea kuna baadhi ya waandishi inabidi sasa kununuliwa au kuhongwa kuandika habari za watu fulani na hii ndio nikasema maadili yanavunjwa pia na watu wengine. Sasa nadhani tuwafikirie sana waandishi wa habari, wanafanyakazi katika mazingira mazito mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hivi waandishi wa habari hapa nchini kwetu hawawezi kuandika habari za uchunguzi (*investigative*) maana wote wanaandika habari za leo tu, mtu kapigwa, kapotelea mahali, kafanya hivi, lakini habari za uchunguzi wa kina kakupa mtu kitu kizito chenye ushahidi wa kutosha sijaziona. Je, taaluma hii haisomeshwi, maana hakuna waandishi wanaofanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa umefika wakati Serikali na Wizara kwa ujumla ijitahidi kusomesha waandishi kwa mintarafu kwanza kulinda maadili yao, lakini pia kuwapa ujuzi wa kuweza kutambaa katika nyanja zote za uandishi ili umahiri wa waandishi uongezeke na wananchi wafaidike na taaluma ya uandishi na kuweza kutuletea maendeleo katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Jecha lakini ilikuwa inanipa shida kidogo kutafsiri maana ya utofauti wa uchezaji wa Msewe na Sindimba kule anakotoka Mheshimiwa Waziri. Sasa sijui Sindimba nayo wanacheza kwa kutikisa vichwa ama Lizombe kule Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, huo utamaduni Mheshimiwa Waziri utautafakari wewe mwenyewe.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nami ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu mchana wa leo.

Lakini pia naomba tu nipongeze Wizara ya Utamaduni na Michezo kwa kazi nzuri wanayofanya na *speed* waliyonayo ni nzuri kwa kweli, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana na bajeti yao ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia upande wa maadili ya nchi yetu ya Tanzania. Ni kweli inawezekana ni jambo la kawaida na wakati mwingine limeshaonekana ni jambo la kawaida mtu akizungumza linachukuliwa tu ni jambo la kawaida. Lakini kimsingi kweli sasa hivi tunakokwenda nadhani siyo kuzuri na kama Serikali itanyamaza na Wizara itaangalia kila kunapokucha mabadiliko yatakuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia upande wa wasanii wa michezo. Michezo ya waigizaji wanayoigiza kwenye *TV* wanaigiza michezo mingi tu. Nashukuru Mungu sasa hivi Tanzania tuko kiwango cha juu sana kwa kuigiza. Uigizaji umekuwa ni mkubwa, unapanda siku hadi siku. Lakini ninachotaka kuzungumza ni jambo moja, pamoja na michezo kuwa mizuri sana lakini naona kuna sehemu fulani ambayo kule tunakokwenda kimaadili inakuwa si nzuri sana na hasa watoto wadogo wanapokuwa wakiangalia ile michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto sasa hivi wanapenda sana kuangalia michezo na bahati nzuri inaonyeshwa wakati wa usiku wametoka shule wamepumzika na wanajua ratiba ya michezo kila siku. Inafikia mahali waigizaji wanaonyesha wakati mwingine kwamba mama na baba ni familia moja, lakini wakati mwingine yule mama anatoroka katika familia yake anakwenda upande wa pili au baba anatoroka anakwenda wanaita nyumba ndogo. Lakini wanapokuwa wamefika kule nyumba ndogo kinachoonyeshwa pale ni kitu kimoja ambacho kwa kweli kwa watoto si kizuri sana. Wanaanza mambo mengine ya kawaida, mabusu kama kawaida na nini. Lakini wakitoka hapo wanaonyesha kwamba sasa wamelala. Lakini wanapokuwa wamelala lile shuka linakuwa liko *busy* sana linatikisika sana. Lile shuka linapokuwa linatikisika mama anaonekana amevua na baba anaonekana amevua. Sasa ule mchezo wa shuka wale watoto wanajiuliza kinachotikisika mle ndani ni kitu gani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja kugundua pamoja na kwamba tunawaona wale ni watoto wadogo, kila kunapokucha anapoangalia anajifunza kitu. Siku moja nimekaa pale naangalia na mtoto wa kaka yangu ananiita shangazi, ana miaka sita tu, sasa

akamuona yule mama ametoka ndani ya ile familia akakimbia akaenda kwa baba mwingine wa nje, walipofika vile vile nilivyowaambia wakaingia chumbani, wakapanda kitandani, kavua nguo mama na baba kavua nguo kapanda kitandani. Shuka wamejifunika hadi huku lakini liko *busy* linatikisika kweli. Sasa yule mtoto akauliza sasa shangazi huyu mama mimba itakuwa ya yule baba wa kule au wa huku? Sasa nikajiuliza yeye amejuaje kwamba baada ya hapo kunakuwa na mimba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la muhimu sana, ni kweli kabisa tunakokwenda siko. Michezo ni mizuri nakubaliana nayo na napenda kutazama lakini wanapofika katika *stage* ile sioni kwamba inamaanisha nini pale. Kwani ni lazima waonekane wamevua na wanatikisa lile shuka? Kwa nini wasiigize wakaonekana wanapendana, mabusu ni jambo la kawaida, mimi naweza nikambusu hata Mheshimiwa Sanya, ni jambo la kawaida, hiyo inatosha. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini si kweli kwamba mvue nguo wote, watoto wanatazama. Mungu pale anaangalia. Yaani hata mama uko pale, baba yuko pale, watoto wako pale, unashindwa hata kutazama. Unaweza ukaondoka ukawaachia watoto na mtoto ukishamzuia kwamba usiangalie, nataka nikuambie atatafuta kila njia mpaka aangalie kwa nini unamzuia asiangalie. Kwa hiyo, nashauri Wizara ya Utamaduni na Michezo hebu wawe na mpaka hawa waigizaji. Sasa hivi hicho ndicho wanapenda sana sijui wamegundua nini kule, huko ndiyo wanapenda kweli, mchezo mpaka mashuka yatikisike, mpaka kufanyike nini. Sasa najiuliza kwani maigizo ni hayo tu, mbona kuna mambo ya kujifunza? Kwa sababu ninachojifunza hapa hawa wanaigiza ili tuweze kujifunza mambo fulani fulani na ambayo kweli yanatokea katika jamii yetu. Lakini siyo lazima kila mchezo mpaka ufanye vile, kwa nini mingine wasicheze tofauti na pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimeona nilizungumze hili na wengi limewagusa na wananchi hawapendi hasa watoto tulionao, watoto ni wadogo, wanakua, kwa hiyo unakuja kujikuta kwamba unajiuliza huyu mtoto kakijuaje kumbe amekijua kwa sababu toka ana miaka sita amekuwa akiangalia mwisho na yeye anaelewa. Tena wakati mwingine hafundishwi na mtu yaani ule mtikisiko atataka ajue mle wakivua wanatikisa nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwa kweli Wizara iwe *serious* kabisa kuwaambia wacheze lakini wawe na mpaka ili watoto wetu wapate cha kujifunza ambacho hakitawaharibia tabia yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tena nichangie kwa upande wa michezo pia lakini hawa wanamichezo wetu, inaniuma sana, ninapoona akina baba wanacheza na suti, tena mimi afadhali wacheze na mashati kuliko suti. Anacheza na suti yake nzuri, kiatu chake kizuri, lakini mama anacheza nakuambia yuko uchi hata hatamaniki tena. Yaani wakati mwingine tumbo mpaka hapa huku sijui katoboa nini kaweka vipini kwenye vitovu, nakwambia kachorachora mwili wote, akicheza huku nakwambia aisee, inaniuma sana. Yaani naona kama wanawake wanachukua nafasi ya kutudhalilisha si kweli eti mtu ucheze uwe uchi ndiyo uonekane unacheza vizuri. Vinginevyo hata sisi tulioolewa, kama kupata mwanamke mpaka awe uchi basi na sisi waume zetu wangetukuta tuko uchi

tumesimama tunawasubiri, nakusubiri nikiwa uchi ndiyo sasa unipende. Kwa hiyo, ninachotaka kusema siyo kwamba mtu akicheza uchi ndiyo unampenda si kweli, hiyo ni kudhalilisha wanawake, ni kweli kabisa tunadhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize, kwa nini wanaume wanakuwa wamevaa suti zao, wasipovaa suti wanavaa tisheti za mikono mirefu. Kuna Mheshimiwa mmoja anapenda kuvaa tisheti ya mikono mirefu meupe, anapendeza sana, akivaa ni nguo ya heshima. Wao wanavaa nguo zao ndefu, suruali safi, anapendeza anacheza muziki. Akina mama wakishatoka kule wanakuja kunengua, basi nakwambia anakuja uchi, ukimwangalia roho inauma sana. Wakati mwingine unaogopa hata kumwambia mtoto twende ukangalie huko michezo na wewe angalau utembee maana ukishafika kule mtoto akiangalia anasema daa! Naona mama naye mchezo wake ndiyo huu nini? Sasa kwa kweli inakuwa haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa kweli kila kunapokucha, yaani kuanzia leo kuja kufikia mwakani kipindi kama hiki watakuwa wako uchi kabisa kabisa. Wakati mwingine wengine wanakuja kucheza Bungeni hapa, eti na wenyewe wanacheza uchi, sisi wanatuchezea uchi, sisi hatutaki uchi. Wanapokuja Bungeni waje kwa nidhamu, wavae nguo zao nzuri wacheze, kama ni kaptura vaa pensi ucheze au vaa nguo ya adabu ucheze. Sasa wanakuja Bungeni, hawaoni hata aibu kwamba hawa ni Waheshimiwa Wabunge, basi ndiyo wanakuja wamejipanga kweli kweli kukaa uchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba iko haja ya kuelewa kwamba hapa mahali ni muhimu, wasije uchi uchi hapa, wanakatikatika, haipendezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Jecha, amesema kwamba kukata kiuno ni lazima? Nasema bora wakate kiuno lakini wavae kwa sababu mtu akikata kiuno kavaa haiumizi sana. Sasa mtu anakata kiuno halafu yuko uchi, mwili wote una mabaka mabaka. Halafu akivaa nguo huku, huko nyuma na kwenyewe hajaridhika kwamba nguo iishie hapa bado anaishusha basi anakatika anageuka huku kututazama. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kugeuka na kututazama kwa kweli haipendekezi. Narudia tena kwa kweli haitupendezi hata sisi wanawake wenzenu kwa kweli mnatuaibisha, mchezo ni mzuri lakini siyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Wizara itaangalia jambo hili, kucheza wanacheza vizuri na sisi tunakwenda tunatazama lakini wavae nguo angalau kidogo zinazoonyesha kiuficho kidogo na nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la michezo mashuleni. Ili mchezaji aweze kuwa mzuri ni lazima aanze michezo akiwa mdogo. Ni kweli kabisa sasa hivi mashuleni mtoto anapoanza darasa la kwanza mpaka kumaliza darasa la saba hajacheza, kiasi fulani michezo imepungua sana, kasi yake imekuwa ni ndogo mashuleni. Lakini nilichokuwa nashauri na bado mashuleni wanahitaji kuwa na vifaa vya michezo kama mipira, jezi na inawezekana. Nafikiri kwamba ipo haja Wizara ijaribu kuangalia ili iweze kumjenga mtoto kutoka mwanzo akiwa mdogo na kipawa chake kiweze kujulikana, michezo ipewe kipaumbele mashuleni ili watoto waanze kujifunza wakiwa

wadogo, wanakwenda anakuwa mchezaji mzuri sana kuliko ambavyo labda angeparamia akiwa labda sekondari, inakuwa ni shida kwa sababu ule mwili wake na akili zake na ufahamu wake unakuwa haujajipanga vizuri kwenye masuala ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba Wizara ijaribu kurudisha kama vile ilivyokuwa zamani michezo mashuleni ili watoto waanze fani ya michezo wakiwa wadogo kabisa na hata hivyo inamsaidia mtoto mwili wake unakuwa ni mzuri, unakaa vizuri na unakuwa ni imara. Hata kama kunatokea tatizo kama mabomu yalivyotokea Mbagala watoto wanakimbia, watoto wana mazoezi inawasaidia sana wakati mwingine kuepuka mambo fulani ya ajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la viwanja vya michezo. Halmashauri nyingi zimetenga viwanja vya michezo kwa ajili ya watoto wadogo. Hawa wadogo nawazungumzia labda darasa la kwanza, la pili, tatu, nne, tano mpaka la sita. Kuna viwanja maeneo fulani yameachiwa mle katikati labda mjini sehemu fulani wajifunze michezo. Lakini alivyosema Mheshimiwa Jecha kusema kweli, ni kweli kwamba viwanja hivi vinataifishwa na kweli wanaotaifisha ni wenye nguvu kama alivyosema, nadhani Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni wao tu wenyewe wanaoweza kuvitaifisha viwanja hivi. Kwa hiyo, nashauri kwamba, kwa faida ya wao na jamii nzima kwa ujumla, iko haja ya viwanja hivi kurudishwa kwa watoto ili waweze kuendelea na michezo yao wanapokuwa wametoka mashuleni jioni au asubuhi kwa siku za Jumamosi, Jumapili na wanapokuwa hawaendi shule ili wajaribu kuendelea na mazoezi. Nadhani hata Serikali ilikuwa na sababu za msingi za kuacha viwanja hivi ili watoto waweze kucheza michezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwamba Wizara iagize na iwaambie Halmashauri zote kama kweli kuna viwanja hivi katika maeneo mbalimbali watoto wapewe uhuru wa kuvitumia viwanja vile na watumie nafasi yao kwa ajili ya kufanya mazoezi na kuendeleza michezo yao kwa sababu viwanja hivi vimewekwa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na machache tu lakini kikubwa ni kule kuchezacheza uchi na mashuka kutikisika. Mambo hayo yananiuma kweli, nadhani Mheshimiwa Waziri ayatilie maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Meryce kwa kweli nadhani atakuwa amevuta hisia za Watanzania wengi katika kuona ni kwa jinsi gani utamaduni wetu na hasa kwenye masuala haya ya muziki wa kileo yanaweza kuzingatiwa. Maneno uliyoyatumia leo kwa kweli tutatafuta Kiswahili chake fasaha kiweje lakini kwa kweli ujumbe umefika mahali pake.

Naomba kabla sijasitisha shughuli hizi niwataje wachangiaji watakaoanza kuchangia mwanzo ili kusudi waweze kujiandaa na kuja ukumbini mapema. Kama nilivyosema tutaanza na Martha Mlata, Mheshimiwa Kingunge Ngombale–Mwiru, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Bakar na muda ukituruhusu basi tutaendelea na

Mheshimiwa Juma Killimbah na kama utaturuhusu zaidi basi tutaendelea na Mheshimiwa Manju Msambya na Hafidh Tahir. Lakini tutaangalia ni namna gani tutakavyokuwa tumejipanga ili tutoe muda kwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri waweze kuhitimisha hoja yao na Bunge liweze kupitia kwenye sehemu ya Kamati na kuhitimisha hoja yenyewe kwa ujumla.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa michango yenu ya asubuhi. Naomba nisitishe shughuli hizi na tutakutana tena saa kumi na moja jioni ili tuweze kumalizia.

*(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge poleni na shughuli za leo, najua wengine mmeunganisha shughuli zenu za mchana, hamjapumzika mmendelea kuwajibika, basi sasa tuingie kwenye shughuli ya jioni ambayo itatupelekea kuhitimisha hoja iliyoletwa leo mezani. Kwa hiyo, kabla sijaendelea nimwite Katibu ili atupe utaratibu wa shughuli yetu. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano na kama nilivyosema msemaji wetu wa kwanza leo jioni atakuwa Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii, pamoja na kwamba ilikuwa nichangie asubuhi lakini nilikuwa sijisikii vizuri ilibidi nikapate matibabu. Lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ameniwezesha kusimama hapa ili niweze kuongea jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa hotuba nzuri ambayo inatia matumaini, hivyo niwatakie baraka za Mungu wetu ili waweze kufanya kazi vizuri kutokana na hotuba jinsi ilivyoeleza. Pamoja na ufinyu wa pesa ambazo wamekuwa wakipata lakini wamekuwa wakifanya kazi kwa moyo na tunaona matunda yake katika sekta mbalimbali Wizarani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa imani kubwa sana aliyonipa kwa kuniteua kuwa mjumbe wa Bodi ya Baraza la Sanaa Tanzania. Basi nimhakikishie tu kwamba imani hiyo nitaitetea vizuri kwa kufanya vizuri kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi na shukrani hizo, nilikuwa napenda nizungumzie suala la sekta ya habari na utangazaji. Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa *TCRA*, wamekuwa wakifanya kazi nzuri katika kusimamia vyombo vya utangazaji hapa nchini na matokeo yake tunayaona kwa sababu yamefika mpaka kule vijijini hata asiye na uwezo wa kununua gazeti lakini anakuwa na redio shambani. Kwa hiyo tunatoa pongezi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachopenda kuomba tu ni kwamba, waendeleze msimamo wao vizuri kwa zile taratibu ambazo wamejiwekea kuweza kuvi-*monitor* vyombo vya habari ambavyo vinaondoka kwenye mstari. Hapa Bungeni tumekuwa tukielezwa Muswada wa Sheria ya Utangazaji utaletwa hapa Bungeni.

Sasa huu ni mwaka nafikiri wa tatu lakini bado haujaletwa na leo tena Mheshimiwa Waziri kasema. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze huu Muswada utakuja lini? Kwa sababu tangu mimi nimeingia Bungeni, imekuwa tutauleta, tutauleta. Naomba uletwe ili uje urekebishwe twende na wakati, kwa sababu Waswahili wanasema hakuna haki bila wajibu, hakuna demokrasia bila nidhamu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba huo Muswada uletwe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nizungumze jambo moja na wenzangu wanahabari wanielewe vizuri kwa sababu nina nia nzuri. Kuna haja ya vyombo vya habari kupigwa msasa. Nikisema kupigwa msasa kwa maana ya kwamba ule Utaifa, kwa maana ya kwamba ile *National Interest*. Maana yake kuna habari ambazo zinakuwa zikitolewa za upotoshaji lakini bado watu wanakuwa hawaelewi nini madhara ya habari zile ambazo zinawekwa kwenye magazeti au kwenye vyombo vyetu. Tunalidhalilisha Taifa letu au tunalinyima Taifa letu haki ya msingi ya kukuza uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema kwa maana hiyo. Zamani kulikuwa na chombo ambacho kilikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kilikuwa kinaitwa *Mass Mobilization*, hawa walikuwa wanapita mashuleni, wanapita majeshini, wanapita maofisini na vyuoni kuelimisha nini maana ya uraia, nini maana ya usawa, nini maana na faida hasa katika utoaji wa habari. Kwa faida ya Taifa letu, kwa usalama wa Taifa letu, kwa usalama wa uchumi wetu, kwa hiyo naomba kabisa Wizara hii iwasiliane na ofisi ya Waziri Mkuu hiki kitengo kirudishwe ili vyombo vya habari vipigwe msasa, watu wawe na Utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano, kwa mfano, gazeti linasema kwamba mafua ya nguruwe yaitikisa Tanzania. Unategemea nini kwa mgeni aliyetazamia kuja Tanzania? Lazima ataahirisha na kama kuna pesa zilikuwa zinakuja Tanzania ndiyo basi. Kwa hiyo, lazima tunapotoa habari tufikirie mara mbili, tatu. Nataka kusema Taifa letu liko katikati ya Mataifa yenye ushindani wa kiuchumi. Sasa kama tuko katika ushindani wa kiuchumi, watu wanaweza kutumia watu kuja kuharibu na kukwamisha uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo naomba tuwe makini Mheshimiwa Waziri awasiliane na Ofisi ya Waziri Mkuu hiki kitengo kirudishwe ili watu waweze kuelewa nini maana na faida ya *National Interest* au kulinda maslahi ya Taifa hili au usalama wa Taifa hili. Lakini bado nataka kusema, kuna habari za upotoshaji ambazo zinatolewa kwa maandishi makubwa sana. Mtu akatoa tu lakini kesho yake anaweza akaja aka-*apologise*. Lakini katika kuomba radhi anaomba kwa maandishi madogo sana na aliyesoma jana sie atakayesoma leo. Kwa hiyo, yule ameshaondoka na ile dhana itakayopelekea Taifa letu kuingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri bado nashikilia pale pale, hiki kitengo kitakuwa ni muhimu sana katika kusaidia utoaji wa habari kwa faida ya Taifa letu. Lakini bado niseme tu kwamba, pamoja na msasa huo, bado waandishi wetu wa habari wapatiwe fursa za kwenda kusoma ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo kuanzia televisheni ya Taifa, televisheni za watu binafsi, vyombo vya watu binafsi viwasomeshe wafanyakazi wao ili wafanye kazi nzuri. Haiwezekani mtu umemchukua miaka mitano yuko palepale. Utoe pesa afanye kazi nzuri upate pesa. Lakini bado hawa waandishi, nasema tunaweza tukawa tunagombana nao kila siku kwa kuwalaumu lakini uangalie wana maslahi gani huko wanakofanyia kazi? Ni kweli wanalipwa vizuri? Ni kweli wanapata stahili yao? Nilikuwa naomba *TCRA* izingatie hili, ifuatilie hili iweke kima kile kizuri kitakachowaridhisha waandishi wa habari au watangazji au wote watakao kuwa wanafanya kazi katika sekta hizo. Isije ikawa watu hawapati chochote, kwa hiyo mtu anaandika habari ile ambayo anaona kwamba atapata mradi wake. Bado ile dhana ya kulinda usalama wa Taifa letu itakuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la Utamaduni. Nikija kwenye suala la Utamaduni, kitengo hiki kimekuwa kikipigwa danadana sana. Tangu nchi hii kupata uhuru hakujawa na Wizara ya Utamaduni peke yake. Imekuwa ikisukumizwa tu mara huku kina–*hang* na wala hakitengewi bajeti, kinagawiwa kidogo, kwa hiyo hata utendaji wake wa kazi unakuwa ni wa kusuasua. Ndiyo maana hata wasanii wote Tanzania na wenyewe wamekuwa ni wa ku-*hang hang*, mara wanaambiwa mwende viwanda na biashara kuna *COSOTA* kule, wakienda kule wanaambiwa rudini, juzi nimeuliza suala la *COSOTA* ananijibu Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Bendera, sasa hakuna mtu wa kujali katika sanaa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wamekuwa wakiibiwa kazi zao, hakuna mtu wa kuwatetea, kazi ziko barabarani tunaziona, maaskari wananunua, Mawaziri wananunua, Wabunge wananunua, Makatibu Wakuu wananunua kazi zile zile zilizo haramu. Hakuna wa kuzikamata na hata wakikamatwa, juzi nikamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, akanijibu faini yake ni elfu 20. Halafu mtu anaachiwa na mzigo ule ulio haramu anaondoka nao. Hiyo haki iko wapi? Tumeomba Sheria ije hapa irekebishwe hakuna wa kujali kwa sababu hiki kitengo cha Utamaduni cha Sanaa kina-*hang* hakina wenyewe. Nikawa nimeomba kwamba pale Wizarani litengwe dawati, kiwe na kitengo maalum cha kushughulikia Sanaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi katika hotuba hii nilitegemea angalau kuna chochote kitasemwa hakuna. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri unisaidie hilo hawa wasanii wako wapi? Lakini pendekezo langu, naomba iundwe Wizara ya Utamaduni na Sanaa peke yake ili iweze kukuza uchumi wa nchi hii kupitia Sanaa. Nchi zilizoendelea wanaendesha kitaalam na ndiyo maana wasanii wote hali zao ni nzuri na uchumi wa nchi zile zilizoendelea unachangiwa na kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, kuna lile jengo la nyumba ya sanaa, ningependa sana Mheshimiwa Waziri anisaidie kunipa maelezo. Lile jengo lilitolewa na

Ikulu, Serikali ya Norway ikajenga kwa ajili ya kazi za sanaa. Sasa hivi imekuwa kijiwe. Mwaka jana nimeuliza sikujibiwa, Mheshimiwa Waziri leo naomba anipe jibu. Lile jengo liko chini ya nani? Nani analiendesha sasa hivi kwa sababu naona kuna *club* pale, kumekuwa sijui ni *business center* na bado kuna majengo mengine yako Kurasini yako chini ya nani? Ni nani anayamiliki na hizo hela zinakwenda wapi na Serikali inapata faida gani na kuna mkakati gani wa kurudisha mikononi mwa wasanii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jengo lile na majengo yote yarudishwe mikononi mwa wasanii ili tuweze kufanya shughuli zetu pale kama ilivyokuwa mwanzo. Walemavu walikuwa wanafanyia shughuli zao pale, nyumba ya sanaa, wanaendesha maisha yao pale na mafunzo yalikuwa yanafanyika pale. Naomba nipate majibu sawasawa, naona pale kama kuna kaufisadi ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine labda nizungumzie ni vazi la Taifa. Wizara hii iliandaa tamasha, Mashindano ya Vazi la Taifa likawa limepatikana. Lakini sijaona juhudi zozote ambazo zimechukuliwa na Wizara hii kuendeleza vazi hilo, lipo au halipo na kama halipo Wizara inafanya nini ili tuwe na vazi la Taifa? Kama viongozi hawavai nani atavaa au nani ata-*promote*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wetu hawakopesheki, zamani kulikuwa na Mfuko wa Utamaduni, naomba Mfuko huo urudishwe ili wasanii wetu waweze kwenda kuchukua msaada pale kama ilivyokuwa zamani. Maanake ukienda kwenye mabenki nani anakujua? Utaitwa msanii, utaitwa msanii kweli na wala hautapata msaada wowote utabakia una–*hang*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri asaidie huo Mfuko urudi ili wasanii hawa waweze kukimbilia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba kujua *COSOTA* inasaidiaje wasanii? Iko Wizara ya Habari na Michezo na Utamaduni au ipo Viwanda na Biashara na kwanini tuwekwe pale katikati? Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, naomba hii *COSOTA* inaingiaje kwenu, nimeuliza maswali ya *COSOTA* ninajibiwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Naomba nipatiwe majibu, lakini bado kuna suala la elimu kwa wasanii, kile Chuo cha Bagamoyo hakitoshi wasanii ni wengi. Hivyo nilikuwa naomba Wizara ishirikiane na wadau mbalimbali ili iweze kusaidia kutoa mafunzo kwa wasanii wetu. Kuna *studios* nyingi ziko zimejaa kila mahali. Vijana wa kike na wa kiume wanahangaika kuingia kwenye *studios* zile hakuna utaalam wowote. Unaanza kurekodi mwezi wa kwanza mpaka mwezi wa kwanza bado hujamaliza unahangaika *studio* na tunasema tunaongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado ninao muda nirudi kwenye Habari ya Michezo Kandanda, Riadha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa kuzungumza Mheshimiwa Mbunge umekwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa mchango wako na kwa kweli nadhani kwa sababu Wizara hii inahusika pia na lugha ya Kiswahili hata ile tabia ya kutoa maana ya usanii kama tafsiri potofu ya kitu kisichofaa inatakiwa nayo ipigiwe kelele ili heshima ya wasanii iendelee kubaki mahali ambapo inatakiwa. Basi nakushukuru Mheshimiwa Mlata Msanii. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru na Mheshimiwa Faida Bakari ajiandae.

**MHE. KINGUNGE N. MWIRU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nishiriki kwenye mjadala huu. Jambo langu la kwanza ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Naibu wake Mheshimiwa Bendera na watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutumia nafasi hii kusema mambo machache. La kwanza, linahusu sekta ya habari. Sisi Watanzania tumepiga hatua kubwa sana katika kupanua uwanja kwa vyombo vya habari na vilevile kutoa nafasi ya uhuru kwa vyombo vya habari. Ukitaka kulinganisha na nchi nyingine za Afrika, ni nchi mbili, tatu tu ndizo ambazo zinalingana na hatua ambazo tumeweza kuzifikia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mafanikio hayo, yako mambo ambayo bado inafaa tuyafanyie kazi kwa sababu vyombo vya habari ni vingi lakini Waswahili walisema wingi si hoja, suala kubwa zaidi ni ubora wa vyombo. Sasa katika fani hiyo ya ubora, tumepiga hatua kubwa. Sasa hivi tunao waandishi wa habari ambao wamesomea vizuri na wana uweredi wa kupigiwa mfano, lakini wengi watahitaji kupata msaada mkubwa. Ndio maana nakubaliana na wenzangu wanaosema kwamba, lazima tuendelee kuwasaidia Waandishi wetu wa habari wapate mafunzo ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio mafunzo tu ya jumla, nadhani waandishi wetu wa habari sasa, waanze kwenda kwenye michepuo, waanze kubobea, wazamie katika maeneo fulani fulani. Katika nchi za wenzetu utakuta waandishi wa habari wamebobea katika masuala ya kilimo, wengine katika biashara, wengine katika masuala ya michezo na kadhalika. Kwetu sisi wengi ni waandishi wa habari wa jumla jumla tu. Kwa hiyo nadhani msaada mkubwa watakaohitaji ni kwamba, wale ambao wamejitokeza, wamejisomesha na wamesomeshwa, basi waingie sasa katika kubobea zaidi katika maeneo fulani fulani kusudi wawe *specialists* watusaidie kufanya uchambuzi wa mambo sio kuandika mambo kwa jumla jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala zima la maadili ya uandishi. Haitoshi tu kuandika lakini kwa sababu uandishi wa habari ni taaluma, kuna maadili yake. Sisi wengine pamoja na kwamba, si waandishi wa habari lakini tunao uzoefu vilevile unaohusiana na maadili ya uandishi wa habari. Nadhani vilevile tunahitaji kazi kubwa ifanyike. Najua yapo mambo mengi yanayoingilia kuvuruga uandishi wa habari, sio waandishi wa habari wenyewe tu, kwa sababu kuna wamiliki nao wanaingiza mambo yao binafsi, lakini kuna watu binafsi wenyewe wa nje wenye maslahi yao wanaingia kuvuruga maadili ya uandishi wa habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningependa niseme kidogo juu ya michezo. Kwanza ni kumpongeza hasa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hatua ambazo amezichukua kwa upande wa michezo, kwanza kwa upande wa mpira wa miguu. Sasa mambo yetu nadhani yameanza kunyokanyoka kidogo, lakini naona sasa Waziri Mkuchika ametuletea *comrades* wa Cuba. Nasema hizi ni hatua za kupongezwa, endeleni kufanya hivyo, vijana wetu wanavyo vipaji wanachohitaji ni msaada wa mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa vilevile nishauri kwamba, lazima tuamue hasa. Michezo ijikite shuleni, ijikite katika vyuo, ijikite katika majeshi yetu, nadhani maeneo hayo ndiyo maeneo ya michezo. Kwanza ni muhimu kwa sababu ndiko waliko vijana. Lakini pili, michezo ni ushindani, kwa hiyo tutaweza kujijengea jina kubwa sana kwa upande wa mashindano ya vijana na vijana wenzao katika sehemu nyingine za Afrika na dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye suala la utamaduni. Suala la utamaduni ni pana na nitasema haraka haraka. Kwanza kuna kilio nchini, watu wanalalamika wanasema kuna mmomonyoko wa maadili, lakini tunachofanya mara nyingi ni kulaumu wengine na mara nyingi tunawalaumu vijana. Vijana wa siku hizi, vijana wa siku hizi, vijana wa siku hizi, kana kwamba vijana wa zamani walikuwa waadilifu sana. (*Makofi*)

Waliosoma *social psychology,* saikolojia ya jamii, niliisoma huko zamani, unajua jambo moja ni tabia ya watu wazee kama mimi, watu wenye umri mkubwa kwa kawaida wanapenda kutukuza yao ya zamani na kufikiria kwamba, ya kwao ndio yalikuwa mazuri lakini ya sasa aah hovyo hovyo tu. Sasa nasema hii tabia ya kuwalaumu vijana tu, kwamba vijana eeh, hawana maadili, zamani tulikuwa sawasawa, nadhani ni kosa lile lile. Ni kosa lile lile. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kama vijana wetu hawana maadili, tujitazame sisi, tunaowakwaza vijana ni sisi watu wazima ndio maana Waingereza wana usemi unaosema: *" Like Father like Son",* naachia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kusema moja kubwa, naomba mnisikilize tena nisitafsiriwe vibaya. Sisi tuna urithi hapa Tanzania, urithi wetu unatokana na mapambano yetu ya kupigania uhuru. Katika kupigania uhuru, Mwalimu alitufundisha kuwa, kazi yetu ni kuunganisha watu kujenga umoja, kwa hiyo tangu Katiba ya kwanza ya TANU, kazi ilikuwa moja tu ni kuwaunganisha Watanganyika na mara tulipopata uhuru kazi ikawa ni kuwaunganisha Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala letu ni umoja, mshikamano na udugu, ndiyo utamaduni wetu na kazi ya viongozi wetu wote na kwa bahati nzuri ingawaje uongozi wa Mwalimu ulikuwa ni wa kisiasa na Chama cha *TANU* na *AFRO* na baade CCM, lakini kwa bahati nzuri viongozi wa aina nyingine waliunga mkono kwamba, kazi yetu ni kujenga umoja, mshikamano na udugu katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema ndiyo maana nchi hii imetulia kwa sababu wote kazi yetu ni hiyo, lakini nasema sasa tumeanza kubabaika. Ndiyo maana nikasema mnielewe. Kuna waraka umetolewa na viongozi wa kanisa Katoliki, nawaheshimu sana, tena wale wakubwa, wale nawafahamu, nawaheshimu kweli kweli lakini waraka huo ni wa kuweka vigezo vya kupatikana viongozi wa siasa. Nilipopata habari nilistuka sana, Eeh! Hili limetoka wapi? Nikatafuta nikasoma, Eeh! Hasa hili Kanisa Katoliki linatoa mwongozo sasa lazima huu mwongozo ni wa Wakatoliki, kwa hiyo KKKT nao watoe mwongozo, kwa sababu wao hawaongozwi na Kanisa Katoliki, ni mantiki tu. Lakini KKKT wakitoa na makanisa ya Pentekoste nao watakuwa bado watatoa wa kwao na Anglikana bado, na Waangalikana itabidi watoe wa kwao. Waislam bado na wao watoe wa kwao. Ni mantiki tu, nasema hivi, kwa heshima zote nawaomba Viongozi wa Kanisa Katoliki, nawapenda sana, nawaomba, warudishe huo mwongozo wao, sisi tunataka nchi moja, watu wameshikamana. Hatutaki tugawanyike kama Lebanon. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa Kingunge na kitu kingine kikubwa ulichonifurahisha ni kutumia maneno ya Kiswahili ambayo ni fasaha. Neno weredi ni neno linatumiwa na Wabunge wachache sana. Nadhani sasa tutalitumia zaidi. Nakushukuru sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba nimwite Mheshimiwa Faida Bakar na Mheshimiwa Juma Killimbah ajiandae.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ili nichangie hoja hii. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa ama kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuchika Comredi kwa kazi nzuri ambayo ametuletea hapa leo akishirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Bendera. Hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru ama kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda, kwa kukerwa na tabia ya baadhi ya wasanii ama washabiki ama watu ambao wana tabia ya kuvaa nguo fupi ama kunengua mbele za watu mpaka ikakithiri haja. Kwa kweli napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye ndiyo dira yetu na sisi tuchukie kama anavyokerwa yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Napenda kuanza kuchangia hoja kwa Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari ni Walimu, Waandishi wa Habari ni wazazi, Waandishi kwa kweli ni kila kitu. Kwa sababu hata humu ndani tusingekuwa tunaendesha Bunge kama hapana Waandishi wa Habari hizi, habari hizi ni Waandishi wa Habari wanaziandika. Hao wanaotuandikia mambo yetu ni Waandishi wa Habari. Kwa hiyo, napenda kwanza kuwapongeza wana Habari wa

nchi yetu ya Tanzania. Ingawa watu wengine wanaongea kwamba Waandishi wengine siyo wazuri, lakini nawasifia Waandishi wa Habari wa Tanzania. *(Makofi)*

Mtu akifanya vibaya atajijua mwenyewe, lakini wengi wa Waandishi wa Habari ni watu wazuri sana na kazi ya Waandishi wa Habari ni ngumu. Wanatumia muda wao wote, si usiku si mchana, Waandishi wa Habari wanatafuta habari huku na huku katika kuelimisha jamii. Napenda sana kuiomba Serikali Waandishi wa habari waelimishwe zaidi. Wapatiwe vifaa zaidi. Vile vile wapatiwe usafiri na mambo ya bima, kila siku nikisimama natetea bima kwa Waandishi wa Habari hasa kwenye vyombo binafsi vya habari. Waandishi wa Habari wengi huwa wanapata matatizo kwenye kazi zao. Wanapigwa, wanavunjiwa vifaa vyao, wananyanyaswa, kama kwenye maandamano, siku nyingine wakati wa uchaguzi wananyanyasika sana Waandishi wa Habari, lazima tuwahurumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Habari uwaone wafanyakazi wako ama uwaone Waandishi wa Habari. Kwa kuwaongezea mishahara minono, posho nzuri, ndiyo watafanya kazi vizuri, tusiwalaumu tu Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu wasanii. Wasanii ni kioo cha jamii. Mtu akiniambia msanii si kioo cha jamii pia sikubaliani naye. Baadhi ya wasanii wanaelimisha jamii sana. Ingawa wasanii wengine pia na wao watakuwa na matatizo yao. Kwa hiyo nasifia sana wasanii na napenda sana wasanii kama wa ngoma, nyimbo za taarabu, mashairi, waimbaji kwaya na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwape nguvu wasanii ili na wao waendelee kutusaidia katika kutuelimisha. Lakini nakerwa sana na baadhi ya wasanii ambao wanatumia usanii wao kutokuwa na maadili ya Kitanzania, hii inanikera sana. Hasa wanenguaji, unaimba unanengua, unanengua mpaka unavua nguo. Inakuwaje, wasanii ninyi ni kioo chetu sisi, sisi jamii. Kwa hiyo, nyinyi mkiwa mnakwenda vizuri, mnavaa vizuri, mnaimba nyimbo nzuri, hazina mambo machafu machafu ndiyo jamii itakapoelimika, lakini wewe ukienda ukiimba nyimbo pale ovyo kabisa, unanengua ovyo kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema juzi hapa, ndiyo maana nikampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jamani wasanii nawaomba sana, waendelee na usani wao na Serikali iwape nguvu wasanii kama mikopo, misaada mbalimbali na wapate elimu zaidi ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Lakini baadhi yao mambo wanayoyafanya si mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu mashindano ya u-*miss*. Mimi naomba kutaka kujua kwamba masharti ya u-*miss* ni nini? Masharti ya u-*miss* baadhi yao kwa kweli, hata hawa ambao wanasimamia hii i*ssue* mambo ya u-*miss* nawaomba kuwauliza masharti yake ni nini? Masharti yake ni vile kuvaa nguo za ufukweni wakakaa vile ambavyo wanakaa. Sisi wazazi hatupendi. Sisi akina mama hatupendi kwa kweli. Kwa sababu wengi wao hawafanyi vizuri. Kama u-*miss* ni labda ni kupata gari ama labda ni kupata fedha, mtu anaenda pale kufanya mambo yaliyokuwa

si mazuri kwa sababu ya gari. Kwa kweli hiyo sikubaliani nayo, sana sana sana ma-*miss* wavishwe vizuri, wapite kwenye *stage* pale wamevaa vizuri, vile vile ziwe nguo za heshima. Sisi akina mama tunanyanyasika sana tukiona vile. Mbona wanaume hawaendi uchi. *(Makofi)*

Hawa ma-*mister* sijui wanaitwa vipi, wanavaa vizuri, kama wenzangu walivyosema. Lakini ma-*miss* wanawake wanasikitisha, watoto wetu wadogo hawa jamani, jamani tupunguzieni, si vizuri, hatupendi sisi wazazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa letu la Tanzania. Lakini naona sasa lugha hii ya Kiswahili, Serikali ama sisi jamii ya Watanzania hatuitendei haki. Kwa sababu lugha hii hata sisi wenyewe hapa tukiongea tunaongea kama vile Kiingereza, Kiingereza sijui bado tuna ule ukoloni ukoloni ule bado haujatutokatoka. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa tuiseme Bungeni, tuiseme kila sehemu. Tukienda kwenye semina, semina kwa Kiingereza! Tukienda kwenye mikutano, mikutano ya Kiingereza, tukienda kwenye makongamano Kiingereza! Kila sehemu Kiingereza. Watanzania sisi tutajisifia nini, hapo baadaye tunakokwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha yetu ya Kiswahili, tuletewe mpaka Miswada hapa ya Kiswahili, Sheria zetu yaani kila kitu tufanyiwe kwa Kiswahili. Tanzania ni ya Kiswahili, lugha ya Kiswahili, tusifie letu kwanza, ndiyo ukasifie la mwenzako. Naomba sana wananchi wa Tanzania, Wizara hii pia ifuatilie sana lugha ya Kiswahili ili iweze kuendelea kama lugha za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki miliki za wasanii. *COSOTA* inafanya nini? Mheshimiwa Martha Mlata nami pia nakerwa sana na *COSOTA*. Wasanii wanafanya kazi kubwa sana katika kuelimisha jamii, lakini wanaporwa haki zao miliki. Tunaiomba Serikali. Naiomba sana ifuatilie *COSOTA* ili haki za wasanii ziweze kuhifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo katika *TV* na Redio. Mimi nafurahishwa na matangazo mbalimbali ambayo yanatoka kwenye *TV* na Redio. Mengine huwa yana makosa makosa kidogo lakini matangazo mengine ni muhimu. Nalipenda tangazo moja ambalo linatoka kwenye *ITV* lakini sielewi. Kuna tangazo la mtoto wa kike ambaye anarubuniwa na watu tofauti tofauti wengine wazee, wengine mpaka walimu, anasema sidanganyiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tangazo limetayarishwa na TAMWA, Chama Cha Wandishi wa Habari Wanawake Tanzania, hongereni sana. Hili ni funzo kubwa sana, ni tangazo zuri sana kwa watoto. Maana yake mtoto akimwona mtoto mwenzake anasema sidanganyiki, kila mtu ananitaka mimi! Wanataka kuniharibia maisha, sidanganyiki! Kwa hiyo mtoto naye anamwiga mtoto mwenzake na yeye anakataa. Kwa hiyo matangazo kama hayo ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya Kijiji cha *Maisha Plus.* Napenda kupongeza sana *TBC*, kwa kutangaza mashindano yale ya *Maisha Plus* na waandaaji na washiriki wote nawapongeza, kwa sababu kijiji kile cha *Maisha Plus* kinafundisha mambo mengi kwa vijana wetu, wale vijana waliokwenda pale yaani hatujaona hata siku moja kukiuka maadili ya Kitanzania, wanavaa vizuri, wanavaa nguo za Kitanzania vitenge, kanga, wanafundisha. Wanapika vyakula vya Kitanzania, nyumba zile za makuti japo hatupendi hizo nyumba za makuti ziwe za Kitanzania, lakini inaonyesha kwamba hiki ni kijiji, ni jamii ya Watanzania na walivyokuwa wanaishi mle ile ni tofauti na ile *Big Brother, Big Brother* mbaya, wanafanya uchafu, uchafu, uchafu. Lakini kijiji cha *Maisha Plus!* Kwa kweli mimi nakipongeza, naipongeza *TBC* na waandaaji na vile vile nampongeza huyu kijana Abdul ambaye amepata ushindi, huyu kijana Abdul anatoka Zanzibar. Anaonekana anaweza na ana maadili ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wenzake wote pia nawapongeza, lakini mshindi *Mr. Abdul* nampongeza na vile vile nampongeza kwenda kupanda Mlima wa Kilimanjaro kwa kutafuta *fund* kujengea kule Zanzibar Hospitali ya matatizo ya kisukari. Kwa hiyo nawaomba Wabunge wenzangu tumchangie huyu Abdul, tumchangieni japo posho ya siku moja kwa kila Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaonyesha njia kwa sababu hakwenda kupanda Mlima Kilimanjaro au kutafuta *fund* kwa ajili ya kwenda kufanya mambo ya kipuuzi. Anaenda kusaidia wagonjwa wenye matatizo ya kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana vile vile kupongeza michezo Tanzania. Nataka kupongeza michezo Tanzania, kwanza lazima nianzie kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu. Kwa sababu yeye ndiye ambaye anatupa nguvu na anatupa hamasa ya kupenda michezo. Kwa sababu yeye anapenda michezo, kwa sababu tunajua kama michezo ni ajira, michezo ni afya, michezo ni furaha na michezo ni kitu kizuri sana hata kwa watu wazima. Hata sisi hapa Bungeni, Wabunge wanakwenda kwenye michezo, wanafanya michezo mbalimbali. Kwa hiyo, napongeza sana michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza *TFF* na *ZFA*, napenda pia kuwapongeza hawa viongozi wote wa michezo. Napenda kuwapongeza kwa kudumisha michezo Tanzania ili Tanzania yetu iwe imara katika michezo na vile vile kuweza kupata ushindi mbalimbali katika michezo tofauti katika jamii yetu ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba tena kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Faida Bakar. Kwa kweli mchango wako umekuwa ni muhimu sana. Tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Manju Msambya ajiandae.

**MHE. JUMA A. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa muhimu ili niweze kuchangia kupitia Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, nampongeza sana. Nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala ambalo ni nyeti sana na suala ambalo linaweza likaleta mifarakano au likajenga au likafanya jamii ikapata uelewa juu ya jambo fulani, Sekta ya Habari ni chombo kimoja muhimu sana sana. Ni suala ambalo naamini Vyombo vya Habari vinaweza vikapotosha jamii kama vinaamua. Vyombo vya Habari vinaweza vikaielekeza jamii kwa kutenda mambo kama vinaamua vifanye kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza niwapongeze Waandishi wa Habari ambao wanafanya kazi kwa umakini na kufanya kazi kwa hali ya juu kwa kuzingatia maadili na kufanya kazi kwa weledi. Hili nalipongeza. Lakini nitakuwa nalaani sana kwa Waandishi wa Habari wasiozingatia misingi ya maadili. Waandishi wanaotumia kalamu zao kuchafua majina ya watu, Waandishi wanaotumia kalamu zao kuumiza watu bila sababu za misingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tusipoangalia kwa sababu jamii ina tabia na imeshakuwa imejenga mazoea ya kuweza kuamini yale yanayowekwa kwenye magazeti. Kwa kuwa wengine hamna mahala pa kusemea na mtu akawa ameandika na amemaliza jamii itabakia na suala hilo bila kuweza kuelewa ukweli uko wapi au kujua upande wa pili unasema nini kuhusiana na yale yaliyodaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nataka niase tu kwanza nasema wamiliki wa Vyombo vya Habari wanafanya vizuri sana. Kwa sababu wameanzisha hivi vyombo na vya Serikali. Naamini kwamba wanaamua kutusaidia ili kwamba tuweze kupiga hatua za kimaendeleo. Lakini nataka nitoe wito, hawa wamiliki wa Vyombo vya Habari, jamani tuwe makini sana kuweza kuchukua watu wasio na uweledi katika fani hii. Kwa sababu kwa kufanya hivyo pengine tukakimbilia kwamba tunataka tupate watendaji walio na nafuu. Matokeo yake ni kuleta mifarakano katika jamii na inaweza ikavuruga hali ya amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala moja ambalo limetokea hivi juzi na nalizungumzia suala hili limetokea kwa kuandikwa na Gazeti la *The Guardian* Toleo Na. 4563, Gazeti lililoandikwa siku ya Jumatatu tarehe 13 mwaka 2009. Ndani ya Gazeti hili ukisoma *front page* baada ya kutoka haya maneno ya juu hapa chini kuna taarifa ambazo zimeandikwa na kwa ridhaa yako Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma hiyo *heading* na halafu baadaye nitaendelea kueleza, linasema hivi:

"*MPs named Pay Scam.* Lakini wakaweka *dots* kwa kusisitiza, wakasema *PCCB confirms in its probing the allegation*". Tuhuma ambazo zinachunguzwa *PCCB*

wanasema na ndani ya gazeti hili wanazungumziwa Wabunge wawili. Anasema, nitasoma hiyo paragraph. *"The Member of Parliament, Mgana Msindai, Iramba East, CCM and Juma Killimbah, Iramba West, CCM are among eighteen people currently under the Regional PCCB scrutiny in receiving payment for Council Meeting they didn't attend"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba huyu Mwandishi anasisitiza bado anauelezea ule ukweli kwamba sisi tumepokea pesa za vikao ambazo hatujahudhuria, vikao vilivyofanyika vya Halmashauri. Lakini ukiangalia hapa anaelezea, anasema kwamba alipowauliza *PCCB* anasema hili suala lipo kwenye uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu hapa ninapoona kwamba suala ambalo lipo kwenye uchunguzi, lipo kwenye *investigation* bado halijapata ule usahihi. Leo linafika linaandikwa na linawekwa kwenye *front page.* Habari hizi zinaumiza watu, na zinaumiza kweli kweli. Naweza nikasema zimeniumiza kwa kiasi fulani, zimeumiza familia yangu na zimeumiza kweli kweli kwa sababu ni habari ambazo kwanza sizijui na wala kitendo hicho kinachoelezwa hakijawahi, wala sijawahi kufanya kwa sababu najua maadili na najua maadili ya kuzingatia utaratibu wa kuwepo vikaoni. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, naamini kwamba sina rasilimali ambayo naweza nikajivunia zaidi ya jina langu na sipendi jina langu likatumika vibaya kwa watu ambao watakavyo wao wenyewe. Ni dhambi kubwa na namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia nafasi hii na ili ni kutaka kuhakikishia Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mwandishi yule yule aliyeandika habari hizi siku ile ile akanitumia *SMS* anasema naamini kabisa haupo kwenye kundi la walaji ila lengo langu ni kuwabaini wanaoihujumu Iramba yetu. Naamini mimi na wewe hatuna tofauti kabisa. Sasa leo umeshaniumiza, umeshaandika lakini unanipoza, unaniambia kwamba wewe huna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na watu wa namna hii ni hatari sana. Ni hatari sana na lazima waandishi wazingatie weledi. Nawaomba wamiliki wa Vyombo vya Habari, tunapoajiri jamani tuwe makini sana. Waandishi wa namna hii ndiyo watu wanasema ni uandishi pasipo elimu kwa maana *UPE.* Ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kwamba ningekuwa najua kama kuna taratibu za kuweza kutoa ushahidi kwa hili suala la *electronics* labda ningeweza nikai-f*orward* kwa Mheshimiwa Waziri na nitafanya hivyo ili aweze kuona. Lakini pia nitahakikisha kwa kutunza rekodi na hili gazeti nitalitoa kwako ili uweze kumkabidhi Mheshimiwa Waziri ili baadaye aone namna ya hivi Vyombo vya Habari vinavyoumiza watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nije haraka haraka kwa sababu nimesikia kengele imegonga. Nije kwenye Sekta ya Michezo. Mimi nalipongeza sana Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *TFF.* Nampongeza sana Rais wa *TFF,* Leodiga Chila Tenga, Makamu wa Rais, Ndugu yangu Athumani Nyamlani. Naamini

hawa watu ni Watendaji ambao sasa wanatoa sura ambayo sasa *TFF* inaonekana inaongozwa na watu kwa lengo la kwamba si *TFF* ambayo ile iliyokuwa inafanya vurugu tupu. Nawaomba sana hawa ndugu zangu na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge tulio wengi, tuliopo hapa ndani, tunaunga mkono juhudi zao. Leo Mheshimiwa Waziri amesema hapa asubuhi na amesema yale mazuri ambayo kwa soka tumeweza kuwa wa juu sana au tumeweza kufanya vizuri sana. Tulijionea kwenye mashindano ya *CHAN* tumefanya vizuri sana. Kwa hiyo nawaomba hawa ndugu zangu wala wasikatishwe tamaa. Maneno mengi yanayozungumzwa, maneno mengi ya kukatisha tamaa. Hiyo ni sehemu ya kazi, lakini sisi tunatambua utendaji wao na tunaheshimu kazi wanaoifanya, tunaheshimu heshima wanayotuletea Tanzania, tunawaheshimu sana. Nasema kwamba waendelee wafanye kazi kwa kila linalowezekana na sisi tuko nyuma yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelezea tu kwamba nawaomba hawa ndugu zangu, kwa sababu wamefanya vizuri Kitaifa, hebu naomba kwamba ule utaratibu hasa huu wa mpira wa miguu, kutoa miongozo kwenye ngazi kuanzia ya Mkoa na tuje Wilayani. Jimboni kwangu tu Iramba Magharibi, timu za vijana ambazo ninazo na ambazo nimekuwa nikifanya juhudi bila kuweza kusaidiwa na chama au tukisaidiana na viongozi wachache ambao wako pale, nina timu zisizopungua 177 na hizi timu ni timu za mpira wa miguu. Utakuta kwenye kijiji kimoja ziko timu zaidi ya mbili au tatu. Lakini huko ndiyo kwenye vipaji. Kwa kupitia hotuba hii namwomba sana Mheshimiwa Waziri tuangalie tunatengenezaje utaratibu wa hawa vijana mpaka ngazi ya chini, kwamba tukawa na utaratibu mzuri badala kwamba sasa hivi Tanzania tunaanza kutoka tunaacha vipaji ndani, tunaanza kukimbilia kuchukua wacheza mpira kutoka nje ya nchi. Lakini wachezaji wako wazuri sana ambao wanaweza wakacheza ligi ya ndani na wakacheza ligi ya nje bila matatizo hapa hapa Tanzania. Lakini inawezekana kama tutafanya maandalizi mazuri na tutahakikisha kwamba timu zetu zinafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kutoa pongezi kwa Mtangazaji huyu wa mpira wa miguu, anayeitwa Juma Nkamia. Juma Nkamia ni Mtangazaji wa kwanza aliyeweza kutangaza mpira wa miguu *BBC* na hii wameitangaza kwamba ni mtangazaji wa kwanza na amekuwa akitangaza mpira kwa umahiri mkubwa sana na amekuwa akitangaza kiasi kwamba hata kama wewe sio mpenzi wa mpira unaamua kusikiliza. Kwa hiyo, ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, watangazaji kama hawa ambao wanafanya kazi kwa namna ya kujitolea na kwa mapenzi ya juu. Hawa ni vema wakapewa tuzo, kuwatunza tu. Kwa sababu wanafanya kazi vizuri na kama wanafanya kazi vizuri na ukimtunza na ukimtambua yeye anazidisha ile ari na mori wa kufanya kazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Killimbah. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, naomba Mheshimiwa Waziri nifanye marekebisho kidogo ambayo nadhani tusipoyafanyia marekebisho yanaweza kuleta matatizo. Nimepokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Vuai A. Shamsa, Khamis samahani, akiniomba nifanye marekebisho yafuatayo, Mheshimiwa Waziri hotuba yako ukurasa wa tano umewataja na kutoa rambi rambi kwa Wabunge ambao

Mwenyezi Mungu amewaita mbele ya haki. Ulipokuwa unataja mwakilishi, umemtaja Vuai Abdallah Khamis badala ya Daud Hassan Daud. Kwa hiyo Mheshimiwa Vuai Khamis naona tuweke rekodi hizo sawasawa, naomba *Hansard* wabadilishe hiyo na wajue kwamba aliyefariki ni Daud Hassan Daud na siyo Vuai Abdallah Khamis. Kwa hiyo, nataka kuweka hiyo vizuri ili rekodi ziweze kuchukuliwa vizuri. Baada ya hapo naomba sasa nimwite Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Hafidh Tahir ajiandae kama tutakuwa na muda.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na nimpe pole na mimi Bwana Vuai kwa mkanganyiko uliotokea. Nawapongeza watumishi wote wa Wizara ya Habari, Utangazaji na Utamaduni, wakiwa chini ya rafiki yangu mpenzi Mheshimiwa George Mkuchika, nampongeza sana. Lakini kuna mahali nitafuta pongezi zangu, na kwasababu ni rafiki yangu ninaamini atanielewa. Lakini kabla sijaendelea, niwapongeze wachangiaji watatu waliosema jioni hii, Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru, Mheshimiwa Faida na Mheshimiwa Juma Killimbah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mheshimiwa Killimbah. Mheshimiwa Killimbah, pole kwa hayo yaliyokukuta, lakini naomba uelewe kwamba kuna waandishi wa habari na waandika habari, hawa ni watu wawili tofauti. Mtu yeyote ambaye anadhani anaweza akachukua *note book* na kalamu akaandika, anajiita mwandishi wa habari, huyu ni mwandika habari. Hawa ndio wale Mheshimiwa Rais, aliwaita “makanjanja.” Uandishi wa habari ni taaluma yenye hadhi. Miaka ya nyuma sana nilikuwa nasikiliza *Voice of Nigeria*, Sauti ya Nigeria, unamkuta mwandishi kama alivyosema mchangiaji mmoja pale nadhani ni Mzee Kingunge, kwamba amebobea katika taaluma yake, mtangazaji ana *PhD*. Sasa huyo hawezi kuandika vitu vya hovyo hovyo. Mheshimiwa Kingunge ameshauri kwamba waandishi wetu wapewe fursa ya kusoma, sio kila mtu akienda pale Buguruni, anapata kale kacheti, anakuja anasema yeye ni mwandishi. Kwa hiyo, naomba wamiliki wa vyombo vya habari ili wasiingie matatani, matata yanayosabishwa na waandishi wao, wawape taaluma inayotosha ili wafanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mzee Kingunge kwa maelezo yake aliyoyatoa yale ya Umoja wa Kitaifa na nitayaunganisha na maelezo ya Mheshimiwa Faida. Hili ninalotaka kulizungumza pengine lingetakiwa lizungumzwe kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini tuelewe utamaduni wa nchi ni pamoja na lugha. Utamaduni wa Waingereza ni pamoja na Kiingereza chao na ukiharibu kukizungumza Kiingereza, Mwingereza halisi anakasirika. Utamaduni wa Wachina ni pamoja na Kichina. Sasa naomba na nimeomba miaka mingi ya nyuma, miaka ya 90 mpaka 2000 na nilipokwenda likizo ya miaka mitano sikupata muda wa kuwepo humu kuomba, nimerudi 2005, bado naendelea kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mawazo potofu miongoni mwa sisi Viongozi na hasa wale waliopewa dhamana ya Serikali, kufikiria kwamba, Kiswahili hakiwezi kuwa lugha ya kufundishia. Hivi hawa Wakorea wanaopigiwa kelele na Wamarekani sasa hivi kwa kupasua hayo mabomu ya nyuklia, wanasayansi wao, wakemia, wafizikia wale,

wanaandika zile mada zao kwa lugha gani, kwa Kiingereza au kwa lugha ya Kikorea? Ni kwa nini mtoto wa Kitanzania asianze shule tangu darasa la awali, elimu ya msingi, sekondari, sekondari ya juu mpaka elimu ya juu akisoma kwa Kiswahili? Hii inampa uelewa wa mambo anayojifunza. Kila siku huwa najinadi hapa kwamba mimi ni Mbembe. Ukimpeleka mtoto wa Msambya shule, aanze kufikiria ni nini cha kufanya. Anapewa hesabu, atazifikiri kwanza Kibembe, halafu azifikiri Kiswahili, halafu ndio azifanye Kiingereza, kwanza muda unapotea halafu uelewa wa somo haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaojenga hoja kwamba Kiingereza ni Kiswahili cha dunia na wanamnukuu Mwalimu. Kama kweli una uhakika Kiingereza ni Kiswahili cha dunia, kwa hiyo unakubali kwamba Kiswahili kiko juu na kwa misingi hiyo, sisi hatusemi kwamba Kiingereza kifutwe, hapana, watoto wetu wajifunze kwa lugha ya Kiswahili na wafundishwe vizuri, walimu wa kufundisha kwa lugha hii wawe wameandaliwa, halafu Kiingereza kifundishwe kama somo, kama vile kinavyofundishwa Kiswahili kama somo, lakini kipewe umuhimu kwa sababu sisi hatuishi kisiwani. Leo wanakuja Wajapani, Wachina, Wajerumani, tunawasiliana nao katika mambo yetu, lakini kuja kwao, kule kwao hawakufanya masomo ya zile taaluma zao kwa Kiingereza, walifanya kwa Kijerumani na ukiongea nae Kiingereza unajua kwamba huyu kinampa taabu kama kinavyonipa mimi lakini tunaelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Faida ameeleza hapa, Miswada inaandikwa Kiingereza, halafu tunaijadili Kiswahili humu, ya nini! Halafu umma huko nje unasema Wabunge wanatumia *"Kiswa-nglish"*, lakini umma hawajui kwamba watawala hawataki tukatumia lugha ile ambayo ndiyo ya kwetu. Mwaka 1974, Mzee Rashid Mfaume Kawawa, alitoa agizo la kukipa Kiswahili nguvu, tangu 1974 mpaka leo haionekani kama Kiswahili kinapewa nguvu. Nasema hili, nikipata fursa kwenye Wizara ya Elimu, nitalizungumza kwa undani zaidi na ndio itakuwa mada pekee. Lakini kwa sababu utamaduni wetu ni pamoja na lugha yetu, nimeona nilizungumze hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 12 ametueleza moja ya shughuli za Wizara, ni kusimamia shughuli za vyombo vya habari. Nakubaliana naye kabisa, lakini sidhani kama Mheshimiwa Waziri, anasimamia shughuli za vyombo vya habari kama inavyotakiwa. Hili nitakalolisema kwa bahati mbaya inawezekana lisifurahishe watu. Katika maswali ya papo kwa papo nilipokuwa namuuliza Waziri Mkuu hapa, nilizomewa, lakini ndio ulikuwa ukweli. Lakini hata kabla ya hapo, Sheikh wa Msikiti wa Mnyamani, kupitia *Channel ten,* katika kipindi chake cha *"A-rrisala"*, alikwishaeleza. Hivi unaweka kipindi cha dini ya Waislam siku ya Ijumaa, saa 06:00 usiku, asikilize nani? Na Waziri anasimamia vyombo vya habari, hivi Jumapili yote ukitoa vipindi vichache, ni mambo ya Kanisa tu. Waziri anasimamia vyombo vya habari na wala haelewi. Bodi ya *TBC*, Bodi yote, ni waumini wa Kanisa la Kikristo, hakuna hata Muislam mmoja. Waziri anasimamia vyombo vya habari na ninalo gazeti hapa la "*Annur*" ambalo limeeleza, sio ya kwangu ya kutunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine huwa nasema ni kibuyu, kibuyu kikiwa na mbegu ukitikisa zitalia tu. Inatakiwa Waziri mwenye kusimamia sekta hii, basi awaelekeze watendaji katika vyombo vya habari, wafanyeje kazi inavyostahili. Ndio

yale aliyosema Mzee Kingunge hapa, ya Utaifa. *TBC*, iwe redio, iwe *television,* ni chombo chetu wote. Sasa chombo hiki kisiwe kinamhudumia mtu mmoja, kikaacha kumhudumia mwingine na kinapomhudumia mwingine ni kwa hiyari ya Mtendaji Mkuu aliyewekwa pale. Tukiichimba sana *TBC* hapa tutakuta hata ajira mle, watu wametoka sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Kabuye, Mungu amrehemu, alipokuwa Mbunge wa *CCM* alizungumzia hapa kuhusu Bodi ya Biashara ya Ndani, na ukafanywa uchunguzi, ukafanywa sijui utafiti. Yeye alituhumu akaeleza, lakini hili sina hata haja iundwe Tume, mkifungua tu vyombo vyenu mtajua watangazaji wanatoka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya Vazi la Taifa. Nashangaa sana, vazi la Taifa linaandikiwa Waraka wa Baraza la Mawaziri, wa nini? Vazi la Taifa ni utamaduni wa watu waliouzoea muda wote. Vazi la Taifa linatakiwa litungiwe sheria? Nawaona watu wa Afrika Magharibi, Wasenegali, Wanaijeria, Waghana, Togo, Gambia, zile nguo zao ambazo zinaitwa Gab, zimetokana na utawala wao wa kimila. Sasa leo unawaita watu wa mitindo waje wabuni Vazi la Taifa, vazi hili litungiwe Waraka wa Baraza la Mawaziri, upelekwe kule Barazani, uletwe Bungeni utungiwe Sheria! Hivi sisi hatuwezi kutazama hata zile picha za viongozi wetu wakati tunapata uhuru walikuwa wanavaaje, japo kuwa ilikuwa ni kwa kuiga lakini tungekwenda tunarekebisha. Hivi mtu akiona lile vazi wanalovaa Wazee wa Kihehe, haliwezi kufanywa likawa vazi la Taifa? Lakini tunapoteza muda kubuni Vazi la Taifa, nashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wenzetu wa *TFF*. Kwa kweli, wamefanya kazi nzuri chini ya Leodgar Chila Tenga, lakini kwa uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwawezesha. Lakini wapo baadhi ya Watanzania wanawapa kero sana, Maximo aondoke, aondoke. Hivi kabla Maximo hajaja tulikuwa na la kujivunia kama Watanzania kwenye mpira wa miguu? Ndio ukweli huo, mpaka Mzee Mwinyi, akasema ni kichwa cha mwendawazimu, walikuwa wanaweza kucheza kumshinda Mzambia, lakini walikuwa hawawezi kucheza kushindana. Kwa hiyo, tuwapongeze hawa viongozi na tuwape fursa wafanye yale ambayo bado hawajayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kuzungumza ni mengi, lakini la mwisho, nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Killimbah, alipomzungumzia Juma Nkamia. Nami ni lazima nimzungumzie mmoja wa watangazaji wa *TBC,* anaendesha vipindi vyake vizuri, na Nkamia ni wa *TBC,* Marine Hassan; wakati mwingine unaweza ukachelewa kuja huku kwenye Vikao. Pia alifanya kazi nzuri sana alipokwenda kusimamia matangazo ya uchaguzi wa Kenya. Lakini kipindi cha Jambo kinakupa mshawasha zaidi kikiwa kimesimamiwa na Marine Hassan, kwa hiyo, tumpongeze. Sina haja ya kumwombea apewe nini wala nini, hiyo namwachia mwajiri wake, lakini nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri, aelewe *TBC,* sizungumzii vyombo vingine, magazeti ambayo ni ya watu binafsi, wana uhuru wa kuyaendesha wanavyotaka bora wasimuathiri mtu, lakini kwa *TBC* ni ya kwetu wote na isiendeshwe kwa kufikiria dini fulani au kabila fulani, hapana, hii nchi ni ya kwetu wote. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nitoe maelezo machache ambayo yanahusiana na Wizara ya Mheshimiwa Mkuchika pamoja na rafiki yangu Joel Bendera. Nimeona nichangie Wizara hii, kwa sababu ni mdau mkubwa wa Wizara yenyewe katika sekta mbalimbali, ili basi niweze kutoa yale niliyonayo kwa faida ya wananchi wa Tanzania, lakini hasa wananchi wa Zanzibar na hususan katika Jimbo langu la Dimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu wake na Makatibu na wafanyakazi wote waliopo katika Wizara pamoja na sekta mbalimbali za Kiserikali zinazoongozwa na Wizara hii. Lakini pongezi zangu zaidi nizipeleke kwenye Wizara pamoja na Mawaziri wenyewe, kwa sababu ya ushirikiano mzuri wanaouonesha baina ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Tanzania Bara na ile Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya kule Zanzibar. Mawaziri hawa wamekuwa wakishirikiana vizuri na wamekuwa wakileta mafanikio makubwa katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo limeleta faraja sana kwa kuonesha ushirikiano wao mzuri. Sasa kwa sababu ya ushirikiano huo mzuri, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna baadhi ya mambo wakayaendeleza vizuri na kuyatilia mkazo ili kuondosha zile dosari, ndogondogo ambazo zipo katika hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye juzi alikwenda Algeria pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Kiongozi kule Zanzibar, Mheshimiwa Shamhuna, katika kuiwakilisha Tanzania kwenye mikutano na Taasisi mbalimbali ambazo wametakiwa waende na kwa faida ya Watanzania. Sasa baada ya kuona hilo, basi niwaombe, sasa hivi wakati umefika wa kuona kwamba yale masuala madogo madogo ambayo yanaleta matatizo yaondolewe na yawekewe utaratibu. Kwa mfano, Wizara hizi mbili zinasimamia sana suala la michezo, tamaduni na mambo mengine, lakini tukirudi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, suala la michezo si la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, halimo katika mambo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kwa sababu hili halimo, lakini Watanzania kama Watanzania, nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa tunatakiwa tuiwakilishe Tanzania kama Tanzania, nawaomba Waheshimiwa hawa wakae pamoja ili watoe tamko na agizo maalum ambalo litaweza kuondosha hizi dosari ndogo ndogo zilizopo na hasa katika Katiba za Vyama vyetu, Bara na Zanzibar, lakini hasa Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumekubali Vyama vya Michezo, Tanzania Bara viwe ndivyo vinavyojisajili au kujichukulia nafasi ambayo itawakilisha Tanzania, kwa maana ya Tanzania. Lakini watakaporudi, basi waweke na vyama vingine vya michezo upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili waunde taratibu nzuri zitakazoondoa dosari katika Jamhuri yetu. Mfano mzuri walioufanya sasa hivi ni wa kuungana baina ya Waziri wa Bara na Waziri wa Tanzania, Zanzibar, ni kigezo muhimu. Sasa wakae basi, Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Shamhuna ili waunde utaratibu mzuri utakaoleta sura nzuri ya Jamhuri ya Muungano na kuondosha haya matatizo. Hili ni jambo ambalo linawezekana na ni jambo ambalo litaleta busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niondoke hapo na hili. Bila shaka Mheshimiwa Mkuchika, ameshalisikia kwa sababu tulishalizungumza. Niende kwenye Timu ya Taifa ya Tanzania. Huku vilevile ni mdau, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwalimu Mkuu wa Timu ya Taifa, Maximo. Nampongeza kwa sababu kuna wakati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alisema kwamba, Tanzania ilikuwa ni kichwa cha mwendawazimu. Imefika mahali Maximo kaichukua Tanzania, akaiweka katika ulimwengu unaojulikana kwamba sasa Tanzania, kuna watu wanacheza mpira. Hili ndilo alilolifanya pale ambapo alikuwa kahamasisha vijana wetu wakaweza kupata nafasi ya kucheza katika timu mbalimbali Afrika na nje ya Afrika. Hiyo ndiyo iliyofanya sasa hivi tuwe tumeondoka katika idadi ya kuwa timu yetu ipo kutoka 105 kwenda katika kiwango cha 97, hii ni kwa sababu ya Maximo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama hii haitoshi, Timu ya Taifa ilipokwenda kule Abidjan, *Ivory Coast* katika mashindano ya *CHAN*, ilichukua nafasi ya tano. Lakini kama hiyo pia haitoshi, timu yetu ya vijana ilipokwenda kule Afrika ya Kusini, ilichukua nafasi ya tatu. Sasa ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali ni kwamba, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kumleta Maximo na wenzie Tanzania, tumeondoka tulipokuwa, tumefika katika hatua nzuri. Sasa nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, sasa hivi mpige hatua nyingine mbili zaidi mbele kwa kumwambia Mheshimiwa Rais, Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata mwalimu katuhamasisha, tumefanya vizuri, tumeondoka kwenye 105 tumekwenda 97, lakini tumekuwa tukishinda zaidi michezo ya kirafiki na hatushindi michezo ya mashindano. Tuko nafasi ya 97 nakubali, kiwango chetu ni kizuri, lakini tushinde mashindano, si mechi za kirafiki. Sasa namwomba Mheshimiwa, sasa hivi kuna mwaka mmoja wa kocha wetu Maximo kumaliza Mkataba wake. Kwa hiyo basi, tumwombe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amlete Maximo mwingine ambaye ataweza kuiondoa Tanzania katika kushinda mechi za kirafiki, tushinde mechi za mashindano, hapo ndio sasa tutaondoka kwenye nafasi ya 97, tutakuja kwenye nafasi ya 60 au 50. Tukifika katika kiwango hicho, nina hakika tutaweza kufanya vizuri na tutajulikana. Nashukuru sana kiwango ambacho kimefikiwa hivi sasa, vijana wetu wamepata nafasi, lakini jambo kubwa ambalo ninataka Mheshimiwa Waziri alizingatie na nalijua ni kwamba, makocha wa aina hii wanakuwa ghali kidogo. Lakini sasa unapotaka kwenda Peponi Mheshimiwa Waziri usiogope kufa, maana Peponi huendi na suti ukitembea. Ufe kwanza, ukamuliwe, utazame heri zako ziko vipi, halafu uende Peponi. Sasa na sisi tunataka kwenda Peponi, basi tumwambie Mheshimiwa Rais, tumempokea Maximo, tunamshukuru sana, lakini sasa hivi tutafute hatua nyingine ya kuweza kushinda. Tumekwenda *CHAN,* tungerudi na Kikombe, lakini baya zaidi, timu yetu ya Tanzania Bara imekwenda Uganda pia haikurudi na Kikombe. Sasa tuwe na walimu ambao wanaweza kutuwezesha kushinda mechi za mashindano, si kushinda mechi za kirafiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoka hapo ili niende kwenye waamuzi. Hakuna mpira utakaochezwa na Mheshimiwa Joel Bendera, hili analijua sana na rafiki yangu

mpenzi sana, Tenga, hili analijua sana. Hakuna mpira utakaopanda katika nchi kama huna waamuzi wazuri. Ukiwa na waamuzi wabovu mpira wako utakuwa mbovu, ukiwa na kocha mzuri kama huna waamuzi wazuri, mkicheza mpira kila siku mtakuwa mnapigana, mtakuwa mnalalamikiana. Kwa hiyo, sasa hivi tuelekeze nguvu zetu kwenye waamuzi na ningeiomba sana *TFF*, hasa Tanzania bara, wakaangalie vijana ambao wanaweza wakawa waamuzi wazuri, watakaoichukua Tanzania kwenda katika mashindano kama tulivyoichukua Tanzania kuanzia mwaka 1983 hadi 1994, wakati ilipokuwa na waamuzi wa Kimataifa, waliokwenda *Africa Cup of Nation* katika miaka 15, wakaenda *World Cup.* Sasa haipendezi kuwa Tanzania kuna mtu mmoja tu ndio anaweza kwenda huko, haiwezekani, ni lazima tuwe na vijana wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo linalotokea sasa hivi ni kwamba, pesa zinazotokea katika kuhudumia waamuzi zinakuwa hazitumiki vizuri. Ningeomba sana wenzangu katika semina mbalimbali za kuwafanya waamuzi wetu wawe wazuri, basi waamuzi waangaliwe katika hali hiyo. Mfano hai, hivi sasa kuna mafunzo mbalimbali yanaendelea katika mikoa yetu huku Tanzania Bara, waamuzi wamekwenda kwenye mafunzo hayo, wanatakiwa wakafanye *Cooper Test* kesho kutwa, lakini wanajihudumia wenyewe, hawapati hata senti tano. Mheshimiwa Waziri, hii sio sahihi, Mheshimiwa Joel Bendera, hii sio sahihi. Huwezi ukapata mwamuzi mzuri ukamtaka atoke nyumbani kwake aende kwenye mafunzo, ajihudumie mwenyewe, hapa ni kukaribisha rushwa, kwa sababu tukifika katika mafunzo haya atamtafuta yule mtu mwenye timu ambaye anajua mwakani watakutana kwenye ligi, atamwambia niko Dodoma lakini sina kitu. Atampa 50,000/= atampa 100,000/=, sasa unapofadhiliwa inabidi na wewe ufadhili baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunakuja kulalamika, waamuzi wetu wanachukua rushwa, watachukua rushwa kwa sababu hatuwahudumii. Sasa tuwahudumie waamuzi wetu katika semina mbalimbali na tuwahudumie waamuzi wetu katika mashindano mbalimbali na tusiwakope, tatizo la kuwakopa lipo, Waamuzi wanakopwa sana katika mashindano. Kwa hiyo ningewaomba sana wenzetu wa *TFF* kuangalia hili ili tumpate Hafidh Ali mwingine ambaye ameiwakilisha Tanzania katika mashindano mbalimbali ya Ulimwengu, ya Afrika. Haiwezekani katika idadi tuliyonayo ya milioni 43 sasa hivi kuwa yuko Hafidh Ali mmoja wa Watanzania ndiye ambaye ameweza kuchezesha, haiwezekani, tuwapate wengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba hili lisimamiwe vizuri ili liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waandishi wa habari ni watu muhimu sana katika nchi. Waandishi wa habari ni watu ambao wanaweza wakaichukua nchi, wakaitangaza vizuri sana. Lakini waandishi wa habari wanaweza wakamchukua kiongozi, wakamtangaza vizuri sana, lakini hatari ya waandishi wa habari wanaweza wakasababisha vita katika nchi, hii ndio hatari ya waandishi wa habari. Sasa tatizo la waandishi wa habari hivi sasa baadhi yao, narudia tena, baadhi yao hawajui kazi wanazozifanya. Sasa hatuwezi kuwa na waandishi wa habari wanaochupa. Mheshimiwa Bendera hili nilishamwambia katika kikao kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii imevamiwa sana na makanjanja. Makanjanja ni watu wanaopenda tu kujiita wandishi wa habari, lakini si waandishi wa habari. Mtu anakwenda wiki zake tatu, anasoma katika kitengo maalum cha mtu binafsi, anajiita mwandishi wa habari, si kweli. Waandishi wa habari wa kwetu baadhi yao wanashindwa hata kujua Katiba ya Nchi hii inasema nini, huwezi ukawa na mwandishi wa habari ambaye haijui Katiba ya nchi yake, haiwezekani. Lakini huwezi ukawa na Mwandishi wa Habari asiyejua *ethics* ya kazi yake ambayo anaifanya. ataandikaje habari? Atatangazaje habari ambazo zinaelekea upande mmoja? Hiyo sio habari, andika habari inayomhusu Hafidh Ali, lakini Hafidh Ali anapomsema Jenista Mhagama, nenda kwa Mhagama kamuulize, Hafidh Ali kasema hivi, unasemaje? Lakini unaandika habari inakuwa kama msumeno, unakata tu, unakwenda mbele na nyuma, haiwezekani. Sasa waandishi wa habari kama hawa, hawatusaidii, hawatusaidii kabisa na hawa ni watu ambao wanaleta uchochezi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nawaomba sana wenzangu, maana mie ni mdau katika hilo na mie ni mwenzao. Nawaomba sana wasije wakajiingiza katika kuleta uchochezi katika nchi, ni jambo baya sana. Katika nchi tuna matatizo mengi, sote tunayajua, tuna matatizo mbalimbali, hali ya nchi ilivyo kisiasa sote tunaijua. Sasa mwandishi wa habari asije akajiingiza katika kundi moja kwa maana ya kuleta uchochezi. Taifa hili halitaweza kumvumilia kabisa, hatuwezi tukawa na watu wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kama nitawahi jambo lingine la mwisho, basi nitazungumzia, lakini napenda kuipongeza sana *TBC*. *TBC* ni chombo ambacho kinaleta hamasa katika nchi hii ya Tanzania na *TBC* imeleta mfumo mpya wa Watanzania kuwafanya wasikilize *TBC*. Kwa hiyo, nampongeza sana Mkurugenzi wa *TBC* kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na nampongeza kwa jinsi anavyoiendesha hivi sasa *TBC.* Namwomba akamate uzi huo huo ili asije akaingia katika redio nyingine tunazozisikia ambazo zinafanya mambo ya maajabu ajabu. Pia nawaomba *TBC* wawe ndio wa mwanzo kulinda lugha ya Kiswahili ya Tanzania. Namuomba sana Ndugu Tido, asiruhusu mtangazaji yeyote wa *TBC* kutuletea lugha za kienyeji za vibarazani na magogoni, kuingia kwenye *TBC.* *TBC* ni chombo cha Taifa, tunataka lugha fasaha, tunataka lugha inayofahamika, tunataka lugha inayozungumzwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri *TBC* ina wazee. Kuna Mzee wangu mmoja Suleiman Hega, huyu mzee kama ulikuwa unasikiliza wakati ule Radio Tanzania, unajua kwamba unasikiliza Redio. Watangazaji hawa wamuige Mzee Suleiman Hega, alipokuwa anatangaza vipindi vyake hadi hivi sasa, wakifanya hivyo tutakuwa na watangazaji wazuri. Kwa hiyo, tusisikilize redio nyingine za uchochoroni, kama maneno ya yule Mkenya: “Radio unatangaza Dar-es-Salaam, inaishia Magomeni” ndio unataka kusikiliza Redio hiyo, haiwezekani. Lakini namwomba sasa Mheshimiwa Waziri, aingie katika redio za watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ambayo sikutegemea kama ningeipata. Lakini awali nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuweza kutuletea hotuba hii ambayo kwa kweli ni nzuri, hasa tukizingatia kwamba, sasa hivi tunaelekea katika karne ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi katika masuala mazima ya michezo, lakini vile vile nitakwenda kwenye vyombo vya habari, Kwa hali halisi ya sasa hivi, michezo imekuwa ni ajira na nichukue fursa hii kumpongeza Mtanzania mwenzetu ndugu Hasheem Thabit, Mtoto wa Sinza, ambaye kwa mara ya kwanza Tanzania tumeweza kupata mchezaji katika ligi ya kikapu kule Marekani na hivyo kwa kweli tunaamini kabisa kama Tanzania tutaweza kuwawezesha vijana wetu, basi wanaweza na ninaamini Wizara hii ikiwezeshwa itaweza kutoa vijana ambao wataweza kuleta pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda niendelee kuzungumzia suala la michezo. Ni wazi kwamba pamoja na kutambua Serikali inathamini michezo, lakini bado tuna tatizo kubwa la viwanja. Katika shule, hasa shule za msingi ambako tulikuwa tunategemea watoto wetu wangeweza kujijengea uwezo na vipaji vyao, tumegundua kwamba viwanja vile sasa hivi vingi yamejengwa majengo. Kwa hiyo, sasa hivi shule zimekosa viwanja. Lakini nikienda katika Mkoa wangu wa Kilimanjaro, ni wazi kwamba siku za nyuma tulikuwa na uwanja unaoitwa *Memorial,* lakini sasa hivi uwanja ule umegeuzwa kuwa soko na hivyo vipaji vya watoto wa Kilimanjaro vitakosekana kwa sababu watakosa mahali pa kuchezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni wazi kwamba michezo ni ajira na wote tumeshuhudia ni jinsi gani wachezaji wa Kimataifa kama Christiano Ronaldo, sasa hivi wanalipwa zaidi ya shilingi bilioni 180 kwa mwaka. Kwa hiyo, naiomba Serikali ione ni wazi kwamba, watoto hawa au watoto wetu wakiwezeshwa wana vipaji na tunaweza tukapata akina Filbert Bayi na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali na hususan Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameleta makocha mbalimbali wa kuweza kujenga uwezo wa vijana wetu. Lakini masikitiko yangu ni kwamba katika upande wa *netball* bado kabisa eneo hilo halijashughulikiwa. Ni wazi kwamba hata akina mama na akina dada wana uwezo na naomba kama ambavyo Mheshimiwa Rais na Wizara kwa ujumla wameweza kuleta makocha wa riadha na soka basi vilevile waangalie upande wa *netball* kwa kuwa naamini kabisa akina dada au watoto wa kike wataweza kubadilisha *netball* ya Tanzania na kuwa ni ajira kama ilivyo soka (mpira wa miguu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka hapo naomba nielekee kwenye suala zima la vyombo vya habari. Najua ukiwa wa mwisho unaongea mambo machache, lakini ni wazi kwamba vyombo vya habari ni muhimu sana na ndiyo maana sasa hivi vinaitwa kama mhimili wa nne wa dola na kwa kweli kwa sasa hivi watu wengi wanapata habari kwa kuangalia luninga. Pia niishukuru *TBC* pamoja na vyombo vya habari binafsi kama *ITV* kwa jinsi ambavyo vimeweza kwenda mpaka vijijini na watu sasa hivi wanaweza kuona vyombo vyetu vya habari pamoja na redio. Kwa kweli naomba niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna tatizo kubwa la maadili ya waandishi wa habari na wenzangu wameshasema kwamba kuna uandishi na kuandika. Lakini niseme tu kwamba tatizo kubwa ni kutokuwa na uwezo kwa wamiliki au kushindwa kuwapeleka waandishi hao shuleni na ndiyo sababu hata hapo nyuma nakumbuka Mheshimiwa Mwakyembe aliwahi kusema kwamba "Uandishi pasipo Elimu' hili ni tatizo kubwa na ndiyo sababu hata Mheshimiwa Rais alishawahi kusema, lakini naamini kabisa kwamba, kama Wizara pamoja na wale wamiliki wa vyombo vya habari wataweza kuhakikisha kwamba wanawapatia elimu waandishi hao ili waweze kuandika habari za uhakika kwa sababu naamini kabisa habari inaweza ikaleta amani lakini vilevile habari inaweza kuleta maafa kama ilivyotokea kule Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa hilo nitoe taarifa ya gazeti la Habari Leo la jana tarehe 14/07/2009. Hili ni gazeti la Serikali lakini katika ukurasa wa 16 limetoa habari ambayo kwa kweli sisi Wanachama wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo imetusikitisha kwa sababu habari zilizoandikwa sio za kweli. Wanasema kwamba makundi yaliyoitafuna CHADEMA Biharamulo na wanasema kabisa kuna kundi la Mwenyekiti yaani Freeman Mbowe ambalo liko na Mheshimiwa Halima J. Mdee na kuna kundi lingine la Mheshimiwa Zitto Kabwe pamoja na Dr. Wilbrod P. Slaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli taarifa hizi ukizisoma ndani zinapotosha sana na kwa sababu gazeti hili ni la Serikali, basi nadhani Mheshimiwa Waziri alichukulie hatua au aangalie kwa nini wameweza kuchafua chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiri, lakini labda niendelee kusema tu kwamba, pamoja na hivyo nakumbuka mwaka jana wakati nachangia tuliongelea suala zima la Wakalimani katika vyombo vya habari hasa *TBC*. Ni wazi kwamba katika nchi yetu tuna watu wenye ulemavu wa kutokusikia, tuliomba sana na Mheshimiwa Waziri akasema atahakikisha kwamba wanaweka Wakalimani ili wale wote ambao hawasikii waweze kupata taarifa kama wananchi wengine. Tuna hakika kwamba tuna watu wenye ulemavu wa kutokusikia wengi sana lakini bado hawapati haki yao ya msingi ya kusikia au kupata taarifa na sisi tunaamini kwamba kikatiba haki ya binadamu yeyote ni kupata taarifa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni kwa nini mpaka leo bado *TBC* haina Wakalimani ili wale watu wote ambao wana ulemavu huo basi waweze kupata taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni suala zima la vazi la Taifa na niunge mkono tu aliyoyasema kaka yangu Mheshimiwa Manju S. Msambya kwamba suala hili limechukua muda mrefu lakini vilevile sioni sababu ya kuwa na waraka wa Baraza la Mawaziri kwa sababu wote tunajua vazi la Taifa ni nini, lakini mchakato huu umechukua muda mrefu mpaka sasa umekuwa hauna tena maana. Kwa hiyo, nadhani tuone ni jinsi gani Serikali inaweza kufanya jambo hili limalizike kwa haraka zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la maadili au utamaduni. Nchi yoyote lazima iwe na utamaduni na utamaduni huo ni pamoja na lugha lakini vilevile ni pamoja na mavazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba kila siku tunaongelea suala zima kwamba maadili ya Tanzania yanaporomoka, lakini bado hatujajua nini chanzo cha mporomoko huo. Mheshimiwa Kingunge N. Mwiru ameyaongelea na mara nyingi tunasema sisi watu wazima hasa wazee wanadai kwamba vijana wa sasa hivi hawana maadili lakini tunajiuliza na hawa wazee nao walikuwa na maadili? Kama walikuwa na maadili ni wapi pamekuwa na tatizo mpaka vijana wa sasa hivi washindwe kuwa na maadili? Kwa hiyo, nadhani kuna tatizo la ujumla ambalo naamini kabisa kwamba linaanzia kwenye familia, lakini vilevile nina hakika kwamba sasa hivi pamoja na utandawazi uliopo bado Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba maadili ya Kitanzania yanakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika shule zetu za msingi nilitegemea kabisa kwamba tungeweza kuwa na somo la maadili au la uraia ambalo linaweza kumfanya kijana pamoja na yale malezi aliyoyapata nyumbani, anapokwenda shuleni hasa tukizingatia kwamba sasa hivi wazazi wengi hawakai na watoto wao kutokana na suala zima la ajira na shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, nategemea kabisa kwamba shuleni sasa tungekuwa na somo au Walimu ambao wangeweza kupita na kuweza kusaidia kujenga haya maadili na siyo tuwe tunatupiana lawama kwamba hawa watoto wa sasa hivi hawana maadili. Naamini kabisa kwamba kuna mahali tumeshindwa kama wazazi, kama walezi lakini vilevile kama Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba suala la maadili lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia katika suala hilo hilo la utamaduni ni kwamba sasa hivi umezuka utamaduni wa mavazi ambayo hayaeleweki. Najua labda wengine wameongea lakini kwa kweli linatutia uchungu sana hasa sisi akina mama. Tunaangalia mara nyingi hasa katika sehemu za muziki. Ni jambo la kusikitisha kwamba wanaume wanavalia vizuri sana kwa mfano unaweza ukachukulia hata wenzetu wa Kizaire unakuta kwa mfano kiongozi wa bendi kama ya Koffi Olomide amevaa suti yake nzuri sana lakini wale wasichana wamevaa vibaya sana. Kwa hiyo, sisi akina mama inatuudhi sana. Pia tukija hapa Tanzania jambo hilo liko wazi sasa hivi imekuwa kama ni *fashion*, ukienda katika sehemu za muziki utakuta mambo ni hayo hayo lakini kibaya zaidi unakuta hata sehemu za ofisini watu hawajui mavazi ya ofisini ni yapi, mavazi ya kutokea ni yapi na mavazi ya kwenda nayo kwenye shughuli za starehe ni yapi.

Kwa hiyo, naomba kabisa Wizara pamoja na kwamba hatuna vazi la Taifa, lakini kuna mavazi yanayoeleweka ambayo kweli ni ya maadili ya Mtanzania, naamini utamaduni ni utu na Watanzania tuna utu. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sasa Serikali ione ni jinsi gani inaweza ikaingilia kati masuala ya maadili hasa ya mavazi na nizungumzie zaidi mavazi hasa kwa upande wa akina mama, najua pia vijana wa sasa hivi wanavaa vibaya lakini haitishi sana kama ile ya akina dada ambao wanavaa nguo tunaweza kusema ni robo tatu uchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie tu kwa kusema kwamba mimi kwa kweli naishukuru Serikali lakini niombe tena na tena waangalie sana masuala ya makocha wanaokuja kusaidia katika kuongeza vipaji vya Watanzania, najua wanalipwa vizuri lakini tuangalie zaidi michezo mingine kama ambavyo nimesema awali hasa masuala ya *netball* ambapo naamini kabisa inaweza kuongeza pato lakini vilevile kama nilivyosema michezo ni ajira na tumeona ni jinsi gani vijana wengi wamekuwa *super stars* huko nje, basi naamini hata Watanzania tunaweza kama ambavyo ndugu yetu na mtoto wetu Hashim ameweza kule Marekani. Naamini kuweza kwake kutawafanya vijana wengine wa Kitanzania waweze kuwa na ari hiyo na nichukue fursa hii kumpongeza sana Kanali Kipingu ambaye nina hakika ndiye amemwezesha kijana huyu baada ya kumtoa pale na kumpeleka Makongo Sekondari ambapo aliweza kufanya maajabu na kufanikiwa kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyoleta bajeti hii ambayo ni nzuri na yenye kutia matumaini kwa wananchi na pia jinsi Wizara hii inavyojitahidi kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo vyake vya habari *TV*, *Radio* pamoja na magazeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu sekta ya habari. Pamoja na jitihada za Wizara hii za kuelimisha jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari, naiomba Wizara hii kuharakisha Muswada wa Sheria ya kusimamia vyombo vya habari, yaani marekebisho ili vyombo hivi vya habari viwe na mipaka au ukomo wa uhuru wa kuandika habari na viwe vinafuata maadili pamoja na kanuni za uandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa imekuwa na malumbano makubwa hasa kupitia magazeti, nchi haina nidhamu, watu wanakashfiana, watu wanapakana matope. Yote hii ni kwamba uhuru wa habari hauna mipaka na ni hatari kwa jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu sekta ya michezo. Pamoja na nia nzuri ya Wizara hii ya kukuza kiwango cha michezo nchini Tanzania bado kuna mambo yanahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuondoa tofauti ndogo ndogo ambazo zinajitokeza. Mfano mmoja, ni suala la *FIFA* ambalo Tanzania ni Mwanachama. Ni kwa nini Zanzibar iwe haifaidiki na Matunda hayo ya *FIFA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote katika Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye suala la taaluma ya uandishi wa Habari hapa nchini. Hivi karibuni, tumeona jinsi gani taaluma hii ilivyovamiwa na vijana wengi. Wengi wa vijana hao wana *basic knowledge* tu ya uandishi na wengi wao hawajui *ethics* za kazi hii na hata kujiendeleza kielimu ni wavivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake uandishi unakuwa ama wa upande mmoja au unakuwa hauna kina na unazingatia upendeleo na hata habari zenyewe kuwa za kununuliwa kwa maana zinatokana na rushwa kutoka kwa yule ambaye habari yake anataka itoke. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ikatenga fedha ili kila mwaka waandishi wa habari waweze kusomeshwa kama *scholarship.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari zinazoandikwa chini ya kiwango huwa za kichochezi, zimejaa hisia ambayo kwa msomaji huona kama zina ukweli.

**MHE. ALOYCE BENT KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa magazeti uendelee, Wahariri wanafanya kazi nzuri lakini makosa yanapotokea wamiliki wasinyooshewe vidole badala yake wabanwe Wahariri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni uzagaaji wa mabaa holela mitaani hata vijijini huku *Band* za Muziki zikipigwa kwa sauti kubwa sana. Mila nzuri kwa vijana wetu ni kutoruhusu waone wakubwa wakilewa. Tabia ya sasa ni mabaa mengi mitaani, vijana wakitoka shuleni wanaona wakubwa wamejipanga kunywa. Tunawafundisha tabia mbaya ya kuona pombe ni kitu kizuri. Nashauri mabaa yote yaliyo maeneo ya wazi yafungwe. Baa ziwe ndani ya nyumba maalum zilizoidhinishwa na Halmashauri za Miji na Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Night Clubs* pia zimeenea sana, utaratibu ufanyike ziruhusiwe maeneo maalum ambapo sio makazi ya watu.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa hotuba yao nzuri yenye ufanisi na muelekeo na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa habari naipongeza sana *TBC* Taifa na *$TBC_1$* kwa jinsi inavyoendesha vipindi vyake vikiwemo uhabarishaji na uburudishaji. Nawaomba wazidi kuendelea hata mimi binafsi nafaidika nayo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo pia napongeza sana kwa kiwango tulichofikia cha Kimataifa hasa kwa mpira wa miguu. Kwa hiyo, naiomba Wizara iboreshe na michezo mingine na wale wachezaji mahiri na wenye vipaji wazidi kuenziwa na kupewa motisha ili wapate kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni nao uendelezwe na ukuzwe na pia ufanyiwe utafiti na tathmini ili kukuzwa utamaduni wetu wenye hadhi katika nchi yetu na

duniani kote.  Pia huu mgogoro wa *TFF* na *ZFA* ufanyiwe kazi haraka ili upatikane ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Idara ya Maliasili na Idara ya Utamaduni inastahili kukaa pamoja kwa kuboresha kwani shughuli zao zinaingiliana.  Na mswada wa Sheria kwa Vyombo vya Habari uletwe haraka Bungeni ili kuondoa usumbufu na matatizo yaliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mavazi hasa kwa wanawake nayo yatafutiwe ufumbuzi maana heshima inazidi kuondoka nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Wizara kwa ndugu zetu walemavu (viziwi), ifanye utaratibu wa kutafuta mkalimani angalau kwenye taarifa ya habari ili nao wafaidike na kupata habari zinazoendelea nchini mwetu na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile na hayo majengo nayo yashughulikiwe na yajengwe kwani yanatia aibu nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara kila la kheri.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kutoa pongezi kwa Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Kapt. Mstaafu George Huruma Mkuchika, Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote ambao kwa namna yoyote ile wameweza kutoa mchango wao katika kutayarisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika sekta ya Utamaduni. Utamaduni hasa katika sanaa ya Michezo ya kuigiza hivi sasa pamoja na kupiga hatua kubwa ya maigizo lakini kwa kweli hali ya michezo yetu ya maigizo yametoka kabisa katika utamaduni na silka zetu za Kitanzania.  Michezo mingi ya filamu zetu, waigizaji wamezama katika tamaduni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefikia wakati sasa hivi mtu mwenye heshima yake hawezi kukaa sebuleni pamoja na watoto wake wakiangalia filamu.  Naiomba Serikali kuliangalia suala hili kupitia mabaraza ya sanaa ili kuweka heshima nzuri wakati wa michezo ya kuigiza ama michezo ya ngoma mbalimbali kama vile miziki ya dansi au taarab.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.  Ahsante.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitumia fursa hii kwa kutoa michango na ushauri wangu kwa hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri. Aidha, pamoja na pongezi kwa viongozi hawa kwa uzuri wa hotuba nawapongeza pia watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kila siku ifanywayo na Wizara hii. Maendeleo mazuri yanaoonekana yanadhihirisha mshikamano wa dhati kati ya Watumishi. Nawapongeza sana kwa mipango mizuri na mshikamano mzuri wakati wa kutekeleza mipango hiyo. Mwaka 2008/2009 umeonesha mafanikio makubwa sana. Ni matarajio yangu mwaka huu tutaona matokeo bora zaidi. Ninawatakia kila la kheri kwa kila waliloomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika Tanzania kama Taifa utamaduni wa Kitanzania ujulikane. Utamaduni wetu katika maeneo mengi unakatika katika. Bado tungali na tamaduni za kikabila sisemi kuwa hali hiyo ni mbaya, utamaduni huu hautuunganishi. Utamaduni unaotuunganisha ni wa lugha tu. Tunayo lugha ya Taifa, je tuna mchezo wa Kitaifa? Je, tuna mavazi ya Kitaifa? Wakati umefika pamoja na kuendelea na tamaduni za Kitaifa, tuwe na tamaduni za Kitaifa ambazo tunaweza kuzitambulisha, tunaweza kuzitumia kututambulisha kama Watanzania. Tufike mahali tuseme huu ni utamaduni wa Kitanzania na tamaduni ambazo zinaweza kuwekewa somo katika shule zetu. Kwa mfano, sindimba na Bugogobo moja wapo inaweza kutambuliwa kama ngoma ya Taifa, ili mahali popote inapohitajika daima kuwa na kikundi cha kucheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia kuwa kila Wilaya ni vema ikatakiwa kuwa na vikundi vya Ngoma, kwaya, michezo vya Kitaifa katika ngazi hiyo. Umuhimu wa vikundi hivyo ni kwa ajili ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusiana na mambo yanayotokea katika jamii. Naamini vikundi hivi vikianzishwa na kusimamiwa vizuri vinaweza kuwa vya manufaa sana katika kutoa elimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza BAKITA kwa kazi nzuri sana linazozifanya. Kazi wazifanyazo ni ngumu, zinahitaji kutumia akili daima, Kiswahili kama sehemu ya utamaduni, kazi zao zinahitaji uzalendo wa hali ya juu. Nawatakia kheri, wasichoke, waendelee kuliongoza Taifa kupitia dirisha hili la utamaduni wetu hususan katika kuendelea kusahihisha makosa ya lugha yetu, kila makosa haya yanapotokea na kuelekea kukithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza BASATA kwa kuendeleza ujenzi wa Ukumbi wa wazi wa maonesho na mafunzo ya sanaa. Kumbi hizi ni nzuri sana. Nashauri BASATA ishawishi kila Mkoa (au ikiwezekana Wilaya) wajenge ukumbi wa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza kwa kazi nzuri. Naomba kama ilivyosemwa basi marekebisho ya sheria yaletwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamishwa ni jambo lipi hasa lililovutia Televisheni zetu nyingi hapa nchini kuwa zinaonesha filamu nyingi kutoka Mashariki ya

mbali. Ni kweli tamaduni zetu zinakaribiana ndiyo sababu? Aidha, naomba vile vile kujulishwa vikundi vyetu vya sanaa vinathibitiwaje? Hasa kwa kuzingatia uwingi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana sekta hii hasa upande wa michezo wa miguu. Tunaendelea vizuri sana. Migogoro michache iliyopo itatuliwe mapema. Nampongeza sana Rais wa shirikisho la mpira nd. Leodggar Tenga na timu yake. Ni vema tukawatia moyo, tuwasaidie wanakoelekea kukwama. Naamini tukiwalea watalifikisha Taifa hili mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta maendeleo katika sekta ya utangazaji naomba *TBC* isaidiweili jengo lao likamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kipindi hiki cha uhuru mkubwa wa utoaji wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni haki ya Raia wa nchi yetu kupata habari na pia kutoa maoni huru bado naamini kuwa Serikali yetu ina jukumu la msingi la kulinda haki hiyo. Vyombo vya habari vina kazi kubwa na muhimu ya kuelimisha, kubainisha, kuhamasisha na kutahadharisha kwa nia ya kuchochea maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vyombo vya habari vimekuwa mstari wa mbele kukosoa na kufichua maovu yanayofanywa na watu waliopewa dhamana za utumishi wa umma. Pamoja na kazi hiyo nzuri ya kufichua maovu ikiwemo matumizi mabaya ya madaraka hususan ubadhirifu na ufisadi wa mali ya umma, bado watendaji wengi wamekuwa na tabia ya kukanusha lakini uzoefu unaonyesha kuwa habari au taarifa hizo zinazoripotiwa mara nyingi huwa ni za kweli tofauti na ukanushwaji wa watendaji wetu. Navipongeza sana vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na majukumu mengine imepewa dhamana ya kuwa msemaji mkuu wa Serikali. Katika miaka ya karibuni tumeshuhudia uanzishwaji wa vyombo vingi vya habari vya binafsi jambo ambalo sina pingamizi nalo. Miongoni kwa waliochangamkia fursa hiyo ni pamoja na wafanyabiashara, wanasiasa na kwa kiasi kidogo wataalam wa fani hiyo walioamua kutumia mitaji yao midogo na taaluma zao kuanzisha na kumiliki vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba matangazo ya Serikali hutolewa kwenye vyombo vya habari ili kufikisha ujumbe mahsusi kwa umma. Ujumbe unaokusudiwa kuwafikia walengwa unalenga kuwafikia iwapo Serikali itatumia vyombo vya habari ambavyo vinawafikia watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na matarajio hayo katika miaka ya karibuni tumeshuhudia matangazo ya Serikali yakitolewa zaidi kwenye magazeti mapya, na yenye kuuza nakala chache na ambayo umiliki wake unahusishwa na wanasiasa wenye dhamana za utendaji Serikalini. Hapa mambo makubwa mawili yanajidhihirisha. Moja, mgongano wa maslahi kwa kuwa ama wao wenyewe watapeleka matangazo ya Wizara yao kwenye vyombo hivyo ambavyo wanamiliki au watatumia nafasi zao kuomba na kushawishi matangazo kutoka kwa Mawaziri wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, iwapo matangazo ya Serikali yatapelekwa kwenye magazeti yanayouza nakala chache ni dhahiri thamani halisi *(value for money)* ya fedha za umma haitapatikana. Huu ni ubadhirifu, ni ufisad na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wakati akijibu hoja zetu alifahamishe Bunge ni vigezo gani vinavyotumiwa na Serikali kutoa matangazo kwenye chombo fulani cha habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Natambua juhudi ya Wizara hii, pamoja na kuwa ni Wizara inayopangiwa Bajeti ndogo sana kila mwaka na hali ikiwa na mzigo mzito sana na mambo mengi kama inavyojionyesha katika *title* yake, mimi huitazama na kuona kuwa kuna Wizara tatu ndani ya moja. Juhudi zao sote tunaziona na mafanikio tunayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa imani yake kwangu na hatima ya kuniteua kuwa Mjumbe wa Bodi ya BASATA. Ni heshima kubwa aliyonipa, hivyo naahidi kufanya kazi kwa uaminifu kwa masilahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi na shukrani hizo naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ni kuhusu Sekta ya Habari na Utangazaji. Nawapongeza sana (*TCRA*) Tanzania kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha sekta hii inakua na kuwa bora kwa maslahi ya nchi. Nawaomba waendelee hivyo na pale palipo na dosari wasisite kurekebisha au kuomba msaada na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Sheria ya Utangazaji iletwe haraka hapa Bungeni ili tuirekebishe, kwani ni muda mrefu sasa tangu Muswada huu utangazwe kuletwa Bungeni. Hakuna haki bila wajibu na hakuna demokrasia bila nidhamu. Kwa mabadiliko ya sheria itatimiza yote haya. Lakini pamoja na sheria kurekebishwa kuna ulazima wa Serikali kuchukua hatua ya kuvipiga msasa vyombo vya habari, kwa sababu

fani hii inatakiwa iendane na dhana ya *National interest,* ambayo kuna usalama wa Taifa, uchumi, maadili na kadhalika. Haya mambo yanatakiwa kupewa kipaumbele katika utoaji wa habari mfano, zamani kulikuwa na chombo kilichokuwa kinashughulika na utoaji elimu *(mass mobilization).* Walipitia kila maeneo, Jeshini, mashuleni,vyuoni na kadhalika ili kitoe elimu kwa vizazi na Watanzania kuona umuhimu wa masilahi ya nchi katika utoaji wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata nyaraka za siri zinazotoka sasa hivi ni mapungufu ambayo chombo hiki kilisaidia sana. Mfano, gazeti lililotoa taarifa ya mafua ya nguruwe yatikisa Tanzania, hivi hapo ungetegemea nini? Moja kwa moja Mataifa yamekosa imani na Tanzania na hata kama kulikuwa na watalii au wawekezaji au jambo la faida tayari tumekosa kwani wataahirisha. Au unaporipoti tofauti na yaliyosemwa na baadaye kuomba radhi kwa maandishi madogo, unategemea nini? Tayari umepotosha umma na unaweza kuhatarisha usalama wa Taifa kwani aliyesoma jana leo anaweza asisome, hivyo atabaki na hoja ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Wizara iombe Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kurudisha kitengo kile cha *mobilization.* Hii itasaidia wengi kuelewa na kutotoa taarifa zisizo na tija kwa Taifa, akidhani anajenga kumbe anabomoa. Ieleweke tuko katika ushindani wa kiuchumi na nchi zingine, bila kuwa na chombo hiki, mtu anaweza kutumiwa ili kukwamisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vyombo vya habari vishirikishwe na Serikali kuanzisha taasisi za kutosha kutoa mafunzo kwa wanahabari pia nafasi (fursa) za nje na kurudi zitolewe ili wakajifunze huko. Pia Wizara iangalie tatizo linalosababishwa na waandishi waliosomea na tena wengine wamesomeshwa na Serikali, kukimbia fani zao na kubadili kabisa na kufanya kazi nyingine. Mimi binafsi naona ni mishahara na marupurupu hayaridhishi, inasikitisha kuona kuwa, hata *TV* ya Taifa, wafanyakazi wanaingia na kutoka kuna nini? Wizara zingatieni hilo mkishirikiana na *TCRA* ili kubaini tatizo na kulitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara iongezwe, pia kuwe na mfanano (mlingano) ili vijana hawa wafanye kazi kwa raha, vinginevyo, tutakuwa tunawalaumu kila mara pasipo muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali, ni chombo gani kinachoongoza kutoa mshahara mzuri cha utangazaji hapa Tanzania? Je, ni kiasi gani? Na kipi kimeshika mkia? Kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu Utamaduni na Sanaa. Tangu uhuru vimekuwa vikiyumbishwa tu, haviko katika Wizara moja, mpaka leo na hakuna kipaumbele hata katika bajeti. Nilipokuwa nauliza swali la nyongeza hapa Bungeni, niliomba Wizara itenge kitengo maalum kitakachoshughulikia sanaa kwa kusimamiwa na BASATA. Sijui suala hili limefikia wapi? Naomba kutoa ushauri, kuwe na wizara ya utamaduni na sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wanamuziki na Waigizaji kuibiwa haki zao, kila siku ukipita barabarani, kanda na *CD* feki zimezagaa, hakuna anayejali, wakikamatwa faini 20,000/= au 200,000/=.  Jamani, huu ni wizi mkubwa tena akipigwa faini na mzigo ule haramu anarudishiwa, ajabu!!  Tafadhali tupatiwe Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wasanii hawakopesheki, zamani kulikuwa na Mfuko wa Utamaduni uliosaidia kuto *Grant* kwa wasanii.  Nashauri urudishwe ili kuboresha kazi za wasanii na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kuhusu Nyumba ya Sanaa. Mheshimiwa Waziri, afuatilie, pale kuna ufisadi, lile jengo ni la vijana wako, jengo lilijengwa na Serikali ya Norway.   Sasa hivi limekuwa *Club* na *center* ya watu wasiohusika.  Viwanja vile ni vya Ikulu, pia kuna viwanja vingine na nyumba zilizokuwa na wafanyakazi wa nyumba za sanaa kurasini.  Naomba maelezo, nani anamiliki? Kwa mkataba huo na hatima yeke nini na Serikali imepata nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni kuhusu Vazi la Taifa.  Wizara iliandaa mashindano ya vazi la Taifa likapatikana, je, ni juhudi gani zimefanywa kutambulisha na kuendeleza vazi hilo?  Kuna viongozi wanaovaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa na naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze wewe kwanza kwa kushika Kiti hicho leo.  Pili, niwapongeze Mawaziri wa Utamaduni na Michezo kwa hotuba yao nzuri na kabla sijasahau naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kusema, kwa kuwa huwa kuna michezo ya wabunifu wa mishono kwa nguo mbalimbali na mitindo mbalimbali na kwa kuwa katika mwaka 2004 mwezi Juni kulikuwa na mashindano ya wanamitindo wa Mavazi ya Taifa hapa Dodoma na mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu Mstaafu Frederick Sumaye na katika mashindano hayo Agness Gabrieli alikuwa mshindi kutoka  Mkoa wa Kigoma na wakati wa kampeni ya 2005, Mama Salma Kikwete alishonewa mtindo huo wa vazi alishinda na kwa kuwa wanamitindo hao wanapomaliza mashindano hayo Serikali haiwajali tena.  Je, Serikali sasa mwanamtindo huyo wa vazi la Taifa la mwaka 2004 inamwambiaje?

**MHE. MANJU SALUM MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu Vazi la Taifa.  Watanzania wengi tusitake kuonekana kuwa ni watu wa aina ya pekee sana.  Tangu  lini vazi la Taifa likapatikana kwa utaratibu wa kufanyiwa mashindano.  Ningependa  nijulishwe nchi yoyote iliyoibua vazi la Taifa kwa utaratibu wa kupiga kura au kushindanisha wana mitindo.  Ninavyoelewa na ndivyo ilivyo kwa Mataifa karibuni yote kama sio yote, vazi la Taifa linapatikana kwa mfumo wa kuigiza mwenendo *(evolution*).  Watu wa Afrika

Magharibi (Nigeria, Ghana, Senegal, Togo na kadhalika) wameyapata mavazi yao kwa kuwaigiza viongozi wao wa jadi hatua kwa hatua hadi kuwafikia wananchi wote wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano wa Congo, Kinshasa (wakati wa Mobutu) wananchi waliigiza uvaaji wake wa kofia ya ngozi ya chui na koti la aina ya Abaccos; Wakongo (Zairois) wa jinsia ya kiume walimuigiza karibuni wote. Hivyo, walivaa kama yeye na wakahesabika wanavaa vazi la kuwatambulisha Wakongo. Kwa upande wa wanawake vazi lao lilikuwa kitenge, lakini chenye uvaaji wa aina ya pekee ambao uliwatofautisha na wavaa vitenge wa sehemu nyingine kama vile Afrika Magharibi. Hivyo kwa Zaire (Congo, Kinshasa) uigizaji wa vazi la kiongozi wao (wanaume) na uvaaji wa kitenge au Mbunda ilikuwa kitambulisho chao kama vazi la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waingereza, hususan wa Ireland huvaa mfano wa kikoi-kipande, au *skirt*. Hili ni vazi la Taifa, tena kwa wanaume. Waganda wanaume huvaa kanzu ndefu, kofia ya tunga (mithili ya zile za wa Morocco) na wakati mwingine na koti. Kwa wanawake huvaa nguo ndefu zilizovimba mabegani na kuongezwa na nguo nyingine toka kiunoni kuteremka hadi miguuni. Huo ndio utambulisho wao. Mzee Nelson Mandela amekuwa akiigwa kwa aina ya mashati avaayo. Hilo ndio vazi la Taifa linavyopatikana kama wengi wa Afrika Kusini watalichagua. Lakini wanalo la kwao tayari. Hivyo, huvaa mashati ya mtindo wa kiongozi wao kutokana na mapenzi juu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi siafiki kupata vazi la Taifa kwa kuandikiwa waraka wa Baraza la Mawaziri au kupigiwa kura toka kazi za wana mitindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Inashangaza kuona si Wizara wala Serikali inayotoa kipaumbele kwa lugha ya Kiswahili. Ni kweli kinatumika kama njia ya mawasiliano katika shughuli zote muhimu za Taifa, lakini hakuna juhudi za makusudi za kukifanya kiwe lugha ya kufundishia tangu shule za awali hadi elimu ya juu (vyuo vikuu). Zimekuwa zikitolewa sababu zisizo na msingi za kung’ang’ania kufundisha katika shule zetu masomo yote kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa Kiswahili. Hivi nani anadanganya kuwa kujua Kiingereza sana ni dalili ya usomi au uelewa wa mambo? Kwa nini tusiigize nchi zilizoendelea hivi karibuni na ambazo zimepiga hatua kubwa katika medani za sayansi na teknolojia. Nchi hizo ni kama Vietnam, Korea zote mbili, Malasyia, Uturuki na kadhalika, kwao Kiingereza, Kifaransa au lugha nyingine yoyote ya kutawaliwa ni lugha ya pili au ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwamba Kiingereza kitaturahisishia mawasiliano kama msingi kwani tunashirikiana na wataalam wa nchi kadhaa kama vile Japan, Italia, Sweden, Finland, Holland na kadhalika ambazo Kiingereza ni lugha yao ya pili lakini wanapokuja kwetu kufanya kazi tunaelewana na haijawahi kutokea tatizo. Ieleweke kuwa hatubezi Kiingereza la hasha, tunachosema tufundishe masomo yote kwa Kiswahili halafu Kiingereza kipewe umuhimu kama moja ya lugha za mawasiliano. Hivi sasa tunafundisha kwa Kiingereza vijana wetu wanashindwa kujieleza vizuri katika lugha

hiyo. Hivyo, Wizara ione kuwa sasa wakati umefika wa kukipa Kiswahili hadhi inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu *TBC* na ubaguzi kwa Madhehebu ya Kiislamu. Ni vizuri Waziri atoe maelezo kwa nini *TBC* haikufuata mwenendo wa *TBC* ya zamani (*RTD*) na halafu *RTD* na *TVT*? Inashangaza kwa mtu aliyeanzia kazi kwenye chombo hicho kabla hajakwenda *BBC* alete ubaguzi na upendeleo wa kidini. Inakuwaje kipindi cha mawaidha ya Kiislam kwa siku ya Ijumaa kinawekwa saa sita usiku wakati huo waumini wengi kama sio wote wapo kwenye usingizi mzito. Hivi ni lini aliweka kipindi kama hicho na muda huo kwa Wakristo siku ya Jumapili saa sita usiku? Hii sio kejeli na dharau kwa Waislamu? Jumapili karibuni yote ni vipindi vya Kanisa. Ni wakati gani alikwishafanya karibuni Ijumaa yote ikawa vipindi ama vya watoto wa Kiislam au Kaswida na dua au kusoma *Qur-an* tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ni kuhusu kumomonyoka kwa maadili kupitia vyombo vya habari. Sasa hivi tunashuhudia mambo yasiyofaa yakionyeshwa kwenye *TV* zetu kwa kisingizio cha uhuru wa vyombo vya habari na utandawazi. Hivi ni nani alisema kuvaa nusu uchi (wanawake) wanenguaji au ni lazima waonekane matumbo wazi. Lazima wacheze kiitwacho mugongomugongo (ambapo ni matusi na uchafu mtupu. Wizara ina kauli gani kuhusu uharibifu huu wa maadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru *Allah Subhanahu Wataala* kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakupongeza wewe kwa kusimamia vizuri majukumu yako uliopangiwa kama Mwenyekiti wa Bunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tatu nampogeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika na wafanyakazi wa Wizara hiyo kwa kusimamia vizuri katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hiyo imefanya na inaendelea kufanya kazi kubwa katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata habari kokote alipo ndani ya nchi na nje ya nchi lakini naishauri Wizara hiyo kutoa semina, kuendesha makongamano na mafunzo mbalimbali kwa waandishi wa habari wetu kuhusiana na maadili ya fani wanayoifanyia kazi *(code of conduct)* kwani waandishi huchukua habari na kuzisambaza katika jamii yetu kwa lengo la kuielimisha jamii na si kuipotosha jamii. Kwani utekelezaji wa maadili hayo ya wanahabari hupelekea Taifa letu kuendelea zaidi kiuchumi, kisiasa na kijamii na kinyume chake ni kulidumaza na kuliangusha Taifa letu, kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara husika kusimamia wanahabari wanaotoa taarifa za uongo dhidi ya Serikali na kuwachukulia hatua za kisheria (kinidhamu) kwani hii hupelekea kudhalilishwa kwa Serikali yetu na wananchi walio wengi kutokuwa na imani dhidi ya Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile upotoshaji wa habari dhidi ya mtu yoyote hupelekea udhalilishaji na jamii kutokwa na imani zaidi ya mtu aliyetolewa taarifa zilizokuwa za kweli.

Mheshimiwa Mwenyetiti naipongeza Wizara hiyo kwa kuleta walimu (Makocha) wengi na wazuri kwa ajili ya kuwafunza vijana wetu wanamichezo Wakitanzania. Lakini naishauri Wizara hiyo wakufunzi hawa pia wapelekwe Visiwani (Zanzibar) kwa ajili ya kuwapatia mafunzo vijana wetu wa Tanzania Visiwani ili na wao waweze kuendeleza na kukuza vipaji vyao kwa kupata taaluma kutoka kwa wakufunzi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi kwa hotuba za Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri. Pamoja na pongezi hizi nionyeshe masikitiko makubwa ya kukosekana kwa uwakilishi wa vyama vingine vya michezo nchini kama wageni waalikwa kwenye siku hii muhimu ya sekta husika. Hakuna uwakilishi wowote kutoka chama cha Riadha Tanzania, Chama cha *Netball* (mpira wa pete) Tanzania, chama cha ngumi Tanzania na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha jinsi ambavyo, pamoja na mambo mengine Wizara yetu imekuwa ikitilia mkazo mpira wa miguu pekee, huku michezo mingine ikipuuzwa. Hali hii imejidhirisha hivi karibuni wakati wa mashindano ya Taifa ya mpira wa pete mbapo CHANETA ililazimika kufanya harambee, kwa kushirikiana na *Radio one* ili kuweza kupata fedha ambazo zitatumika kugharamia michezo husika. Hali kama hii pia itajitokeza kutoka mashindano ya Kimataifa yanayotarajia kuanza mwezi Septemba, mwaka huu ambapo mpaka dakika hii hakuna dalili za msaada wowote kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri mwenye dhamana anifafanulie mambo yafuatayo:-

Moja, ni vigezo gani vilivyotumika kuchagua chama kimoja pekee cha michezo kuja kama mdau wa michezo?

Pili, nini kilichofanya Serikali isitoe msaada wowote CHANETA wakati wa TAIFA *CUP* zaidi ya shilingi milioni moja, tena baada ya mashindano kwisha na baada ya kubembelezwa sana.

Tatu, nini mikakati ya sasa na baadaye toka Serikalini yenye dhamira ya kufufua mchezo wa *netball* nchini?

Nne, fungu linalotengwa maalum katika mikoa (*RAS*) yenye madhumuni ya kusaidia sekta ya michezo mikoani zinafanya shughuli gani mpaka kupelekea baadhi ya mikoa kushindwa kushiriki TAIFA *CUP*?

Tano, kwa nini hakuna ruzuku ya michezo, hasa kwenye vyama vya michezo ya ngumi, riadha na *netball*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Baraza la Michezo (BMT) limekuwa bila Katibu, ni lini nafasi ya Katibu itajazwa ili kufanikisha utendaji bora wa kazi wa Baraza husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ningependa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni kwa namna gani Wizara yake inashiriki moja kwa moja katika kulinda maslahi hasa ya waandishi wa habari wa kawaida ambao wanakuwa wakilipwa na waajiri wao *(has private sector)* mishahara midogo sana. Kuna mikakati gani ya kuhakikisha kunakuwa hakuna *gap* kubwa ya mapato baina ya waandishi wa habari (wa kawaida) na Wahariri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa inashangaza jinsi ambavyo vyombo vya habari vya Serikali, vimekuwa vikitumika kutoa habari za uongo, uzushi na zenye malengo ya kuleta uchochezi. Gazeti la Habari Leo, kwa siku za hivi karibuni limekuwa ni gazeti linalotoa taarifa ambazo hazina ukweli wowote. Cha kusikitisha Mhariri wa habari anathubutu kuruhusu habari itoke huku akijua kwamba habari husika ni za kupikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu, atalichukulia hatua gani gazeti la Habari Leo, pale ambapo ataletewa ushahidi kuthibitisha madai tajwa hapo juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda Mheshimiwa Waziri anipe mkakati wa Serikali hasa kuhusiana na haki na maslahi ya wasanii wetu ambao haki zao zimekuwa zikiishia kwa wajanja wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuboresha michezo. Hata hivyo napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mila na utamaduni. Kumekuwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa vijana wetu na hili linachochewa kwa kiasi kikubwa na vyombo vyetu vya habari hasa *TV* La kushangaza zaidi ni kuwa *TBC* imeshika bango katika hili. Naomba Serikali isirushe hewani vipindi vya aina hiyo kwa sababu vinatudhalilisha sana. Mifano ya kuporomoka kwa maadili hayo ni katika mavazi na maongezi na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi cha *Comedy* hufanya kazi nzuri ya kuelimisha na kuburudisha lakini wanaanza kupoteza mwelekeo kwa wanaume kujifanya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhuu chama cha mpira wa miguu *TFF* na *ZFA*. *TFF* inafanya kazi nzuri ya kukuza mpira wa miguu nchini kiasi kwamba Tanzania si kichwa cha mwendawazimu tena. Hata hivyo *ZFA* ni chama cha mpira wa miguu Zanzibar ambacho kina majukumu sawa na *TFF*. Tatizo ni kuwa *TFF* wanapata misaada ya kifedha na kiufundi kutoka *FIFA* kwa niaba ya Tanzania, kwa nini basi Zanzibar isifaidike na misaada hiyo ya *FIFA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni kielelezo kikubwa cha Mtanzania na kimetumika sana kujenga umoja wa Kitaifa Tanzania. Kwa hiyo, kuna haja ya sisi wenyewe kukikuza Kiswahili. Kwanza kwa kukitumia sana kila mahali, katika Miswada ya Bunge na katika Ofisi na Mikutano yote ya Kitaifa. Vile vile Kiswahili kisomeshwe kwa vijana katika ngazi ya Shahada ili watumike kusomesha nchi nyingine. Lugha ya Kiswahili inatambulika kama lugha rasmi katika vyombo vya Kimataifa kama AU, UNO na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo shuleni. Serikali ya Awamu ya Tatu ilifanya kosa kubwa kuondoa michezo mashuleni yaani uamuzi ule wa kufunga mtaala wa michezo katika shule zetu. Kwa kuwa shule ndio chemchem ya kuwapata wanamichezo mbalimbali, hali hii iliifanya nchi yetu kurudi nyuma sana katika fani ya michezo ya riadha na mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwe makini sana na viongozi ambao hawaangalii mustakabali wa nchi na raia zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TBC 1. Chombo hiki kimeleta mapinduzi makubwa katika utangazaji hata kuweza kushindana na *TV* za watu binafsi. Hongera sana *TBC 1* na *Radio* yake. Ila Serikali iwaone kwa maslahi zaidi wafanyakazi wake.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa Habari na Mheshimiwa Bendera, Naibu Waziri kwa kazi nzuri na ngumu ambayo kwa kweli wanaimudu na kuisimamia vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee *TBC*. *TBC* wanafanya kazi nzuri kwenye mazingira magumu sana ambayo kwa kweli hayafai hasa ukizingatia chombo hiki ni cha Serikali. Jambo hili ni la aibu ukiangalia majengo mabovu na yanavuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* wanalo jengo kubwa na la kuwatosheleza kama litashughulikiwa ili kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa zimechukuliwa na *TBC* kumaliza jengo hilo lakini Hazina haijakubali udhamini (*guarantee*) kwa *NSSF* kulimaliza jengo hilo kwa visingizio visivyo na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina kuna jambo na kuna haja kuchunguzwa kwa sababu pia Wizara hii hii imekosa kununua jengo ambalo lilikuwa litumiwe na Idara ya BAKITA na Hazina ilicheleweshа taratibu na jengo likauzwa kwa wanunuzi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Waziri alibebe suala hili kama mali yake, afuatilie hata kama atafika kwa Mheshimiwa Rais lakini ujenzi uanze mara moja kusitiri aibu iliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kupongeza sana kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii na sina tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kwanza nizungumzie juu ya Waandishi wa Habari. Nashauri wenzetu hawa pamoja na kuvutia biashara pia wawe ni watafiti wa mambo wanayoandika kabla ya kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia kuhusu suala la utamaduni. Ni kweli kabisa unamomonyoka sio vijana tu hata wazee. Napenda kusema sio ile lugha tunayoongea eti watoto wa siku hizi, ni wazazi wa siku hizi. Sisi ndio hasa wa kulaumiwa, tunashindwa kulea kwa sababu tumekua *busy* sana na kutafuta maisha. Tunasahau wajibu, wazazi sio tu kuwatafutia watoto chakula, elimu na mavazi bali pia kuona watoto hawa wanapata malezi bora ya kulinda utamaduni wetu. Suala la mtoto kuvaa ovyo tunaanza sisi wazazi kuwanunulia watoto nguo hizo wakiwa wadogo hasa watoto wa kike. Mbaya zaidi nguo nyingi za aina hiyo tunaagiza wenyewe kutoka nje, aidha mpya au mitumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanzisha kikundi cha taarab. Si Mheshimiwa Waziri wala Naibu Waziri, wote wanafahamu kuwa taarab ni ngoma ya kistaarabu. Leo ngoma hii baadhi yetu tumeigeuza geuza eti ni *Modern* Taarab. Matokeo yake mavazi yanayovaliwa na baadhi ya wacheza taarab sio kabisa. Mbaya zaidi huo uchezaji unashangaza. Siku hizi kuna eti rusha roho, mwanamke nyonga. Huko kunyonga ni hatari. Siwezi hata kueleza tangu vijana hata wazee wanaaibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliacha kwenda muziki wa *dance* baada ya kuja *brake-dance* na hiyo mitindo yao mipya ya Kizaire. Sasa leo hata taarab ambayo imo ndani ya damu ya watu wa Pwani nikiwemo na mimi nayo huwezi kwenda na mtu unayemstahi. Maneno ya nyimbo balaa na uchezaji ndio usiseme. Naomba Mheshimiwa Waziri, hatujachelewa turudishe heshima yetu. Baadhi ya nyimbo hazifai kurushwa hewani. Tulikataa baadhi ya nyimbo hapo nyuma sasa nini kimetokea tukajisahau? Taarab ni mafumbo au sifa zinazokubalika au maneno ya matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na Mheshimiwa Mzee wetu kuongea kama nilivyoandika mimi. Sio watoto wa siku hizi bali wazazi wa siku hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Kaptain Mstaafu G. H. Mkuchika. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa J. Bendera, Katibu Mkuu na Wataalam husika kwa hotuba hii ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa juhudi zinazofanywa kuboresha utendaji wa kazi katika nyanja zote za shughuli za Wizara hii lakini nitajikita hasa kwenye michezo. Kuna wachezaji wazuri wanaoibuka katika Wilaya zetu kwenye *football, Netball, Basketball* na hata riadha. Tatizo ni kwamba hatuna Maafisa Michezo wenye sifa katika baadhi ya Wilaya zetu ambao wangeweza kufuatilia kwa karibu vipaji mbalimbali vya michezo. Pia Halmashauri zetu hazitoi kipaumbele kubuni namna ya kuanzisha Mfuko wa kudumu wa kuendeleza michezo. Kugharamia michezo katika Halmashauri zetu inaonekana kuwa ni usanii, hivyo hakuna msukumo wa dhati unaotolewa kwa lengo la aidha kuibua vipaji katika michezo au kuboresha. Hivyo, nashauri Serikali kupitia Halmashauri zetu kuajiri watu wenye sifa husika ili kuendeleza michezo katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Mkapa kwa kuthubutu kuamua ujenzi wa uwanja wa michezo wa Kimataifa, *National Stadium* Dar es Salaam. Pia nampongeza Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa J. M. Kikwete kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha michezo nchini hatua hizo ni pamoja na kuajiri makocha kwa timu ya Taifa ya Mpira wa miguu na sasa riadha. Mwelekeo huu wa viongozi wetu wa Kitaifa kwa upande wa michezo ni mzuri na ni chachu kubwa kwa Serikali kwa ujumla na kwa wapenda michezo wote. Tunachotakiwa ni kuunga mkono jitihada hizo ili kuinua hali ya michezo nchini hali ambayo itasaidia kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa mfano mdogo nilioupata mwaka 1973/74. Nilikuwa Bucharest Makao Makuu ya Romania kikazi, niliulizwa na baadhi ya kundi la wenyeji niliokutana nao, waliniuliza ninatoka eneo gani, nikataja Tanzania. La kushangaza hawakumjua hata Rais wa wakati huo hayati Mwalimu Julius Nyerere, badala yake walikumbuka kwamba Tanzania ndiko alikotoka Mwanariadha Filbert Bayi. Hivyo nchi yangu ilitambuliwa hivyo. Hii ina maana kwamba michezo inasaidia sana kuiuza au kuitangaza nchi. Hivyo, Serikali ina sababu zote za kuhimiza na kuboresha michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kueleza kwamba Wilaya ya liwale tunatenga uwanja wa michezo kwa kushirikiana na nguvu za wananchi na Halmashauri yetu. Ukuta wa kuzunguka uwanja wote kwa matofali ya kuchoma unaendelea vizuri.

Tunahitaji msaada wa kukamilisha ujenzi huo. Bado kazi kubwa na muhimu kama sehemu ya kujenga jukwaa kuu, plasta, kujenga sehemu ya watazamaji na kadhalika. Hata hivyo, mikakati ya kuomba misaada ya kukamilisha ujenzi huu inaendelea. Mimi mwenyewe nikiwa kama Mbunge nimekwishaandika *writeup* kwa kuwatumia wataalam wa Chuo cha Ardhi, Dar es Salaam na kutuma kwa wafadhili, tunasubiri matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kutuunga mkono jitihada zetu. La msingi zaidi ni kuomba atembelee Liwale katika siku za karibuni. Kwa mwaliko huu naungwa mkono na *DC* wangu ndugu Chiwile na uongozi wa Halmashauri na Chama kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akubali mwaliko wetu. Mungu ambariki kwa shughuli zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na narudia kusema nunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Michezo ni afya, michezo ni ajira, michezo ni burudani, michezo ni sekta ambayo ikitumiwa vizuri inaweza kusaidia kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Ni vema michezo ikaimarishwa katika shule za msingi hadi sekondari, Mijini na Vijijini kwa makundi mbalimbali wakiwemo vijana na wazee.

Mheshimwa Mwenyekiti, michezo ni pamoja na ile michezo ya jadi ambayo inasaidia kutangaza Utaifa wa nchi yetu katika nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya michezo inaweza kuwafikia wananchi wengi kupitia vyombo mbalimbali kama vile redio, magazeti, *television*, majarida, vipeperushi na kadhalika. Hivyo, ni vema Serikali ikaandaa utaratibu ambao utasaidia kuwafikishia wananchi taarifa mbalimbali zilizo sahihi kuhusu michezo ili wavutike na suala zima la michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni wetu wa asili unaharibiwa kwa kufuata tamaduni za kigeni. Ni vema Serikali kuliangalia suala hili kwa makini zaidi ili tuendelee kuimarisha tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguo wanazovaa baadhi ya vijana wa kike hazifai kabisa kwani zinaonyesha hata sehemu za siri ambazo hazistahili kuonekana. Ni vema Serikali ikaliona tatizo hili na kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vipewe nafasi ya kutoa taarifa mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii pamoja na wale wanaohujumu uchumi wa nchi bila ya upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malumbano baina ya waandishi mbalimbali wa habari hayaleti sura nzuri na yanababaisha jamii na hivyo kushindwa kuelewa wafuate taarifa za waandishi gani wa habari. Ni vema wakielewana ili kujenga mustakabali mwema wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya michezo vya aina mbalimbali vijengwe na kuimarishwa katika maeneo mbalimbali. Hii itasaidia kujenga uzoefu na kuibua vipaji vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili kama lugha ya Taifa na Kimataifa iendelezwe, kukuzwa na kuimarishwa pamoja na kutumika katika taasisi mbalimbali badala ya kutegemea zaidi lugha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa habari wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kuendana na wakati ndani na nje ya nchi badala ya kulaumu tu taarifa zinazotolewa na baadhi ya waandishi huenda ikawa ni kutokana na taaluma ndogo waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JAMES DAUDI LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ni pamoja na kusimamia shughuli za vyombo vya habari nchini na kusajili magazeti na majarida na kukusanya na kusambaza taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu shughuli za Serikali kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kukusanya na kusambaza habari ni kazi ambayo inahitaji fedha nyingi na rasilimali watu. Hivi, gazeti la nchi yetu limekwenda wapi? Kama lipo linatolewa mara ngapi katika mwaka? Napenda kufahamu Idara ya Habari ina watumishi au waandishi habari wangapi na ina vituo vingapi Mikoani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi ya kuandikisha au kusajili magazeti pamoja na waandishi wa habari naona kazi hii haifanyiki kwa uadilifu, inakuwaje kila siku magazeti yanaanzishwa lakini baada ya kuanza kutolewa magazeti haya yameonyesha kutozingatia maadili? Je, ni kwa nini maudhui yaliyomo katika maombi ya kuanzisha magazeti hayo huwa hayazingatii yaliyomo katika madhumuni ya kuanzishwa kwake lakini wakati huohuo Idara inayohusika kushindwa kudhibiti magazeti kama hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, gazeti la Habari Leo, toleo la jana, gazeti hili ni la Serikali lakini ni miongoni mwa magazeti ambayo mara kwa mara badala ya

kutekeleza sera ya kuanzishwa kwake kama gazeti la Serikali hujihusisha katika mambo tofauti kabisa kama ya ushabiki wa kisiasa. Katika gazeti la jana kuna habari inayowahusisha baadhi ya Wabunge kuwaonea kijicho Mawaziri. Je, habari kama hiyo inafaa kweli kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali?

**MHE. SIGFRIDI SELEMANI NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa hongera kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake Mheshimiwa Joel Bendera, Katibu Mkuu na Watendaji wake. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ili adumu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura wangu wa Ruangwa wameniomba nimwulize swali moja tu. Je, mipira mizuri ya mpira inapatikana wapi? Zamani walikuwa wananunua Ndanda *Mission*, sasa wananunua Dar es Salaam lakini wakichezea siku moja tu inapasuka! Je mipira mizuri waende wakanunue wapi? Hata hivyo, mipira hiyo ni ghali sana, ni Tshs. 40,000/= lakini mechi moja tu imepasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wenyeviti, Wakurugenzi na Makatibu wa Mabaraza, Taasisi na Vyama vya Michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Rais wa Chama cha Mpira wa Miguu, wote ni wanamichezo, kwa bahati mbaya wote ni wanachama na washabiki wa Timu ya Yanga. Naomba wapunguze ushabiki na kulea pia Timu ya Simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo na angalizo, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu Chama cha Madaktari wa Tiba ya Wanamichezo Tanzania (*TASMA*). Nashauri Chama kipanue huduma zake hadi mikoani kwa kuanzia na baadaye Wilayani. Lengo la Chama ni kuwahudumia wanamichezo katika michezo mbalimbali. Matokeo ya uchunguzi na tiba ya wanamichezo yatunzwe katika Ofisi za *TASMA* – Mkoani. Mimi kama Rais wa kwanza wa *TASMA* nitakuwa tayari kutoa michango yangu kuhusu uboreshaji wa *TASMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu Sera ya Michezo. Ushauri wangu ni kwamba, sera hii ilitolewa mwaka 1995. Tangu Sera hii itolewe, michezo imeboreka na kuleta mabadiliko makubwa duniani. Ili Tanzania iweze kwenda na wakati kuhusu mabadiliko makubwa ya kimapinduzi, itabidi sera hii ipitiwe tena kwa lengo la kuiboresha. Nashauri wakati sera ya michezo inapitiwa wadau wengi washirikishwe hasa Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu waamuzi katika klabu Bingwa. Nashauri timu ambazo zinalalamikia waamuzi kupendelea timu zingine, waruhusiwe kutoa mapendekezo yao katika *TFF* kwa mfano, timu moja imeomba maamuzi kutoka nje ya Tanzania isimamie mchezo kati yake na timu nyingine inayobebwa na waamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES ALEX MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Komredi G.H. Mkuchika, Waziri wa Wizara hii kwa ujasiri na umahiri wake katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii ambayo mambo yake yako katika habari kila uchao. Pia nampongeza sana Naibu wake, Mheshimiwa Joel N. Bendera kwa umahiri wake mkubwa katika kutoa maelezo na majibu kuhusu hoja mbalimbali zinazoelekezwa kwa Wizara hii, lakini pia kwa mchango wake mkubwa katika kusimamia yote yanayoshughulikiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inasimamia maeneo makuu matatu ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii yetu. Habari zikiwa sahihi na kwa muda muafaka basi mpokeaji atazitumia kwa manufaa na kupata ufanisi katika shughuli zake. Manufaa hayo ndiyo pia yatakayomjenga mwananchi huyu kiutamaduni pia. Utamaduni wake utakuwa umejielekeza kwa msingi wa taarifa au habari sahihi zilizofikishwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari au taarifa zisizo sahihi zikimfikia mtu, basi yote atakayoyafanya yatakuwa katika msingi huo na hakika hayatakuwa ya kuleta tija kwa jamii husika. Ndiyo maana dhana hii ya habari inachukua nafasi ya msingi sana katika yote anayofanya mtu katika kuendeleza jamii yake. Maana yake ni kwamba, Wizara na nchi nzima kwa kweli tuwe makini katika suala zima la habari, kuanzia katika utafutaji mpaka utoaji wake, usahihi wake, malengo yake na hadi katika kutolea taarifa tena kufikiwa kwa malengo hayo au vinginevyo. Ni muhimu sana habari kama dhana ikapewa umakini stahiki ili mwelekeo wa mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla ukabakia katika dira iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa ni kwamba, lazima kuwa na usimamizi wa karibu sana ili tusipoteze malengo yetu. Basi napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wizara nzima kwa kuifanya kazi hiyo kwa mafanikio endelevu. Juhudi ziendelee na tutawaunga mkono kwa kadri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante.

**MHE. BENITO MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kabisa napenda kutambua mashindano ya Kombe la Muungano Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano haya yalianza mwaka 1994 yakiratibiwa na Ndugu Daud Yasin, mimi Benito Malangalila nikiwa Mwenyekiti. Naomba tutambuliwe na tusaidiwe katika kuyaendesha mashindano haya.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mnisaidie kupata majibu haya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni lini Taifa letu litabuni vazi la Taifa ili mtu aweze kutupambanua na watu wengine kwa vazi tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hivi huu unyago na jando vimehamishwa majumbani na kuhamia kwenye *TV*? Ni lini mtayafanyia kazi mambo haya? Shukrani.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia hoja hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Naibu wake jinsi walivyoiandaa hoja yao na kuiwasilisha kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tuna mila na tamaduni zetu ambazo tumezirithi toka kwa wazee wetu, lakini kinachotokea sasa ni kuacha mirathi yetu na kuiga tamaduni za nje ambazo zinaharibu ama kupotosha mila na silka zetu za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii ni kama Walimu kwani wanafundisha kutokana na maigizo yao, hivyo watoto wetu wanajifunza mambo mengi kutoka kwao. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba wanaoigiza hawapotoshi jamii, yaani kuwe na mipaka katika maigizo. Mambo ya ndani kuonyeshwa hadharani sio jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mavazi ya wasanii wa kike yaangaliwe ni sababu gani inayofanya wanaume wasitiri maungo yao na wanawake wacheze uchi? Hivi hatuoni kwamba Watanzania tunajitukanisha? Hivi hatuoni kwamba wanawake tunadhalilishwa kupita kiasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa waigizaji wetu wa *TBC the Comed* ni wazuri tunawapongeza sana kwa namna moja au nyingine wanaelimisha jamii lakini mambo mengine wanayofanya sio mazuri. Wanafundisha vibaya watoto wetu na pia lugha nyingine wanazotumia sio nzuri, naomba tuwaangalie ili kulinda na kudumisha mila na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma mashuleni kulikuwa na somo la michezo ambalo lilikuwa na *syllabus* yake kabisa na kila wiki lazima lifundishwe kwa vile lilikuwemo kwenye *time table*. Ni kwa nini haturejeshi utaratibu ule? Kwa kuwa michezo ni afya na mwanafunzi anashawishika zaidi kunapokuwa na kipindi cha michezo katika masomo yake ya kutwa, naiomba Serikali ianzishe tena mfumo ule kuanzia shule za msingi ili watoto wetu waweze kujulikana vipaji vyao tangu wadogo kwa nia ya kuvikuza na kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kushauri kwamba kuwepo na Sheria itakayowalinda wanawake waigizaji ili kuzuia akinamama wasiigize wakiwa uchi na badala yake wajistiri wanapofanya shughuli zao za uigizaji kwani kwenda uchi sio uzuri wa mchezo bali ni kumdhalilisha mwanamke.

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, kwa kazi nzuri anayofanya. Zipo changamoto nyingi, sitarajii kwamba zitashughulikiwa mara moja na kuisha lakini ni vema Wizara hii ikathaminiwa na kuongezwa bajeti yake hasa katika ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyombo vya habari. Taarifa za habari mara nyingi zinatoa kipaumbele kwa habari za kimataifa zaidi kuliko za ndani. Tubuni kwa makusudi programu za Watanzania kuipenda nchi yao, watoto na vijana kufahamu historia ya Tanzania na kuwathamini na kuwafahamu viongozi wa Kitaifa, Wilaya, Kata mpaka Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti yaache kuangalia zaidi kuuza tu gazeti bila kutilia maanani maadili na utamaduni wa nchi yetu. Hii inaweza kufanyika bila kuathiri uhuru wa vyombo hivi, ni suala la uzalendo au Tanzania kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari za Wilaya na Vijijini, natarajia magazeti na *TV* za Umma, zitafanya kazi zaidi na hasa kuangalia mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali Kuu, Halmashauri na hata Wabunge. Programu ya *TBC* kuhusu barabara toka Mtwara hadi Bukoba, ni mfano bora sana. *TBC* walimpa zawadi ya kanga Bibi Mzee, hii ni nzuri. Tufanye zaidi, hongereni sana tuondokane na kuonyesha mambo mabaya tu au *scandals* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vyombo vya habari vina jukumu la kufukuza uovu lakini isiwe ni agenda hiyo. Maana lipo jukumu pia la kuonyesha mafanikio na mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali, kampuni na hata watu binafsi. Kwa mfano, barabara ya Kilwa sasa imeleta unafuu mkubwa kwa wananchi wa Mbagala, sijaona habari yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa Habari, pengine *specialization* itafaa si vyema leo Mwandishi anatupa habari za michango, kesho yupo kwenye uchumi. Tuwatie moyo Waandishi kujikita katika taaluma fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Utamaduni Wilayani, mara nyingi wanajihusisha na shughuli za mwenge na ngoma tu. Nadhani wanaweza kufanya zaidi. Lakini pia hawana vitendea kazi. Je, upo mwongozo wa wao kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo mashuleni, sasa inarudi lakini tatizo ni vifaa. Naomba tuongeze nguvu. Huu ni utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiongezee nguvu timu yetu ya Taifa. Hatua tuliyofikia ni nzuri na inahitaji pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni unafanya kazi nzuri sana. Ni matumaini yangu Mbinga pia itaangaliwa. Tunao utaratibu kule wakati wa kiangazi tunateremsha ngoma na kuanza kufurahia mazao yetu na kujipongeza kwa kazi. Ukifika wakati wa masika, ngoma zinapanda darini na majembe yanateremka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawakaribisha Mbinga mwezi huu wa nane. Itakuwa vyema kama Mheshimiwa Waziri ataongoza msafara huo. Tunaweza kuwa na filamu nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara mafanikio na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mungu kunijaalia kupata fursa hii ili kuchangia Wizara hii. Nichukue hatua za mwanzo kumpongeza Mheshimiwa *Commrade* George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri na ukweli usiopingika, Wizara hii ni nyeti sana hasa kama mdau wa kuhabarisha jamii katika masuala mbalimbali. Hivyo, ni Wizara inayoweza kabisa kuchochea maendeleo ya nchi na wananchi wake kwa ujumla. Katika kukua kwa sekta ya mawasiliano Duniani, ni sekta inayoambatana na umakini au ubora wa habari unaotokana na wanahabari wenye taaluma inayokubalika au inayotambulika Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mungu na kutoa pongezi kwa vyombo vya habari vile vinavyoandika au kutoa habari baada ya kufanya uchunguzi wa kina *(investigation news).* Inashangaza na inahuzunisha pale ambapo vyombo vingi vya habari hasa magazeti ambayo mengi sasa yanaibuka kama uyoga kuandika habari za watu, jamii za kitaifa hata kimataifa bila kufanya *'cross checking'* na wahusika, uandishi wa aina hii ni hatari sana sio tu inaleta mifarakano katika jamii bali pia inasababisha au kushusha heshima za watu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti tatizo hili kubwa kwa jamii, naomba Wizara ikamilishe taratibu za mchakato ili kuleta Muswada katika Bunge ili kuwe na Sheria madhubuti ambayo itaondoa kwa kiasi fulani tabia ya baadhi ya watu kutumia vyombo vya habari kuumiza jamii ama watu kwa maslahi binafsi. Kadhalika Sheria ya Usajili wa Vyombo vya Habari hasa magazeti, Sheria hii nayo kwa kiwango fulani inasikitisha. Inashangaza kuona mtu mmoja amekuwa mmiliki wa magazeti au vituo vya television zaidi ya kimoja. Uholela huo sio wa hatari tu hata kwa usalama wa nchi bali unanyima fursa kwa wadau wengine wenye nia ya dhati kabisa ya kutaka kuwekeza kwa sekta hii. Ninachosisitiza ni juu ya kutumia vyombo vya habari kuchochea mambo muhimu ya kimaendeleo kwa nyanja za uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuzungumzia suala la utamaduni, nchi yetu ni nchi ambayo inayo makabila mbalimbali na makabila haya kila kabila linalo utamaduni wake. Utamaduni wa kufuata mila za makabila mbalimbali pamoja na kwamba zipo mila ambazo zimepitwa na wakati lakini kwa kiwango fulani tamaduni za makabila zilisaidia sana kuwa chanzo cha maadili mema kwa jamii. Kwa kuzingatia mila na desturi, jamii ilihamasishwa kushiriki kwenye shughuli za kimaendeleo, kuaminiwa miongoni mwa jamii, kuheshimiwa kupiga vita wizi, ulevi na kadhalika. Pamoja na juhudi za Kiserikali kulinda na kuimarisha maadilii ya Kitaifa bado nashauri Wizara kupitia Halmashuri za Wilaya, kwa Maafisa Utamaduni wa Wilaya, uwepo utaratibu wa uendelezaji wa mila na desturi za makabila zile ambazo ni mfano wa kuigwa ili zioanishwe na za Kitaifa katika ujenzi wa misingi imara ya jamii yenye maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, ninapenda kutoa wito kwa Wizara kuwa makini na hali ya upotoshaji wa uhalisia wa utamaduni wa Mtanzania. Yapo mambo mengi yanayoingizwa katika kupotosha ukiwemo muziki. Miziki asilia kama ile ya akina Marehemu Mbaraka Mwishehe, Mwaluko, Juma Kilazi Marijani, Shabani Marijani na wengine wengi ambao wengine wametangulia mbele ya haki lakini wengine wapo, inapotoshwa na kugubikwa na muziki wa kizazi kipya. Taarabu nayo sasa inaondoka, kuna muziki wa mwambao uliosheheni utunzi wa nyimbo nzuri na kuliwaza na kutoa raha kwa msikilizaji sasa imegeuzwa sawa na muziki kutoka Zaire ule wa Ndombolo ya Solo au Sebene na sasa maarufu kama Rusha Roho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Wizara kukutana na wasanii ili kuwahamasisha zaidi miziki yao isiende nje ya maadili ya utamaduni wetu wa Kitanzania. Pia Wizara kuwa na Sheria madhubuti ya kuwalinda wasanii hasa kwa Haki Miliki *(copy rights)* ili kudhibiti wizi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wanaowaibia wasanii na hivyo kufanya hali za wasanii kuendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na mchezo wa mpira wa miguu. Namshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kumlipa kocha wa Taifa Marcio Maximo, lakini inashangaza sana suala la migogoro au kukwazana kwa maamuzi kwa Sekretarieti ya *TFF*. Hivi inakuwa vipi watu wa ofisi moja kuwe na kauli mbili tofauti? Inashangaza kuona Katibu Mkuu wa *TFF*, ndugu Mwakalebela anatoa kauli lakini Afisa Habari wa *TFF*, ndugu Florian Kaijage akitoa kauli inakuwa tofauti, mbaya zaidi yupo mwingine, Mkurugenzi wa Ufundi, naye amekuwa na kauli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Rais wa *TFF*, ndugu Leodiger Chille Tenga pamoja na Kamati yake ya Utendaji, wawe makini na wababaishaji hawa na ikiwezekana kama bado wataendelea na ushindani wao basi wawajibishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Habari na Michezo kwa kusoma vizuri taarifa. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Waziri na Wizara yake kwa kuleta wataalamu wa michezo wa *boxing, judo* na kadhalika makocha hao kwa kweli watatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru *VODA* kwa kuendeleza michezo Kusini Lindi na Mtwara. Wameweza kufadhili mipira, majezi, chakula na malazi kwa Mikoa kadhaa, lakini Mtwara na Lindi sisi shukrani zetu hatutawasahau, wametusaidia sana sana. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Coca Cola* pia wameweza kusaidia michezo mbalimbali hadi timu zile za watoto wakawa wa tatu (3) Kimataifa katika *Copa Coca Cola*. Tunawaomba mashirika mengine waige mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lugha ya Kiswahili, tuangalie sana watu wanapoongea lugha ya Kiingereza au Kiswahili, wasichanganye Lugha. Imegundulikana kuwa, inataka kuzoeleka, wasomi wanachanganya lugha wakati wa kuandika makala au wakati wa kueleza kitu, wanaingiza lugha mbili tofauti hivyo kuwachanganya wananchi, hasa Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mwaka jana, Rais wa TFF, alitangaza kuanza kwa mpira wa *football* wa wanawake. Mpira huo, kwa bahati nzuri nchi nzima umeanza lakini sasa wamejikuta wanawake hao hawana msaada wowote kutoka popote, hawana jezi, hawana mipira, hawana chakula na malazi wanapoanza shughuli hizo. Tunaomba Serikali iwasaidie fedha za kuanzia ili waendelee kujitangaza.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya utamaduni, sasa kunajengeka matumizi ya neno utamuduni wa Mtanzania, maadili ya Taifa na kadhalika. Nadhani kisayansi, matumizi haya na dhana hii inatumika vibaya hasa ikizingatiwa kuwa hakuna utamaduni ulio *static* wala maadili yanayokuwa *static*. Mambo hayo yanabadiliko na nyakati, *generation*, na teknolojia. Nchi kama Tanzania, yenye makabila zaidi ya 130 na mengi yakiwa na *dialects* zao au na mchanganyiko mkubwa wa Madhehebu ya Dini, suala la utamaduni, maadili, mila na desturi *(customs)* linakuwa gumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inafanya nini kuainisha mila na desturi sahihi za Kitanzania, upi hasa utamaduni wa Kitanzania (mfano Sindimba inakubalika kwa makabila fulani na inaonekana dhambi kwa mengine). Tusipofanya utafiti wa kisayansi na kuwa na *common denominator* katika mambo hayo, tutaendelea kuwa na dhana zinazogongana, jambo ambalo hata hapa Bungeni sasa limeanza kujitokeza.

Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa kina kujenga misingi ya kitaifa na isiishie kusimamia michezo, vikundi vya sana na kadhalika kwani hivyo ni viashiria tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Waandishi mbalimbali wamelalamikiwa na kulaumiwa kwa maandishi yao yanayoonekana kutofuata maadili ya uandishi. Hata hivyo, Taifa lina program gani ya uhakika kwa Waandishi wa Vyombo vya Umma na hata wa vyombo binafsi *(at least as a standard and or minimum requirement).* Waandishi wasio na sifa, au wanaopita tu kwenye kozi fupi fupi, wasitegemewe kutimiza kazi zao kikamilifu. Serikali imetoa mwongozo gani au inaishia tu kutoa *'press card'* na mwisho kulalamika kwa maandishi *sub-standard?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi katika nchi za wenzetu wanafanya *'specialization'*. Michezo inaandikiwa na mtu aliyesomea uandishi wa habari za michezo, vivyo hivyo siasa, mambo ya uchumi, au afya ili Mwandishi aandike akiwa na taaluma husika na kufanyia tathmini mada husika, tofauti na *copy typing or reproducing* hotuba ya mtoa hotuba tu na au hata kuiandika tofauti kutokana na uelewa usiotosha wa suala husika. Hii itaondoka si kwa Waziri kukemea bali kwa Wizara kutafuta *root cause* ya matatizo hayo na kuyatafutia ufumbuzi sahihi. Idadi ya watumishi wa Serikali ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waaandishi wa Habari wa Serikali na hata binafsi hawana "*Scheme of Service*" au "*Salary Scales*" zinazoeleweka. Magazeti mengine huwalipa Waandishi wake na hasa "*Correspondents* Shs.1,500/=; Shs.3,000/= wa juu sana Shs.10,000/= kwa *story*. Kwa mtindo huu, hata rushwa, Waandishi kushawishiwa na wanaowalipia gharama ni mambo yasiyoepukika. Wizara inatoa kauli gani kuondoa hali hii na hasa kuwa na "*scheme of service*" na "*salary scales*" za uhakika kwa Waandishi wa vyombo vya Serikali na kuweka "*minimum requirement*" au "*Standard*" kwa vyombo vya binafsi na labda kuwa na chombo huru cha kusimamia maslahi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, majukumu ya Wizara katika habari ni pamoja na kutunga sera na kuzisimamia. Hata hivyo, dhana ya uhuru wa vyombo vya habari haionyeshwi kwa uwingi wa vyombo vya habari, wala wa vyombo hivyo kuandika wanavyotaka. Uhuru wa vyombo vya habari ni pale panapokuwa na "*Objective Standards*", ambazo zinajulikana kwa wote ambazo zinatumika kusimamia maadili ya Waandishi wa Habari. Kwa sasa "*standard*" hizo ziko kwa Waziri au Mkurugenzi wa Habari, ambao ndio wana mamlaka ya kukemea, kufunga na kufungia gazeti. Hili halikubaliki kwa *'standard'* yoyote katika nchi ya demokrasia yaani Wizara kuwa *'regulator'*, Polisi na Hakimu kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alieleze Bunge hili, anatoa utaratibu gani katika *'role'* yake kama *'regulator'* kuwa na *standards/requirements objective criteria* ambayo ikivunjwa ina-*call for penalty* na *penalty* ya aina gani. Hii ni muhimu ili kuepuka "*double standard*" kitu ambacho tumekiona hivi karibuni ambapo gazeti moja limefungiwa kwa kuandika habari (Mwana Halisi) wakati na habari hiyo hiyo iliandikwa na "Habari Leo" na kukemewa na Bunge, Waziri akaahidi kuchukua hatua, lakini hadi leo kimya. Hali hii ya "*double standard*" haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vya Serikali na vya binafsi, pamoja na kuwa kila kimoja kina malengo yake, lazima kuwe na *'standard'* angalau *'minimum'* ya maadili. Magazeti au vyombo vya Serikali, vinawajibu wa kusimamia maadili ya hali ya juu zaidi na hasa kusimamia ukweli. Waziri anatoa kauli gani pale vyombo vya umma, *"Print and Electronic"* vinapotoa taarifa ya upotoshaji katika demokrasia ya kweli. Uzito wa kosa hili ni kubwa zaidi kuliko kosa hilo linapofanywa na chombo binafsi kwani vyombo vya umma ni vya umma na vina wajibu wa kutoa ukweli na haki kwa walipa kodi wote kwa usawa. Waziri anatoa kauli gani katika matumizi mabaya na ya kipropaganda katika vyombo ya umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Waziri atatoa majibu ya kina katika hoja hizi, ambapo tusipokuwa makini, naogopa tunapeleka Taifa letu pabaya.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hatma ya majengo ya *TBC* kule Mikocheni? Nashauri Serikali itumie Mashirika ya Umma kama *NSSF* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Randama, makisio ya mapato yalikuwa shilingi 313,451,000/=, makusanyo yalivuka kiwango kwa kiasi cha Tshs.583,436,698/=. Kwa vipi makadirio ya mwaka 2009/2010 yakawa chini ya makusanyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe *'support'* katika vyombo vyote vya habari vya umma na vya binafsi, kwani Wizara hii ni sawa na muhimili wa vyombo hivyo vyote bila kujali upande wa vyombo vya umma na Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Waandishi yaboreshwe pamoja na vitendea kazi. Hasa pale wafanyakazi wanapopokea mishahara ya ngazi za chini wakati wameshajiendeleza na vile vile wameshafanya kazi kwa muda wa miaka zaidi ya sita (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itupie macho michezo mingine siyo tu mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nawapongeza kwa hotuba yenu.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuunga mkono hotuba nzuri ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, iliyowasilishwa kwenye Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza ninapenda kuelekeza ufanisi mbovu wa gazeti la Serikali hasa *Daily News* kwa jinsi linavyosuasau kwa muda mrefu sasa. Mimi ni msomaji wa muda mrefu wa gazeti lako, tangu miaka ya sitini na miaka hiyo nilikuwa kijana mdogo. Unaponunua gazeti hilo, kazi ya mwanzo kwa mteja ni kuzipanga kurasa zake na kazi hiyo inahitaji uzoefu na ni kazi ngumu kwa mtu wa kawaida kuifanya. Naomba jambo hili lifanyiwe kazi mara moja ili kero hiyo iweze

kupatiwa ufumbuzi wa kudumu kwani hali hiyo ikiachwa kuendelea, itatubidi baadhi ya sisi wateja tuanze kufikiria kuacha kulinunua. Hali hii siyo nzuri na ni hatari kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba nifahamishwe ni jinsi gani magazeti yetu yanavyofuatilia utaratibu wa kuandika habari zao. Nimefuatilia kwa karibu hasa michango ya Wabunge wetu katika Bunge hili hasa la Mkutano wa Kumi na Sita, utaona kwamba kuna Wabunge wengine wanapata *'coverage'* kubwa na wengine hata maswali au hotuba zao hazitoki kwenye magazeti yenu. Wakati mwingine hata swali la msingi haliandikwi, badala yake wanaaandika jina, picha kubwa ya Waziri au Mbunge anayeuliza swali la nyongeza, kama kuna utaratibu wa siri wa kuwanadi au kutowaanadi wanasiasa wetu, basi ninaomba swali hili likawekwe bayana ili utaratibu ueleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu klabu yetu ya Miembeni Sports Club na kocha wetu Ali Bushiri, naomba muelewe kwamba klabu hiyo iko kwenye Jimbo langu na kwa kweli yaliyotokea hivi karibuni kwenye mashindano ya *CECAFA*, inanisikitisha sana. Kwa heshimiwa na taadhima, naomba Wizara itumie busara na hekima ya juu ili kama pana uwezekano wa kuiomba msamaha klabu hiyo kwani kitendo cha kuifungia klaba hiyo pamoja na Kocha Ali Bushiri, ni hasara kubwa kwa Jimbo letu la Kikwajuni na Taifa kwa ujumla. Ahsante.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu maduka ya vifaa vya michezo. Karibu maduka yote hapa nchini ya vifaa vya michezo humilikiwa na watu binafsi. Isitoshe maduka mengi na makubwa yapo Dar es Salaam. Hali hiyo imesababisha kuwepo na bei kubwa kwa vifaa hivyo. Kwa nini Serikali isianzishe maduka yake mikoani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu ubora wa vifaa vya michezo. Vifaa vingi vya michezo vinavyoingizwa nchini ni *second-hand materials*. Kwa mfano, baadhi ya vifaa kama vile mipira kwa mchezo wa mpira wa miguu huweza kupasuka baada ya kuchezewa mara moja tu. Ingekuwa vema *TBS* ikahakiki vifaa vyote vya michezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu ukosefu wa viwanja vya michezo Wilayani. Wilaya nyingi hazina viwanja vya michezo. Serikali ingekuwa na mipango ya ujenzi wa viwanja vya mchezo vyenye viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu utitili wa magezeti. Miaka ya hivi karibuni kumezuka magazeti mengi ambayo yanakiuka maadili na utamaduni wetu wa Kitanzania. Hivi hakuna chombo chenye jukumu la uhakiki wa magazeti hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni kwamba, wakati wa ukoloni kulikuwepo na msukumo mkubwa wa kuendeleza utamaduni wetu. Karibu kila mkoa ulikuwa na vikundi maalum vya utamaduni na michezo. Hali hiyo imekuwa ikifutika na kupotea. Hivi sasa utamaduni ulioibuka ni *Bongo Flavour* na maonyesho ya urembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kwamba, wakati wa ukoloni kulikuwepo na utaratibu wa shule za msingi kushindanisha timu zao za michezo baina ya shule na shule. Mbona utaratibu huo haupo tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara bila kumsahau Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na pia nawatakia mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na sekta ya habari. Nawapongeza kwa kutoa habari, kuelimisha na kuhabarisha. Wanafanya kazi nzuri kwa jamii, kwa viwango vya hali ya juu, wanaibua matatizo ambayo yapo kwenye jamii, makundi mengi yametetewa kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) kwa kazi nzuri na yenye viwango vya hali ya juu. Nampongeza sana Mkurugenzi wa *TBC* Ndugu D.Tido Mhando kwa kazi nzuri, kwa kweli ameleta mabadiliko makubwa kwenye shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuiongezea *TBC* ruzuku ili waweze kurusha matangazo yake kwa Watanzania wengi hasa waishio vijijini ili nao wapate habari za uhakika, pia kuboresha mitambo ili kuboresha usikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha itoe umuhimu wa kuidhinisha mkopo ili kukarabati majengo ya *TBC* yaliyopo Mikocheni. Kwa kweli inasikitisha sana na ni aibu kwa Taifa letu kutokuthamini majengo ambayo jiwe la msingi liliwekwa na mpendwa wetu Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu tatizo la Kiswahili kutotumika vizuri, licha ya kuwa ni lugha ya Taifa nchini na ni mojawapo ya lugha rasmi inayotumika katika Umoja wa Nchi za Afrika. Hata humu ndani ya Bunge kuna baadhi ya Wabunge hawatumii vizuri lugha ya Kiswahili, wanatumia lugha ya Kiingereza zaidi, inashangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kupata nafasi hii. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya na pia kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii, hivyo naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania imeanza vizuri kwa kulipa umuhimu suala la michezo kwa kuwa na kiwanja chenye hadhi, Uwanja wa Taifa. Tunampongeza mwanzilishi wa ujenzi wa uwanja huo Rais Mstaafu, Mheshimiwa

Benjamini Mkapa na bila kumweka kando Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete ambaye michezo kwake ni damu damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo juhudi zinatakiwa ziendelezwe hasa kwa kuendelea kujenga viwanja vyenye hadhi vingi. Mfano, niliwahi kuahidiwa kuwa baada ya ujenzi wa Uwanja wa Taifa kukamilika uwanja wa Mwanza CCM Kirumba ungejengwa, je, suala hilo likoje? Naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa Nyamagana ni uwanja unaozalisha wachezaji, hivyo ukiondoa uwanja wa CCM Kirumba ni Nyamagana, tunaomba Serikali iuboreshe uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya *TFF* kulikuwa na vitu viwili *FAT* ambayo ilikuwa Tanzania Bara na *ZFA* ilikuwa Zanzibar. Baada ya chombo hiki *TFF* upande wa Tanzania Bara kumeanzishwa Kanda ambazo zipo saba, kwa nini upande wa Zanzibar usiwe ni kanda na kufikisha kanda nane? Hii itafanya Muungano wetu uwe safi na utaratibu uwe kama Rais wa *TFF* akitoka Bara, basi Makamu atoke Zanzibar, hivyo hivyo kama atatoka Zanzibar basi Makamu atoke Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa michezo mashuleni, ni muhimu kuimarisha toka shule za misingi si sekondari tu. Hata hivyo, baada ya kuwapata vijana wenye vipaji wawekwe kambini ili kuunda timu itakayokuwa ndiyo kiongozi na jambo hili liwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usajili wa vikundi vya sanaa ni tatizo hasa kutokana na kucheleweshwa kwa kusajiliwa hivyo vikundi, hufika hatua ya kukata tamaa. Ushauri ni kwamba, ni vema pakawa na msajili katika kanda kuliko kila kitu kuwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la viwanja vya kuchezea michezo mbalimbali hasa kutokana na matatizo ya ardhi, ni jukumu la Serikali kutoa maelekezo na kuyafuatilia kwa karibu au utaratibu maalum wa kisera ulazimishe kila kijiji kiwe na viwanja. Vijiji visitegemee viwanja vya shule za misingi na sekondari, sehemu kubwa kwa sasa vijiji vinategemea viwanja vya shule. Hata hivyo, ubadilishaji wa viwanja kuwa *Supermarket* linaendelea mfano wa wazi ni Uwanja wa Nyamagana, Mwanza isingekuwa Wizara yako kuwa upande wa wanamichezo uwanja huo usingekuwepo, ndiyo maana tunamwomba Mheshimiwa Waziri aweke nguvu zake ili tuuboreshe uwanja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za wanahabari unazifahamu Serikali isikilize kwa makini matakwa yatakayowekwa katika Sheria, wadau wapewe nafasi kubwa wasibaniwe. Habari ni jambo muhimu, maslahi yao yaboreshwe na pia wapewe habari hasa katika ofisi za Serikali bila vitisho ili umma ufahamu kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWAJUMA HASAN KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kufika hapa Bungeni bila ya kukamatwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika na Naibu wake, pamoja na Wenyeviti wake wote kwa umahiri katika kutuongoza na kutuvumilia pale ambapo tunakosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa hotuba yao ilojaa maendeleo katika nchi yetu. Nasema Hongereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia nianze kwa vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni muhimu sana, kwani mara nyingi vyombo hivi hutoa taaluma katika jamii, pamoja na kukosoa pale palipo na makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malumbano wakati mwingine katika vyombo vya habari. Jambo ambalo huonekana kuna udhaifu katika taaluma ya habari. Ni vema Wizara iwe msimamizi pale inapotokea suala kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhuru wa habari, naipongeza Wizara kwa kutoa uhuru wa habari almuradi vyombo hivi havivunji sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya vyombo vya habari ni kutoa taaluma kwa umma, vyombo vya habari vinaweza kuchochea mambo, mara nyingine inawezekana vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa jitihada zake katika kusimamia vyombo vyetu vya habari na mpaka leo nchi yetu iko salama. Hongera Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni na maadili katika vyombo vya habari. Nchi yetu kupitia vyombo vya habari tumefanya makosa makubwa juu ya vyombo vyetu yaliyopelekea kufeli katika kutoa mchango wa kukuza maadili yetu. Vyombo hivi vina baadhi ya vipindi kama *TV* vinatoa vipindi kinyume na maadili yetu. Vipindi kama hivi vinapaswa vitengewe wakati maalum hasa usiku mkubwa ambapo watoto wetu watakuwa wameshalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wasanii. Bado wasanii wetu hawajapewa kipaumbele. Ni vema Wizara iwaandalie mikakati mahsusi ya kuthaminiwa kwa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo. Ni ukweli usiofichika kuwa nchi yetu imepiga hatua ya maendeleo katika michezo ila bado dosari kubwa ipo. Tukumbuke maendeleo ya michezo kuanzia utotoni. Mtoto maisha yake yako shuleni. Kuna

ongezeko la shule ila viwanja vya michezo katika shule hizo hamna.  Naiomba Wizara inieleze imejiandaa kiasi gani kuzipatia shule zetu viwanja vya michezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. OMAR ALI MZEE**:  Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kuipongeza Shirika la Utangazaji (*TBC*) kwa kazi nzuri linayoifanya kwa kutoa elimu, kwa wananchi pamoja na habari za leo leo, hivyo kuwafikia wananchi wengi hasa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika hili limekuwa mkombozi kwa mwananchi kwani linafanya kazi kwa ufanisi na mpangilio ulio bora na hata kumfanya msikilizaji na anayetazama vipindi vyake aburudike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Taifa umezinduliwa, uwanja huu ni wa kisasa na wa kileo hivyo, lazima utunzwe na ulindwe ili ubaki kuwa ni uwanja ulio bora ili uwe chachu ya maendeleo na uweze hata kutumika katika michuano ya Kombe la Dunia na kuliingizia Taifa letu mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu lazima ufanyiwe ukarabati na matengenezo mapema pale tu dosari au uharibifu unapotokea ili kulinda hadhi yake na tuachane na ile tabia ya kutofanya marekebisho mapema pale ambapo dosari imetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni afya na furaha hivyo ni lazima tuwe na timu bora ambazo zimeandaliwa mapema na kupatiwa vifaa na makocha walio bora na kuiondoa nchi yetu kuwa ni nchi ya ushiriki tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu yetu ya Taifa imeendelea kufanya vizuri kutokana na maandalizi yaliyo bora, hivyo basi ushiriki wa timu hii kama ya Taifa uonekane kwa pande zote kwani kila upande una haki na wachezaji wazuri wako kila upande.  Kwa hiyo, tiliangalie hili ili tuwe na timu imara na iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mila na desturi za Mtanzania zinalindwa kutokana na maslahi ya nchi hii, lakini kumekuwa na tatizo la mila hizo kupotoshwa hivyo ni lazima maadili yalindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni lini sasa Tanzania, Zanzibar itakuwa mwanachama wa *FIFA* ili kuondoa matatizo baina ya vyama viwili *TFF* na *ZFA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa wazima na salama.  Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Michezo kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa ushirikiano wake na uchangamfu wake kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kuwa nimewahi mara nyingi kuulizia juu ya viwanja vya michezo kama vile Ali Hassani Mwinyi, Tabora; Julius Kambarage Nyerere, Shinyanga; Jamhuri, Dodoma na vingine kuwa vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi na nilielezwa kuwa viwanja hivi vinamilikiwa kisheria. Sasa nataka kujua kuwa ni sheria namba ngapi na ya mwaka gani? Mheshimiwa Waziri nakuomba hii sheria uitaje ili nisije nikasimama kwenye vifungu jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kuhusu Kiwanja cha Gombani, Pemba kuwekewa nyasi na *FIFA*, je suala hili limefikia wapi?

**MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na wenzangu kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri sana inayogusa kila hitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natoa pongezi kwa juhudi na zoezi la kuorodhesha simu za mkononi kwa usalama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pongezi kwa jitihada ya ku-*support* mpira wa miguu na matokeo mazuri tunayona. Hongera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, pongezi kwa juhudi nzuri ya kuingia *digital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya wanawake isipuuzwe *netball* na *football* ya wanawake (wapewe *support* kubwa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ianze kupewa kipaumbele tangu madarasa ya chini, (shule ya msingi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya michezo vipatikane na vitumike kwa watoto wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu magazeti. Waandishi wa magazeti wawe na Uzalendo. Vyombo vya habari viongee pia na mazuri ya Tanzania na sio kutangaza mabaya tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Malya kiimarishwe ili kitoe wana habari bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makocha wa *Athletics* mngechukua na Kenya ambao wana historia nzuri ya kufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafutieni dawa ya waandishi *Blackmailers* tumechoka kuonewa.

**MHE. MOHAMEDI ALI SAIDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vipindi vinavyooneshwa kwenye *TV* zetu haviridhishi kwani vinapotosha mila na tamaduni zetu. Kwa mfano, watu wanaonekana wakicheza huku vitovu vyao vikiwa uchi na hasa wanawake, huo ni mfano mmoja tu lakini iko mifano mingi. Kwa hivyo, naiomba Bodi ya Filamu hili ilishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni jambo muhimu sana katika sehemu yoyote duniani. Hivyo basi, ni lazima kila mtu aweze kupata habari kwa njia mbalimbali kama Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano inavyosema. Lakini la kusikitisha ni kuwa, huu ni mwaka wa 48 toka uhuru wa mwaka 1961, lakini bado kuna baadhi ya sehemu katika Tanzania hii, hawajaweza kupata habari kwa njia yoyote. Hili ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye vyovyote awezavyo, aboreshe habari ili watu wote Tanzania waweze kupata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni muhimu sana katika Taifa letu kwani michezo inaongeza ukakamavu, inajenga mwili, inajenga mahusiano mazuri kati ya mtu na mtu, jamii na jamii, Taifa na Taifa na kadhalika. Lakini mchezo pekee unaopewa kipaumbele ni mpira wa miguu wakati kuna michezo kama riadha, mpira wa vikapu, magongo, mchezo wa bao, mchezo wa ng'ombe na kadhalika. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, michezo yote ipewe kipaumbele. Kwani tunao watu wengi wenye vipaji katika michezo hii wanaoweza kuleta heshima katika Taifa letu kama walivyotuletea heshima akina Filbert Bayi, Suleiman Nyambui na kadhalika.

**MHE. GOSBERT B. BLADES**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa hotuba nzuri waliyoiwasilisha leo hii. Pia nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za kipekee zimwendee Mheshimiwa Joel Bendera kwa kutupa, kutuongoza na kujenga afya zetu sisi Wabunge kutokana na mazoezi ya hali ya juu anayotupatia katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Kwa niaba ya Wabunge wenzangu namwomba aendelee na moyo huo huo na Mwenyezi Mungu ampe afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara kwa kuboresha mchezo wa mpira wa miguu hasa timu yetu ya Taifa, sasa nchi yetu siyo kichwa cha mwendawazimu bali wembe mkali. Hongera sana na wasikubali kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mavazi ya warembo, maarufu kama vichupi, haya hayafai hata kidogo na hayaendani na utamaduni wa Mwafrika hasa Tanzania. Nashauri tabia hii ya kuvaa vichupi ife mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magazeti. Hivi karibuni baadhi ya magazeti yamekiuka taratibu na kanuni za habari kwa kuandika habari zinazoweza kuhatarisha amani kwa kuendekeza malumbano yasiyokuwa na tija. Nashauri magazeti hayo yachukuliwe hatua za kinidhamu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo mashuleni. Michezo mashuleni imedorora sana. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ipeleke vifaa vya kutosha vya michezo kama ilivyokuwa zamani. Pia Serikali ianzishe shule za michezo za kisasa na za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni, Wilaya ya Karagwe inayo makumbusho ya Mtemi Rumanyika wa Karagwe, huko Kata ya Bweranyange, Wilaya ya Karagwe. Baadhi ya vifaa vya kale vya Mtemi Rumanyika vilichukuliwa na Wajerumani. Tunaomba Serikali ifuatilie na ivirudishe. Pia Serikali ijenge makumbusho ya Mtemi Rumanyika kwa ajili ya vizavi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya habari. Je ni lini mchakato wa kuandaa Muswada wa habari utakamilika na kuletwa hapa Bungeni ili tuupitishe na iwe sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Redio, *TBC*. *TBC* haisikiki vizuri Wilayani Karagwe. Tunaomba Serikali iliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa utendaji wao uliotukuka kwenye Wizara hii. Kwa maana hiyo, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwenye Wizara hii utagusa suala la michezo hasa Mpira wa Miguu. Kwa kuwa natokea Zanzibar, sipendezwi na hali ya malumbano yanayoendelea baina ya *TFF* na *ZFA*. Hali hii inayoendelea ni dalili ya wazi kwamba lipo tatizo ingawa sitokinyooshea kidole chombo chochote kati ya hivi viwili ingawa vinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina maswali kwa Wizara hii kuhusiana na kadhia hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imechukua hatua zipi katika utatuzi wa mgogoro huu? Kama hatua zipo zilizochukuliwa na Wizara, zimefikia wapi na Watanzania pande zote za Jamhuri wategemee nini? Kumekuwa na juhudi za chombo

kimoja wapo (*ZFA*) kuwa na uwakilishi wake katika chombo kikuu duniani kinachosimamia masuala ya mpira wa miguu *FIFA*. Je, Wizara hii haioni kwamba hiyo ni njia mojawapo katika utatuzi wa mgogoro huo? Kama Wizara hii inaunga mkono hoja ya ZFA kujiunga na FIFA, imeisaidiaje SMZ katika kufikia azma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara inahisi *ZFA* isijiunge na *FIFA* na ibakie *TFF* pekee, Wizara ina wasiwasi gani juu ya hili? Kama suala hapa ni Muungano, mbona Uingereza inawakilishwa *FIFA* mara nne kupitia England, Scotland, Wales na Northern Ireland? Kama hilo liliwezekana Wizara hii haioni kwamba itakuwa ni faida ya Watanzania na si mtu mmoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kukamata mshahara wa Waziri kwenye mafungu, lakini naomba Wizara inisaidie kujibu maswali yangu ili Watanzania wote wajue kinachoendelea na msimamo wa Wizara hii kwenye kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, utendaji wao maeneo mengine umetukuka na wala sina haja ya kuondoa madoa kwa sababu hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo mnatakiwa muisimamie vizuri ni sehemu ya uandishi wa habari na sheria inayotaka kuletwa inayohusiana nayo. Kwa ujumla mko imara eneo hili na naomba mwendelee kuwa imara. Hapa nakupongezeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu aubariki utendaji wao, Mungu atubariki Watanzania, Mungu atubariki Waafrika.

**MHE. GRACE S. KIWELU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa maoni na michango katika Wizara hii. Pia nichukue nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wake wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo leo imesomwa katika Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa masikitiko yangu kwa kile nilichokiona wakati wa kutambulisha wageni na kuona katika orodha hiyo hakuna jina la Mwenyekiti wa Chama cha *Netball*, Anna Bay, hata kwenye kundi la wageni la Wizara hiyo. Sina hakika kama viongozi wa vyama vingine vya michezo wanapewa taarifa au kushirikishwa na kutoa maoni yao katika bajeti ya Wizara hii ambayo ndiyo yenye kusimamia vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti ushirikishwaji ni jambo la muhimu sana katika jambo lolote lile na inasaidia kuondoa malalamiko kwa pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni jambo muhimu sana kwa mwananchi na Taifa kwa ujumla, ila inatakiwa taarifa inayotolewa iwe ya kweli, iliyofanyiwa utafiti wa

kutosha ndiyo inayoweza kuwa habari ya kweli. Siku za hivi karibuni yamezuka magazeti mengi yanayoandika taarifa za uongo kupitia kwa waandishi wachache ambao wamesahau maadili yao ya uandishi wa habari, wanajali maslahi yao na ya hao wanaowatuma, hii ni hatari sana kama hatua kali hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana katika gazeti la Habari Leo kuna makala iliyoandikwa yenye Kichwa cha Habari kinachosema Chadema kuna makundi mawili, moja la Zitto, la pili ni la Freeman Mbowe (Mwenyekiti wa Taifa). Kilichofuata baada ya kichwa hicho cha habari ni majungu na umbea, hakuna jambo la kweli. Mwandishi huyo aliamua kujifungia ndani na kuandika makala hiyo kwa maslahi yake binafsi na kwa yule anayemtumia kuandika mambo ambayo hayamsaidii kabisa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ikiachwa hivi italifanya Taifa letu kuwa Taifa la majungu na kusahau mambo muhimu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka taarifa au habari ambazo zitalisaidia Taifa letu kwenda mbele na sio kurudi nyuma. Tunaomba sana waandishi kama hawa wasiachwe huru kiasi hicho au gazeti lisikubali kuandika habari hizo ambazo hazijafanyiwa utafiti, zinapotosha ukweli halisi (hasa kwenye magazeti ya Serikali wawe makini sana inaharibu sifa za gazeti).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo naomba nimpongeze Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza michezo katika nchi yetu wakishirikiana na Rais wetu pamoja na viongozi wote wa michezo.

**MHE. MARGARET SITTA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na maadili mema katika Taifa letu ni muhimu maadili mema yaanzie kwenye familia. Tuimarishe familia zetu, tuongee na watoto na vijana wetu kuhusu maadili mema. Familia zikiimarika kimaadili na Taifa litakuwa na maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa kazi nzuri.

**MHE. FATMA OTHMANI ALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vazi la Taifa bado Tanzania hatujawa na vazi la Taifa kwani kama kungekuwa na vazi hilo isingekuwa la hapa kwenye Bunge japo kanuni inasema tuvae nguo za heshima lakini kama kungekuwa na vazi rasmi la Taifa ingekuwa vizuri zaidi kuonesha mfano kwa Wabunge kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni nyimbo za siku hizi. Kumekuwa hakuna sensa za nyimbo wala sensa za filamu kwani nyimbo nyingi zinazoimbwa ndani ya vyombo vyetu hazina maadili na michezo mingi ya kuigiza kwenye *TV* zetu nayo pia iko kinyume kabisa na maadili yetu kwani nyimbo hazifundishi lolote wala hiyo michezo haifundishi wala kuelimisha kitu. Ningeomba Wizara kama ile Bodi ya Sensa mmeivunja basi bora iundwe tena hasa kusaidia hii jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii lugha ya Kiswahili kila siku inazungumzwa lugha ya Kiswahili itumike hapa Afrika Mashariki kama ya Taifa lakini wanaoifanya hii lugha isiendelee kutumika ni sisi wenyewe Watanzania kwani kila tukikaa kuzungumza lazima tuzungumze Kiingereza, hapa Bungeni wakati wa kujibu maswali lazima japo kidogo waseme Kiingereza. Kwa hali hiyo naomba hii lugha ya Kiswahili ikuzwe kwa kutangazwa kwenye vipeperushi na kusambazwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa hongera watu wa Radio ya *TBC* na *TV* kwa kazi nzuri na jitihada kwa kueneza habari kwa wananchi walio wengi pia nawapongeza waandishi wa gazeti la Habari Leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa uwezo kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Mkuchika na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Bendera kwa kusimamia vema majukumu ya Wizara hii. Pia nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kuwasaidia vema Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sekta ya michezo. Hii ni sehemu muhimu sana ambayo siku hizi imejitahidi na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Wananchi wengi wanapendelea mchezo wa mpira wa miguu kuliko michezo mingine, hali hii imetokana na Wizara kutilia nguvu zaidi katika mchezo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iachane na tabia hiyo na ijikite katika michezo mingine kama riadha, ngumi, *netball*, kuogelea pamoja na michezo mingine ambayo hapo nyuma imetuletea sifa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu Uwanja wa Taifa. Niipongeze Serikali kwa kutujengea Uwanja mpya wa kisasa ambao umetuletea sifa nyingi na tegemeo la wengi ni kuwa nchi yetu sasa itapiga hatua katika michezo na hasa utakapokamilika pindi awamu ya pili ya ujenzi itakapomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu baada ya kupata wana michezo bora pia uwanja huu mategemeo ya wengi utaingiza fedha nyingi za viingilio pamoja na *parking* za magari. Naiomba Serikali kuutunza na kuuenzi uwanja pia kudhibiti vema mapato yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia Serikali kwa nia njema ya kutaka kuondosha kasoro na migogoro iliyoko baina ya *TFF* na *ZFA* ambao umedumu kwa muda mrefu. Suala hili naomba lishughulikiwe kwa kina na haraka ili kukuza michezo kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kutuandalia hotuba nzuri iliyosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na pongezi hizo ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, naunga mkono hatua ya Serikali ya kuruhusu uhuru wa vyombo vya habari. Lakini kwa sasa uhuru huo hasa wa magazeti unatumika vibaya na vyombo hivyo kwani vinavuka mipaka. Magazeti mengi badala ya kuandika taarifa za kuelimisha jamii kwa yale mazuri yaliyofanywa na Serikali, wao wanaripoti mapungufu tu na mengine ya upotoshaji. Baya zaidi kupendelea zaidi kuripoti taarifa za mtu na mtu binafsi na wakati mwingine bila hata ya kumhoji mhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya magazeti wanapoandika hoja zinazotolewa na Bunge, badala ya kuandika Mbunge fulani acharuka, wao huandika Wabunge wacharuka. Taarifa kama hizi zinapotosha jamii, ni vema wakamsema mtu badala ya kusema Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC*, naunga mkono maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu *TBC* kwamba iongezewe fedha na Serikali, pia itoe udhamini ili jengo lililokwama muda mrefu liweze kukamilika. Hivi sasa *TBC* inafanya kazi katika mazingira magumu japokuwa kazi yake ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maafisa Utamaduni. Naishauri Wizara iwaangalie kwa huruma Maafisa Utamaduni walioko Wilayani. Hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Hawana mafungu yoyote ya fedha kwa ajili ya kufanyia kazi. Viongozi wa Halmashauri na Serikali Kuu wanawatumia panapokuwa na ugeni wa Kitaifa vinginevyo wapo wapo tu. Ni vema wakiwa na fungu lao la fedha ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kuandaa hotuba nzuri na inayoeleweka kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kupata habari ni haki ya msingi ya binadamu, naishauri sana Serikali kuhakikisha kuwa viziwi nchini wanapata fursa ya kupata habari kwa kuwapatia kundi hili la ulemavu Wakalimani wa lugha ya Alama ambayo ndiyo lugha ya viziwi wanayoielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata malalamiko mengine katika ziara mbalimbali ninazofanya kuhusu suala hili. Kwa vile siku hizi kuna matumizi ya Televisheni basi katika vile vipindi muhimu Wakalimani wa lugha ya alama wangetumika ili watu wenye ulemavu waweze kupata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 wa hotuba Wizara imeelezea kuhusu kugharamia ushiriki wa wanamichezo wa Olimpiki wakiwemo wenye ulemavu wa viungo huko Beijing, China Septemba, 2009. Kwa hili naipongeza Wizara kwa kugharamia michezo ya wenye ulemavu. Nashauri kuwe na mwendelezo wa kugharamia ushiriki wa michezo mingine ya watu wenye ulemavu nchini kwa vile kundi hili wakiandaliwa vizuri huwa wanashinda vizuri na kuleta medali nchini kwa sifa ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na mwendelezo wa kuendesha matamasha ya sanaa na utamaduni wa Mtanzania na taasisi ya sanaa na utamaduni Bagamoyo (TASUBA). Hata hivyo nashauri, ingefaa taasisi ione uwezekano wa kushirikisha vikundi vya sanaa vya watu wenye ulemavu nchini kwa mfano *Seven Blind Beats* – bendi ya wasioona saba, *Albino Revolution Group* na kadhalika. Taasisi ihamasishe suala hili ikishirikiana na Maafisa Michezo wa Wilaya ambao sina uhakika kama wapo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kwa muda sasa kumekuwa na malalamiko kuwa taaluma ya uandishi wa habari inatolewa na vyuo visivyo mahiri hivyo kuzalisha waandishi wa habari uchwara, nimefurahi sana kuona kuwa kutaanzishwa Mfuko mahsusi wa kuendeleza taaluma ya habari. Naamini kuwa kwa elimu hiyo matatizo madogo madogo yatatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kuna jitihada ya Serikali kusomesha walimu wa michezo ya aina mbalimbali natoa rai kuwa zifanyike jitihada mahsusi ili kutoa mafunzo kwa walimu wa michezo ya watu wenye ulemavu ili waweze kuwasaidia kundi la wana michezo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. MAGADALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake kwa kazi nzuri ya kuendeleza sekta hii ya habari na michezo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuingia kwenye ushindani wa biashara kwa kutumia vyombo vyake vya habari ni kukandamiza vyombo vingine vya habari. Wote tunatambua mchango wa vyombo vya habari vya binafsi katika kuelimisha jamii ya Watanzania. Kitendo cha Serikali kujipendelea na kuruhusu *TBC,* peke yake kutangaza mipira ya nje ya Kimataifa na kunyima fursa hiyo kwa *Television* nyingine ni umwinyi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutumia fedha za walipa kodi wanaingia mikataba ya kulipa kwa bei ghali matangazo kutoka nje ili mradi kuleta ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetamka hapa mara kwa mara kwamba haitajiingiza kwenye biashara na badala yake itaweka mazingira mazuri ya watu binafsi na vyombo mbalimbali kufanya biashara, leo kwa nini imeingia kwenye biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ambazo ni muhimu kama kilimo, mifugo, viwanda na biashara wamejitoa iweje kwenye michezo au habari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mamlaka anayopewa Waziri ya kuzuia hata kufuta kabisa gazeti lolote ambalo litaandika habari za upotoshaji. Fursa hii aliyopewa Waziri inanyima uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Waziri atakapoona habari haijamfurahisha anaweza kufungia gazeti lolote. Gazeti lolote linatakiwa kuandika habari yoyote iwe ya kufurahisha au ya kuchukiza ili mradi anaifanyia utafiti wa kina. Sasa kama fulani yeye hakufurahishwa afuate taratibu zilizopo kuchukua hatua kwa kufuata sheria na siyo kutumia fungu lake kuona vyombo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa ya wanenguaji wanawake kuvaa nusu uchi sio heshima wala utamaduni wetu. Ni aibu kwa Taifa letu na linatudhalilisha sisi akinamama na kufundisha watoto vibaya. Nani aliyesema kuonyesha sehemu za mwili tumbo, maziwa, kiuno na kadhalika ni sifa? Mbona wanenguaji wa kiume wanavaa vizuri *fully* hata *suit* lakini wanapendeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea kuruhusu wasichana hawa kucheza nusu uchi kwenye majukwaa na kambi za muziki ni hatari kwa Taifa la leo na kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wanaelimisha sana jamii lakini wakivuka mipaka wanapotosha jamii vile vile. Juzi wasanii wa *Ze comedy*, waliigiza kwamba mtoto anahadithia rafiki zake kuwa mama yake usiku alikuwa analia kwa sauti Fulani, watoto wakaamka wakijua mama amepigwa na baba yake kidogo wakasikia baba ameanza kulia na kutoa sauti fulani. Hili kwa watoto linafundisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu hapa Tanzania wamepanda chati na hata kuwa wachezaji, wanamuziki wazuri, waigizaji wazuri kwa kuwezeshwa na kupewa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Bongo *Star Search* ni kizuri na kimekuza vipaji vya wasanii wetu. Nimeshtushwa na tabia ya wale waamuzi watatu kuanza kuwadhalilisha wale wanaojitokeza kuwania nafasi hizo, hasa huko mikoani. Waamuzi wale wanatakiwa kuwaelekeza, kama walimu wanatakiwa kuwaelekeza ili wawajenge lakini maneno wanayowambia yanawakatisha tamaa kabisa. Mfano, ehee hivi kweli nani kakwambia kwamba unaweza kucheza muziki? Liangalie kwanza, sura mbaya! Umevaa

Shebby, hili halipendezi. Kama wamejitolea kutafuta vipaji kwa vijana wetu wawaheshimu na wao ni binadam.

**MHE. DR. SAMSON MPANDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuvuta hisia yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, Tarafa ya Kipatimu, kuna vivutio vingi ikiwemo ngoma ya asili, pamoja na mapango makubwa yapatayo ishirini na sita. Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani wa kuhamasisha upigaji picha mapango hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Lindi katika mashindano ya soka tumekuwa kama kichwa cha mwendawazimu cha mchezo huo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua kiwango cha mchezo huo ili nasi tuonekane katika ulimwengu wa kimichezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka huu tutasheherekea Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji Kilwa. Je, Serikali itachukua hatua gani za makusudi ili iweze kuitangazia ulimwengu sherehe hiyo ili Kilwa nayo iweze kutambulika kidunia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MWANTUMU S.B. MAHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napongeza kwa hotuba na malengo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu ni kwamba:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mavazi katika ngoma na shoo mbalimbali bado Wizara inalo jukumu la kutoa mwongozo haiyumkini wanaume wawe na mavazi yanayohifadhi umbile, wanawake wao wako hovyo ati kama hatupendi tusiangalie, jamani mwanamke anadhalilika kweli katika sanaa hizi iwe katika ngoma au dansi. Nadhani sasa tuwasaidie kuelimisha jamii ili kupunguza athari kwa kuporomoka kwa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashairi katika nyimbo za taarab zimevuka mipaka, tuheshimu fani ya ushairi, mafumbo yatumike isiwe ni uwazi wa kupitiliza mfano, “nampa mchezo wa kisasa”, “nampa malavu ya nguvu”, “hazitaki nyeti zako”. Hapa tumefika mahali lazima Baraza la Kiswahili na Sanaa waingilie kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa filamu umeachwa kabisa, mambo ya hovyo yanaonyeshwa bayana, hali hii ni mbaya. Tunaomba filamu zote za aina hiyo sasa ziondolewe sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandishi wa habari, kwanza, magazeti mengi hayafanyi uchunguzi wa kina kwa habari wanazoandika. Hivi hata gazeti la Mzalendo nalo linaandikwa na makanjanja? Kwa nini gazeti kongwe kama hilo nalo linaandika

habari zisizo za ukweli! Inasikitisha sana. Nashauri uchunguzi wa kina ufanyike kabla ya kuandika.

Pili, magazeti yaache kuandika habari za kuchochea, habari zinazoashiria kuvunja amani. Mambo yakiharibika hata wao wataathirika waelimishwe kuacha uchochezi kwa jamii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Tatu, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa uandishi wa habari ni taaluma *(Professional)* na kuna *professional ethics* katika uandishi wa habari; kuna waandishi wa habari ambao hukiuka maadili ya uandishi na kupotosha habari. Je, Serikali imewachukulia hatua waandishi wangapi waliokiuka maadili ya uandishi na hatua gani zilizochukuliwa? Je, ni lini Serikali italeta Muswada hapa Bungeni ili Bunge litunge sheria itakayodhibiti hali hiyo ya ukiukwaji wa maadili ya uandishi wa habari?

Kwa kuwa Mkurugenzi Mkuu - Ndugu Tido Mhando wa *TBC* ameboresha sana vipindi vya *TBC* Taifa na *TBC1* na *TBC FM* na vipindi vya *TBC* Taifa na hata hivyo watumishi wa chombo hiki wanafanya kazi katika mazingira duni, maslahi duni, nyumba za kuishi ni tatizo, vyombo vya usafiri, (wapate vyombo vya usafiri hata kama ni mikopo) upungufu wa watumishi hasa katika kanda ikiwemo Kanda ya Kati Dodoma. Je, Serikali imeweka mikakati gani ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi watumishi wa *TBC*?

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Waandishi wa Habari kila Wilaya ili kuandika habari za maendeleo katika maeneo hayo na pia wapatiwe vitendea kazi kama vile ofisi, magari, computer na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wengi wanapenda Mchezo wa Mpira wa miguu na kwa kuwa mchezo huu umetawaliwa na migogoro mingi ikiwemo migogoro ya kugombea madaraka, matumizi mabaya ya fedha, kung’ang’ania madaraka hata kama muda wao umekwisha kikatiba: Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kutatua migogoro hiyo ili kupunguza/kuondoa hiyo ili kuendeleza michezo hapa nchini?

Je, Serikali ina mipango gani ya kuimarisha michezo mingine kama vile Volleyball, Handball, Riadha, Masumbwi, Netball na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara kwa kuhakikisha Habari, Utamaduni na Michezo zinatekelezwa ipasavyo. Kwa

upande wa habari, napenda kuvipongeza vyombo vya habari vya Taifa na vya binafsi kwa kuweza kutoa habari mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda kuzungumzia kuhusu kile kikundi cha maigizo kinachoonyeshwa na Televisheni ya Taifa *(TBC)* kinachojulikana kama *"Komedi Original"*. Kwa kweli kikundi hiki kinaonyesha vituko mbalimbali kiasi cha kuvutia jamii na wengi wao wakiwa watoto wadogo. Kikundi hiki kimekuwa maarufu sana na kila mtu wakati wa kuonyesha vituko vyao ambavyo ni mambo yanayotendeka kila siku, mengine ni ya kweli yametokea na bado yanaendelea kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya sifa hizo za kikundi hicho, lakini kumejitokeza baadhi ya maigizo au vituko wanavyoonyesha au maneno yale wanayoyatamka kwa kweli kinakishushia hadhi kikundi hiki. Kuna yule anayejiita Masanja, katika vipindi vyao vya hivi karibuni alikuwa akielezea kuhusu matendo mbalimbali yanayofanyika mara tatu akafananisha kama "Paul Young", lakini matamshi hayo yanatamkwa ki matusi. Hiyo haitoshi, onyesho lao la juzi, yule wanayemwita Joti alizungumzia kuhusu alipolala usiku akamsikia mama yake analia na baadaye baba naye akawa analia na yeye alipomwuliza mama yake kuwa kwa nini analia akaambiwa wewe lala tu.

Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu kikundi hiki cha Komedi. Je, hakikiuki maadili? Au je, ni mafunzo gani wanayopata wale wanaoangalia kipindi hiki kwa baadhi ya vituko ambavyo havifai watoto wadogo kuvisikia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni, bado nazidi kuulizia, hivi katika vikundi vile vya bendi za muziki vinavyoonyesha shoo zao, ni sababu zipi zinazopelekea wanaume wanenguaji wanavaa vizuri nguo zao, lakini wanawake wanavaa nusu uchi, kitovu nje, nguo ya ndani kuonekana na unenguaji ambao hauna maana? Je, huu ndio utamaduni wa Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana tunaiga mambo ya wenzetu wa Mashariki ya mbali ambao baadhi ya tamaduni zao hazionyeshi kuwaheshimu wanawake. Sasa hivi kuna matukio mengi ya ubakaji yanayotendeka siku hadi siku, haya ni matunda ya kuporomoka kwa maadili. Je, tunajenga Tanzania gani wakati hata mtoto wa miaka mitatu anaweza kunengua kutokana na kuangalia TV humshinda hata mtu mzima kutokana na mwili wake kuwa laini *(Flexible).* Huoni watoto wengi wenye uwezo wa kunengua hukutwa na balaa la kubakwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni lini Wizara itarekebisha suala hili la unenguaji ambalo ni udhalilishaji wa jinsia au hivi watu hawawezi kuingia kwenye majumba ya muziki iwapo hakuna wanenguaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Wizara kwa kuupa mchezo wa Mpira wa miguu kipaumbele. Lakini naomba Wizara sasa iangalie na michezo ya riadha.

Tunao wanariadha wengi wenye vipaji, lakini vipaji vyao havionekani kwa vile hawana pa kufanya mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanariadha hao ni wakimbiaji, waruka Vihunzi, Waruka juu *(high jump)* waruka chini *(long jump)* kurusha mkuki na hisani *(javeling* na *shotput)* wako wenye vipaji vya michezo hii na tunaomba michezo hii itiliwe mkazo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi kuhusu kuendeleza michezo hii iliyobakia ambayo sio sana kuchezwa. Tunaiomba Wizara iimarishe michezo hiyo iliyobaki ili kupunguza vijana kukaa vijiweni bila shughuli. Michezo huwashughulisha vijana sambamba na kuwapatia ajira vijana hao.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara kwa kuboresha Michezo kwa vijana wetu na kuwapatia ajira. Pamoja na pongezi hizo, ni kwa nini Mkoa wa Kagera Wizara (Serikali) haiweki nguvu ya pamoja na hamasa kama inavyoweka mji au jiji la Dar es Salaam ifanyike hata kwenye Mikoa mingine pamoja na wadhamini, Wizara iwaombe wasambae Mikoani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo mashuleni inajenga miili ya vijana. Ni kwa nini imepungua kasi? Ni tatizo gani lililosababisha Wizara kupunguza kasi katika michezo? Wizara ina mikakati gani kuhusu mavazi kwa wanamichezo pamoja na wanamuziki wanaotia aibu kwa mavazi yao? Je, wanawake kwanini wasivae kama wanaume? Wanawake kuvaa nusu uchi ndio michezo inapendeza au ndio utapendeza? Sisi Watanzania ni watu wenye mavazi yenye heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mikakati gani katika uboreshaji viwanja Mikoani pote? Viwanja havina hadhi kulinganisha na Mkoa: Je, Wizara pamoja na Serikali ina mikakati gani? Wizara ielewe kuwa michezo ni ajira pamoja kipato kwa Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vazi la kanga lilikuwa ni vazi la heshima Tanzania na Zanzibar, lakini sasa limekuwa halina heshima tena, wanalishona matumbo yako nje. Lidhibitiwe kurudisha heshima ya Tanzania na Zanzibar kwenye misiba, kwenye harusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda za video zimekuwa zinatudhalilisha wanawake. Zithibitiwe mara moja! Baadhi ya tamaduni za kiutalii zisimalize tamaduni zetu. Tuzienzi, tusiwe tunasubiri watalii. Wizara ifanye mikakati kutangaza na kupeleka watoto shule kwa malezi ya tamaduni zetu, tuendelee kuenzi tamaduni zetu. Kuna watu wanajitolea kutengeneza vifaa vingi vya utamaduni, wanakosa nyenzo za kuboresha shughuli zao za utamaduni wanaondoka na umaskini. Pamoja na nyimbo za taarabu kwamba hazina maadili kama zamani, wapewe onyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Wazoro atafakari michango yangu ijibiwe kama ilivyo. Nawatakia utendaji mwema na bajeti njema.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri na Naibu pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwapongeza wamiliki wa vyombo vya habari hapa nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwa sikivu hasa pale nilipokuwa naulizia suala la Tabora kupata habari kwa Redio Tanzania na hivi sasa inasikika ingawa baadhi ya maeneo haisikiki vizuri sana. Napongeza kutuwekea *TBC1* ambayo inasaidia sana wananchi kupata habari za nchi yao na dunia. Naipongeza sana *TBC1* kwani inaonekana vizuri sana na Tabora hakuna chombo cha *TV* kinachoonekana bila ya kuwa na *Cab,* naipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kushukuru kwa awamu ya kwanza chombo cha *ITV* baada ya kuwapelekea maombi ili kuweka mtambo wake katika Mkoa wa Tabora kuonyesha wazi kuwa wataleta mitambo hiyo ya *ITV* na *Radio One*. Natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maadili ya michezo au sanaa. Naomba vyombo husika BASATA kuzingatia maadili ya Tanzania kwani hivi sasa wasanii hucheza nusu uchi na hatujasikia kutoa kauli yoyote ile kuhusu hili. Pia kuwepo na mipaka katika nyimbo zao, kwani uhuru zaidi ni mbaya kwani jukwaa la kisiasa likihamia katika sanaa inaweza kujenga hisia kiurahisi sana kwa wananchi kuwa nchi yao ifikapo kipindi cha uchaguzi huomba kura na kushindwa kufanya kazi kwa wananchi na kusikiliza matatizo yao. Haya ni mambo muhimu sana ya kuzingatia kwa nchi yetu, uhariri wa nyimbo hizi ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuipongeza serikali kwa kushirikiana na *TFF* kuifikisha Tanzania katika mabadiliko ya michezo, kwani sasa ina sifa na inajiuza na inatia moyo katika michezo yetu ya soka. Cha maana sasa tusirudi nyuma ili kuongeza sifa nzuri ya michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zanzibar na Tanzania Bara kuvutana kwa michezo kuona mmoja ni mkubwa zaidi, hili liwe bayana kabisa kwa wananchi na pia nawashukuru *TFF* kwa kazi ambayo wameanza kuomba maoni mikoani ndio kuwe na maamuzi. Ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini pamoja na hayo nashauri kuanzishwa vyombo vingi vya habari kwa maana ya Magazeti/Radio na vituo vya *Television*, umewekezwa zaidi na wafanyabiashara na kwa upande mmoja Serikali. Serikali haioni mtindo huo wa wafanyabiashara na Serikali ni namna fulani ya kuhodhi na kuwanyima waandishi uhuru wao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahimiza waandishi kuanzisha vyombo vyao? Tumekuwa nyuma katika michezo Kimataifa na hasa riadha. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa mchango wa kupata kocha. Je, mikakati gani iliyoandaliwa kuhakikisha tunarudisha hadhi yetu ya riadha kimataifa?

Tumepanda kiwango cha soko hadi kuwa kwenye idadi 100. Kwa kuwa timu zetu (kubwa) zimekuwa na tabia ya kuleta na kuajiri wachezaji wageni: Wizara haioni kuwa na timu zetu zenye wageni wengi kutaathiri timu yetu ya Taifa? *TFF* haiwezi kuweka kiwango cha ukomo wa idadi ya wachezaji?

Kwa kuwa Taifa lolote hujitambulisha kwa ngoma, sanaa ambao ndio utamaduni na kwa kuwa Wizara imekuwa haijihusishi moja kwa moja na kuandaa michezo ama mashindano yao sanaa hizo na utamaduni (i.e. ngoma za kiasili kama Uswezi, Bayeye, Bagika na kadhalika): Je, ni lini Wizara itajihusisha kuendeleza michezo hii ya jadi Ngoma/bao/mikuki?

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Napendekeza Wizara itenge fungu la fedha kwa ajili ya kuendeleza mafunzo kazini kwa kada ya Waandishi wa Habari wa vyombo vyote nchini. Mafunzo haya yatasaidia kuboresha utoaji wa habari wenye kina, utafiti, ukweli na ikizingatia miiko na maadili ya fani ya uandishi wa habari.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikisisitiza michezo kurudi mashuleni na pia tunatambua michezo ni afya. Ni dhahiri kwamba bila kuwepo na viwanja vya michezo, nia nzuri hii ya Serikali haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Moshi mjini hatuna kabisa Kiwanja cha Michezo. Kile cha *Memorial* kilichokuwepo, Halmashauri waliamua kukibadilisha matumizi na kukifanya soko la kuuzia mitumba. Sasa hii migongano kwamba Serikali Kuu inahimiza michezo, kwenye Halmashauri wanageuza matumizi ya viwanja: Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kiwanja kile kinarudishwa kwenye matumizi yake ya awali kwa ajili ya michezo? Kwa sasa hivi hata sikukuu za kitaifa kama Saba Saba, siku ya Uhuru Moshi hakuna kabisa uwanja wa kwenda kuisherehekea.

Maeneo ya Wazi, kwa sasa hivi maeneo ya wazi kwa ajili ya michezo mingi yamevamiwa na kujengwa *Bar*, maduka na kadhalika. Watoto walikuwa wakitoka shule wanapata sehemu za kuchezea, lakini sasa hivi sehemu nyingi hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kwamba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Ardhi ili maeneo yote ya wazi yaliyojengwa yarudishwe na yatumike kwa ajili ya michezo.

Shule za Kata, Serikali imerudisha michezo mashuleni. Je, katika shule za Kata kuna maeneo kwa ajili ya michezo? Shule nyingi hazina viwanja. Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuna viwanja katika shule hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tumekuwa na malalamiko ya kwamba maadili yameporomoka, lakini tunasahau wengi utamaduni wetu wa Kitanzania wa adabu na heshima. Siku hizi katika *Television* kuna vipindi ambavyo siyo vizuri kwa malezi ya

watoto wetu na cha kusikitisha, vipindi hivyo vingine vinarushwa na Televisheni ya Taifa. Unakuta kuna kipindi vijana wa kiume wanavaa mavazi ya kike, wanaweka matiti bandia, wanaongea lugha ambazo siyo nzuri. Je, hapa tunatoa elimu gani kwa watoto wa kiume ambao wanakua? Lazima vipindi kama hivi tuangalie vina tija gani kwa Taifa?

Uhuru wa habari, kwa kuwa kupata habari na kutoa habari kwa uhuru ni sheria ya kikatiba, basi Serikali iwaachie uhuru waandishi watoe habari bila uwoga wa kufungiwa magazeti yao kama la Mwanahalisi na pia wawe na uhuru wa kujieleza kama chombo kilichosaidia Taifa kwa kuwataja mafisadi papa bila uwoga. Lakini badala yake baadhi ya viongozi wakawa wanatetea mafisadi badala ya kufanyia kazi tuhuma zile.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Wizara hii, lakini nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migongano kati ya *TFF* na *ZFA* kwa muda mrefu sasa kumekuwa na migongano kati ya Chama cha Mpira wa miguu Zanzibar. Migongano hiyo pia ilijiri hapa Bungeni wakati mbunge mmoja kutoka Zanzibar alipomtuhumu Rais wa *TFF* kwamba haitendei haki Zanzibar kwa kuinyima fursa za kushiriki kwenye mashindano/michezo ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo siyo nzuri kwa maendeleo ya michezo nchini mwetu. Napenda kushauri kwamba sasa ni wakati muafaka kabisa kwa Waziri wenye dhamana ya michezo kutoa ufafanuzi na maelezo ya kina kabisa kuhusu nafasi ya Zanzibar na ushiriki wake katika michezo mbalimbali ndani ya nchi, Afrika na duniani kwa ujumla. Waziri akifanya hivyo, atakuwa pia anaondoa dhana potofu ya kwamba upande mmoja wa Muungano unaonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha michezo ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji, kwanza naipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ametilia umuhimu maendeleo ya michezo nchini. Hali hiyo inathibitishwa na ukweli kwamba baada ya Serikali kuajiri kocha wa mpria wa miguu Maxio Maximo, kutoka Brazili kiwango cha mpira wa miguu kwa timu yetu ya Taifa kimekua kwa kiwango cha kuridhisha sana. Jitihada na juhudi hizo zinapaswa ziendelee kwa ari, nguvu na kasi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo katika ngazi ya Taifa, bado michezo katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji haijapewa umuhimu unaostahili. Kwa ujumla ni kama michezo katika ngazi hizo imekufa. Michezo kama mpira wa miguu inayofanyika katika ngazi hizo ni kwa jitihada za watu binafsi wakiwepo baadhi ya wabunge ambao huendesha *"leage"* za mpira kwenye maeneo yao. Napenda kujua Serikali inajihusisha kwa kiasi gani katika kuinua michezo katika ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo mbalimbali, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, Serikali iliahidi kuendeleza michezo mbalimbali ukiwepo mpira wa mikono *(netball)*, mieleka, bao na kadhalika. Hata hivyo, bado hakuna

jitihada za dhati zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza ahadi hiyo. Naishauri Serikali ijielekeze katika kuhakikisha kwamba ahadi hiyo inatekelezwa.

Ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Capt. George Mkuchika – Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa J. Bendera - Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi waandaaji kwa kuleta hotuba safi ya bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maudhui ya bajeti yao na nina machache ya kuongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Habari hasa vyombo vya Habari Kitaifa *TBC Radio* na *TV* Waziri atueleze ana mipango gani ya kuhakikisha kuwa kunakuwa na usikivu wa vyombo hivi katika Mikoa ya pembezoni kama Mtwara, Rukwa, Kigoma, Kagera na kadhalika? Kulikuwa na taarifa hapo mwanzoni mwa mwaka 1995 kuwa Serikali ilipata vifaa vya *FM* toka Serikali ya China, ilipeleka vifaa hivi katika Mikoa ya pembezoni ikiwemo Mtwara. Je, taarifa hii ni ya kweli? Kama ni kweli, mtambo wa *FM* Mtwara ulipelekwa wapi? Naomba Wizara yako itafiti ili Mtwara ipatiwe mtambo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri akaze uzi katika sheria ya habari anayotaka kuleta Bungeni kwamba wamiliki wa vyombo wadhibitiwe kwa kutokuwa na chombo zaidi ya kimoja. Tumeona jinsi fani baadhi ya wamiliki wanavyoharibu uhuru waliopewa kwa kutumia vyombo vyao kuwachafua wenzao, kuwapaka matope kwa kutumia magazeti mbalimbali wanayomiliki. Utaratibu huu ni hatari, unaweza kuwa chokochoko ya kuharibu umoja wa kitaifa na utulivu tulionao nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utamaduni kitaifa na mmomonyoko wa maadili kutokana na vyombo vya habari hasa luninga, nashauri kuwepo na utaratibu wa mazungumzo ya kitaifa hasa kwa wazazi ili sote tushauriane hatua za kuchukua dhidi ya watoto wetu wanaokosa maadili mema. Tusiache hivi hivi bila kuchukua hatua. Vyombo vyetu navyo ndivyo vinavyoweza kutusaidia sana katika kukabili hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara na kuunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari na Utamaduni na Michezo pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuimarisha na kudumisha utamaduni wetu na michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo, kwa nini vipindi vyetu vya *TBC (TV)* na *TBC (radio)* ratiba zake hazitolewi kwenye magazeti yetu ya Uhuru, Habari leo na *Daily News* kama vile tunavyoziona ratiba za *ITV, Radio One* na kadhalika, katika magazeti ya Nipashe na Alasiri. Kutolewa kwa vipindi vya *TBC* kwenye magazeti kutatusaidia kufuatilia vipindi hivyo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu hasa tukizingatia kuwa vyombo vya habari siku za karibuni vimeonekana kama mhimili wa nne wa dola. Lakini pia Wizara hii ndio inayopaswa kulinda utamaduni wa Taifa na kuuenzi. Kinachosikitisha, bado nchi yetu haina utamaduni tunaoweza kusema huu ndio utamaduni wetu hasa tukizingatia kutokuwepo kwa vazi la Taifa. Jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu, lakini bado tunaambiwa mchakato unaendelea. Hadi lini?

Ni lazima Watanzania tuwe na vazi kama walivyo wenzetu wa nchi za Afrika Magharibi au kama imeshindikana, basi itamkwe wazi. Utamaduni unaendana sana na maadili. Ni kweli kwamba familia ndio chimbuko la maadili. Lakini pia Serikali Kuu ina jukumu la kuwajengea mazingira ya kimaadili shuleni ili waendeleze yale waliyokuwa nayo. Lakini kibaya ni kwamba hakuna somo la maadili, hivyo vijana wanakosa msukumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo, hufurahisha, hujenga urafiki lakini pia hujenga afya za wanamichezo. Ni wazi kuwa uwanja wa mpira wa Taifa umesaidia sana katika kujengea Taifa letu sifa. Lakini pia ni wazi makocha walioletwa wamesaidia kukuza vipaji vya wanamichezo wetu. Lakini kibaya ni kuwa upande wa *netball* bado ni tatizo. Fani hii ya michezo ni ajira na wote tumeona ni jinsi gani wanamichezo walivyoweza kununuliwa kwa bei kubwa kama Ronald Christian, Kaka na wengine wengi. Ni wazi kwamba hata Watanzania wanaweza. Hivi karibuni kijana wetu Tabeet Hasheem mtoto wa Sinza ameweza kuingia katika ligi kuu ya kikapu kule Marekani – *NBA*. Hii ina maana Watanzania tunaweza. Bado Wizara inahitaji kuwezeshwa zaidi ili kuweza kuwajengea uwezo vijana wetu katika fani hii kama riadha na michezo mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari ni mhimili wa nne wa dola na hivyo vinapaswa kuboreshwa ili kweli vitoe taarifa sahihi na sio za upotoshaji. Uwepo wa wingi wa vyombo vya habari na magazeti mengi haina maana ya kuwa na uhuru wa kutosha, bado vyombo hivi vimekuwa vikilalamikiwa kutokana na uhuru wa kutosha.

Mwisho, tunaomba wanahabari wasomeshwe ili waweze kutoa taarifa sahihi na wawe wenye maadili.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kwa kuanza na:-

Utaratibu wa Shirika la Utangazaji *(TBC)* wa kufunga mitambo ya *FM*. Imepangwa na Shirika la *TBC* kwa fedha za maendeleo 2009/2010 kukamilisha ufungaji wa mitambo ya Redio za *FM* kwenye Mikoa kumi ikiwemo Zanzibar. Kwa upande wa Zanzibar tungependa kujua mtambo huo utafungwa Unguja au Pemba. Swali hili linaibuka kutokana na ukweli kwamba Pemba kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekosa njia muhimu za kupata taarifa mbalimbali zinazohusu nchi yao kama vile kupitia magazeti au redio za uhakika. Hivyo, kama utaratibu huu wa kufunga

mitambo ya *FM* pia utaelekezwa Kisiwa cha Pemba, utawasaidia sana Watanzania waishio huko Pemba kupata taarifa zaidi zinazohusu nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili inahusu ukamilishwaji wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Televisheni ya Taifa iliyopo Mikocheni. Jambo hili limepigiwa kelele sana na wadau mbalimbali na wapenda maendeleo ikiwemo Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Vikao mbalimbali vya Wadau wakiwemo Wizara ya Habari, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Fedha, Shirika la *NSSF* na kadhalika vilishapitisha utaratibu wa ukamilishwaji wa ujenzi huo, lakini imebainika kuwa Wizara ya Fedha inajaribu kulipiga chenga jukumu walilokwishalikubali. Kwa kuzingatia gharama walizokwishapata *TBC* kulipiga chenga jambo hili, hakuna nia njema kwa shirika na kwa maslahi ya Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vikiwemo Televisheni, Magazeti, Redio na kadhalika vina jukumu kubwa la kulinda utamaduni wa Taifa. Imedhihirika kupitia vyombo vyetu vya habari kuwepo na mambo ambayo hayaendani na utaratibu wa kulinda utamaduni na utu wetu. Haipendezi, haisaidii, wala kujenga Taifa jema kuona vyombo vinaruhusu kuonyesha mavazi yanayokashifu ambayo hayaendani na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii kubwa ya Watanzania ingependa kupata taarifa sahihi juu ya umiliki wa viwanja mbalimbali vya michezo kama vile vya Jamhuri - Dodoma, Kirumba - Mwanza, Ali Hassan Mwinyi - Tabora, kuwa chini ya umiliki wa Chama cha Mapinduzi. Hii ni kutokana na hoja kwamba viwanja hivyo vimejengwa kwa nguvu ya wananchi wote kabla ya mfumo wa Vyama vingi na hivyo ingestahili raslimali hiyo kuwa chini ya umiliki wa Serikali ili kufaidisha wananchi wote kinyume na ilivyo sasa. Tendo la chama kilichopata usajili sawa na vyama vingine kuhodhi mali iliyochumwa na umma wote halijakaa sawa, hivyo linahitaji kutolewa ufafanuzi mzuri leo hii.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kuendesha kazi vizuri ambazo mara nyingi kuna vitengo vilivyo chini ya Wizara wanajaribu kurudishia vyama azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu waandishi wa habari, kumekuwa na tabia mbaya hivi sasa kwa watangazaji ambao ni miongoni mwa waandishi wa habari wachache wanaojaribu kupotosha lugha na matumizi mazuri ya Kiswahili Sanifu na badala yake Watangazaji hao hutumia lugha za kihuni au za Mitaani ambazo baadhi yake hazifai kabisa kusikika katika jamii kwa mfano watangazaji wawili wanapokuwa *studio* wakiendesha kipindi kimoja anathubutu kumwambia mweziwe “shika adabu yako” sio maneno yanayokubalika.

Wizara hivi sasa umeshafika wakati wa kutoa maelekezo na kuviomba vyombo husika na viongozi wa vyombo hivyo kuhakikisha wanaajiri waandishi wenye ujuzi na wenye kufahamu vizuri kazi zao na sio “makanjanja”. Uandishi wa habari utatimia kama

mwandishi wa habari atakuwa na uelewa wa yale anayoandika na sio waandishi wa staili ya Waziri kasema, Katibu kasema au mambo kama hayo. Habari zinatakiwa waandishi wenye uwezo wa kuchambua mambo kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo, napenda kuipongeza sana Serikali pamoja na Wizara kwa hatua nzuri iliyofikiwa Tanzania ya kuwaleta walimu wa soka na wale wa riadha na ngumi kutoka *CUBA*. Nafahamu vizuri kuwa ili uweze kupata walimu wazuri hasa wa soka, ni ghali kidogo. Nampongeza sana Mwalimu wa Soka Maximo kwa hatua aliyoifikisha Tanzania katika nyanja ya soka, lakini naiomba Wizara kwa kuishauri Serikali kutafuta mwalimu mwingine ambaye ataiondoa Tanzania kisoka hapa ilipofika na kuipeleka kuwa ni Tanzania yenye kushinda vikombe katika mashindano mbalimbali. Kazi iliyoifanywa na Maximo ya kuwahamasisha wachezaji wetu na kufikia hapa ni nzuri na tumekuwa tukishinda michezo ya majaribio na kirafiki lakini sasa anatakiwa mwalimu atakayekuja na mbinu za kushinda kwenye mashindano.

Maximo ameshindwa kuchukua kikombe kule Uganda kwenye *Challenge* wakati akiwa na takriban wachezaji wote wa *Taifa Stars* na akashindwa kuchukua kikombe kule *Ivory Coast* kwenye *CHA* akiwa na wachezaji kamili wa *Taifa Stars*. Hii ni dhahiri amefika kiwango chake cha kuhamasisha na sasa tutafute mwalimu wa soka atakayeiondoa Tanzania hapa ilipo na kuanza kuchukua vikombe kwenye mashindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFF* hivi sasa ni muda mrefu chombo hiki kimekuwa kikifanya kazi zake za kuinua soka hapa nchini. Lakini ili uwe na wachezaji wazuri na mpira wa nchi, upande ni lazima uwe na waamuzi wazuri, wenye ujuzi, waadilifu, waaminifu na wasiohadaiwa na tamaa mbalimbali. Waamuzi wetu ni muhimu na wanahitajiwa kuangaliwa sana, *TFF* kwa ajili ya semina na mashindano pamoja na matayarisho ya kuwapata waamuzi hao. Waamuzi wa Tanzania Bara wamekuwa wakienda kwenye mashindano mbalimbali bila ya kupewa nauli, posho ya kujikimu jambo ambalo huwa linakaribisha rushwa kutoka kwenye timu zinazoshiriki mashindano husika.

*TFF* imekuwa ikiwakopa waamuzi hao fedha zao kwa kisingizio kuwa fedha hakuna jambo linaloleta mashindano mengi kuwa yenye usumbufu kwa waamuzi wetu. Hivi sasa Tanzania Bara kunafanyika mafunzo kwa waamuzi wetu kote Tanzania Bara ili waamuzi wetu waweze kupata taaluma juu ya mabadiliko ya sheria ya *FIFA* zilizotoka hivi karibuni pamoja na kujitayarisha na ligi. Waamuzi hao wamekuwa wakihudhuria mafunzo hayo wakitoka makwao sehemu mbalimbali bila kulipwa fedha za kujikimu jambo linalopelekea baadhi ya waamuzi hao kuwaendea watu wenye timu kuomba msaada hivi sasa kutoa sura ya kulipa fadhila hapo baadaye katika michezo mbalimbali.

Mwisho, naipongeza sana Wizara kwa kuonyesha nia thabiti ya kuondoa tofauti na migongano inayoletwa na baadhi ya viongozi wasiojali utanzania katika vyama vya soka vya Tanzania. Mzozo unaotajwa kuwa ni wa *TFF* na *ZFA* unafanywa kutokana na baadhi ya viongozi kutokuzingatia Katiba, udugu, ushirikiano na nia thabiti waliokuwa nayo waasisi wa Muungano wetu.

Naiomba sana Wizara kulisimamia jambo hili ili badala ya kuangalia mambo mengine muhimu na kero zilizopo soka la Tanzania liende mbele.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo -Mheshimiwa George Mkuchika, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Joel Bendera, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Redio ya Taifa *TBC*, kaka yangu Tido Mhando pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye nia thabiti ya kuboresha sekta za Wizara hii kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda nitamke rasmi kuwa ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo mia kwa mia. Hivyo ninawatakia afya, nguvu, maisha marefu na mshikamano wa dhati katika kutekeleza bajeti yao vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu televisheni ya Taifa Singida, ninayo faraja ya pekee sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kusikia Serikali itaanza kuonyesha televisheni ya Taifa mwaka huu mwezi Oktoba. Wasiwasi wangu kwa mradi huu ni kwa vile umekuwa wa muda mrefu sana, takriban miaka saba. Hivyo, imani kwa wananchi wa Singida imekuwa ndogo sana kwa Serikali kuwasha Televisheni ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iwathibitishie wananchi wa Mkoa wa Singida kwani wanapata televisheni hii kwa kutumia mitambo ya mfanyabiashara anayewatoza gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa wako waandishi wa habari wenye uwezo mdogo sana na kusababisha upotoshaji wa habari wanazotoa. Hii imetokea baadhi yao huacha kuandika habari muhimu na kuandika jambo dogo ambalo halina maslahi na umma wa Tanzania ama kuwapaka watu matope hususan viongozi wakiwemo Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali katika kusajili waandishi wa habari, suala la taaluma liwe kigezo cha kwanza. Naomba Serikali idhibiti matumizi mabaya ya kuandika habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dalili za kuaminika kuwa wapo waandishi wa habari ambao wanaandika habari kwa lengo la kuwachafua baadhi ya watu wakiwemo viongozi. Ninaiomba Serikali, jukumu la kuwashitaki waandishi wa habari wenye tabia hii badala ya kumwachia mwananchi aliyechafuliwa kushitaki, ni bora aliyechafuliwa kuwa shahidi tu. Nina hakika Serikali ikitekeleza hoja hii, waandishi Makanjanja watapungua. Naomba nipewe majibu wakati wa Mawaziri wanajibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna tatizo kubwa sana la waandishi wa habari kufanya kazi zao katika mazingira magumu sana kwani waandishi wengi hawana usafiri jambo ambalo linawafanya waandishi kutokuwa huru na kazi zao na kusababisha kununuliwa na baadhi ya watu wenye uwezo kuchagua watu wengine. Ni vyema Serikali

kutoa wito kwa wamiliki wa vyombo vikubwa vya habari kutoa vyombo vya usafiri kwa watumishi wao ili waweze kufika kwenye matukio haraka iwezekanavyo. Vile vile waandishi wapewe *video camera* na kamera za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali itambue umuhimu wa waandishi wa habari kwamba ni watumishi sawa na watumishi wengine. Hivyo ni vyema kutazama upya viwango vyao vya mishahara pamoja na marupurupu yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waandishi wengine huweza kununuliwa na baadhi ya watu kupotosha habari kwa sababu ya maisha duni waliyonayo. Hivyo, ni vyema sana Serikali kuongeza mishahara yao pamoja na wamiliki wa vyombo vya habari kufuata viwango vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vipato vya waandishi havitoshi. Napenda kuishauri Serikali kutoa elimu kwa waandishi Mikoani kuwa na umoja wao na ndani ya umoja wao kubuni miradi ya uzalishaji mali iwemo *SACCOS*/VIKOBA kwa lengo la kuinua vipato vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuinua vipato vyao ndani ya umoja wao pia watapata nafasi ya kukosoana wao kwa wao kabla hata Serikali haijawadhibiti waandishi watovu wa nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kuwa michezo ni muhimu sana kwa vijana kuanzia na umri mdogo. Ikumbukwe kuwa zamani michezo ilikuwepo shule za msingi na sekondari ambayo ilijulikana kwa majina ya UMITASHUMTA kwa shule za Msingi na UMISETA kwa shule za sekondari. Michezo hii ilikuwa ni changamoto kubwa sana na ilisaidia sana vijana kuonyesha vipaji vyao mapema sana na ilisaidia kupata wachezaji wazuri wa kitaifa na kimataifa ambao walileta sifa kubwa kwenye mikoa walikotoka pamoja na Taifa kwa ujumla pamoja na kuinua pato la nchi kupitia michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza juhudi za viongozi wa michezo kusimamia michezo ya mipira ya miguu na mikono kuanzia ngazi ya kijiji hadi ngazi ya Mikoa. Inasikitisha sana juhudi ya vijana ya kuonyesha uwezo wao wa michezo mbalimbali na inasikitisha sana pale wachezaji wanaposhindwa kwenda kushiriki michezo ngazi ya Taifa kwa kukosa fedha za kuwasafirisha. Ninaiomba Serikali kuhakikisha kila Mkoa kuwa na Akaunti yake ili wachezaji wanapotakiwa kwenda kushiriki kitaifa mzigo ambao huachiwa Wabunge kuwasafirisha na pale Wabunge wanapokuwa hawapo Mikoani, basi wachezaji hukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuwa na utaratibu wa kutoa motisha ya kuwaajiri vijana wenye kuonyesha vipaji vya juu kwa michezo mbalimbali. Hii itawatia moyo vijana wenye vipaji hivi vya michezo kutokukata tamaa na kukatisha vipaji vyao hadi umri wa utu uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikitoa ajira kwa vijana wachezaji wazuri wenye sifa ya kuajiriwa itakuwa changamoto kubwa sana kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kusema tena, naunga mkono hoja hii nikiwa ninasubiri ufafanuzi wa mchango wangu. Natanguliza shukrani zangu za dhati.

**MHE. MOHAMMED A. CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kuchangia hoja iliyokuwepo mbele yetu. Kwanza, naanza kwa kuunga mkono hoja. Mchango wangu kwenye hoja hii, napenda kuzungumzia suala la mmomonyoko wa maadili na utamaduni wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa imefikia mahali pa kutisha na kusikitisha kwa hali ya vijana wetu ambao ndio mategemeo ya Taifa letu la baadaye kwa kila nyanja, wanavyopotoka na kutojali kabisa kudumisha na kulinda utamaduni wetu wa Tanzania na kufuata maadili yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliokoa Taifa letu la Tanzania Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, inabidi kuliangalia na kulichukulia hatua zifaazo na haraka sana, suala la utunzaji wa utamaduni wetu na maadili yetu ikibidi hata kuleta Muswada wa Sheria hapa Bungeni wa kuzuia mavazi ambayo yanakwenda kinyume na utamaduni na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mavazi ambayo yanavaliwa na vijana wetu hasa wa kike, ni jambo ambalo linatia aibu na kichocheo kikubwa cha uvunjaji wa utamaduni na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kuandaa taarifa nzuri ya bajeti kwa Wizara yao. Aidha, pongezi za pekee zimwendee Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake anazozichukua ili kukuza sekta ya michezo nchini, matokeo ambayo nchi yetu imepanda kimchezo wa mpira wa miguu Afrika na dunia *(ranking).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nachukua nafasi hii nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *ranking* ya nchi kimichezo hutokana na matokeo mazuri ya michezo inayocheza timu husika na hapa nazungumzia hasa timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu. Ili kuunda timu nzuri, maana ya wachezaji Wazalendo wanaotokana na vilabu mbalimbali vya mpira wa miguu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza utamaduni kwa vilabu vyetu hapa nchini hasa vile vya Simba na Yanga kusajili wachezaji wengi wageni *(foreigners)* na hivyo kuwanyima nafasi wachezaji wazalendo kupata fursa ya kucheza kwenye vilabu hivyo ambayo mara kwa mara hufanikiwa kupata nafasi ya kucheza michezo ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni hatari kwa timu yetu ya Taifa ambayo hujengwa na wachezaji wanaotokana na vilabu nchini kukosa ubora wa kupata wachezaji watakaoinua *FIFA ranking* kwa nchi kimichezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na wachezaji wageni ni jambo zuri. Hata hivyo, *TFF* ni vyema ikaweka utaratibu mzuri wa kuwa na idadi maalum ya wachezaji wa kigeni kwa klabu yenye uwezo wa kuwasajili ili kulinda soko la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soka la wanawake duniani nalo linakuja juu. Ni vyema sasa *TFF* ikahamasisha soka la wanawake nchini kama ilivyo kwa nchi za Ghana, Nigeria na kadhalika. Aidha, *TFF* iwashawishi wafadhili mbalimbali wa michezo pia wafadhili akina dada kwenye ligi la mpira wa miguu nchini ili kupata wachezaji bora wa timu ya Taifa ya soka la wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo wa riadha uliiletea hadhi sana nchi yetu miaka iliyopita. Ni vyema Serikali ikaangalia upya pale ilipoteleza mpaka hali ya mchezo wa riadha kufikia hapo ulipo. Ni kwa nini mbinu za enzi za wachezaji walioiletea sifa nchi yetu (Suleiman Nyambu, G. Shahanga, F. Bayi, Mwanjala na wengineo) hazifuatwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alifahamishe Bunge lako Tukufu na Taifa kwa jumla, Serikali imejipanga vipi kuitumia fursa ya mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2010 litakalofanyika Afrika Kusini kwa timu Shiriki kuvitumia viwanja vyetu vya Uhuru, Mnazimmoja, (kama *Memorium stadium*), uwanja mpya wa Taifa na Uwanja wa Amani ulioko Zanzibar ambao hivi sasa unafanyiwa ukarabati mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa *TFF* na *ZFA* upate ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mmomonyoko wa maadili kwa jamii, uvaaji wa mavazi hasa kwa akina dada zetu hauridhishi, kitu ambacho hushawishi kitendo cha kuwa na fataki kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na uhuru kwa kila raia wa nchi hii ni vyema Wizara iweke taratibu za uvaaji wa mavazi kwa jamii yake ambayo ni ya heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Wizara ya Ulinzi imeweka sheria kali ya kifungo cha miaka 20 kwa kosa la kuvaa sare inayofanana na ile ya Jeshi, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ndiyo msimamizi wa wasanii nchini. Wasanii wetu (baadhi) wamekuwa wakivaa sare zinazofanana na zile za Jeshi la Ulinzi na JKT. Isitoshe tabia hii imekuwa ikifanywa hata wakati wa kunakili *(recording)* miziki yao kwenye

kanda za *video* na kuuzwa kwa watu.  Wizara inachukua hatua zipi kuzuia ukiukwaji wa uvaaji wa vazi hilo na hasa kwa zile kanda za *video* vilizokwisha sambazwa kwa wateja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* inafanya kazi nzuri sana, Wizara iiwezeshe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Muswada wa Sheria wa Vyombo vya Habari utawasilishwa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kuzijibu hoja nilizoziuliza.

**MHE. ENG. STELA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Naibu wake kwa kazi kubwa ya kurejesha na kuzipandisha chati shughuli zinazoratibiwa na Wizara hiyo.

Vile vile nachukua nafasi hii kuwapongeza watendaji wengine wote wakiwemo kaka yetu ndugu Florence Ruruka, Tido Mhando, Dada Joyce Mhavile na waandishi wote ambao wanalenga kuisaidia nchi yetu pamoja na kuimarisha maadili ya Watanzania. Kwa namna ya pekee nilipongeze gazeti letu la Uhuru, vijana akina Epsoni na wenzake kwa kweli wanajitahidi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni moja tu kubwa, waandishi na vyombo vya habari, tuache kuwa *biased*, wote sisi ni wenu.  Vyombo vya habari vina nafasi kubwa kuisaidia jamii, kwani ndio jicho na sikio la Watanzania.

Mara ya mwisho nilichangia juu ya umuhimu wa kutangaza mji wa Songea kuwa wa kihistoria na kishujaa kwa ajili ya utalii.  Utalii huo pia unaambatana na ngoma za asili pamoja na simulizi zetu. Pamoja na shukrani nyingi kwa siku ya utamaduni iliyofanyika mjini Songea mwaka huu Mei, tunaomba Wizara itusaidie kufanya *documentation* ya mambo ya vivutio vya utalii kutoka Mkoa wa Ruvuma ili kuzidi kutangaza Mkoa wetu.

Hata hivyo, napenda kumpongeza sana kijana wenu *TBC1* Bw. Gerson Msigwa. Kwa kweli yule kijana ni mfano wa kuigwa na ni *asset* ya Taifa.  Ni vyema vijana kama hawa waendelezwe ili kulisaidia Taifa.

Lakini pia vijana kama akina Jerry Muro na akina Kubenea ambao wanaandika habari za uchunguzi ni vyema wasaidiwe kujua zaidi namna ya kuandika habari hizo kwa uzuri zaidi.  Tatizo limekuwa ni *mushrooming* ya vyombo vya habari tukiwa na ujuzi mdogo lakini huu ni mwanzo, badala ya kuvipunguza vyombo hivyo tuboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari toka vijijini hazipatikani, ni vyema kutoa *subsidy* kwa ajili ya habari za vijijini.  Pia luwe na utaratibu wa kukusanya magazeti ya zamani na kuwasaidia kuwapa watu wanaoishi vijijini hata kama watayapata baada ya

siku tatu, sio mbaya. Hivyo, ni vyema kuwa na maktaba ndogo za Kata ili kutoa nafasi ya watu kupata habari kupitia magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunaweza kupata viredio vya kata (masafa mafupi) kwa ajili ya kuhamasisha maendeleo ya Kata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nazidi kuipongeza Wizara na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Waziri Mheshimiwa George Mkuchika na Naibu wake - Mheshimiwa Joel N. Bendera wa uwasilishaji chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Dr. Florence M. Turuka na watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana *TBC* kwa kazi nzuri sana hasa kwa kutoa taarifa zenye kweli nyingi bila kuwa *Biased*. Nilibahatika kuingia katika jengo lao la utangazaji, kweli hali ni mbaya ya *"pathetic"*. Vijana/wanahabari wanafanya kazi katika mazingira mabovu, pafinyu, pamechakaa! Panahitajika ukarabati na uboreshaji wa haraka. Naamini kitu kama kapeti, kukipangwa vizuri chumba cha Televisheni inawezekana ili kuipa hadhi *TBC.*

Pia nashauri utamaduni, tuendelee kutoa elimu ili jamii indelee kuthamini tamaduni zetu. Naipongeza TASUBA, lakini bado juhudi ziendelee hasa kutafuta vipaji vingi vya wasanii walioko vijijini. Najua utambuzi wa mafunzo yanaendelea, lakini tuongeze kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuwa na vazi rasmi la kitaifa, ni kitendawili! Tatizo ni nini? Tumalize mchakato huu ili liwepo vazi rasmi ambalo litaitambulisha nchi yetu.

Michezo sio mbaya hasa katika eneo la mpira wa miguu, bado iko haja ya kufufua michezo mingine hasa katika ngazi za Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Vipaji vipo.

Ujenzi na ukarabari wa viwanja vya michezo *(stadiums)* Wizara iwasaidie wabia kuboresha viwanja kama vile cha Mkwakwani, kiwe cha kisasa. Maafisa michezo Wilayani bado hawajitumi vizuri au Halmashauri za Wilaya, hazioni umuhimu wa michezo. Nashauri wapatiwe usafiri ili waweze kuhamasisha michezo kuanzia ngazi za Kata.

*Otherwise,* nawapongeza wadau wote wa michezo, sasa Tanzania inaweza kuwika katika chati ya dunia. Kila la kheri.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndio chimbuko la lugha ya Kiswahili. Ziko nchi nyingi zinahitaji walimu wa Kiswahili kwenda kufundisha katika vyuo vyao. Ninaomba Wizara kwa kutumia fursa hiyo wanieleze ni kwa namna gani Watanzania wenye utaalam (walimu) wamefaidika na kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fursa hiyo haikuchangamkiwa sio ajabu nchi za jirani wakaitumia fursa hiyo licha ya kuwa hapa kwetu ndio chimbuko la Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni ndio kielelezo cha Taifa lolote. Utambulisho wa Taifa fulani unajulikana kutokana na utamaduni wake. Vyombo vyetu vya habari hususan redio ya *TBC* na televisheni *TBC*, ni lazima vyombo hivyo vihakikishe vipindi vyao viwe vinalinda utamaduni wetu licha na utandawazi uliopo. Vyombo hivi vya habari visishindane au kuviiga vyombo binafsi kwa vipindi ambavyo haviendani na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inang'ang'ania taratibu ambazo baadhi yake hazisaidii huendeleza mchezo wa mpira wa miguu kimataifa. *TFF* imejiunga na *FIFA* na inapata misaada mbalimbali kuendeleza mpira wa miguu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itakosa nini kutoka *FIFA* kama Zanzibar kwa kupitia *ZFA* itajiunga na *FIFA.* Nionavyo, ipo haja tena haraka sana taratibu zifuatwe ili *ZFA* iwe wanachama wa *FIFA*. Hii itafanya misaada inayotokana na *FIFA* kwa *TFF,* iwe haina haja kutakiwa yagawiwe kwa *ZFA.* Kufanya hivyo sio kudhoofisha Muungano.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kufika hapa Bungeni ili na mimi niweze kutoa mchango ambao utasaidia kulisukuma mbele Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti wote kwa jinsi mnavyotuvumilia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, nitakuwa sikuwatendea haki kama sijawashukuru na kuwapongeza Waziri, Naibu na Watendaji wote kwa kutayarisha hotuba iliyojaa matumaini kwa Tanzania. Tatizo ni utekelezaji. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awasaidie katika utekelezaji wa nguvu, ari na kazi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejua kwamba kwa mujibu wa Katiba ya nchi kupata habari ni lazima kwa kila mwananchi ilimradi mtu asivunje sheria, naiomba Serikali itoe uhuru kamili kwa watoa habari ili wananchi wajue mambo muhimu ya nchi na nje ya nchi kwani sasa kuna sera ya utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari kwamba sheria mpya ya habari itakuja hapa Bungeni, lakini mpaka leo hii haijaletwa. Naiomba Serikali iangalie kwa kina na kuhakikisha inafuata sheria ambayo inaelekea sio kuwabana watoa habari kama ilivyofanya kwenye gazeti la Mwanahalisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni, nchi yetu ni nchi ambayo ina maadili mazuri sana, lakini leo hii sote ni mashahidi kwamba maadili na utamaduni wetu umeporomoka kutokana na hali inayojitokeza ndani ya *TV* kuonyesha mambo ambayo sio

mazuri kwa watoto wetu. Wakati mwingine mzazi kukaa pamoja na watoto kuangalia *TV*, unashindwa kutokana na mambo yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za wenzetu mambo mengine ambayo sio mazuri kuangalia pamoja na watoto, mambo hayo au vipindi hivyo huonyeshwa kuanzia usiku wa manane, watoto wameshalala. Kutokana na hali ya utandawazi sio vibaya kuonyesha vipindi hivyo lakini iangalie wakati muafaka ambao hautaleta madhara kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kurudisha michezo mashuleni, lakini cha kusikitisha nafasi za kufanyia michezo hiyo bado ni kitendawili, kwani hakuna nafasi nzuri kwa wanafunzi kufanyia michezo yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichukue juhudi za makusudi kuangalia namna ya kupata viwanja vya michezo katika shule ambazo hazina nafasi nzuri za kufanyia michezo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile michezo ni afya, naipongeza sana Serikali na shukrani za pekee zimwendee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa michezo na kuleta makocha tofauti wa kuwafundisha wananchi wa Taifa hili michezo ili waache kuitwa kichwa cha mwendawazimu. Naiomba Wizara waendeleze juhudi hizi ili pesa za walipa kodi wa nchi hii zisiteketee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. RAJABU HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya leo ambayo kimantiki na kimawasilisho kwa kweli ni mazuri. Hotuba ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongezi zangu kwa timu yetu ya Taifa ya mpira wa miguu kwa hatua yake ya maendeleo makubwa ya soka kiasi kwamba ni tishio kwa nchi za Afrika Mashariki na kati na pengine kwa Afrika nzima. Hivyo ni hatua kubwa sana na inafaa ipongezwe kwa nguvu zote. Nchi yetu kimichezo na hasa kwa mpira wa miguu ilikuwa ni kichwa cha mwendawazimu. Wizara, *TFF*, kocha, wachezaji na wapenzi kwa jumla yao na kwa ushirikiano wao ndio tukafika hapa. Aidha, shukrani za kipekee zimwendee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukaribu wake na vyama vyetu vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa) ni chombo muhimu sana cha kukuza lugha ya Kiswahili nchini petu. Hata hivyo, chombo hiki bado hakijaweza kukamilisha mambo mengi muhimu yanayohitajika kusimamiwa na Baraza hili. Kwa mfano, mambo yafuatayo ni vyema yakatayarishwa na chombo hiki:-

1. Kamusi la Kiswahili;
2. Maneno mapya yaliyotoholewa; na
3. Maneno yasiyofaa kuendelea kutumika katika jamii kama ni Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza hili linafanya kazi nzuri ya kuelimisha kupitia vyombo vya habari, lakini sijaona nyaraka kama nilizozisema hapo juu ambazo kwa maoni yangu ni nyaraka muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima pamoja na familia yangu. Pia kukupongeza wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na wenyeviti kwa huduma zenu kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Mkuchika, utafahamu kuwa Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Naibu wake - Mheshimiwa Bendera utaona nia yao njema ya kuiendeleza silka za kitanzania, michezo pamoja na kukua kwa habari katika kuelimisha jamii. Kama kuna wa kupewa medali katika Wizara, basi Waziri Mkuchika na Naibu wake ndio wangelikuwa wa kwanza kupewa medali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu habari, vyombo vya habari ni muhimu sana kwani mara nyingi hutoa taaluma kwa kuelimisha jamii pamoja na kutoa makosa pale ambapo pana udhaifu fulani. Pamoja na umuhimu wa habari, kumejitokeza matatizo ya vyombo hivi kuhusiana na sheria. Imeonekana sheria inayoongoza vyombo hivi kuhusiana na sheria zimepitwa na wakati jambo ambalo hupelekea kukosekana kwa uhuru. Hivyo, naiomba Serikali iwe tayari kubadilisha sheria hizo ili vyombo hivi vifanye kazi zake bila kushikwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuviruhusu vyombo hivi na kufanya kazi yake kwa uhuru mradi havivunji sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utamaduni, kwa kuzingatia utangazaji, naona kuna udhaifu mkubwa katika vyombo vyetu vya habari. Vyombo hivi vinaondoa maadili yetu ya kitanzania. Ni makosa makubwa yanayotendeka juu ya vyombo vyetu hivi. Ninaiomba Wizara idumishe mila zetu ndani ya jamii kupitia vyombo vyetu vya habari. Hivyo, Wizara haiyoni mambo yanayotendwa na vyombo vyetu kama sio mila za kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kusita napenda kuipongeza Wizara kwa kuweza kukuza michezo katika nchi yetu. Kwa kweli taasisi zote za michezo zimepiga hatua sana. Pamoja na jitihada za Wizara kukuza michezo, kuna tatizo kubwa katika Wizara. Kwa kuzingatia umuhimu wa michezo, ni kuwepo kwa viwanja. Kuna tatizo kubwa la viwanja vya michezo katika nchi yetu. Hii ninasababishwa na mijengo miji inayoendelea siku hadi siku, jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kurudisha michezo katika mashule yetu. Katika hili, kuna upungufu mkubwa katika maeneo haya, kukosekana kwa viwanja vya michezo. Mashule mengi yaliyojengwa hayana viwanja. Tukumbuke kila mwanamichezo huanzia utotoni. Mashule ndio chimbuko la kupatikana wachezaji wazuri. Hivyo basi, Wizara itafanikisha kwa kiasi gani kuwepo ama kupatikana viwanja katika mashule yetu?

Baada ya Maelezo yangu hayo, naipongeza Wizara kwa kazi zake nzuri. Natoa hongera kwa Mheshimiwa Mkuchika na kwa Mheshimiwa Bendera.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli nichukue nafasi hii niwaombe radhi sana wale ambao ningewapa nafasi ya kuzungumza, baada ya kufanya sasa hesabu zangu za dakika nilizobakiwa nazo kwa umakini nimegundua kwamba shughuli hii ya uchangiaji inanilazimu tu niikatishie hapa. Kwa kusema hivyo, sasa nawapa dakika 45 Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika zake 15 na baadaye Mheshimiwa Waziri kwa dakika 30.

Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika siku hii ya leo. Aidha, nakushukuru sana wewe binafsi kwa kusimamia vizuri mjadala huu na pia kunipatia fursa ya kuchangia hoja kwa niaba ya Waziri wangu wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kutoa maelekezo kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, aidha kwa kuzungumza au kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa idhini yako nitoe pongezi na shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kufika hapa leo.

Kwanza, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete kwa kuendelea kuwa na imani na mimi kuendelea kuhudumia Wizara hii kama Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Pili, namshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Captain Mstaafu George H. Mkuchika kwa ushirikiano mkubwa na wa hali ya juu anaonipa na kuniongoza katika kutekeleza majukumu haya. Kwa kweli, ni Mwalimu mzuri na ni mshauri mzuri pia, namshukuru sana na hongera sana Mheshimiwa Mkuchika.

Tatu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Katibu Mkuu Dr. Turuka, Wakurugenzi wa sekta zote, Wakuu wa Taasisi, *Board* zote na wafanyakazi wa Wizara hii kwa ushirikiano mzuri ambao wanatupatia. Napenda kuvipongeza vyombo vya habari, *TV*, Redio na Magazeti kama wadau wetu kwa jinsi ambavyo tunafanya nao kazi vizuri. (*Makofi*)

Nne, napenda kuwapongeza wasanii na wanamichezo wote kwa jinsi ambavyo wanawaburudisha Watanzania na kulitangaza Taifa letu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Mjini kwa jinsi wanavyochapa kazi za kujiletea maendeleo. Aidha, nawashukuru kwa kuendelea kuwa na imani na mimi kwani hii ni awamu ya tatu, yaani ni vipindi vitatu mfululizo nimekuwa Mbunge. Hii inaonyesha kwamba wana imani na mimi na ninawatakia kila la kheri na nitawafanyia kazi kwa kadri Mwenyezi Mungu anavyoendelea kunijalia. Leo Korogwe Kata zote zina shule za Sekondari, Zahanati, barabara safi na mji sasa unaendelea kuwekwa lami, hii ni kuonyesha kabisa kwamba ilani ya chama inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kumshukuru na kumpa pongezi mke wangu Mwalimu Flora, wanangu watatu Herbert, Jasin na Glory kwa jinsi wanavyonishauri na kunilea hasa ukizingatia kwamba kazi yetu ni ya mazingira magumu kwani muda mwingi tuko nje ya nyumba zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimejikita katika sekta tatu za Wizara yetu, yaani Sekta ya Habari, Sekta ya Utamaduni na Sekta ya Michezo.

Hoja zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi sana, tunahitaji kujibu zote, lakini naomba mtukubalie kwa ushauri wetu kwamba tutazijibu zile ambazo tutazijibu na nyingine tutawaletea kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nianze na kuipongeza Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na ushauri wao tumeupokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kambi ya Upinzani imetoa maoni mazuri nayo tumeyapokea. Lakini kwa kweli naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wametusaidia, nilikuwa naandika Wabunge waliozungumza kwa maandishi wamefika sabini na zaidi. Hii inaonyesha jinsi ambavyo sekta hii ilivyokuwa muhimu katika jamii kwa sababu hasa ndiyo ambayo inashughulika na maadili ya nchi yetu na mila na desturi pamoja na maadili yote ambayo Watanzania tunahitajika tuyafanye. Kwa hiyo, naomba sasa nianze kuchangia hoja hizi kwa sekta hasa nikianza na sekta ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Wabunge wengi ambao wamechangia, nitazungumza hoja ambayo imezungumzwa na nitajaribu kutoa majibu kwa jinsi wote walivyochangia kwa sababu ziko ambazo zimeingiliana na wengi wamechangia hoja hiyo hiyo moja wanaweza wakawa Wabunge watano, Mheshimiwa Waziri atawataja majina lakini naomba mimi nitaje tu zile hoja ambazo wamezielezea.

Mheshimiwa Mweyekiti, wameelezea umuhimu wa michezo na kuendeleza vipaji, mchezo wa *netball* upewe kipaumbele. Napenda kusema tunashukuru kwa

ushauri huo na hivi sasa mchezo wa *netball* umeanza kujipanga vizuri na Serikali inasaidiana na Viongozi kuweza kuinua mchezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Dr. Getrude P. Lwakatare, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa na Mwadini Jecha wote wamezungumzia namna ya kuendeleza mchezo wa *netball* na tuuhuishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kabisa kwamba mchezo wa *netball* tutausaidia kwani tuna mkakati mzuri tumeshauanza kwa kufanya semina mbalimbali. Mwaka jana walishiriki *Taifa Cup* timu tisa lakini mwaka huu ni timu kumi na saba na Serikali inasaidia. Mheshimiwa Halima J. Mdee mchango tumetoa kuendeleza mchezo huu kwenye *Taifa Cup* na Serikali imetoa milioni moja, utaonekana ni mchango mdogo lakini ukumbuke kwamba tuna michezo 30 na bahati mbaya hatuna bajeti ya kutoa ruzuku kwenye vilabu, lakini kwa uwezo wetu tumeweza kuchangia angalau milioni moja ili mashindano yale yafanikiwe na tunaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni viwanja hasa kiwanja cha Moshi kugeuzwa soko na katika shule za Kata kwamba hazina viwanja na katika Kata zetu na Mikoa na Wilaya vijengwe viwanja. Ushauri huo tunauzingatia lakini kama ambavyo nataka nizungumze hapa ni kwamba, tunaziomba Halmashauri za Wilaya zipange miradi ya ujenzi wa viwanja kwenye Halmashauri, Wilaya na Mikoa yote na hii ipitishwe kwenye Baraza la Madiwani, iwe ni mradi mmojawapo kama ambavyo tunakuwa na mradi wa shule, zahanati na hata barabara. Michezo nayo iko katika maendeleo, kwa hiyo, tunategemea kwamba wenzetu kule katika Halmashauri zetu watakuwa na mpango wa kutayarisha *program* za kujenga viwanja ili na sisi Serikali tuweze kuingilia huko kusaidia kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana M. Chilolo amezungumzia kuimarisha michezo shuleni pia Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti amezungumzia hilo. Mheshimiwa Kingunge N. Mwiru, Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Eustace O, Katagira, Mheshimiwa Juma H. Killimbah pia amezungumzia hilo na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kwamba sote tunakubaliana kwamba huwezi ukaendeleza michezo kama huanzi katika shule za msingi, huwezi kuendeleza michezo kama huendi kwenye majeshi, huwezi kuendeleza michezo kama huendi kwenye shule za Sekondari. Tunashukuru Serikali yetu sasa imerudisha michezo katika shule na mashindano yale ya UMISETA na UMITASHUNTA na wote mmeshuhudia mwezi uliopita mashindano haya ya UMISETA yamefanyika Kibaha. Mwaka huu Desemba tunaanza mashindano ya shule za msingi. Kwa hiyo, tumerudisha haya mashindano tunaamini kabisa kwamba tusiporudisha mashindano haya shuleni hatuwezi kufika popote na wenzetu dunia nzima ndivyo wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachezaji wengi katika vilabu vya mpira ni wageni. Hili limezungumzwa na Wabunge wengi ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Fatma, Mheshimiwa Nuru Bafadhili na hata Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Tunakubaliana nao na ushauri huo tunauchukua, TFF watazingatia hilo ili angalau wachezaji wengi ambao watasajiliwa kwenye vilabu wawe ni wa humu humu nchini bila kutegemea wachezaji wa kigeni kwa nia nzuri ya kuweza kuendeleza mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumziwa suala la vifaa vya michezo kwamba vipelekwe katika shule zote, suala la pongezi kwa Rais na pongezi kwa timu yetu ya Taifa. Bahati nzuri kwa Wizara ya Elimu kila shilingi elfu moja inapelekwa kwa ajili ya kununua vifaa vya michezo. Tunasisitiza kwamba, Wakuu wa Shule wajue hilo kwa sababu wanatakiwa kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anayeingia kwenye shule shilingi elfu moja ni kwa ajili ya kununulia vifaa vya michezo. Kwa hiyo, ni fedha nyingi na kwa hiyo, hiyo ni kusisitiza tu kwa wale Walimu wanaohusika waweze kununua vifaa hivi ili shule ziwe na vifaa na hilo tutaliwekea mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni jinsi tulivyojiandaa kufaidika na Kombe la Dunia litakalofanyika Afrika ya Kusini. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na pia limezungumziwa na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma na Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumejiandaa vizuri sana na Mheshimiwa Rais ameunda Kamati ya Kitaifa ambayo Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa ndiye Mwenyekiti, lakini pia wako Mawaziri wengine. Hii Kamati tayari ina mkakati mzuri ambao tunajiandaa ili tuweze kufaidika na mashindano ya Kombe la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine la kwamba *TFF* inawakopa waamuzi, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir amezungumza. Ushauri huo tunauchukua na *TFF* wameuchukua pia ili kuhakikisha kwamba waamuzi wanapokuwa kwenye michezo hawakopwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine la msingi sana ambalo limezungumzwa hapa ambalo ni migogoro ya vyama na matumizi ya fedha. Mkakati wa Serikali kuimarisha michezo katika sehemu mbalimbali yaani katika Mikoa. Hili tunamshukuru Waziri Mkuu ametusaidia sana kwani ameshapeleka *circular* katika Wilaya zote na Mikoa yote kwamba sasa Wilaya na Halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuendeleza michezo na bahati nzuri hiyo inahusiana na taaluma na Watendaji kazi katika Wizara yetu. Hilo linashughulikiwa na tayari katika ikama ya Serikali sasa hivi kila Halmashauri itakuwa na Afisa Michezo na Afisa Utamaduni na Mkoani kutakuwa na Afisa Michezo na Afisa Utamaduni ili kuendeleza michezo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la viwanja na kuendeleza michezo mingine. Hili naomba nilizungumze kwa sababu nimeshalijibu pia hata katika

maswali ya kawaida. Ni kweli yapo malalamiko kwamba, tunaendeleza mchezo mmoja lakini Serikali ina Baraza la Michezo, Baraza la Michezo ndiyo linalosimamia michezo yote, michezo mingine yote iko zaidi ya 36 na kila mchezo unatakiwa uwe unagangamaa ili uweze kufanya mambo yao wenyewe. Chama cha Mpira kinasifiwa kwa sababu wao wanachacharika kuandika *write ups* wenyewe, *TFF* wanapata misaada kutoka *Vodacom*, Serengeti na sehemu mbalimbali, lakini vyama vingine havihangaiki kutafuta fedha, matokeo yake ni kwamba watu wanaonekana kwamba wanapendelea mchezo mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye michezo kwani yako mengi katika eneo hilo na suala la *ZFA* na *TFF* tumelichukua na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi dakika mnazotupa ni chache sana, lakini sasa nije kwenye Sekta ya Utamaduni. Suala ambalo limezungumzwa sana hapa ni vazi la Taifa na kila mtu amelizungumza. Nataka niseme hivi, mchakato unaendelea wa kulitafuta vazi la Taifa kwa sababu sisi tuna makabila 127, hilo wote mnalijua hatuwezi tukakurupuka kuchagua vazi la kabila fulani, ni lazima kuwe na mchakato tufikie mahali tukubaliane wote na ndiyo maana inakwenda kwenye Baraza la Mawaziri na Tanzania siyo kisiwa ndivyo nchi nyingine zinavyofanya. Haya yamezungumzwa na Waheshimiwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa sana ni mmomonyoko wa maadili. Hili limezunguzwa na karibu Wabunge wote nikiwatamka hapa nitachukua muda mwingi. Lakini nataka niseme kwamba, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wasanii na wamiliki wa vikundi vya sanaa ili suala hili watu walielewe zaidi na bahati nzuri tumekubaliana katika bajeti hii mkipitisha fedha, tutakuwa na vipindi maalum kwenye redio, televisheni na magazeti vya kuzungumzia mila na desturi, mmomonyoko wa maadili ili angalau wananchi wetu wawe na ufahamu wa kuelewa mambo haya. Lakini kubwa zaidi maadili jamani ni ndani ya familia yaani baba, mama na watoto, lazima tujikite huko kubadilisha watoto yaani tukae nao na tuzungumze nao na sisi wazazi tuonyeshe mfano, lakini tukisema tutatoa maonyo, tutaongea lakini kama sisi wenyewe ndani ya familia hatubadiliki na watoto nao hawatabadilika. (*Makofi*)

Suala lingine ambalo limezungumzwa ni suala la *COSOTA*, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Martha M. Mlata, amezungumzia sana *COSOTA* na kwamba *COSOTA* iko wapi? *COSOTA* iko Wizara ya Viwanda na Biashara, sisi tunaingia kwenye *COSOTA* na kujibu maswali hapa kwa sababu ndiyo tunaotayarisha wasanii, inapofika kwenye biashara tunawaachia wenzetu wa Viwanda na Biashara. Lakini nataka nikuhakikishie kwamba, Sheria tunaihuisha ili wasanii wapate haki zao kusiwe na tatizo hili ambalo linatokea sasa na mchakato huu tutauanza mara moja na bahati nzuri kwa sababu na wewe tumekuteua kwenye Bodi utatusaidia kutupa *input* ili tuweze kufanikisha masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine ambayo yamezungumzwa kwenye Utamaduni ni BAKITA Mikoani. Hili nimeshalizungumza la BAKITA kuhusu tatizo la

Kiswahili na bahati nzuri tuna mchakato wa nyumba ule tunaendelea, Serikali katika bajeti imetupa milioni 500 utaziona, tunahangaika na tunaendelea lakini tukifanikiwa kupata nyumba basi BAKITA itakuwa imepata mahali pazuri zaidi pa kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *night clubs*, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro amelizungumzia pamoja na masuala ya kumbi kutoa makelele na kufanya vitu vya hovyo. Katika hili tayari Kamati iliundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe, Kamati hii imekaa, imeshaweka mkakati na tumerudisha kwenye Halmashauri za Wilaya kwamba katika Halmashauri za Wilaya tunawaomba wao ndiyo wanasheria, wazingatie Sheria zile, wao wamelegeza kamba kidogo ndiyo maana unakuta *disco* linapigwa kila mahali na sisi tumewaambia wenzetu wa BASATA sasa waorodheshe *nights clubs* zote, maholi yote ili tuyajue na *grades* zake na waepuke taratibu za kupiga *disco* hovyo hovyo na kusumbua watu. Hili litasaidia kama Sheria ile itafuatwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine ambalo limezungumzwa na Mzee Kingunge N. Mwiru, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Halima J. Mdee na wengine wote, hili ni suala linalohusiana na maadili. Haya yote tunayazingatia, sisi kama Wizara tutaendelea kupiga kelele, lakini pia tutaweka Sheria ngumu ili wananchi wajue kwamba kweli vichupi, shuka kuinuka na kadhalika yote haya tutasaidia kuyapunguza ili kusiwe na migongano katika masuala haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine ambayo yamezungumzwa hapa ni je, *COSOTA* kwa nini iko katika Wizara hiyo? Hilo nimeshalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni nyumba ya sanaa. Nataka nimueleze Mheshimiwa Martha Mlata kwamba nyumba ya sanaa inamilikiwa na Bodi ya Udhamini. Baada ya kutokea mgogoro wa umiliki, suala hili liko Mahakamani, sisi hatuwezi kuliingilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda masuala mengine atayajibu Mheshimiwa Waziri, lakini napenda niipongeze hotuba na naomba niunge mkono hoja na ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mjadala unaendelea ulitoa taarifa ya marekebisho ya mwakilishi aliyefariki Jimbo la Magogoni kuwa ni Daud Hassan na siyo Vuai Abdallah Khamis. Sisi tuliligundua hilo na nataka kupitia Bunge lako hapa kumwomba radhi Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis kwa kosa hili ambalo limetokea na pia naahidi kwamba nitamwekea katika maandishi kumwomba radhi kwa kosa hili la uchapaji ambalo limetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Wizara yetu, Waheshimiwa Wabunge wametutia moyo kwa sababu waliojitokeza kuchangia ama kwa maandishi ama kwa kuongea hapa na ama kwa kuongea wakati wanachangia hotuba ya Waziri Mkuu wamekuwa ni watu wengi jambo linaloonyesha kwamba Bunge hili linathamini sana shughuli za Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza katika kuchangia mada hii nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani; Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Eliatta Switi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mbunge wa Wete; Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mbunge wa Viti maalum; Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kingunge N. Mwiru, Mbunge wa Kuteuliwa; Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera; Mbunge wa Korogwe Mjini; Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi; Mheshimiwa Alhaj Manju S. Msambya, Mbunge wa Kigoma Kusini; Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafuatao wamechangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa; Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini; Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, tena, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe; Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani; Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu; Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga; Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki; Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mbunge wa Kitope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani; Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboni, Mbunge wa Magomeni; Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mbunge wa Bububu; Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Mashariki na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Willibrod Slaa, Mheshimiwa Maua Daftari, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Guido Sigonda, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma,

Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Mohammed Ali Said, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Zuber Ali Maulid, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Fatma Othman Ali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dk. Samson Mpanda, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Usi Ame Pandu, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Dk. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Dk. James Msekela, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Benito Malangalila na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafuatao walichangia mambo yanayohusu Wizara yetu walipochangia hotuba ya Waziri Mkuu na tunawashukuru sana. Mheshimiwa Dk. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Ameir Ali na Mheshimiwa Mohammed Missanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Naibu Waziri, kujibu baadhi ya hoja ambazo kama alivyosema mwenzangu, hoja ni nyingi, mmeona watu zaidi ya 80 na muda wa nusu saa hatuwezi kumjibu kila mmoja, lakini tutapitia yale mambo ambayo tumeona kwamba, pengine yanahitaji kufafanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianzia na upande wa Kamati, kusema kweli Kamati hii tunafanya nayo kazi kwa ukaribu. Mengi waliyoyasema pale wametusaidia sisi ili tupate kusaidiwa zaidi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa hoja kwamba, Shirika la Utangazaji liongezewe ruzuku. Ushauri tumeupokea na Waziri Mkuu, Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, ametusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili (BAKITA) lisaidiwe kukabiliana na tatizo la Kiswahili ili kitumike vizuri, licha ya kuwa lugha ya Taifa nchini, na pia lugha hii inatambulika kuwa miongoni mwa lugha rasmi inayotumika. Kusema kweli ushauri tumeuzingatia na tunaomba kama tulivyokuwa tunaambiwa kwenye Kamati kuwa, pengine hapa Bungeni pawe ndipo mahali hasa pa kuzungumza Kiswahili sanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaloomba kupitia Bunge hili ni kwamba, tangu Baba wa Taifa alipoamua kwamba, Kiswahili ni lugha rasmi ya Taifa,

bado iko kasumba unakuta Bodi ya Shirika wanaokutana wote ni Waswahili lakini mikutano inaendeshwa kwa Kiingereza. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tunayosimamia masuala ya lugha, tunaomba sana jambo hili lizingatiwe, watu wote wanaofanya vikao vya kiserikali wajitahidi kila inapowezekana itumike lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni Serikali imeongeza bajeti yake mwaka huu kutoka shilingi milioni 200 za mwaka jana lakini tunaahidi kwamba, tutaboresha kwa kadri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kutokana na upotevu mkubwa wa mapato hasa katika mpira wa miguu, Kamati inashauri BMT ishirikiane na *TFF* kuweka utaratibu wa usimamizi mzuri. Ushauri umepokelewa na tunauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya picha za Rais. Kama tulivyoeleza picha za Rais zilichapishwa nakala zaidi ya 50,000 na hadi sasa zimeuzwa zaidi ya nakala 1000. Tulipowasiliana na Ofisi nyingi za Serikali walisema wakati wa kuchapisha picha hizo, bajeti zao zilikuwa zimekwishapita, lakini sasa hivi tumeandikia ofisi zote za Serikali, Makatibu Wakuu na Mikoa pamoja na Wilaya kwamba, waje kuzinunua na tunaendelea na jitihada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa vyombo vya Habari. Ushauri umezingatiwa na hivi karibuni Waraka wa Sheria hiyo utafikishwa katika vyombo husika. Leo nimefarijika sana na michango ya Wabunge hapa, wengi mmezungumzia kuboresha Sheria ya Vyombo vya habari, tumeyachukua yale yote, tutayaleta hapa na mtakapoona kwamba yapo ambayo mliyasema lakini hatukuyaweka patapatikana nafasi ya ninyi kuchangia na kuweza kuboresha zaidi. Nia ya Wizara ni kwamba, vyombo vya habari viendeshwe na Bodi, Waziri asiwe tena mtu wa mwisho, asiwe peke yake ndiye anayetosheka kama hapa kuna uchochezi au hakuna. Lakini pia tunataka wale wote wanaomiliki vyombo vya habari na wao pia washiriki katika suala la mafunzo kwa Waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kushirikiana na Wizara ya Mambo ya nje. Ushauri umepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Uwanja wa Taifa wakati wa mashindano ya Kombe la Dunia. Tayari Serikali imeunda Kamati, tunawasiliana na nchi mbalimbali na sisi kama Wizara tunawasiliana na zile nchi ambazo tunajua zinakwenda Afrika Kusini, zile ambazo zimeingia katika fainali ili waweze kutumia uwanja wetu hapa kwa mazoezi na kwa bahati nzuri Tanzania, Zimbabwe, Msumbiji na nchi za Kusini mwa Afrika, umbali wake kutoka Afrika Kusini, unaruhusu watu kuweka kambi hapa na kupanda ndege kwenda kucheza Afrika Kusini na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la mahusiano kati ya *TFF* na *ZFA*. Niseme hivi Watanzania wenzangu wa Bara na Visiwani, naomba niwaelezeni kabisa kabisa, mahusiano kati ya *TFF* na *ZFA* ni mazuri sana, ni mazuri sana na nitatoa

mfano, mnaweza mkawa mnafanya jambo pamoja, mwenzenu akateleza katika jambo moja, basi lisiue yale yote. Tatizo lililoletwa hapa ni kwamba, mara ya mwisho *TFF* wamekwenda kwenye mkutano, katika ujumbe ule hakuwepo mjumbe kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Kikatiba, ya Kisheria hayo sitaki kuingia huko lakini nataka kusema, mimi kama Waziri wa Habari na mwenzangu, kaka yangu Shamhuna kule Zanzibar ameshatoa tamko, tutakaa na hawa *TFF* na *ZFA*, kama hoja yenyewe ni kwenda katika msafara wakaungana, hilo halina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyomfahamu Rais wa *TFF*, mdogo wangu kwa umri, katika vijana ma-*gentlemen* wa nchi hii ambao nawajua, Tenga mmoja wao. Katika vijana wastaarabu katika nchi hii, Tenga mmoja wao, katika watu wanaoujua mpira, Tenga mmoja wao, katika watu wanaoweka maslahi ya taifa mbele, Tenga mmoja wao na katika watu wanaolinda Muungano nchi hii, Tenga mmoja wao. Wameandaa *Copa CocaCola*, wamewakaribisha Wazanzibar na kwa taarifa nilizonazo timu ya Mjini Magharibi wameingia fainali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi walishirikiana na *ZFA* kuleta timu ya Taifa ya Zanzibar kushiriki, wameshirikiana na sasa hivi wameamua msaada wa fedha za mwaka huu kutoka *FIFA* zikatengeneze Uwanja wa Gombani, Pemba, wapande nyasi badala ya kuchagua kiwanja cha Bara, wamesema safari hii pesa ziende wapi, Kisiwani Gombani Pemba. Ndugu yangu Mheshimiwa Hafidh pale kapendekezwa na Tenga na watu wake, yeye ndiye Kamisaa anayewakilisha Tanzania katika mechi mbalimbali za Kimataifa katika Bara la Afrika. Leo yuko Kongo, kesho yuko Msumbiji, keshokutwa yuko Malagasy na kadhalika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema, mimi kama Waziri wa Habari, natosheka kabisa kwamba, *TFF* ina dhamira nzuri na inafanya kazi pamoja na wenzao lakini kama dosari, hilo ni suala dogo, walikwenda safari bila wenzao, hilo linarekebishika kwa sababu *logic* ipo ya kuongozana na Mjumbe kutoka Zanzibar kwa sababu wao tunapigania wawe wajumbe *Independent* wa *FIFA* lakini hawajapata huo ujumbe. Sasa kipindi hiki ambacho hawajapata huo ujumbe, si lazima na wao wapate mahali pa kusemea? Basi tutakwenda nao, sikuona kama ni zogo kubwa la kusababisha mara watu wakavutana mashati, jambo dogo tena linapokuwa chini ya *President* wa *TFF*, *gentleman* kama Tenga, hili limekwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Upinzani, maoni ya Waziri mwenzangu kivuli, mengi ametoa hoja nzuri sana, wahusika katika sekta ya filamu wameshindwa kutumia uasilia wa mila na utamaduni. Tumekubali, Bodi inahamasisha jamii na kutoa elimu endelevu kwa wadau hasa Wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amehoji pia, je kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya BAKITA kimepatikana au hadi sasa mchakato bado unaendelea? Kiwanja hakijapatikana, tulipata kiwanja lakini kile kiwanja muuzaji alikuwa anataka alipwe papo kwa papo. Sisi ndani ya Serikali tuna taratibu zetu, kwanza inabidi tutafute kibali, kinaitwa *Single Source*. Sasa wakati mchakato wa kupata kibali hicho unaendelea, yule

akaona tunakawia akakiuza, lakini sasa hivi Serikali inamiliki majengo ya lililokuwa Shirika la Bima ambayo walikuwa wanakaa watumishi kule Kijitonyama, tumeomba pale *flats* walizokuwa wanakaa familia tisa. Hilo tumeandika kwa Waziri wa Fedha na Uchumi na ametuahidi kwamba, muda ukifika suala hilo litashughulikiwa na tukipata yale majengo tutayakarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, nchi yetu ina Maafisa Utamaduni na Michezo? Katika mambo ya *reform* (mambo ya mabadiliko katika muundo wa Serikali) huko nyuma tulikuwa na Maafisa Utamaduni wa Mikoa, Maafisa Michezo wa Mikoa, wakaondoshwa. Lakini katika Serikali ya Awamu ya Nne, tumejenga hoja Wizara ya Utumishi, tumekubaliwa sasa kuajiri Maafisa Habari wa Mikoa na Maafisa Michezo wa Mikoa na kule Wilayani, Maafisa Utamaduni wa Wilaya na Maafisa Michezo wa Wilaya. Kwa hiyo, kusema kweli masuala mengi ambayo ameyaeleza ni mambo ya msingi na sisi tumeyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Watumishi wa Vyombo vya Habari wa Serikali na binafsi. Nataka niseme hapa kwamba, maslahi ya watumishi wa vyombo vya habari vya Serikali ni mazuri sana kuliko yale ya wa vyombo binafsi. Lakini pengine nieleze hapa tatizo linalowakumba waandishi wa habari wa vyombo binafsi kiasi kwamba, wanalipwa malipo madogo. Tatizo kubwa ni kwamba, waandishi wengi wa habari wanaoitwa waandishi wa habari, wengi wao hawajakwenda chuo chochote kusomea masuala ya habari, ndiyo maana anakuwa yuko tayari kulipwa kiasi chochote kile ilimradi apate chochote. Lakini wale wachache ambao ni *Professionals*, wamesomea taaluma ya uandishi wa habari, wengi wao wanalipwa vizuri, iwe katika vyombo vya Serikali au vyombo vya watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Bendera ameshughulikia sehemu ya michezo na utamaduni, nisingependa kutaja kila mmoja ambaye amezungumza, maana muda wenyewe umekuwa mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itenge fungu la fedha kwa ajili ya mafunzo kazini. Hili tumelizingatia katika waraka wa kuanzisha chombo cha kusimamia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya watumishi wa vyombo vya habari, nyumba, usafiri, upungufu wa wafanyakazi wa Serikali na vyombo binafsi. Nadhani hilo tumelizungumza kwamba, tutalizingatia na kuhusu taaluma ya Uandishi wa Habari, Sheria ya Habari tutakayoileta hapa Bungeni, itaweka kipengele cha wamilki wa vyombo vya habari kuchangia Mfuko Maalum wa kuwasomesha waandishi wa habari, wale wapya na wale ambao wako makazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inachukua hatua dhidi ya waandishi wanaokiuka maadili ya taaluma yao? Nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Sheria iliyopo sasa hivi ni Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Sheria ile ya Utangazaji. Hatuwezi kuwa na *vacuum*, haiwezekani kukawa na mahali tupu tu kwamba, kosa limetendeka halafu hatuwezi kuchukua hatua kwa sababu Sheria iliyopo imepitwa

na wakati.  Sheria zilizopo zinabaki kuwa Sheria mpaka pale tutakapozibadilisha Bungeni na Rais akaweka sahihi yake.  Kwa hiyo, wale waliofanya hivyo wengi wao wamechukuliwa hatua, sisi katika Wizara yetu tunapenda sana kulea Waandishi wa habari maana bila wao sisi hatuna kazi.  Kwa hiyo, wengi tunawapa maonyo mara ya kwanza, mara ya pili, na mara ya tatu akizidisha tunamfungia kama ambavyo imewahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyombo vya Habari imepitwa na wakati. Nadhani hilo nimelieza. Kuhusu uwezo mdogo wa waandishi wa habari, tumeeleza sababu zake kwamba, wengi hawana mafunzo na hili nataka niseme Waheshimiwa Wabunge, kazi nyingi tulizonazo hapa Tanzania, kwa mfano kazi ya Ualimu, huwezi kuitwa Mwalimu mpaka umemaliza kidato cha Nne na una cheti cha ualimu, hapo ndiyo unasajiliwa, unapewa namba ya kutambuliwa kama wewe ni Mwalimu.  Ukienda kwa Wakunga, ukienda kwa Madaktari, ukienda kwa Wahandisi na kadhalika, kazi zote hizo ili uitwe fulani wa cheo kile, lazima uwe umesomea kwa kiwango fulani, kwa hiyo hilo tutalizingatia katika sheria ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course* kwa siku za mwanzo hatutaweza kusema kwamba, kuanzia leo watu ambao hawajasomea wasiandike, hatutaweza. Tutatoa kipindi kama ni miaka mitano, minne ili watu wapate kufundishana halafu itafika muda tutasema aah, sasa basi, kama huna cheti cha msingi cha Uandishi wa Habari, marufuku kujiita Mwandishi wa Habari, kama ilivyo kwamba ni marufuku mtu kujiita Mwalimu kama hujasomea taaluma ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachukua hatua gani kuitangaza ulimwenguni kumbukumbu ya Vita vya Majimaji?  Serikali imeviagiza vyombo vya habari kwa ujumla kwenda Mikoa ya Kusini kuandika na kutangaza kumbukumbu hizo na nafikiri tutakwenda Kilwa kuna sherehe za miaka mia moja ya Vita ya Majimaji. Wameahirisha, wameahirisha, lakini sisi katika Wizara tutashirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kukamilisha na kufanikisha uhamaji kutoka mfumo wa Analojia kwenda Digitali.  Tunajiandaa kufanya hivyo, malengo ni mpango huo ukamilike ifikapo 2025, lakini *TBC* wamekwishaeleza kwamba, watakamilisha zoezi hili miaka mitatu kabla ya ile tarehe iliyowekwa na Shirikisho la Mawasiliano Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani kuwahimiza Waandishi wa Habari kuanzisha vyombo vyao wenyewe?  Nimefurahi kuwa juzi hapa mwandishi mmoja wa habari aliyebobea amesema kwamba, kuna umuhimu wa wao kuanzisha vyombo vyao wenyewe vya habari.  Wangependa sana kuanzisha vyombo vyao vya habari, lakini najua tatizo kubwa ni mtaji.  Hata hivyo, pale watakapojitokeza sisi tutashirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa habari. Waandishi waachiwe uhuru watoe habari bila uoga wa kufungiwa.  Hapa nataka kuweka mambo wazi kwamba, hakuna Sheria ambayo haina kikomo chake.  Uhuru wa habari uko katika Katiba yetu lakini pia

uhuru wa habari unaishia pale unapoingilia uhuru wa mtu mwingine, hakuna uhuru ambao hauna mipaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo liko wazi, kwa hiyo kutoa habari kwa uhuru ni haki ya kikatiba na Umoja wa Mataifa. Hapa ningependa kuzungumzia maamuzi yaliyofikiwa na Serikali. Siku za nyuma tulikuwa tunazungumzia kuleta Sheria mbili hapa, Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari na Sheria ya Uhuru wa kupata habari "*access to information*". Sasa Serikali imeamua kwamba, ni vizuri tukaanza na Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari ndani yake vikawepo vipengele vinavyoelezea uhuru wa kupata habari, kwa sababu kwa uzoefu waliopata nchi ambazo zina Sheria kama hizi, India, Afrika kusini, Uingereza na kadhalika, imewachukua miaka mitano kupitisha Sheria inayohusu *access to information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana, kwanza tu kupata maelewano, kuelewana nini maana ya *access to information* ilichukua karibu miaka mitano na walipopitisha wakajipangia kipindi cha miaka mitano mingine ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu nini maana ya *accesss to information*, uhuru wa kupata habari. Sasa sisi tumeona katika Wizara tukisema tungoje zote mbili zikamilike tutachelewa, kubwa sana ambalo sasa hivi linahitaji tuchukue hatua za haraka ni hili la kuwa na chombo cha kusimamia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti ya Serikali tumepata malalamiko hapa kwamba mnunuzi akinunua anapewa kazi ya kuanzia kupanga *page* zile yeye anazotaka na nini, tumelisikia, wenyewe wanajitetea kwamba, wakati mwingine wanachelewa kumaliza. Sasa nadhani kwa mnunuzi anachotaka ni kitu kilichokamilika, kazi ya kupanga magazeti ukurasa wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne si la mnunuzi. Kwa hiyo, nami kama Waziri wa Habari, nadhani Shirika la Magazeti ya Serikali huko walipo wamenisikia. Mimi ni mmoja pia ninayekerwa na kazi ile ya kupanga zile *page*, nataka nikinunua nipate kitu kizima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Utangazaji, mna mipango gani ya kuhakikisha kwamba, kuna usikivu wa vyombo vya *TBC* na hasa katika mikoa ya pembezoni ambako sasa hivi hali ni mbaya zaidi kama Mtwara na Rukwa na juzi hii mnafahamu nilikuwa Kagera, Biharamulo kule, nilikwenda kule kwa shughuli binafsi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Biharamulo *TBC* haisikiki, mie Waziri wa Habari nimekaa Biharamulo pale hotelini wiki tatu na ushee, sikuwahi kusikiliza redio yangu. Kwa hiyo, nasema sio mikoa hii tuliyoweka hapa lakini kama tulivyoeleza mwaka huu tutakuwa na mikoa karibu 17 ambayo itakuwa inasikika kwa sababu ya kufunga mitambo ya *FM*. Bajeti ya mwaka endapo tutapata fedha mapema, itakapofika mwezi wa Sita au wa Saba mwakani, mikoa yote Tanzania Bara pamoja na Pemba na Zanzibar, watakuwa wanaisikia Redio Tanzania kwa usikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwamba Serikali ilipewa mtambo wa *FM* kutoka China kwa ajili ya mikoa ya pembezoni. Serikali haijawahi kupokea mitambo kama hiyo ya *FM* lakini tukipata kutoka China, tutaifunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikamilishe haraka mchakato utakaowezesha *TBC* kupatiwa mkopo wa Shirika la *NSSF* ili iweze kumalizia na kukarabati majengo yake. Nadhani hili sisi tumeliafiki na tunashukuru sana Kamati yetu imelisema katika maoni ya Kamati tutalifuatilia. Halafu jambo moja nataka kuliweka wazi hapa, kwamba imetolewa hoja kwamba Serikali kujipendelea kwa kuiruhusu *TBC* peke yake kutangaza mipira ya nje ya Kimataifa, kitendo ambacho ni sawa na Serikali kuingilia kwenye ushindani wa biashara kupitia vyombo vyake vya habari. Nataka niseme kwamba, suala hili limeendeshwa na Umoja wa Watangazaji katika Bara la Afrika. Waliwaita wanachama wao na hapa Tanzania wanachama sio *TBC* peke yake, wanachama ni pamoja na Watangazaji wengine. Sharti la kupewa kazi hii lilisema, mtangazaji yule awe hadaiwi kiasi chochote na Chama cha Utangazaji cha Bara la Afrika na kwa Tanzania mwanachama ambae alikuwa amelipia ada zake hadaiwi alikuwa *TBC* peke yake, akachaguliwa bila kupingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa hapakuwa na upendeleo wowote uliofanyika isipokuwa kwamba, ndugu zetu hawa wa *TBC* walikuwa wanachama wazuri wa chama chao hicho na hicho chama chao kwa nini kimefanya kazi hiyo? *FIFA* iliwapa Chama cha Utangazaji cha Bara la Afrika, kazi ya kuteua nani afanye kazi hiyo. Kwa hiyo, nao wakaweka kigezo hicho kwamba, madhali tumepewa kazi hiyo sisi, basi wanachama wetu ambao hawadaiwi ada wachukuliwe wao kwanza. Kwa hiyo, ndiyo maana *TBC* wakapata, hawakuwa na mshindani na wala hapakuwa na upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ishiriki kulinda maslahi ya Waandishi wa Habari hasa wa binafsi ambao wamekuwa wakilipwa mishahara midogo sana ili kupunguza *gape* baina ya Waandishi. Nadhani hili nimekwishalielezea kwamba, chanzo ni kwamba tuna Waandishi wa Habari, hata mkafanya utafiti, wale waandishi wa habari ambao wana *certificate* (cheti) katika uandishi wa habari, Mwandishi wa Habari ana *diploma* au ana *degree* wanalipwa vizuri sana.

Wengi sana ambao wanalipa mapato kidogo ni wale ambao hawajaingia darasani kusomea taaluma ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vimekuwa vikitoa habari za uongo, uzushi na uchochezi na zimeelezwa hapa. Tumeeleza hatua ambazo tumekuwa tunachukua, lakini nasema mimi kama Waziri wa Habari, siku ambapo tutakuwa tumepitisha Sheria hapa ya Kusimamia Vyombo vya Habari ambavyo Waziri wa Habari atakuwa anakaa pembeni, anangalia tu mambo yanavyokwenda, nitalala usingizi, kwa sababu yako matatizo katika hali tuliyonayo sasa ambayo lazima turekebishe na haya yanayosemwa hapa, sisi katika Wizara yetu tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Manju Msambya hapa amezungumza jambo, naogopa lakini sasa limezungumzwa ndani ya Bunge. Bodi ya

*TBC* ina Wakristo tupu. Nataka nieleze misingi ya kuteua Wajumbe wa Bodi ya *TBC,* wengi wale wameteuliwa kulingana na nyadhifa zao, lakini moja nataka niliweke wazi, maana yake hapa inaingia kwenye *hansard*, amesema kwamba Bodi haina Muislam. Bodi ile ina Muislam, Hassan Mitawi ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, mimi ni kada katika chama changu, naipenda nchi yangu, naheshimu umoja wa nchi hii, tukianza kuchunguzana kila Shirika Waislam wangapi, Wakristo wangapi, je ikija ikatokezea limekutwa shirika lina Waislam tupu au Shirika lina Wakristo tupu, itakuwaje? Nadhani jamani sisi tumekomaa, tunaangalia nani tumweke pale atufanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niweke rekodi hapa, *TBC* inayo Muislam anaitwa Hassan Mitawa, nimemteua na ndiye mwakilishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika bodi ile, katika kujenga mahusiano sisi na Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kipindi kinachoanza saa nane mchana kipindi ambacho kimebadilika, ni kwamba, la msingi hapa katika vipindi vyote vya dini, *TBC* inakaa na viongozi wa madhehebu. Kwa hivyo, ukikuta kipindi kinaendeshwa ni makubaliano kati ya madhehebu yanayohusika na *TBC*, pale madhehebu yanaposema tunaomba tufanye mabadiliko, basi wanakaa na uongozi wa *TBC*, halafu wanafanya hayo mabadiliko kwa kukubaliana kati ya madhehebu na uongozi wa *TBC*. Sifikiri kama Watanzania tulivyokomaa kuna mtu anaweza kusema kwamba, tuwapangie watu fulani muda fulani ili wasisikike. Kwa umoja na mshikamano tulionao Watanzania ndugu yangu Alhaji nadhani huko tumehama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la nchi yetu limekwenda wapi? Gazeti hilo lipo ila limeboreshwa na hivyo kutolewa nakala chache kutokana na gharama kubwa na hivyo halienei sana sehemu nyingi. Bado tunarudi pale pale kwamba, tatizo letu kubwa ni ukwasi lakini nia yetu ni kwamba, tutoe gazeti hili kwa nakala nyingi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malumbano baina ya Waandishi wa Habari mbalimbali hayaleti sura nzuri na yanabainisha jamii kushindwa wafuate taarifa za Waandishi gani. Haya ni matatizo tuliyonayo katika mfumo wetu wa sasa na haya tunataka kuyaweka katika Sheria mpya ya Uandishi wa Habari. Jana nilitoa mfano kwenye kikao fulani hapa, nilikwenda kukabidhi bendera kwa timu ya Taifa yetu ilipokuwa inakwenda Sudan. Lakini lile gazeti lilisema halitaki kuandika Habari za Waziri wa Habari, Naibu wangu Bendera alinisindikiza basi waliandika kwamba, timu imeagwa na Naibu Waziri Joel Bendera wakati nilikuwepo. Walinidhalilisha, lakini mimi mtu mzima nilikaa kimya kwa sababu aaah na picha yangu waliiweka haitokei, Naibu Waziri anaiaga timu wakati Waziri yupo, lakini nilinyamaza. Sasa mjue kwamba, tunawavumilia hawa ndugu zetu, ukisema uchukue ghadhabu kila wakati, nadhani tusingefika hapa. Moja kati ya mambo ambayo Mheshimiwa Khalifa na wengine mnapaswa, ni kwamba, inafaa kumpongeza Waziri wa Habari anavyowavumilia wadogo zake hao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matatizo kama haya, kwa mfano huyu kaandika habari ambayo ni ya uongo alikuwepo pale, aliyeaga timu anamjua lakini aliyesema ameaga timu mtu mwingine makusudi. Kwa nini, kwa sababu amesema hataki kuandika habari za Waziri wa Habari. Tulikaa kimya, lakini sasa pale watu wanajiuliza imewezekanaje Naibu Waziri anaiaga timu wakati Waziri yupo? Kumbe ilikuwa nini, *disinformation*. Sheria tunayoitunga akikutwa mtu amefanya makosa ya makusudi kama haya tutamchukulia hatua kwa mujibu wa sheria tunayoiandaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umekwenda na kengele hapana shaka itapigwa karibuni. Serikali itumie kwa nguvu wanaotumia vyombo vya habari vibaya, haya ni maoni ya waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu, tumesikia. Serikali idhibiti vyombo vya habari, viachane na kutoa taarifa za uchochezi tumesikia. Kwa kweli mengi yaliyozungumzwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, yametajwa leo katika baadhi ya hotuba ambazo zimechangiwa na watu waliochangia leo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ili nisipigiwe kengele tena, nachukua nafasi hii tena kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, nimefarijika sana kwa jinsi ambavyo Wabunge mlivyojitokeza kuchangia hotuba ya Wizara yangu. Michango yenu yote ilikuwa ni ya kujenga, michango ya kwenye *opposition*, michango ya upande wa Chama Tawala mmezungumza lugha moja, ishara ya kuonesha kwamba, Watanzania tunataka kulinda umoja na heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuahidini kwamba, kule Rwanda walikochinjana waliochochea mauaji ya Rwanda, walianza na redio, wakaenda na kwenye magazeti, ikaendelea polepole, siku waliposema *on your marks get set go*, sasa anzeni kuchinjana, sumu ile ilikuwa imekwishafanywa. Mimi kama Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama changu nakuhakikishieni Waheshimwa Wabunge na Watanzania wenzangu wote kwamba sitoruhusu mtu yoyote atakayeanza kuendesha propaganda au maandishi kwenye habari kwenye televisheni mahali popote yatakayohatarisha usalama wa Taifa letu, Utanzania kwanza vitu vingine baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli naomba nichukue nafasi hii nikushukuru na nikupongeze sana kwa umahiri wako katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Muda ni mchache lakini ndivyo hivyo inavyotakiwa twende. Baada ya hapo namwita Katibu atuambie hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 – *Administration and General... ... ... ... ...* …Shs. 1,681,603,000/=

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kujibu hoja zetu vizuri lakini nina swali moja tu nataka maelezo, nakumbuka zamani kila Wilaya ilikuwa na Afisa Habari na katika mchango wangu wa maandishi nilitaka maelezo kwamba katika Halmashauri zetu za Wilaya kuna Wakuu wa Idara karibu wote. Je, ufinyu wa bajeti uko kwenye Wizara hii tu, kwa nini wasipeleke Afisa Habari kila Wilaya?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli zamani walikuwepo Maafisa Habari Wilayani na *District Information Officer* japo kama haikuwa Wilaya zote. Lakini kama tulivyosema wakati Serikali inataka kupunguza ukubwa wa Serikali kuna baadhi ya Maafisa walifutwa na kama nilivyosema Mkoani tulikuwa na Afisa Utamaduni wa Mkoa, tulikuwa na Afisa Michezo wa Mkoa, nao ni miongoni mwa watu waliokuwa wamefutwa. Kama nilivyosema pia kwamba, tumejenga hoja Serikalini na tumesikiwa vizuri tu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi tumepewa kibali sasa kwenye Sekretariet kuwaajiri Maafisa wa Habari na Maafisa Utamaduni. Tunadhani kwamba ngoja tupate hao Maafisa Habari, Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo, baadae tutakwenda mpaka ngazi ya Wilaya hali ya uchumi itakaporuhusu.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ningeomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Tulishuhudia katika siku za karibuni baadhi ya magazeti yakifungiwa na mengine kuachiwa. Kwa mfano, gazeti la Mwanahalisi lililoandika juu ya wagombea watarajiwa wa Urais wa mwaka 2010 lilifungiwa lakini gazeti la Serikali la Habari Leo ambalo limeandika jambo hilo hilo halikufungiwa. Sitaki kuamini kwamba Serikali ilipendelea kwa hili kwa sababu ni gazeti lake. Lakini labda niseme tu nipate ufafanuzi Serikali ilitumia vigezo gani katika kufungia hili na kuliacha lile wakati mambo yaliyozungumzwa ni yale yale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kabla hujajibu. Waheshimiwa Wabunge naomba nitumie kanuni Na. 104, tumebakiwa na dakika 10 ili muda wa kumaliza shughuli za Bunge uweze kuwa umetutupa mkono. Kwa hiyo, kwa kuwa mjadala huu unaonekana utaendelea kuwa mrefu basi natumia kanuni hiyo sasa ambayo inanipa mamlaka kuongeza dakika zisizozidi 30 na bila ya kulihoji Bunge. Kwa hiyo, kwa mamlaka hayo sasa naongeza dakika hizo kutoka muda ambao tunatakiwa tumalize na kuahirisha shughuli zetu ili tuweze kumalizia mjadala ambao unaendelea kwa wakati huu hapa ndani, Mheshimiwa Waziri sasa naomba uendelee.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu, na kanuni. Moja katika sheria iliyopo mambo ya habari inasema akifanya mtu kosa mara ya kwanza anaonywa, mara ya pili anaonywa, ya tatu anaonywa, baada ya hapo anapewa adhabu kali zaidi. Mwanahalisi alikwishamaliza hizo tatu na pengine zaidi ya tatu. Kwa hiyo na

huyu mwingine unayemsema si kama tulimwacha hivi hivi alionywa kwa sababu ilikuwa ni kosa lake la kwanza.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, naomba nimwite Mheshimiwa Martha Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Jecha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimehoji kwamba kuna Waandishi wa Habari ambao wamesomeshwa na Serikali na wana *qualification* nzuri tu, ujuzi wao ni mzuri lakini wanapoajiriwa katika Shirika la Utangazaji la Taifa unakuta kwamba hawachukui muda mrefu wanaacha kazi na wengine wanabadilisha hata fani kwa kukimbilia maslahi katika Mashirika mengine. Nikasema kwamba, je, Wizara imeshabaini hilo na kuona kwamba tatizo huenda ni mshahara mdogo na imejipanga vipi katika kuweza kuwatumia wasomi hawa ambao Taifa limetumia fedha nyingi kuwasomesha? Naomba ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba niwakumbushe tunakwenda kwa swali moja kwa kila Mbunge. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nafikiri na wewe utajibu kwa utaratibu huo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba wako watu husomea taaluma ya Uandishi wa Habari wakaajiriwa baadae wakahama. Lakini nataka niseme hili liko katika taaluma zote, wapo Madaktari wamesomeshwa na Serikali wanafanya Serikalini baadae wakiona hakuna maslahi mazuri wanahama, wako walimu wanahama wanakwenda shule za *Private*, si Waandishi wa Habari peke yake. Kwa hiyo, nadhani dawa ni Bunge letu hili kutuwezesha sisi tulipe mishahara mizuri, tushindane na hao watu wengine ili Waandishi wa Habari wazuri wasituhame.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jecha atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Kahama.

**MHE MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kadhalika nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake pamoja na *TFF* kuuteua Uwanja wa Migombani kuwa ni miongoni mwa viwanja ambavyo vitafanyiwa ukarabati hasa kuwekwa nyasi bandia.

Katika mchango wangu nilitaka kupata ufafanuzi kwamba, pale kuna minara ambayo imewekwa ya kufungwa taa kwenye kiwanja kile, nilitaka kujua katika ukarabati huo taa hizi zitahusika katika ukarabati huo na ukarabati huo utaanza lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri swali moja tu, hakuna (a) na (b).

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Mbunge linahusu taa kukarabatiwa na pili kwamba shughuli zitaanza lini? Niseme tu kwamba taa hata Dar es Salaam, Ilala hakuna taa.

Wao wanachotengeneza ni uwanja pamoja na kupanda zile nyasi bandia. Lilikuwepo tatizo kidogo kwa sababu wanatakiwa na wenzetu nao *ZFA* wachangie kidogo maana fedha zinazotoka hazitoshi. Tumezungumza na wenzetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waziri anayehusika na Michezo kule amewatafutia fedha kama bajeti *inshallah* ikipita ya Wizara ile kule Visiwani fedha ile ikapatikana, shughuli za ujenzi zitaanza.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri sasa namwita Mheshimiwa Mama Janet Kahama na Mheshimiwa John Cheyo ajiandae.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi nilikuwa na wasiwasi na maeneo ya mazoezi ya viungo ambayo ni *gym* na nikasema kuwa baadhi ya maeneo hayo ya watu binafsi imejulikana wazi kabisa wanauza vipodozi ambavyo vingine wanapaka kwenye tumbo ili matumbo yawe madogo, wanapaka kwenye maziwa matiti yawe makubwa, wanapaka kwenye makalio, makalio yakue, lakini inaonekana yote hayo yameleta athari kubwa sana matiti yamerefuka kupita kiasi, makalio mengine yamepasuka na inaelekea watu wengine wameanza kupata kansa na haya ni maeneo ya mazoezi ya viungo *gym*. Je, kuna *any inspections* ambazo zinafanywa katika maeneo kama haya na kama hakuna, je, wako tayari wao kama Wizara kuanza kukagua maeneo kama haya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja tu hiyo (b) unaiacha.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kwamba anachozungumza Mama Kahama ni kwamba hizi *gym* zote ambazo ziko hasa Dar es Salaam kuna *gym* nyingi sana zinaendeshwa, ambazo ni biashara binafsi haziko chini ya Wizara. Lakini tuna utaratibu ambao tunauanzisha kwamba tutakuwa tunazikagua kwa sababu hilo ndilo tunaanza kulipata. Kwa hiyo tutalifanyia kazi tujue kama watu wanapotoshwa au mazoezi yanayofanywa sio ya kitaalam, basi sisi kama Wizara kwa sababu tunao wataalam wa kutosha tutatoa mafunzo kwenye *gym* hizo na hayo yanayovimbisha vikalio.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa lugha nzuri ya Kiswahili ni makalio.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani wanaovimbisha makalio na maziwa basi tutajitahidi kwa kweli kuhakikisha kwamba suala hilo tunalishughulikia.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nitaomba ujifunze Kiswahili tena zaidi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri juu ya uongo ulioandikwa na gazeti la Tanzania Daima juu ya Ofisi ya Bunge ambao nakana kabisa kwamba ni uongo lakini nimeelezwa kwamba tunaweza kuliita hili gazeti mbele ya Kamati na tukapata mambo ambayo wameandika kule.

Kwa hiyo kitu ambacho nataka kuuliza tu ni ile dhana ya televisheni na redio kusoma haya magazeti na zaidi magazeti ambayo ndani yake kuna uongo, je, hawaoni kwamba na wenyewe wanaendelea kuvunja sheria sawa sawa na yule ambaye ameandika haya mambo na Waziri anasemaje juu ya jambo kama hili?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale Wizarani ninao Maafisa wawili kazi yao ni kusoma magazeti kuangalia yaliyoandikwa ili kuona kama kuna mtu amekwenda kinyume. Lakini sasa inapotokea wameandika habari zinazokuhusu wewe na unaona kwamba zile habari si sahihi una wajibu wa kulalamika ili tumchukulie hatua yule mtu anayetakiwa. Kwa mfano, yakitokea malalamiko sisi tunaandika barua kwamba fulani amelalamika hivi tunataka maelezo yako na wengine tukishasoma kama hatukuridhika nayo tunawaambia kwamba andika barua ya kuomba radhi na wanafanya hivyo.

Juzi hapa nadhani Mama Malecela alilalamika kwamba gazeti halikumwandika vizuri, tulichukua hatua hiyo, wanaohusika waliona wapi wamefanya makosa wakaomba radhi na tukalimaliza. Kwa hiyo, naomba endapo Mheshimiwa Cheyo kwa neno la Kiingereza kama umekuwa *offended* na hilo gazeti maana hujanionyesha bado basi utuandikie au utupatie tutachukua hatua kwa kadri tutakavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Zubeir Maulid ajiandae.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata ufafanuzi wa Serikali au Wizara inayafuatilia kwa namna gani magazeti hasa ya Serikali na hapa namaanisha gazeti la Habari Leo ambalo limekuwa likichapisha makala na taarifa ambazo kwa kweli zinaidhalilisha Serikali hiyo hiyo ambayo kazi yake ni kusimamia utekelezaji wa sera ya habari. Kwa mfano, katika gazeti la jana kuna makala imeandikwa ukurasa wa 11 na 12 ambayo lengo lake kwa kweli ni kuwachonganisha Wabunge na Mawaziri. Sasa ningependa kupata ufafanuzi kwa gazeti la Serikali ambalo linaandika habari kama hizo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio uandishi wa habari. Nimefurahi kwamba hata gazeti letu linalalamikiwa kwa sababu mara nyingi tunasema tu gazeti la fulani, gazeti la fulani, ninamwomba tu Mheshimiwa Lembeli kwa sababu gazeti analo hapa na hajaeleza Waziri gani, basi atuletee tutalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Zubeir Maulid atafuatiwa na Mheshimiwa Benito Malangalila.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi niligusia hamu ya Zanzibar kujiunga na *FIFA* ambayo katika maelezo niliyoyatoa nikasema itasaidia sana kuondoa huu utata baina ya

*TFF* na *ZFA*. Nilitoa mfano kwamba, kama Uingereza inawakilishwa mara nne ndani ya *FIFA*. Inawakilishwa kama England, Scotland, Wales na inawakilishwa kama Northern Island. Tanzania tukiwa na uwakilishi wa Tanzania na uwakilishi wa Zanzibar ndani ya *FIFA* tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje sisi tunaotoka Zanzibar kuhusiana na hili na Wazanzibar wanataka kusikia?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza ndugu Zubeir ni sahihi, juhudi zimefanywa na wote tunatambua kwamba Zanzibar inashiriki mashindano ya *CECAFA*. Lakini Zanzibar hiyo hiyo tumefanya juhudi kupata wanachama wa *CAF* (Shirikisho la Afrika), tumeshafikia *stage* hiyo. Sasa tunaendelea na mchakato wa kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo inafanikiwa kwenye *FIFA*. Suala hilo linashughulikiwa na bado tunaendelea kulishughulikia, naomba tuvute subira iko siku Zanzibar itapata nafasi yake.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Malangalila na Mheshimiwa Haroub Masoud ajiandae.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwamba alikuwa mgeni rasmi katika fainali za Kombe la Muungano Mufindi na lile kombe lilianza mwaka 1996. Sasa swali langu katika mchango wangu wa maandishi ni kwamba je Serikali itaendelea kutuchangia na yenyewe? Kwa sababu tumekuwa tukipata wahisani kama *VODACOM* na wahisani wengine katika miaka ya nyuma, je, Serikali iko tayari kuanza kutuchangia?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalitambua Kombe la Muungano, mashindano haya ni makubwa sana na mashindano haya kwa kweli yameshirikisha viongozi wengi wa Zanzibar pamoja na Bara. Baadhi ya Mawaziri humu wamekuwa wageni rasmi na kuyafungua. Sisi kama Wizara wote tunatambua bajeti yetu ni ndogo na mashindano kama haya yanafanyika sehemu nyingi sana na mikoa mingi sana. Ninachoweza kuahidi ni kwamba, sisi kama Serikali tutaendelea kutoa mchango wetu mdogo wa kiutalam na tutakapokuwa na fedha tutasaidia kwa sababu tunayatambua mashindano yale.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwite sasa Mheshimiwa Haroub Masoud na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ajiandae.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina neno dogo tu ambalo labda kama atakuwa na uwezo hapa Mheshimiwa Waziri aweze kulifafanua ili litusaidie sisi Wabunge na vile vile Waandishi wa Habari.

Tulipokuwa Dar es Salaam kwenye Kamati sijui kama ulikuwepo Mwenyekiti, Wizara ya Habari ilitufanyia semina na ambayo iliendeshwa na Baraza la Kiswahili Tanzania. Walituletea orodha ndefu ambayo inazungumzia suala la upotoshaji wa lugha

tukiwemo sisi Wabunge, lakini sasa nasikia ndani ya redio kila wakati hata humu ndani Bungeni kwamba wanasema "Maguzo ya Umeme yamesimikwa". Hasa hili ni neno kweli sahihi la Kiswahili? Kwa sababu tusije tukaendelea tu sisi tukajiona tunatukana maana yake naona kichefuchefu kulitaja kila wakati.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Haroub. Mheshimiwa Waziri sasa hiki sijui ni Kiswahili cha Kiunguja ama………

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Haroub Masoud. Najua watu wanawaza makabila yao kwanza halafu wanakwenda kwenye Kiswahili. Sehemu nyingine ukisema lile alilosema sitaki kusema kwa sababu, lakini njia sahihi ni kusema nimewakuta wanasimamisha nguzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu umegusia lile la semina Wizara yangu kwa sababu tumesema kwamba sisi tunataka tutoe mfano hapa ndani inatafuta fedha tuandae semina ya Waheshimiwa Wabunge ya lugha ya Kiswahili ili tupate kuelezwa yale maneno ambayo yanakosewakosewa sana. Waingereza wanayo *common mistakes in English* sasa tunataka kuleta ya kwetu sisi *common mistakes in Swahili* na pengine kuanzia leo hapa tunapochangiachangia. Nimengoja muda wa masaa, hakuna neno "masaa" na sisi tunafanya jitihada ingawa kimyakimya. Kama ukienda kwenye mabenki humo waliandika *ATM* masaa 24, tumewaandikia barua wote na sehemu nyingi wamefuta.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri. Namwita Mheshimiwa Zarafi atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia mchango wangu wa maandishi na wa kusema nilizungumzia maslahi ya Waandishi wa Habari na nilizungumzia mazingira bora ya kufanyia kazi. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alijibu kuhusu la maslahi lakini bado sitaweza kulizungumzia zaidi kwa sababu wale Waandishi wengine aliowataja kwamba maslahi yao madogo inawezekana hawana elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala hili la mazingira bora ya kufanyia kazi. Nilipozungukia *ITV* niliona maeneo mazuri ya kufanyia kazi Waandishi wa Habari na nilizungukia pia *TBC*. Lakini nilikuta ndoo za maji zimekingwa wakati wa mvua na nilikuta ma-*carpet* yote yamelowa na nyaya za umeme zinapita huko. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu jengo la *TBC* lililopo Mikocheni nini hatma yake? Ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika hotuba yangu na maoni ya Kamati tumezungumzia juu ya uwezekano wa kupata mkopo kutoka *NSSF* kwamba Serikali ikubali kutoa *guarantee* ya asilimia 100 badala ya 70 na tukipewa zile fedha tunakusudia kufanya hiyo kazi ya ukarabati japo ile shughuli ya kuvuja kule Pugu *Road* tumeanza kuchukua hatua kidogo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kwa kuwa gazeti nililolinukuu la Serikali la Habari Leo liliwahi kuandika kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA yaani Mheshimiwa Zitto alichoma bendera ya CCM wakati wa Uchaguzi kule Busanda na chama kiliandikia gazeti hili na vile vile Msemaji wa Polisi wa Busanda alikiri kwamba si kweli kama Zitto alichoma bendera. Lakini vile vile gazeti hili limeendelea kuandika habari za upotoshaji kuhusu Chama cha Demokrasia na Maendeleo. Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari kuwaelekeza vijana wake waombe radhi kwa upotoshaji huu?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nadhani kila chama nikisema kieleze malalamiko waliyonayo kuhusu magazeti, nina uhakika na watu wa chama fulani wanaopiga makofi wana mambo yao kuhusu haya magazeti.

Sasa turudi katika sheria, taratibu na kanuni. Kama nilivyomweleza kaka yangu pale Mheshimiwa John Momose Cheyo kwamba gazeti limeandika jambo ambalo si kweli na wewe unaamini kwa hakika si kweli unatakiwa kuja kulalamika kwetu. Hukutosheka na maamuzi au hatua tutakazozifanya ruksa wewe kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoitoa inawezekana kwa sababu nilikuwepo kijijini naifahamu zaidi kuliko yeye, lakini sio kwa sababu hoja yenyewe iliyoulizwa, tunachosema waliojihisi walifanyiwa vibaya walikwenda kulalamika kituo cha Polisi na hatua za Kiserikali zilichukuliwa kwa chombo kinachohusika. Sasa kama kesi hiyo hiyo iwe *handled* na Polisi, kesi hiyo hiyo tena ije kwa Waziri wa Habari, wangekuja kwangu kwanza ningewashughulikia, lakini wamekwenda Polisi na Polisi wamelishughulikia kwa mujibu wa taratibu za usalama wa raia.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Diana Chilolo atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimewapongeza viongozi wa michezo pamoja na Maafisa Utamaduni wa Wilaya na Mikoa jinsi ambavyo wanajitahidi sana ku-*promote* michezo kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya mpaka Taifa. Lakini tatizo ambalo linajitokeza katika fani hii ya michezo ni kwamba pale wachezaji wanapofikia ngazi ya Mkoa kwenda Taifa panakuwa na utata wa upatikanaji wa fedha za kusafirisha wachezaji. Kwa mfano juzi juzi wachezaji walicheza kule Mkoa wa Pwani Wasichana, Ngazi ya Taifa, Mkoa wa Singida na Mikoa mingine hawakushiriki kwa sababu ya fedha tu. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutenga bajeti katika Halmashauri zetu kupitia Maafisa Utamaduni wa ngazi ya Mkoa ili utata huu wa kusafirisha wachezaji uondoke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kama suala linahusu Halmashauri ni suala la TAMISEMI moja kwa moja. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri kama una majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, jibu lipo. Katika Sheria ya *Sports Administration* katika nchi yetu ngazi ya chini kabisa kiutawala ni klabu yenyewe halafu inakuja chama husika halafu unakuja kwenye chama cha Kitaifa mpaka unafika Wizarani. Lakini bahati nzuri ukitazama ile sera ya maendeleo ya michezo wenzetu wa Mikoa na Wilaya, Mwenyekiti wa Maendeleo ya Michezo katika Wilaya ni *DAS* ambayo ni Serikali, katika Mikoa ni *RAS* na wao wana Kamati ya Maendeleo ya Michezo ya kupanga mikakati ya namna gani timu zao zishiriki. Moja ya tatizo ambalo tunalipata Tanzania ni yale ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametusaidia kutoa waraka kwamba Wilaya zote na Halmashauri zote sasa wachangie, watoe fedha na wapange bajeti ya maendeleo ili timu hizi zinapofikia katika hatua hiyo anayoizungumzia Mheshimiwa Chilolo ziweze kushiriki kule. Lakini tatizo ni kwamba hamna fedha na ndiyo maana yako matatizo haya na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu akatusaidia. Hapa naomba nitoe wito kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa agizo, tekelezeni huko katika Halmashauri zenu ili angalau mikoa nayo iweze kushiriki katika mashindano mbalimbali katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ole Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliomba maelezo ya Waziri kuhusu vigezo vinavyotumika katika utoaji wa matangazo ya Serikali hasa katika magazeti na hasa baada ya kujiridhisha kwamba katika siku za karibuni kumekuwepo na magazeti ambayo yameanzishwa yanayomilikiwa na wanasiasa na hasa yale yanayomilikiwa na Mawaziri ambayo yanachapisha nakala chache lakini matangazo ya Serikali yanaelekezwa katika magazeti hayo badala ya kuelekezwa katika magazeti ambayo yanachapisha nakala nyingi zaidi, jambo ambalo linadhihirisha kutokupatikana kwa thamani halisi ya fedha za Serikali zinazotumika. Kwa maana hiyo niliomba Waziri atusaidie kueleza vigezo gani vinavyotumika kutoa matangazo haya ya Serikali?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayepeleka tangazo kwenye gazeti ni mwenye tangazo. Anaangalia tangazo langu nilipeleke mahali gani kwa sababu magazeti yapo mengi na asubuhi tumetaja idadi yake. Lakini mimi ni mtu muwazi na mkweli. Wewe umesema hutaki kumtambua Msemaji wa Serikali na hutaandika habari zake. Sasa mambo mengine haya ni watu kutokuelewa, ukimsusia Msemaji wa Serikali ndiyo umeisusia Serikali, halafu unataka Serikali ikuletee matangazo. Si umesema hutaki kufanya kazi na Serikali. Mambo mengine mnajimaliza wenyewe. (*Kicheko*)

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia jinsi ambavyo Wizara imeitelekeza

CHANETA na hili limejithibitisha hata leo, ukiangalia ugeni wa wageni wa Wizara kama wadau na hii ilitokea pia mwaka jana wanaletwa tu viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu. Sasa hili pia lilithibitika katika michuano ya Taifa *Cup* ambapo tulishuhudia CHANETA kwa kushirikiana na *Radio One* walikuwa wanaomba fedha kwa watu mmoja mmoja kama watoto yatima. *Actually* Waziri au Wizara ilikuja kutoa pesa milioni moja baada ya mashindano kwisha na baada ya CHANETA kulalamika kwamba kuna deni la ziada la milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka Waziri aniambie ni nini nafasi ya Wizara katika sekta nzima ya michezo kwa mapana yake?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba aliuliza suala la CHANETA. Kwanza kwa kutokutambulishwa asubuhi hapa. Vyama vyote vya Michezo vya Kitaifa viliandikiwa kuja kushiriki katika shughuli hii ya leo. Jana nimepigiwa simu na Makamu Mwenyekiti wa CHANETA Bi. Shy-Rose Banji akiniambia. "Mheshimiwa Waziri katika orodha ya wageni wako kesho mimi nawakisha CHANETA." Lakini sijamwona. Kwa hiyo, sisi tulivyotoa mialiko hatukubagua vyama, lakini la pili kusema ukweli katika kipindi kilichopita tulikuwa na uongozi dhaifu sana wa CHANETA. Wizara inatambua kwamba kama kuna mchezo umetuletea heshima Kimataifa ni CHANETA, *East and Central Africa* kwa timu za Jeshi *Stars*, Bima Bandari na wengine. Sisi tunalitambua hilo na ndiyo maana tunashirikiana nao. Lakini katikati hapa hata uendeshaji kazi, kazi moja ambayo ameifanya Ndugu yangu Bendera na mimi ni kufufua mashindano ya CHANETA ambayo yamesimama kwa muda mrefu. Mwaka jana yalikuwa Mikoa tisa tu. Tukamwomba Waziri Mkuu alipokuja akaona aibu ile. Nchi ina Mikoa 21 Tanzania Bara, walikuja Mikoa Tisa. Kutokana na sisi kuipenda *Netball* tukamwomba Waziri Mkuu akatoa maagizo kila Kiongozi wa Mkoa ahakikishe Mkoa wake unashiriki mashindano ya *netball*. Ndiyo imepanda kutoka ile tisa mpaka 17. Kwa hiyo, tunakwenda polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwezi ukamleta mwalimu kutoka Uingereza, anakuja kufundisha *Netball*, anakuta hata uongozi wenyewe utakaompokea uko *disorganised*. Lakini sasa hivi mambo yameshakuwa mazuri, tuna uongozi *serious, committed* katika mchezo wa *netball* na kwamba kutokuja hapa leo ni bahati mbaya, lakini sisi tunashirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwapa ruzuku, basi si angalau wamepata hiyo milioni moja. Nadhani vitabu mnavyo hapo, hakuna fungu lolote mlilopitisha la Waziri kusaidia mashindano mbalimbali. Waliosaidia na tuliowataja hapa ni *Mohamed Enterprises, ADB, Coca Cola* wametafutwa na Chama chenyewe cha *TFF*. Naamini akina mama kwa jinsi mlivyo hodari kujieleza nina uhakika mtakapokuwa mnaomba misaada katika mashirika mbalimbali mtasaidiwa na nina hakika mtafanya vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita msemaji anayefuata naomba niwakumbushe tu Kanuni namba 104(2). Inatupeleka katika kufanya maandalizi

sasa ya kupitisha Bajeti yetu na mafungu yaliyosalia kwa kutumia utaratibu wa *guillotine*. Itakapofika saa mbili na robo nadhani tutaingia katika utaratibu huo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie maelezo yafuatayo. Nilipokuwa nachangia leo sikuchangia kuhusu *TFF* na *ZFF* sikugusa kabisa. *ZFA* kama Zanzibar katika sakata ambalo linaendelea hivi sasa tarehe 21 litakuwa limekwisha. Tumekwishasafiri sana sisi. Nilichochangia kwa maandishi leo na kwa kusema ni Utaifa wa Tanzania ndani ya Bunge na hili namwomba sana Mheshimiwa Waziri akalifanyie kazi kama nilivyosema baina yake yeye na Waziri wa Michezo Zanzibar. Sisi tunakufa, watabaki vijana wetu waje kurithi mambo mazuri. Nilichochangia leo ni kumwomba Mheshimiwa Waziri akae na mwenzie atoe agizo au maelekezo kwamba uwakilishi wa Tanzania nje unaweza ukasajiliwa na Tanzania Bara kama ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu wao ndiyo wenye mambo ya nje.

Lakini vyama vinapojisajili huko nje wakishapata usajili humu ndani warudi waweke taratibu na vyama vingine vya Zanzibar ili wanapokwenda nje ijulikane kama ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndicho nilichosema. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba ili Tanzania itambulike huko nje, vyama vyetu humu ndani viwe na Katiba ambayo inazungumzia kwamba ndani ya Jamhuri ya Muungano tuna vyama viwili lakini tukienda nje tuna Utanzania ambao tunakwenda nao. Sikuzungumzia *ZFA* hapa. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri ili kuliweka Taifa letu vizuri na vizazi vije kurithi mambo mazuri hili lifanyike tuondoe hii mizozo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru ndugu yangu Hafidh. Mimi na yeye tumezungumza labda anataka yale tuliyozungumza mimi na yeye yaingie katika *Hansard*. Kwanza ukisema uingize katika Katiba maana yake Zanzibar waache kudai uanachama. Maana huwezi ukaingiza katika Katiba ya *TFF* na pia ukaingiza kwenye *ZFA*. Tulichosema na ambacho nimekuahidi ni kwamba wenzetu nchi za nje, wakishaleta mwaliko Dar es Salaam labda kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wanasema mwaliko umeshafika Tanzania. Kule nje hawafahamu wao kwamba habari utamaduni na michezo si suala la muungano. Sasa kwa kutumia busara namuuliza kaka yangu Shamhuna, je, mwaliko huo umeupata huko au tumeletewa mwaliko mmoja? Tukishabaini mwaliko ni mmoja mimi na kaka yangu Shamhuna tunaamua. Tunatengeneza *delegation* ya bara na visiwani. Mara nyingi nimekwenda safari naongozana na Naibu wa Zanzibar na mara mbili ameshakwenda Mheshimiwa Shamhuna na Naibu wa Bara. Ndivyo tunavyokwenda lakini haimo katika Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema suala la *ZFA* na *TFF* uliingize katika Katiba tutadhoofisha hoja ya Zanzibar kwamba wao wabaki *independent* kama chama kinachojitegemea kinachoomba unachama kwenye *FIFA*. Acha tuendelee kama tulivyo, tudumishe mahusiano kama yalivyo, tukishindwa kupata uanachama *FIFA* tutakaa sasa tuseme jamani imeshindikana tutengeneze chombo cha pamoja sasa. *TFF* ya Tanzania nzima bara na visiwani.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge nimewaelewa tulikuwa hatujaelewana katika uongozi wangu wa Kiti. Kwa hiyo, baada ya kubakiza dakika kumi kabla ya kufika saa mbili na robo tunatakiwa sasa tuingie kwenye mafungu. Kwa hiyo, nitamwita sasa Katibu tunafunga mjadala tunapitisha kwa mafungu.

**MWONGOZO WA MWENYEKITI**

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA**: Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA**: Kanuni ya 68(7).

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 68(7)!

**MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikimwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu vigezo vinavyotumika katika utoaji wa matangazo ya Serikali na nikahusisha utoaji huo unaotolewa na Wizara mbalimbali na magazeti kwenye magazeti yanayomilikiwa na baadhi ya watendaji wa Serikali wakiwemo Mawaziri. Waziri badala ya kunijibu hilo alielekea kuniunganisha na magazeti ambayo hayamwandiki yeye wakati nimeelezea mgongano wa maslahi ulipo kati ya Mawaziri ambao wana dhamana katika Wizara kutoa hotuba zao kama matangazo ya Serikali kwa magazeti yenye nakala chache wanayomiliki wao. Sasa badala ya Waziri kunijibu mgongano wa maslahi uliko ananielekeza kana kwamba nimetetea magazeti ambayo hayamwandiki yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata mwongozo wako katika hili kwa sababu nilikuwa nimelenga katika masuala ambayo yana maslahi kwa nchi na kutaka Watanzania wapate thamani halisi ya fedha zao zinazolipia matangazo kwenye magazeti ya wanasiasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza naomba niendelee kuitii Kanuni kwamba sasa ni kipindi cha kupitisha kwanza Bajeti hii kwa mafungu. Baada ya hapo nitatoa mwongozo wa maelezo yako.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … shs 400,361,000/-
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … shs 464,103,000/-
Kif. 1004 - *Information, Education and Communication* ... ... … shs 259,606,000/-
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit* ... ... ... ... ... … … … … … shs 201,461,000/-
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit* … … … … shs 159,064,000/-
Kif. 6001 - *Culture and National Languages* ... ... … … … … …shs 3,565,562,000/-
Kif. 6004 - *Sport Development* … … … shs 2,388,006,000/-

Kif. 7003 - *Information Services* .. ... ... ... .shs 6,606,322,000/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo**

Kif. 1001 - *Administration and General*.. shs 418,043,000/-
Kif. 1003 - *Policy and Planning* . ... ... ... ... .shs 450,000,000/-
Kif. 6001 - *Culture and National Languages*... ... .. … … … … …shs 2,000,000,000/-
Kif. 6004 -*Sport Development* … … … shs 1,629,221,000/-
Kif. 7003 - *Information Services* ... ... ... ...shs 2,100,000,000/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2009/2010 na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Bajeti ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado hatujamaliza, tusianze kumpigia makofi Mheshimiwa Waziri, bado Bunge halijapitisha hayo makadirio sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa fedha 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kutangaza kwamba Bunge limefanya kazi yake na limepitisha makadirio ya Wizara hii. Kinachotakiwa ni

Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yetu nzima ya wataalam kufanya kazi vizuri kwa maslahi ya Taifa letu kupitia bajeti hii ambayo tumeipitisha leo. Nawatakia kila la kheri sana.

Kabla sijamaliza hizi shughuli za leo, toka asubuhi tuna mgeni mmoja muhimu sana na nisipomtangaza hata wenzake watashangaa kwa nini hakutangazwa. Katika timu ya Mheshimiwa Waziri alikuwepo pia Mzee Kassim Mapili ambaye ni Mwenyekiti wa Tanzania chini ya Chama cha Wanamuziki Tanzania. Mzee Mapili karibu sana na ametupigia saluti kubwa sana.

Baada ya hapo, naomba nitoe mwongozo kwa suala la Mheshimiwa Sendeka. Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa katika kupitia makadirio haya ya leo kumekuwa na matatizo mengi yanayohusiana na mageuzi na Mheshimiwa Waziri amesema kila tatizo lililojitokeza katika sekta hiyo ametoa nafasi watu wakutane nae na kuona ni namna gani hatua za kisheria zinaweza kuchukuliwa. Nakuomba sana Mheshimiwa Sendeka katika kipengele hicho hicho, hebu fanya utaratibu wa kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri tuone matatizo hayo yataweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kiasi gani. (*Makofi*)

Baada ya kutoa mwongozo huo, nawashukuru sana na nawaomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho Saa tatu Asubuhi.

*(Saa 02:15 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 16 Julai, 2009, Saa tatu Asubuhi)*